Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA SABA

**Kikao cha Saba – Tarehe 18 Aprill, 2012**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati Zifuatazo ziliwasilishwa Mezani na:-

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. PEREIRA AME SILIMA)**

Taarifa ya mwaka na hesabu za Chuo cha Usimamizi wa Fedha kwa mwaka 2009/2010 *(The Annual Report and Accounts of the Institute of Finance Management for the year 2009/2010).*

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIITAA (TAMISEMI):**

Taarifa ya Matoleo yote ya Gazeti la Serikali Pamoja na Nyongeza zake Yaliyochapishwa tangu Kikao cha mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 82

### Mgogoro wa Viwanja-Wananchi wa Manispaa ya Bukoba

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA** aliuliza:-

Uko mgogoro mkubwa wa viwanja kati ya wananchi na Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba ambapo wananchi zaidi ya 800 walilipa fedha zao ili wapatiwe viwanja tangu mwaka 2002 na sasa ni miaka kumi imepita hawajapatiwa viwanja hivyo na Halmashauri hiyo haionyeshi juhudi za kutoa viwanja badala yake wananchi hao wanaambiwa kulipia gharama zaidi za wakati huu:-

Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Halmashauri hiyo ili iweze kuwapatia wananchi hao haki yao ya kupata viwanja hivyo walivyokwishalipia tangu mwanzo?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIITAA (TAMISEMI)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Conchesta Leonce Rwamlaza, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba upo mgogoro uliojitokeza katika baadhi ya wananchi waliochangia fedha zao kutopatiwa viwanja katika Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba.

Mwaka 1996 Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba ilipitisha Azimio kuwa wananchi wanaohitaji viwanja katika eneo la Kyabitembe kwa ajili ya makazi, biashara na huduma za jamii wachangie gharama za upimaji ambazo zilikuwa ni

shilingi 50,000/- kwa *high density*, shilingingi 60,000/- kwa *medium density* na shilingi 70,000/- kwa *low density*. Maeneo ya taasisi yalichangiwa shilingi 100,000/- hadi 200,000/-. Baada ya upimaji wananchi wote walipatiwa viwanja na hapakuwa na mgogoro.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la uchangiaji liliendelea mwaka 2003, 2004, na 2005 katika maeneo ya Kyabitembe II , Rwazi/Rwome, Kiteyagwa na Kibuye ambapo jumla ya shilingi 58,562,600/= zilichangwa na wananchi 1,049. Hata hivyo, eneo pekee ambalo viwanja vilipimwa ni Kyabitembe II sawa na viwanja 476. Eneo hili halikuwa na makazi ya watu lakini walijitokeza wananchi na kudai maeneo hayo wanayamiliki kimila hivyo walitaka kulipwa fidia kwanza ndipo upimaji uweze kufanyika. Halmashauri ilisitisha upimaji na hivyo kuzua mgogoro na wananchi hao wakidai fedha walizochangia jumla ya shilingi 58,562,600/=

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba imeingia ubia na shirika la dhamana na uwekezaji Tanzania *(UTT)* na kupatiwa shilingi bilioni 2.9 kwa ajili ya kupima viwanja 5000 ambavyo vitauzwa kwa wananchi wote.

Hii ni sehemu ya mkakati wa Serikali kutatua mgogoro kati ya wananchi waliochanga fedha zao na Halmashauri. Azimio limetolewa na Halmashauri kupitia Kamati ya Fedha , Uongozi na Mipango iliyokaa tarehe 16/11/2011 na Baraza la Madiwani lililokaa tarehe 16/4/2012 kwamba wananchi wote waliochangia fedha lakini hawakupata viwanja, wauziwe viwanja kwa bei ya punguzo sawa na fedha zilizochangwa kwa wakati huo na kwa thamani ya sasa. Aidha, watakaoshindwa kulipa warudishiwe fedha zao kwa thamani ya sasa. Vikao hivyo vimepitisha Azimio kuwa ili kupata thamani ya sasa ya fedha zilizochangwa kwa wakati huo riba ya asilia tano itawekwa kila mwaka kuanzia kwenye mwaka waliochangia hadi sasa. *(Makofi)*

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimepokea majibu ya swali langu kutoka kwa Waziri. Kwanza napenda kusema kwamba Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba imewatapeli wananchi wa Manispaa hiyo, siyo kuwatapeli tu, lakini pia inaendeleza kufanya dhuluma kutokana na majibu niliyoyapata hapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumwuliza Waziri, si kweli kwamba wananchi wa Manispaa ya Bukoba walichangia upimaji, ukifuatilia fomu zilizojazwa kutokana na fedha walizochanga zinaonesha wazi wazi kwamba yalikuwa ni maombi ya viwanja, ninashangaa kwa miaka kumi wananchi wamekuwa wakidai viwanja vyao na mpaka sasa hawapatiwi, naomba Waziri kwa sababu jambo hili nilishakueleza hata wakati unafanya majumuisho ya ziara yako utamke utawasaidiaje wananchi wapate viwanja vyao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu la pili, ukitazama mkataba ulioingiwa na Manispaa kutokana na mkopo walioupata kutoka *UTT* ni mkopo wa kibiashara, huwezi ukauza viwanja 5000 chini ya milioni sita ili kulipa deni.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa sasa swali?

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika swali, wananchi wale watalipwaje asilimia tano ambayo kwa mtu aliyelipa elfu arobaini ni elfu ishirini kwa miaka kumi, utawasaidiaje wananchi hawa waweze kupata fedha zao kama hawakupata viwanja kwa thamani ya sasa na kwa riba inayoendana na biashara kwa sababu Halmashauri inaonekana wanafanya biashara.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante umeshaeleweka, Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa ufupi.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa

Naibu Spika, mimi Bukoba nimekwenda na hili jambo analozungumza Mheshimiwa Mbunge ninalifahamu. Nilikwenda kule kwa sababu ya boti ambalo lilileta maneno na yeye ndiye alileta jambo hili hapa, tukaenda nalo kama tulivyokwenda na wala sitaki nimpuuze Mbunge hapa kwa jambo analozungumza. Ametaka tusaidie Halmashauri ya Manispaa ya Bukoba ili iondoke katika tatizo hili na ninamwomba Mbunge anisikilize vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo limekuwa *mis-handled* miaka kumi iliyopita, hata ukiwatafuta hawa waliohusika wengine hawapo, Halmashauri ikafika mahali ikaachana na hilo eneo moja kwa moja, wakafika mahali wakapata viwanja elfu tano ili kweza kupima hivyo viwanja elfu tano wakaomba mkopo kutoka *UTT* wa bilioni mbili na *point* tisa (bil. 2.9) wakapata. Wamekwenda kupima viwanja elfu tano. Anachozungumza hapa anasema miaka kumi iliyopita mtu alilipa shilingi elfu hamsini na mimi nikasema ni kweli, sasa elfu hamsini iliyolipwa tukaulizana kwamba shilingi elfu hamsini kwa leo ni sawa na shilingi ngapi ili anapokwenda kuchukua kile kiwanja apate punguzo la kiasi hicho ili aweze kupata kiwanja.

Mheshimiwa Conchesta, dada yangu anasema kwamba twende tukawape wananchi wale viwanja vile bure, swali tunawapa bure na huu mkopo uliochukuliwa unakwenda kulipwa na nani? Wamekutana juzi tarehe 16 tumetoa maelekezo kama Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa tukawaambia wakae watuondoe hapo tuliposema. *It is my judgment* kama *Deputy Minister* ninayefanya kazi katika Ofisi ya Waziri Mkuu kwamba kama mkikataa jambo hili hamtaondoka katika mgogoro ule itakuwa ni vurugu, namna pekee ya kuondoka katika jambo lile ni kukubali sasa wananchi wale waseme kwamba mimi kama sitaki kiwanja bei itakuwa ni kubwa nirudishieni hela zangu kwa thamani ya sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sauti hii ni msisitizo tu mzee wangu wala siyo ugomvi hapa. Lakini mimi nataka niisaidie Serikali nimezungumza na Kagasheki Mbunge wao, nimezungumza mimi na Mkurugenzi Mtendaji, nimezungumza na baadhi ya wale waliopo kule na wote wanaona kwamba hii ndiyo njia pekee ambayo itatuondoa katika jambo hili. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Naibu Spika, ninakuomba Conchesta Dada yangu toa msaada shirikiana na Halmashauri yako nenda sasa ukazungumze na wananchi wapewe viwanja vile wavichukue, hakuna namna nyingine ya kisayansi ya kuondoka katika tatizo hili bila kufanya kama nilivyosema. (*Makofi*).

**MHE. OMARY A. BADWEL:** Mheshimiwa Naibu Spika nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa miji mipya imeendelea kukumbwa na migogoro ya viwanja ikiwemo Mji wa Bahi na wananchi wa Bahi tayari walishamwandikia barua Waziri Mkuu kutaka awasaidie kutatua mgogoro uliopo baina yao na Halmashauri yao juu ya viwanja pale Mji wa Bahi.

Je, ofisi ya Waziri Mkuu sasa inatoa tamko gani kusaidia mara moja Halmashauri ya Bahi imalize mgogoro wa viwanja wao na wananchi wa Bahi?

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MIITAA (TAMISEMI):** Mheshimiwa Naibu Spika, bahati nzuri tena Bahi nimekwenda na nimekaa na wananchi na hao wananchi wamekuja mpaka ofisini. Mheshimiwa Badwel alikuwa kabla ya kuja hapa alikuwa ni Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Bahi. Wameshindana kule wakaja ofisini, tukaketi nao. Wale wananchi wakaja pale nikawaambia maandamano hapa sitaki, lakini tukaelewana.

Nikawapa mimi watu wangu wamekwenda nao kule wameshindana mimi kiwanja changu kilikuwa hiki, mimi nilitaka nipewe hiki, eneo nililokuwa nakaa ni hili nilitaka nipewe hili, tukafika mahali mpaka nikamwambia Mkurugenzi kwamba jambo hili liishe.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilishasema hapa Serikali haitapuuza mawazo ya Wabunge, kama Mheshimiwa Badwel anasema bado tatizo hili lipo saa saba nitakaporudi ofisini kwa kibali cha Waziri wangu Mheshimiwa Mkuchika nitawaita Halmashauri waje tena pale ofisini, na Mheshimiwa Badwel saa saba kamili tukutane pale ofisini halafu tumalize jambo hili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, bado tupo Wizara hiyo hiyo tunaelekea Singida swali la Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji.

Na. 83

**Ukarabati wa Majengo ya Sekondari ya Mwenge**

**MHE. DIANA M. CHILOLO (K.n.y. MHE. MOHAMED G. DEWJI)** aliuliza:-

Shule ya Sekondari ya Mwenge ni miongoni mwa shule kongwe hapa nchini na sasa majengo yake yamechakaa sana.

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati majengo ya shule hiyo na kujenga uzio wake?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU-ELIMU** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri Mkuu naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mohamed Gulam Dewji, Mbunge wa Singida Mjini, kwanza kwa kutoa maelezo mafupi kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa nchini kuna shule za sekondari kongwe 90 ambazo baadhi zilijengwa enzi za ukoloni na nyingine baada ya kupata uhuru. Miongoni mwetu tumesoma katika shule hizo zikiwa katika hali nzuri lakini kadiri miaka ilivyopita miundombinu ya shule hizi imechakaa kama ilivyo katika shule ya Sekondari ya Mwenge iliyopo Mkoani Singida.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo naomba sasa kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa kutambua hali ya uchakavu wa majengo katika shule zote kongwe nchini imeweka mkakati wa kuzikarabati kwa awamu ili kuzifanya shule hizi ziwe na mazingira bora ya kujifunzia na kufundishia.

Katika kutekeleza azma hii, mwaka 2009/2010 Serikali ilipeleka katika mamlaka za Serikali za Mitaa jumla ya shilingi bilioni 2.1 ambazo ziligawiwa katika shule za sekondari ya Serikali 41 kwa ajili ya kuzifanyia ukarabati wa majengo yote ya shule na kujenga uzio kadri ya vipaumbele vya shule yenyewe au Halmashauri yenyewe.

Kwa mwaka 2010/2011, Serikali ilitoa fedha tena jumla ya shilingi 2.5 ambazo ziligawiwa katika shule za sekondari 50. Shule ya Serikali Mwenge ilipatiwa shilingi milioni 50 kwa mwaka wa fedha 2009/2010. Kama nilivyosema awali aina ya ukarabati na ujenzi hutegemea zaidi vipaumbele vya shule yenyewe au Halmashauri husika, katika shule ya sekondari Mwenge fedha hizi zilifanya kazi zifuatazo.

- Ukarabati na ujenzi wa vyoo vya wanafunzi.
- Ukarabati wa ujenzi wa jiko jipya.
- Ukarabati wa nyumba nne za walimu.

- Ukarabati wa mfumo wa maji taka na maji safi katika maabara na jiko.

- Kuweka mfumo wa umeme katika vyumba vya madarasa na vyoo.

- Ukarabati wa samani za shule ikiwemo vitanda, madawati na viti.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa kufanya ufuatiliaji wa hali ya miundombinu katika shule zetu nchini. Naomba kupitia Bunge hili nimthibitishie kuwa Serikali inayo dhamira ya dhati kuhakikisha shule zote chakavu zinafanyiwa ukarabati na kurejeshwa katika hali nzuri.

Kazi hii ni kubwa na inahitaji kiasi kikubwa cha fedha, Kwa mfano makadirio ya kukamilisha ukarabati wa shule ya sekondari Mwenge, ni shilingi bilioni moja zikiwemo shilingi milioni 580 kama gharama za kujenga uzio wa shule nzima. Hivyo Serikali itaendelea kutenga fedha na kufanya ukarabati kwa awamu kadri fedha zinavyopatikana. Aidha, Serikali inaendelea kushawishi wahisani na mashirika yasiyo ya kiserikali katika upatikanaji wa fedha ili kuongeza uwezo wa serikali katika kumudu jukumu hili.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Naibu Waziri nina maswali mawili madogo ya nyongeza.

Swali la kwanza, kwa kuwa shule hii ya Mwenge ya Sekondari ya kidato cha tano na cha sita upungufu wa madawati ni mkubwa mno na upungu huo umetokana na wizi kwa sababu madawati hayo yanahamishika, Je Serikali itakuwa tayari sasa kutenga hela za kutosha kutengeneza madawati yasiyohamishika kama ya Vyuo Vikuu ili kuondokana na wizi?

Swali la pili, kwa kuwa suala la uzio ni muhimu mno. Je Serikali itakuwa tayari kutenga fedha hizi alizozitaja Naibu Waziri kidharura ili uzio uweze kujengwa kuondokana na wizi mkubwa uliokithiri katika shule hii ambao unapoteza mali nyingi za shule?

**NAIBU WAZIRI OFISI YA WAZIRI MKUU-ELIMU:** Mheshimiwa Naibu Spika, suala la utengenezaji wa madawati na kumaliza tatizo hili nchini, Serikali kwa maana ya Ofisi ya Waziri Mkuu imeshatoa mpango thabiti wa kumaliza tatizo la madawati nchini.

Kama ambavyo Waziri wa nchi alieleza na kutoa msimamo wa Serikali kwamba sasa tumeazimia kumaliza tatizo hili. Mkakati huo upo lakini suala la kutengeneza madawati yasiyohamishika ni utaratibu tu ambao unaweza kufikiwa na Halmashauri yenyewe kadiri tatizo linavyokabiliwa kwenye eneo lile.

Mheshimiwa Spika, kama wameshaona ufumbuzi wa kutatua tatizo hili ni kutengeneza madawati yasiyohamishika ni mpango ambao tutajiwekea kwenye Halmashauri yenyewe na shule yenyewe kadiri mazingira yalivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni nyongeza na zile fedha za *BSA* ambazo Serikali za Mitaa zimetengewa bilioni mia moja themanini na nne pointi nne kwa ajili ya kutengeneza madawati nchini. Huo ndiyo mkakati wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la kutenga fedha kwa ajili ya uzio ambao unapelekea mali nyingi kuhamishwa shuleni kwa maana ya wizi kama ambavyo nimeeleza kwenye swali langu la msingi kwamba Serikali inaendelea kutoa fedha kadiri ambavyo zinapatikana Serikalini ili kuwezesha kuzipelekea shule hizi kama fedha za nyongeza na shule sasa inayo uwezo wa kuupa kipaumbele ujenzi wa wigo kama ambavyo

nimeeleza kwa Singida bado inahitaji bilioni moja ili kuweza kutengeneza, kukamilisha pia na eneo la wigo.

Kwa hiyo, fedha itakavyotumwa sasa Mwenge Sekondari au Halmashauri ya Manispaa inaweza kuipa kipaumbele kutengeneza wigo. *(Makofi)*

Na. 84

**Wilaya ya Makete Kukosa Miradi ya Wakala wa Umeme Vijijini**

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE** aliuliza:-

Mojawapo ya majukumu ya Serikali ni kuhakikisha kwamba rasilimali chache za kitaifa zinagawanywa kwa uwiano na kuhakikisha kwamba kila Wilaya inapewa miradi ya maendeleo kwa kuzingatia vipaumbele vya uchumi na mahitaji ya sehemu husika katika kipindi cha miaka mitano iliyopita. Wilaya ya Makete, haikuweza kupata mradi hata mmoja wa Wakala wa umeme Vijijni *(REA).*

(a) Je, Serikali inasema nini kuhusu Wilaya kukosa miradi ya wakala wa umeme vijijini?

(b) Je, Serikali itakuwa tayari kuingiza katika ratiba ya usambazaji umeme vijiji kata za Ikuo, Kitulo, Iniho na Ipelele?

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Binilith Satano Mahenge, Mbunge wa Makete lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, kuna namna mbalimbali ambazo wakala wa Nishati vijijini *(REA)* inavyojishughulisha na kuboresha upatikanaji wa nishati na huduma za nishati ikiwemo huduma ya umeme ikiwa ni pamoja kati ya kazi zake. Wakala

wa nishati vijiji *(REA)* katika mwaka wa fedha 2009/2010 iliandaa mafunzo ya ujengaji uwezo kwa mafundi wanaohusika na uendeshaji wa vyanzo vya ufuaji umeme utokanao na maporomoko ya maji.

Mojawapo ya mafundi walioshirikishwa katika mafunzo hayo yaliyofanyika Mjini Njombe na mafundi hao walitoka Hospitali ya Bulongwa iliyopo Wilayani Makete.

Pia wakala kwa sasa unashirikiana na Uongozi wa Kanisa la KKKT, Diakonia ya Tandala Wilayani Makete, katika kuendeleza chanzo cha Mto Ijangala ambacho kinategemewa kufua umeme wenye uwezo wa karibu MW 3 kitakapokamilika. Hivyo kulingana na uwezo wa kifedha Serikali inagawanya rasilimali zake sawa kwa wananchi wake katika kusambaza umeme vijijini kadiri inavyokuwa inawezekana ikiwemo na Wilaya ya Makete.

(b) Mheshimiwa Spika, miradi ya kusambaza umeme kwenye kata zilizotajwa na Mheshimiwa Mbunge imeshafanyiwa tathimini na *TANESCO* Wilayani Makete. Makadirio ya gharama za utekelezaji wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

(i)Gharama ya usambazaji umeme katika kata ya Ikuo ni shilingi milioni 95.

(ii) Katika Kata ya Kitulo, *TANESCO* katika mwaka wa fedha 2011 ilitenga jumla ya shilingi 7,356,679 ili kukamilisha mradi wa kata hiyo. Kazi ya usambazaji umeme imeashanza nguzo zimeshasimikwa. Kazi zilizobaki ni kuvuta nyaya na kuweka *transforma.*

(iii) Ili maeneo ya Kata za Iniho na Ipelele yapate huduma ya umeme inahitajika ujenzi wa laini ya msongo wa 33 kV yenye urefu kama kilomita 40 kuanzia eneo la Kitulo. Mradi huo utagharamu kama shilingi bilioni 1.430.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 9 Novemba, 2011 wakati nikijibu swali la Mheshimiwa Dkt. Mahenge hapa Bungeni nilifafanua kuhusu mikakati mbalimbali ya kuboresha upatikanaji wa huduma ya umeme Makete.

Nilieleza kuwa sehemu za Nduramo, Kisinga, Magu, Lupalilo, Ikonda Hospitali na Tandala, Matamba zinatarajia kufikishiwa umeme kupitia mradi wa *MCC* unaofadhiliwa na Serikali ya Marekani. Maeneo mengine ambayo miradi yake haimo katika ile itakayotekelezwa na *MCC* itaingizwa kwenye orodha ya miradi ya Turnkey awamu ya pili inayotegemewa kutekelezwa kwenye mwaka wa fedha huu unaofuata 2012/2013 kutegemea upatikanaji wa fedha za kuanzisha miradi mipya.

**MHE. DKT. BINILITH S. MAHENGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimshukuru sana Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri na ya kipekee niwapongeza *REA* kwa kazi nzuri wanayofanya. *(Makofi)*

(a)Ni lini Serikali kupitia Wizara hii italeta mpango mkakati unaoonyesha uwazi namna ya usambazaji umeme vijijini katika nchi nzima utakaogusa kila Wilaya na kila kijiji?

(b)Kwa kuwa kutoa umeme kutoka Kitulo kwenye Kata za Ipelele na Iniho ni hela nyingi bilioni 1,400,000,000 na kwa kuwa hizo Kata za Iniho na Ipelele zina mito na maporomoko madogo na makubwa Mheshimiwa Waziri atakuwa tayari kuwaagiza *REA* wafanye utafiti na ulinganisho ili kubaini kwamba pengine uzalishaji umeme wa maji ungekuwa nafuu na kwa kuzingatia kwamba umeme unaweza ukawa mwingi na ukaingizwa kwenye *grid? (Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI NA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali ya nyongeza ya Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka jana wakati wa bajeti tulifanya tathimini ya jumla ya nini kinachohitajika kupatikana REA ili tuweze kuwa na utekelezaji mpana sana wa miradi hasa hii ya vijijini na hii miradi midogo midogo kwa ajili ya kufikisha umeme, kuongeza upatikanaji wa umeme kwa Watanzania ambao kwa sasa hivi ni kama asilimia 14, asilimia 15 *at least* katika miaka mitano inayokuja tufike kwenye asilimia 30. Mahitaji yake ni kama bilioni 400 mpaka bilioni 500.

Kwa hiyo, kama mnavyofahamu nchi yetu ni kubwa na kwa hiyo mzigo wa kazi hiyo ni kubwa nayo. Nakubaliana na Mheshimiwa Dkt. Binilith Mahenge kwamba kuna umuhimu wa kutengeneza huo mpango mkakati ambao kwanza utafafanua malengo tuliyojiwekea ni kumaliza ile miradi ambayo imeshatekelezwa kwa sababu tusipomaliza ile tukaanzisha miradi mipya tutakuwa tunabebesha tu mizigo ambayo tunakuwa sasa tuna miradi mingi ambayo yote haijakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, sasa hivi mkakati ni kukamilisha kwanza ile miradi ambayo tunamaliza. Nikubaliane na Mheshimiwa Daktari Binilith Mahenge kwanza tutaleta ratiba ya ukamilishaji wa miradi inayoendelea sasa hivi halafu tulete utekelezaji wa miradi hiyo mipya kulingana na huo upatikanaji wa fedha tukizingatia kwamba haziwezi zikapatikana bilioni 400 kwa mwaka mmoja wa fedha na wala haziwezi kutumika kwa mwaka mmoja wa fedha. Kwa hiyo, nikubali kwa yote mawili kwanza tulete ukamilishaji wa ratiba ya miradi inayoendelea halafu tulete utekelezaji wa miradi mipya kama alivyopendekeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili la pili la Iniho na Ipelele kuangalia tathimini ya vyanzo vya maji pale hiyo ndio kazi ya REA inafanywa, sasa tuna miradi mingine iko Mbozi kule kwa Mheshimiwa Silinde kuna mingine inaendelea kwa Mheshimiwa Malocha tumekwenda kuiangalia juzi na kuna mingine inaendelea Makete.

Kwa hiyo, ikiwa huu ni utaratibu mzuri wa kumaliza matatizo haya kwa maeneo ambayo hayana *grid* nikubaliane tu na Mheshimiwa Mbunge kwamba tuiongezee *REA* majukumu ya kwenda kuangalia vyanzo vya maji na kuangalia zaidi ya hii MW 3 ambayo imeshafanyiwa tathimini haya maeneo mengine haya maeneo mengine kama yanaweza nayo yakaleta *mini hydro solution*.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, niwakumbushe tu yale ambayo Mheshimiwa Spika, anaeleza mara kwa mara kuhusiana na maswali mafupi na majibu mafupi tusaidiane katika kuendesha kikao kwa sababu hata ninyi mkiwa mashahidi mkitazama saa yetu ni nusu saa imepita na maswali ambayo tumesha-*cover* ni matatu tu.

Kwa hiyo, ni kwamba tunatumia dakika 10 kwa swali moja. Kwa hiyo, naomba sana kila anayepata nafasi aitumie kwa kifupi kusudi isaidie katika kutoa maswali ya nyongeza kwa wengine. Vinginevyo mtakuwa mnalaumu meza kwamba hatuwapi fursa kumbe haiwezekani.

Na. 85

**Biashara ya Binadamu**

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR** aliuliza:-

Katika ulimwengu huu wa sasa bado kuna wimbi kubwa la biashara ya binafsi jambo ambalo ni kinyume na haki za binafsi:-

Je, Tanzania inaguswa vipi na tatizo la biashara hiyo haramu?

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya ndani ya nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Faida Mohamed Bakar,  Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Tanzania ni sehemu ya dunia, kwa sababu ya utandawazi na wepesi wa njia za mawasiliano hatuwezi kuacha kuguswa kwa njia moja au nyingine kwa matokeo mbalimbali yanayotokea duniani. Tatizo la biashara ya binadamu tunalo hapa nchini lakini siyo kubwa tukilinganisha na mataifa mengine duniani.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka  2008 Bunge lako Tukufu lilipitisha sheria ya ukomeshaji wa biashara ya binadamu *The Anti – Trafficking in Persons Act, 2008* yenye lengo kuu la kuzuia na kuondosha tatizo hili katika mipaka ya nchi yetu. Sheria hii inaweka utaratibu wa kuzuia biashara hii haramu, utaratibu wa uchunguzi na wa Kimahakama lakini pia utaratibu wa kuwaokoa na kuwasaidia watu ambao wanakumbwa na janga hili.

Aidha kwa kipindi cha kati 2007 – 2011 kulikuwepo na jumla ya kesi 8 za biashara haramu ya binadamu ambapo watu 48 wakiwemo Wasomali 14 Mkenya 1 na Watanzania 33 waliathirika na biashara hiyo ya binadamu ama kwa kuingizwa nchini au kusafirishwa nje ya nchi. Watuhumiwa 10 waliohusika na matukio hayo walikamatwa na baadhi yao kufikishwa mahakamani.

**MHE. FAIDA MOHAMED BAKAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipatia nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa sambamba na biashara ya binadamu lakini hivi sasa hapa nchini kwetu kumijitokeza wimbi kubwa la mauaji ya watu wenye ulemavu wa ngozi Albino ama kuwakata viungo vyao wakiwa hai kitu

ambacho ni ukiukwaji wa haki za binadamu, maana yake wanakata viungo halafu wanakwenda kuviuza kwa mambo yao mbalimbali. Je, Serikali ina mkakati gani wa kukomesha unyama huu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Faida Bakar, kama ifuatavyo:-

Kuhusu mauaji ya ndugu zetu walemavu wa ngozi Albino kweli wimbi hili lilikuwepo lakini kwa hatua ambazo Serikali imechukua kumekuwa na upungufu mkubwa kwa maana ya kusema kwamba tumedhibiti hali hii na tutaendelea kuidhibiti na mikakati ambayo tuliyonayo tunaona kwa kweli inafanya kazi lakini jitihada bado zitaendelea kuwepo na tutapenda sana pawepo na ushirikishwaji mkubwa wa wananchi ambao utaweza kufichua watu ambao wanaendeleza vitenda kama hivi. Isipokuwa naomba nimwambie Mheshimiwa Mbunge na Bunge lako Tukufu kwamba ni zile imani potofu, imani za ushirikina ambazo zinatupelekea mpaka hapo. Kwa hiyo, ipo haja ya kuweka elimu ya kutosha kwa wananchi wetu na kusema kwamba vitendo kama hivi havifai wala siyo vitendo vya maendeleo lakini vitendo ambavyo vinaliwekea taifa letu doa ambalo si jema katika mataifa ya dunia.

**MHE. JOSEPH ROMAN SELASINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Tatizo la biashara hii ya binadamu lipo kwa sababu katika mipaka yetu tunasikia baadhi ya Wasomali, watu kutoka Ethipia na kadhalika wanavuka. Sasa Serikali ituambie ni hatua gani za makusudi ambazo zinachukuliwa kukabiliana na tatizo hili ambalo linaweza likahatarisha usalama wa nchi yetu? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge Joseph Selasini, kama ifuatavyo:-

Hapo yapo mambo mawili kuna suala ambalo linahusu biashara ya binadamu lakini kuna suala ambalo linahusu uhamiaji haramu. Katika mipaka yetu utakuta tatizo kubwa tulilokuwa nalo ni tatizo la uhamiaji haramu ambalo wako Waethiopia, Wasomali, wako watu kutoka mataifa mbalimbali. Mpaka sasa hivi tunapata watu kutoka Bangladesh, kutoka Pakistan. Lakini ni tatizo tofauti ambalo kwa kweli tunafanya kila jitihada kuhusu mipaka yetu ilivyokuwa mikubwa. Lakini pia utekelezaji ule ambao kwa kweli unadhoofishwa kwa sababu ya vitendea kazi ambavyo kwa kweli havitoshelezi.

Kwa hiyo, upande wa biashara haramu mimi siwezi kusema kwamba uuzaji wa biashara ya binadamu ni tatizo lakini siyo kubwa zaidi kama lile tatizo la uhamiaji haramu. Lakini hata hivyo yote ni matatizo na tunafanya kila jitihada kutumia vyombo vyetu hususan vyombo vya polisi na vyombo vya uhamiaji kuhakikisha kwamba tunakabiliana na tatizo hili hasa tunapokuja katika suala la usalama wa nchi yetu. Lakini kikubwa zaidi nafikiri itabidi tutazame hata katika Bajeti yetu kupata vitendea kazi ili vijana wetu waweze kudhibiti hali hizi. (*Makofi*)

Na. 86

**Ahadi ya Minara ya Simu Jimbo la Chilonwa**

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE** aliuliza:-

Ni muda mrefu umepita tokea utafiti wa kuweka minara ya simu za mikononi ufanyike katika kata mbalimbali za Jimbo la Chilonwa.

Je, ni lini Serikali itawapelekea mawasiliano ya simu za mkononi wananchi wa vijiji vya Kata za Membe, Dabalo na Zajilwa ambao tayari walikwishaahidiwa kuwekewa minara ya simu za mkononi kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mbunge wa Chilonwa, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kampuni mbalimbali za simu za mkononi zimekuwa zikifanya tafiti katika maeneo mbalimbali nchini yakiwemo ya Kata za Jimbo la Chilonwa, ili kufikisha huduma za mawasiliano na zimekuwa zikijitahidi kufikisha mawasiliano kulingana na mipango yao ya biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kuhakikisha kuwa nchi nzima inakuwa na mawasiliano yenye uhakika, Serikali imeanzisha Mfuko wa Mawasiliano kwa wote wenye lengo la kufikisha huduma za mawasiliano hususan katika maeneo ambayo hayana mvuto kibiashara.

Sanjari na hilo Mfuko wa Mawasiliano kwa wote (*UCAF*) tayari umeshayaingiza maeneo ya Kata za Membe, Dabalo na Zajiliwa kwenye orodha ya maeneo yanayofanyiwa tathimini ili kuwekewa mawasiliano chini ya mpango wa miradi itakayofadhiliwa na Mfuko huo kwa kushirikiana na watoa huduma binafsi. Serikali inaamini kuwa kupitia juhudi hizi huduma za mawasiliano zitawafikia wananchi wa vijiji vya kata za Membe, Dabalo na Zajilwa.

**MHE. HEZEKIAH N. CHIBULUNJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, ninaomba niulize maswali mawili ya nyongeza.

(a) Pamoja na maeneo haya niliyoyataja ya Membe, Dabalo na Zajiliwa ambayo yalishaainishwa kusema kweli na kuahidiwa kwa muda mrefu.

Lakini pia yako maeneo mengine katika ukanda huo wa uzalishaji wa mazao ya chakula na biashara yaliyoko katika Tarafa ya Itiso ikiwemo Segala, Izava na Kimeji ambayo kwa bahati nzuri yana mtandao mzuri wa barabara. Waziri anawaahidi nini wananchi wa maeneo hayo?

(b) Ili kuondoa ile shauku ya kusubiri muda mrefu kwa maeneo ambayo yaliahidiwa kuwekewa minara ya Serikali itakubaliana na mimi kwamba iko haja sasa ya kuweka ratiba ya utekelezaji wa uwekaji wa minara nchi nzima ili kuondoa shauku hiyo ya kusubiri kwa muda mrefu?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Chibulunje, kama ifuatavyo:-

Maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Chibulunje ni pamoja na yale niliyoyasoma katika jibu langu la msingi yako katika mpango wa *UCAF* kama ambavyo niliwaleta watalaam wiki iliyopita Jumamosi kuweza kuelezea.

Kuhusu Serikali kuweka mpango nakubaliana naye kabisa ndio sababu tumewaomba Wabunge wote waweze kuleta vijiji vyao mpaka sasa hivi tumeshapokea vijiji 2175 ambavyo vinaonyesha kwamba havina mawasiliano. Hii inatuongezea takwimu katika takwimu zetu tulizonazo na kwa kutumia takwimu hizi tutapanga mpango mkakati kabisa na tutasambaza kwa Wabunge kuonyesha wapi tunaanza na wapi tunamalizia ili kila mmoja aweze kuona mpango huo kama ambavyo Mheshimiwa Mbunge ameshauri.

**MHE. JUMA S. NKAMIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kuniona nilitaka niulize swali dogo tu kwamba tayari kampuni ya *Airtel* ilishafanya tathimini na kubaini maeneo ya kujenga minara katika vijiji vya Jangalo, Itolwa,

Tandala, Makorongo na Ovada. Lakini hadi leo wananchi wa maeneo yale wanasubiri minara hii itajengwa lini.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba Mheshimiwa Naibu Waziri awahakikishie wananchi hawa ni lini minara hii itaanza kujengwa?

**NAIBU SPIKA:** Ni lini Minara hii itajengwa Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia.

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Juma Nkamia, kama ifuatavyo:-

Ni kweli maeneo aliyoyataja Mheshimiwa Juma Nkamia na nimpongeze sana kwa kufuatilia sana huduma za mawasiliano katika jimbo lake. Kama tunavyofahamu makampuni mengi ya simu mwaka wake wa fedha unaanza tarehe 1 mwezi wa 4 na sasa hivi Bajeti yao wameanza ku-*implement* katika mwaka wao wa 2012/2013 niwaombe tu wananchi wa maeneo hayo na nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba mipango inaendelea na kuna taratibu ndefu zinazohusika katika kuhakikisha kwamba mnara unajengwa, mara taratibu hizo zitakapokamilika ambapo si muda mrefu minara itajengwa katika eneo hilo kwa sababu tayari iko kwenye mipango ya kampuni ya *Airtel*. *(Makofi)*

Na. 87

**Kamisheni ya Sayansi na Teknolojia**

**MHE. ASHA MOHAMED OMARI** aliuliza**:-**

Kamisheni ya Sayansi na Tekinolojia ni chombo cha Muunganbo:-

Je, taasisi hiyo ina mpango gani wa kufungua ofisi yake Tanzania, Zanzibar ili kutoa taswira halisi ya kuwa ni chombo cha kimuungano?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKINONOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, sayansi na Tekinolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Asha Mohamed Omar, Mbunge wa Viti Maalum, kama itakavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli Tume ya Sayansi na Tekinolojia ni chombo cha Muungano na imekuwa ikifanya kazi zake katika sehemu zote mbili za Muungano. Wizara ya Mawasiliano, Sayansi na Tekinolojia imekuwa ikifanya juhudi kubwa ili Tume hii ifungue ofisi Zanzibar. Juhudi hizo ni pamoja na kufanya mawasiliano ya moja kwa moja na Serikali ya Mapinduzi-Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu na Mheshimiwa Mbunge kwamba kufuatia juhudi kubwa zilizofanywa na Wizara yangu, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kupitia Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, imeipatia Tume ya Sayansi na Tekinolojia vyumba vitatu kwa ajili ya kufungua ofisi katika jengo la Ofisi ya Makamu wa Rais wa Jamuhuri ya Muungano iliyoko Tunguu.

Tayari Mkurugenzi Mkuu wa *COSTECH* amekwishatembelea sehemu ambazo *COSTECH* imepewa kwa ajili ya kufungua ofisi. Aidha, Mratibu wa shughuli za *COSTECH* katika ofisi inayotarajiwa kufunguliwa amekwishapatikana. Mchakato wa kununua na kuweka vifaa muhimu katika Ofisi hiyo unaendelea na ni matarajio yetu kuwa ofisi hiyo itafunguliwa mwezi Mei, 2012.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nichukue nafasi hii kuishukuru Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar kwa kulipa suala la kuipatia ofisi *COSTECH* umuhimu mkubwa na kuweza kutoa vyumba vitatu vya ofisi kwa ajili ya Tume ya Sayansi na Teknolojia kwa kipindi cha miaka miwili hadi Disemba, 2013.

Aidha, azma ya Serikali ni kujenga jengo la ofisi kwa ajili ya Tume huko Zanzibar ili kuimarisha uratibu wa shughuli za utafiti na maendeleo na pia maendeleo katika Sayansi na Teknolojia kwa ujumla wake.

**MHE. ASHA M. OMAR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri katika swali lake mama, bado swali langu liko pale pale. Je, jengo hilo litajengwa lini?

**NAIBU WAZIRI WA MAWASILIANO, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mawasiliano, Sayansi na Teknolojia naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Utaratibu wa Serikali ni kuweka Bajeti, tukishaweka Bajeti baada ya kuwa tumepanga ndiyo tunaanza kujenga. Nimwombe tu Mheshimiwa Mbunge awe na subira, pale ambapo Bajeti yetu itaruhusu na tutakuwa tumepata sehemu ya kuweza kujenga jengo hilo kazi hiyo itaanza mara moja.

Na. 88

**Kuboresha zao la Minazi - Lindi**

**MHE. SALUM K. BARWANY** aliuliza:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuboresha zao la minazi Mkoani Lindi kama yalivyo mazao mengine kama Pamba, Korosho, Kahawa nakadhalika?

(b) Je, Serikali ina mpango gani kwa kupambana na magonjwa yanayosababisha Minaz kukauka?

(c) Je, ni tafiti gani umefanyika kwa kujua chanzo cha ugonjwa huo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salum Khalfan Barwany, Mbunge wa Lindi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilianza kufanya utafiti wa uendelezaji wa zao la minazi kupitia mpango wa Taifa wa kuendeleza Minazi (*National Coconut Development Programme (NCDP)* mpango ambao ulitekelezwa kwa gharama ya Tsh. 8,904,775,000/= kati ya 1979/1980 na 2003/2004 kwa lengo la kufufua zao hilo. Katika juhudi za kuendeleza utafiti wa nazi, mwaka 1996 Serikali iliamua kuanzisha kituo cha utafiti wa kilimo cha minazi cha Mikocheni ambacho ndicho kina jukumu la kuendeleza utafiti wa zao la nazi?

Utafiti wa muda mrefu unaonesha kwamba mbegu asilia yaani minazi mirefu itaendelea kutumika kutokana na kustahimili ukame na magonjwa. Halmashauri za Wilaya za Mtwara na Lindi zinashauriwa kuweka mipango ya kuvisaidia vikundi vya wakulima kupata mbegu hizo bora za minazi kutoka Songosongo huko Lindi, Vuo, Mwabani na kituo cha utafitio wa mifugo *(LBS)* huko Tanga. Aidha, kituo cha utafiti cha Mikocheni kimevipatia vikundi viwili katika Vijiji vya Ng'apa Lindi na Rwelu Mtwara mashine za kusindika mafuta ya mwali. Juhudi hizi za Serikali zitaendelea ili kuwasaidia wakulima wa nazi kusindika zao hilo kujipatia mafuta na bidhaa nyingine zinazotokana na nazi.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, ugonjwa unaoathiri minazi na kusababisha mnyauko au kunyong'onyea kwa minazi unaitwa "*Coconut Litho Disease*". Hadi sasa tiba ya ugonjwa huu unaosababishwa na virusi bado haijapatikana na utafiti unaendelea. Wakulima wanashauriwa kuendelea kutumia mbinu za kupambana na mnyauko wa minazi kwa kukata na kuchoma moto minazi iliyoathirika na kupanda miche inayotoka katika vituo vya utafiti ili kuepuka kuenea kwa ugonjwa huo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, utafiti wa zao la minazi unaendelea sambamba na utafiti wa usindikaji ili kuongeza thamani ya zao la nazi.

**MHE. SALUM K. BARWANY:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu amabyo yanawakatisha tamaa wakulima wa zao hili la minazi katika Mikoa ya Pwani.

(a)Inaonyesha dhahiri kabisa kwamba tiba ya minazi haijapatikana takribani miaka ishirini leo. Je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi katika kulinusuru zao hili ambalo zaidi ya asilimia 50 ya wakazi hao wanalitumia kwa ajili ya maisha yao?

(b)Zaidi ya asilimia 50 pia ya wakazi wa Mikoa ya Pwani hususani Lindi hutegemea zao hili la minazi, vikundi viwili vya Rwelu na Ng'apa ambavyo vinasemwa kwamba Serikali imetoa msaada kwa kuwapa mashine,Serikali haioni kwamba ni mzaha kwa wakulima hao katika kipindi cha miaka ishirini ya utafiti wao kuona kwamba inaweza kuwafanya wakulima hawa wa minazi kupata tija tukizingatia kwamba minazi ina faida kubwa magogo kwa ajili ya mbao na vitu vingine ambavyo vinapatikana kutoka kwenye minazi hiyo. Je, Serikali ina mkakati gani sasa wa makusudi katika kuwaendeleza wakulima wa minazi, zaidi ya mashine hizo mbili ambazo wamepatiwa wananchi katika Vijiji viwili hivyo?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Khalfan yote kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Kwanza nikubali kwamba kweli zao la nazi kama anavyodai Mheshimiwa Mbunge halijashughulikiwa ipasavyo kama mazao mengine, hata mimi naliona hilo. Lakini nataka niseme kuhusu tiba hii, mimi nimesema kwamba utafiti unaendelea. Utafiti ni suala endelevu na utafiti wa minazi wataalamu wanasema walichukua mpaka hata miaka 25. Kwa hiyo, ni kitu ambacho ni endelevu hata tiba ikipatikana magonjwa mengine tena yatapatikana kwa hiyo utafiti hautasimama ni suala ambalo litaendelea.

Naomba tu nimhakikishie Mheshimiwa kwamba kituo hiki kimewekwa mahususi cha Mikocheni ni kwa ajili ya kuhakikisha kwamba tunaendelea kushirikiana na wenzetu ambao wanaathiriwa na ugonjwa huu. Ugonjwa huu uko katika nchi nyingi, uko katika nchi za Caribbean, uko katika nchi zingine za Afrika na nchi zingine ambazo zinalima minazi. Kwa hiyo, hili tunaendelea nalo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nikija kwenye suala la kuwasaidia wakulima, naomba niseme kwamba kweli vikundi viwili ni vichache, lakini Mheshimiwa Mbunge basi kama nilivyosema tushirikiane na Halmashauri zetu, tuweke mipango hii ya kuendeleza zao la minazi katika mipango ya maendeleo ya kilimo, Halmashauri nazo zishirikiane na sisi na sisi wenyewe wote sio tu Serikali Kuu,Wizara ya Kilimo kuja kupanga hapana, tuanzie kwenye Halmashauri, tuweke mipango kama nilivyosema halafu tuanze kuipatia fedha ya kutekeleza maendeleo ya zao la minazi pamoja na usindikaji wa zao lenyewe.

**MHE. MODESTUS D. KILUFI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Napenda kumwuliza Mheshimiwa Waziri kwamba mfereji wa Mwendamtitu ni sehemu ya ahadi ya Serikali kwa Kata za Rujewa, Ubaruku, Songwe Mariro na Mapogoro na kazi ile ya kuchimba ule mfereji imeshaanza lakini Serikali bado haijapeleka fedha. Nataka kujua ni lini Serikali itapeleka fedha kwa ajili ya kusaidia kazi hiyo muhimu?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika mfereji wa Mwendamititu na minazi ni vitu viwili tofauti, lakini nalifahamu suala lake analolizungumzia,Serikali imekwishatenga shilingi milioni 500 kwa ajili ya mfereji huu na nilipokwenda kule niliwaahidi wakulima wale na fedha hizi zimekwishatengwa na zitatolewa kwa ajili ya maendeleo hayo na nashukuru kwamba tayari tumeshaanza na juhudi za kuchimba mfereji ule. Kinachotakiwa sasa ni kuendelea kuchangia mafuta katika uchimbaji na Mheshimiwa Mbunge nikuhakikishie kabisa kwamba Mwendamtitu fedha zake zitatoka na mradi ule utatekelezwa kama nilivyoahidi nilipotembelea mradi mimi mwenyewe.

Na. 89

**Tiba ya Ugonjwa wa Kifafa**

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED (K.n.y. MHE. CLARA D. MWATUKA)** aliuliza:-

Ugonjwa wa kifafa ni miongoni mwa magonjwa sugu yanayowahangaisha wananchi wa rika zote:-

(a) Je, Serikali inawatumiaje wanasayansi tulionao kuchunguza asili na suluhisho la ugonjwa huo?

(b) Je, kwa nini wagonjwa wa ugonjwa huo wasipelekwe kutibiwa nje kama inavyofanyika kwa magonjwa mengine yanayoshindikana?

(c) Je, ni kweli kwamba wanasayansi wetu wameshindwa kabisa kupata dawa ya ugonjwa huo au hawajapania kufanya uchunguzi wa dhati?

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa Wabunge hili ni moja ya mfano wa maswali marefu kwa vyo vyote litakuwa na majibu marefu. Mheshimiwa Waziri majibu?

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, ninaomba kujibu swali la Mheshimiwa Clara Diana Mwatuka, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a),(b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a)Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu kupitia wataalam walio vyuo vikuu pamoja na wataalam wanaofanya kazi katika vituo vya wagonjwa wa akili, wanafanya tafiti mbalimbali kuhusu maradhi ya kifafa. Kutokana na tafiti hizo za kisayansi matokeo yanaonyesha kuwa visababishi vya kifafa ni kurithi, ajali, athari zitokanazo na homa kali inayoambatana na degedege, uvimbe kwenye ubongo na athari za matumizi ya dawa nyingine (*metabolice disorders*), wataalam wameshauri Serikali ichukue hatua mbalimbali za kuzuia hivyo visababishi na kupunguza athari zake.

Kwa mfano kuboresha huduma za mama wajawazito, kutumia vyandarua vya kuzuia malaria yanayosababisha homa kali na hivyo kupelekea degedege na kadhalika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, wagonjwa wenye ugonjwa wa kifafa (kama wagonjwa wengine) wenye matatizo makubwa yasiyoweza kushughulikiwa hapa nchini. Kwa mfano wale walioko kwenye kundi la sababu zinazojulikana na

kutibika kama vile uvimbe kwenye ubongo, hupewa rufaa ya kwenda kutibiwa nje. Wataalam wetu hushirikiana kwa karibu sana na wataalam wa nje ili kuweza kujenga uwezo wa kuwatibu wagonjwa hawa. *(Makofi)*

Mathalani, Serikali ina mpango wa kujenga kituo kikubwa cha upasuaji wa ubongo na mishipa ya fahamu katika taasisi ya *MOI,* ikiwa ni pamoja na kuongeza idadi ya wataalam na vifaa tiba katika fani hiyo.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali yetu kupitia wataalam waliyoko vyuo vikuu wanasayansi wa ugonjwa wa kifafa wapo, dawa zipo, na hata hivyo matokeo ya tiba ya ugonjwa wa kifafa hutofautiana kati ya wagonjwa, wengine wanapona kabisa, wengine ugonjwa utadhibitiwa na wengine hawapati nafuu. Ushauri wa Wizara ni:-

Jamii watimize masharti wanayopewa na Daktari, wawahi kuwapeleka wagonjwa mara wapatapo dalili za kifafa au degedege na waachane na mila na desturi nyingine zisizokuwa na manufaa kwa wagonjwa wa aina hii. Wataalam wa afya nao wanahitaji kuwahudumia kina mama wajawazito wakati wa kujifungua na kutoa huduma za haraka pamoja na uangalizi wa karibu wa watoto wanaopatwa na homa kali.

**MHE. THUWAYBA IDRISA MUHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Kwa kuwa katika jibu lako la msingi umesema kwamba Serikali inataka kujenga kituo cha kufanya utafiti wa ubongo au kupasua ubongo.

(a) Je, ni lini kituo hicho kitajengwa?

(b) Kwa kuwa mnaitaka jamii mara tu inapoona dalili za kupata kifafa wawapeleka wagonjwa hospitali. Je, Serikali mmetoa elimu yeyote kuhusu jambo hili? Na kama hamkutoa mna mkakati gani wa kutoa elimu hiyo? (*Makofi*)

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Thuwayba, maswali mawili kama ifuatavyo:-

Kama utabahatika kufika kwenye hospitali ya *MOI,* pale tumeshaanza kutoa huduma hizo za upasuaji wa mishipa ya fahamu pamoja na ubongo, lakini huduma ile ni bado inatolewa katika kiwango kidogo na ndiyo maana Serikali tumejipanga kutegemea na upatikanaji wa fedha kujenga kituo kikubwa zaidi cha huduma zile ambazo tunazitoa sasa hivi pale kwenye hospitali yetu ya *MOI.*

Swali la pili kwamba dalili za wagonjwa hawa wa kifafa, tunashauri zinapopatikana wagonjwa hawa wakimbizwe au wapelekewe kwenye vituo vinavyotoa huduma za tiba.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge ukifuatilia vipindi vyetu ambavyo vinatoa elimu ya afya ni moja wapo ya vitu ambavyo mara kwa mara tunawapa Watanzania elimu ni namna gani ya kuweza kukabiliana na maradhi pamoja na kutambua dalili na kwenda kupata tiba haraka iwezekanavyo kwenye vituo vyetu vya Serikali na hata vituo binafsi.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, naomba kutambua uwepo wa *Chief whip* wa upande wa Upinzani, Mheshimiwa Tundu Lissu, sijui alikuwa wapi ndiyo leo anaingia, karibu sana. Mheshimiwa Vita Kawawa, swali la nyongeza.

**MHE. VITA R. KAWAWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa fursa ya kuuliza swali. Kwa kuwa katika Wilaya yetu ya Namtumbo kwenye Kata zetu mbili ya Hanga na Msindo kumekuwa na ugonjwa usiojulikana kwa watoto wetu, wasichana kukosa nguvu za miguu ambayo inajitokeza kila mwaka mwezi wa pili mpaka mwezi nne.

Je, Serikali inaweza kuja kufanya utafiti wa kuona tatizo hilo ambalo linasumbua sana watoto wa kike tu na wanashindwa kusoma?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nijibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Vita Kawawa kama ifuatavyo:-

Kwanza naomba nikupongeze kwa kutoa taarifa hizi, lakini rasmi naomba nikiri kwamba ndiyo tumezipokea sasa hivi na naomba Mheshimiwa Vita Kawawa tukitoka hapa tuonane unipe taarifa kwa undani zaidi, kwa kina zaidi mara moja.

Nitatuma watendaji wangu sio tu baada ya Bunge hapa, ila ni kuanzia kesho waende kule kwenye Kata ya Hanga - Namsimbu kwenda kuangalia tatizo hili na chanzo chake ni nini ili tuweze kupata tiba yake. (*Makofi*)

Na. 90.

**Ujenzi wa Barabara za Nagomba- Mtambaswala na Magaka kwa Kiwango cha Lami**

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA** anauliza:-

Je, ni lini barabara za Nangomba-Mtambaswala na Mangaka-Mtambaswala zitajengwa kwa kiwango cha lami?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Ujenzi napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mbunge wa Nanyumbu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, usanifu wa barabara ya Mangaka-Nanyumbu-Mtambaswala (km 65.5) na kipande cha Nangoma-Nanyumbu (km30) ulikwishafanyika na kukamilika.

Serikali imekamilisha majadiliano ya mkopo wa fedha kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika *(ADB)* wakishirikiana na Shirika la Maendeleo la Japan *(JICA)* kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi wa barabara ya Mangaka-Nanyumbu-Mtambaswala (km 65.5) kwa kiwango cha lami. Majadiliano ya mkopo yalifanyika kati ya Serikali na *ADB* mnamo tarehe 8 Februari, 2012.

Makisio ya gharama ya ujenzi kwa kiwango cha lami wa barabara ya Tunduru-Mangaka-Mtambaswala yenye urefu wa kilometa 202.5 ikihusisha barabara ya Mangaka-Nanyumbu-Mtambalaswa yenye urefu wa kilometa 65.5 ni shilingi bilioni 240.313 ambapo *ADB* watatoa shilingi bilioni 158.126 sawa na asilimia 65.8, *JICA* watatoa shilingi bilioni 70.171 sawa na asilimia 29.2 na Serikali itachangia shilingi 12.016 sawa na asilimia 5.

Mheshimiwa Naibu Spika, mara baada ya Bodi ya Wakurugenzi ya *ADB* kutoa uamuzi wa kuidhinisha mkopo na fedha za mkopo kutolewa, ujenzi utaanza mara moja. (*Makofi*)

**MHE. DUNSTAN D. MKAPA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa majibu mazuri ya Serikali ambayo yanaleta matumaini. Nina maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa usanifu wa barabara ya kutoka Nangomba mpaka Nanyumbu umekwishafanyika na kwamba hii ilikuwa ni ahadi ya Rais wakati anaomba kura kwa ajili yangu. Je, barabara hii sasa itaanza kujengwa lini kwa kiwango cha lami?

(ii) Kwa kuwa kuna wananchi katika Barabara hii ya Nangomba – Nanyumbu – Mangaka – Nanyumbu mpaka Mtambaswala wamewekewa alama za X; ni lini sasa hawa wananchi watapatiwa fidia zao ili waweze kuhama rasmi? Ahsante.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kipande cha barabara cha Nangomba mpaka Nanyumbu, chenye urefu wa kilomita 30 tu, ningependa kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba pesa tunatafuta. Nilidhani itakuwa taarifa nzuri kwake kwamba sasa ile barabara ndefu zaidi yenye urefu wa kilomita 202 tunaitafutia pesa na tayari tumeshasaini mkataba. Kwa hiyo, asitie shaka hicho kipande kifupi cha kilomita 30 tutakijenga na tulishaanza vizuri kwa kukamilisha *studies* zote.

Pili, kuhusu masuala ya fidia; nilimwomba Mheshimiwa Mbunge, atupe fursa wenzake tumeze mate kwanza tupate hiyo mikopo inayotakiwa na wananchi watapata fidia kamilifu kama ambavyo tunafanya kwa barabara zote.

**MHE. ENG. STELLA M. MANYANYA:** Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniona. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri kuhusiana na ujenzi wa barabara zinavyoendelea, nina swali moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa barabara ambazo tulikuwa tumezipangia kwenye bajeti ya mwaka 2011/2012 zinaonekana nyingi zimeanza hasa zile zinazohitaji pesa kutoka katika Serikali yetu zimeanzishwa lakini zinaendelea kwa kasi ndogo; na kwa kuwa sasa tunajipanga kwa ajili ya bajeti ijayo; je, hatuoni ni vyema sasa badala ya kuja na bajeti ya aina mpya na kuharibu tena karatasi nyingi katika kuchambua mipango mingine tukamalizia kwanza hizi ambazo tayari tulishaziahidi na

zimeanza na hazijaweza kutekelezwa kadiri inavyowezekana? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, wazo la Mheshimiwa Mbunge ni zuri sana kwa kulisikiliza lakini kiutendaji angeelewa mzigo ambao tunaubeba Kitaifa nafikiri asingesema hivyo; kwa sababu kwa sasa hivi tuna barabara 64 ambazo tunazihangaikia kwa ujenzi katika ngazi mbalimbali zenye urefu wa kilomita 3,880. Huo ni mzigo mkubwa sana kwa Serikali lakini hatuwezi tukautua pembeni, bado tunadaiwa barabara zingine kuzijenga na sasa tusimame mpaka tumalize kwanza hizi ndipo tuweze kuendelea na zingine. Kuhusu kusuasua kwa Miradi, nataka kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba, hatuwezi kwenda kwa kasi zaidi ya hapo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishasema katika Bunge lako hapa kwamba, lipo pia tatizo la uhakiki ambalo hatuwezi kulikwepa. Barabara nyingi inaonesha kwamba tutakwenda pole pole hasa katika malipo, si kwa sababu Serikali imefilisika au ina pesa hapana ni kwa sababu ya kazi ya uhakiki kuhakikisha kwamba pesa ya Serikali haiendi kwenye Miradi hewa au hailipwi kwa kazi ambayo imefanywa hovyo hovyo.

Na. 91

**Ujenzi wa Kipande cha Barabara cha Tabora – Sikonge**

**MHE. SAID J. NKUMBA** aliuliza:-

Serikali katika bajeti ya mwaka 2011/2012 imeanza kutenga fedha kwa ajili ya kujenga kwa lami kipande cha barabara chenye urefu wa km 71 cha kutoka Tabora - Sikonge:-

(a) Je, ni maandalizi gani yanayofanywa ili ujenzi huo uweze kuanza katika mwaka wa fedha unaofuata (2012/2013)?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kumalizia ujenzi kwa kiwango cha lami sehemu zitakazobaki za Barabara ya Ipole – Rungwe na Sikonge – Mpanda?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Said Juma Nkumba, Mbunge wa Sikonge, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kukamilika kwa kazi za upembuzi yakinifu na usanifu wa kina, maandalizi yanayofanyika kwa ajili ya kuanza ujenzi kwa kiwango cha lami kwa Barabara ya Tabora – Sikonge, yenye urefu wa kilometa 71, yanahusisha utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa ajili ya ujenzi wa kiwango cha lami. Aidha, katika bajeti ya mwaka 2011/2012, Wizara imetenga shilingi milioni 590.31 kwa ajili ya kutangaza *tender* na kuanza ujenzi wa sehemu ya Tabora – Sikonge kwa kiwango cha lami. Pia fedha za ujenzi zitaendelea kupangwa katika bajeti inayokuja ya 2012/2013.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali katika Mwaka wa Fedha wa 2011/2012, imetenga shilingi milioni 269.11 kwa ajili ya kuanza upembuzi yakinifu na usanifu wa kina wa sehemu iliyobaki ya Barabara ya Ipole – Rungwa, yenye urefu wa kilometa 95 ikiwa ni maandalizi ya ujenzi kwa kiwango cha lami. Aidha, upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni kwa Barabara ya Sikonge – Ipole – Koga – Mpanda umekamilika mwezi Januari, 2012 ikiwa ni sehemu ya kazi ya upembuzi yakinifu na usanifu uliofanyika katika Barabara ya Tabora – Sikonge – Ipole – Mpanda, yenye urefu

wa kilometa 359. Hatua inayofuata ni Serikali kutafuta fedha ili kazi za ujenzi kwa kiwango cha lami zianze kwa sehemu ambazo usanifu umekamilika. Kuhusu sehemu ya Ipole hadi Rungwa, Serikali inatafuta fedha za ujenzi baada ya usanifu wa kina na maandalizi ya nyaraka za zabuni kukamilika.

**MHE. SAID J. NKUMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuuliza maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Wakati Wananchi wa Sikonge wanaendelea kusubiri ujenzi huo wa kiwango cha lami; je, Mheshimiwa Naibu Waziri anaweza kutuhakikishia kwamba fedha kiasi gani zimetengwa ili barabara hiyo iendelee kupitika wakati wote? *(Makofi)*

(ii) Mkoa wa Tabora unazo barabara mbili zinazopita pale;
moja inatoka Nzega kuja Tabora na nyingine inatoka Manyoni – Tabora – Urambo – Malagarasi mpaka Nguruka. Barabara hizi zinajengwa kwa kusuasua kama alivyosema Mheshimiwa Stella Manyanya hapa. Naomba kwa kutoa matumaini ya kwa wananchi kwa Mkoa wa Tabora; Mheshimiwa Naibu Waziri atoe maelezo ya matumaini. Nashukuru.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, naomba nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia kwa karibu sana na kwa makini masuala ya Jimbo la Sikonge, siyo hapa Bungeni tu lakini hata Wizarani. Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Mbunge kuwa, tutaendelea kuiweka Barabara ya Tabora hadi Sikonge na siyo mpaka Sikonge tu mpaka Ipole, kilomita zote 92.8, katika hali nzuri. Leo asubuhi nilikuwa naongea na Meneja wa *TANROADS* Mkoa wa Tabora, akanihakikishia kwamba siyo kwamba katika kipindi cha fedha cha mwaka 2010/2011 tumetumia shilingi milioni 634, lakini mwaka huu vile vile tuna shilingi 855 ambazo tunaendelea na ukarabati wa barabara hiyo ambayo nimeshaipita na Mheshimiwa Mbunge alinipokea.

Mbili, kuhusu kusuasua kwa ujenzi wa barabara ambazo zimeshaanza. Ninaomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, Mkoa wa Tabora una makandarasi watano wanaoshambulia barabara mbalimbali na nimehakikishiwa leo asubuhi kwamba barabara zote zimefanya maendeleo kuanzia asilimia saba mpaka kumii, ambayo ni kubwa kwa sababu ni Miradi ambayo imeanza hivi majuzi. Lengo letu kubwa ni katika miaka miwili ijayo Mkoa wa Tabora uwe na sura mpya kabisa.

**MHE. MOSHI S. KAKOSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa Mkoa mpya wa Katavi upo nyuma sana kimiundombinu na hasa ya barabara; na kwa kuwa barabara ambayo inaunganisha Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Tabora ni mbaya sana na upembuzi yakinifu umefanyika: Je, ni lini Serikali itatuhakikishia kwamba katika bajeti ijayo itatenga kiasi cha fedha ili iweze kuwasaidia Wananchi wa Mkoa mpya wa Katavi ambao wanaitegemea sana Barabara ya Mpanda – Tabora? Licha ya Barabara hii kutegemewa na Wananchi wa Mpanda, bado Wananchi wa Mikoa ambayo ina uhaba wa chakula wanaitegemea sana Barabara hiyo; ikikamilika wataweza kupata huduma ya kimsingi.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, katika jibu langu la msingi nimeongelea kuhusu upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na utayarishaji wa nyaraka za zabuni wa Barabara ya Sikonge – Ipole – Koga mpaka Mpanda kwamba umekamilika mwezi Januari mwaka huu. Hii yote ni juhudi ya kuunganisha Mkoa wa Tabora na Mikoa ya Kusini, ukiwepo Mkoa wa Katavi na Mkoa wa Rukwa. Kazi tuliyonayo sasa kama Serikali, baada ya kukamilika hizo nyaraka ni kutafuta fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba, kazi ya kutafuta fedha vile vile ni ngumu kwa sababu nchi yetu ni kubwa, mahitaji ni

makubwa. Tunamhakikishia kuwa, tutaipa kipaumbele barabara hii, tutatafuta hiyo fedha na tutalitaarifu Bunge lako Tukufu tutakapopata hiyo fedha.

**MHE. DEOGRATIAS A. NTUKAMAZINA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuniona. Mwaka jana, Naibu Waziri wa Ujenzi alituahidi Wananchi wa Ngara kwamba katika bajeti ya 2011/2012, wangeanza kuweka fedha kidogo kidogo ili kutekeleza ahadi ya Rais ya barabara ya lami kutoka Munzani kupita Rulenga mpaka Ngara. Wananchi wa Ngara walinishangaa wakasema kumbe siku hizi ahadi za Mawaziri ambazo zinaingia kwenye *Hansard* siyo za kweli! Nikasema hapana hebu tuwe na subira. Baadaye nikamwandikia Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi kuhusu barabara hiyo kwa ajili ya bajeti ya mwaka huu. Ninaomba Naibu Waziri atupe ahadi nyingine tena kama katika bajeti ya mwaka huu wa 2012/2013 barabara hiyo imefikiriwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI (BARABARA NA VIWANJA VYA NDEGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, tumeshapata barua ya kina kabisa kutoka kwa Mheshimiwa Mbunge kuhusu Barabara ya Rulenge kwenda Ngara. Mimi naomba atupe nafasi basi tuifanyie kazi na nina uhakika ataridhika na kazi ambayo tutaifanya.

Na. 92

**Ukaguzi wa Magari Yanayoingia Nchini**

**MHE. VINCENT J. NYERERE** aliuliza:-

Ukaguzi wa ubora wa magari yanayoingia nchini hufanyika nje ya nchi na kuacha fedha nyingi katika nchi hizo:-

Je, Serikali haioni umuhimu wa ukaguzi huo kufanyikia nchini ikiwa ni pamoja na kuyafanyia marekebisho magari yenye kasoro kabla yayajaingia barabarani ili kuongeza ajira kwa vijana?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Vicent Joseph Nyerere, Mbunge wa Musoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wa kukagua ubora wa magari kabla ya kuletwa hapa nchini una faida ambazo ni pamoja na kuhakikisha fedha nyingi za kigeni hazipotei bure, kwani gharama za ukaguzi huu ni ndogo ikilinganishwa na gharama inayotumika kwa matengenezo baada ya kununua gari likiwa bovu; kuwezesha wanunuzi kununua magari yenye ubora unaofaa kwa matumizi barabarani na hivyo kuzuia ajali zinazotokana na ubovu wa magari; kuzuia Tanzania isiwe jalala la kutupa magari mabovu; kuzuia uchafuzi wa mazingira kutokana na mrundikano wa magari mabovu na wakati wa kuyaharibu au kuyateketeza kwa vile magari mengine yanaweza kuwa na mionzi yenye athari kwa binadamu, athari kwa mimea na wanyama; vile vile kuzuia mnunuzi kupata hasara kwa kununua gari bovu ambalo baada ya ukaguzi linaweza kuzuiwa kutumika katika barabara zetu za Tanzania kutokana na Sheria ya Viwango Na. 3 ya Mwaka 1975, ambayo ilifanyiwa marekebisho kama Sheria Na. 2 ya Mwaka 2009.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na faida nilizozitaja hapo juu, kukagua magari yaliyotumika hapa nchini kuna changamoto zifuatazo: Kuanzisha vituo vya ukaguzi vya kutosha katika mipaka yote kwa nchi nzima ili kuwezesha ukaguzi na kuchelewesha utoaji wa mizigo bandarini na hivyo kusababisha hasara kubwa kwa mnunuzi ambaye gari lake

litashindwa kufikia kiwango cha ubora na kuharibiwa au kurudishwa lilikotoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, faida za kufanya ukaguzi wa magari yaliyotumika nje ya nchi ni nyingi kuliko zile za kufanya ukaguzi huo hapa nchini. Hivyo, Sera ya Ukaguzi wa Bidhaa Nje ya Nchi kama inavyoungwa mkono na Shirika la Biashara Duniani *(WTO)* ni nzuri na inafaa iendelee kutumiwa nchini kwetu.

**MHE. VINCENT J. NYERERE:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika. Kutokana na majibu ambayo siyo ya kweli ya Waziri, nilikuwa napenda kuuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Kuna ushahidi wa dhati wenye vielelezo kwamba magari hayo hayakaguliwi na yanakuja nchini. Je, anatoa kauli gani?

(ii) Katika kampuni nane ambazo Wizara imezipa kazi hiyo bila kufuata Sheria hiyo na bila kufuata Kanuni ya Manunuzi; kampuni saba ni za maswaiba wa Watendaji wa Wizara. Je, nikileta ushahidi huo wapo tayari kuwajibika? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, namshukuru kwa kufuatilia jambo hili ambalo hivi karibuni lilizua utata mkubwa. Nimhakikishie tu Mheshimiwa Nyerere kwamba, majibu ambayo Serikali imeyatoa kuhusiana na Sheria iliyotungwa hapa Bungeni, Sheria Na. 3 ya Mwaka 1975, ambayo ilifanyiwa marekebisho na Bunge hili hili ikawa Sheria Na. 2 ya Mwaka 2009, *Part II - Section Four,* ilitoa maelekezo kwa Serikali kufanya *pre-shipment verification of conformity,* kwa magari na baadhi ya bidhaa muhimu kabla hazijafika hapa nchini. Kwa hiyo, Serikali inachofanya, inatekeleza Sheria iliyotungwa na Bunge hili na itaendelea kufanya hivyo na kwa wakati wowote Mbunge

mmoja mmoja au kwa pamoja, tunaweza tukairekebisha Sheria hii kwa mfumo wetu wa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, cha pili ambacho Mheshimiwa Mbunge amekisema ni uwezekano wa baadhi ya haya magari hayakaguliwi.

Mheshimiwa Naibu Spika, hili jambo tumelisikia, limepelekwa kwa Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG).* Mimi nilielekezwa na Mheshimiwa Waziri, kukutana na Kamati hizi zote mbili kwa pamoja chini ya Mheshimiwa Cheyo, tulifanya mazungumzo na Kamati ya Hesabu za Serikali na Kamati ya Mashirika ya Umma. Baada ya ule Mkutano wa pamoja ambao *CAG* pia alihudhuria, kulikuwa na tuhuma nyingi sana ambazo zilielezwa juu ya utendaji wa *TBS,* ikiwa ni pamoja na shutuma kwamba, baadhi ya magari hayakaguliwi na baadhi ya Kampuni zinazofanya ule ukaguzi ni za watu ambao ama wana uhusiano na *TBS* ama wanafanya kazi na *TBS.*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ilichoagiza ni moja kwa moja Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, apewe kazi yake ya kuthibitisha, ya kufanya ukaguzi wa haraka. Ile kazi imekamilika imefika katika mikono ya Serikali. Naomba niliahidi Bunge hili, Serikali haitasita kuchukua hatua mara baada ya kupitia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

**MHE. GRACE S. KIWELU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa zipo taarifa kupitia Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwamba, hao Mawakala waliopo nje ya nchi wamekuwa wakikusanya fedha nyingi, lakini walizokuwa wanapeleka Serikalini kupitia Mkataba waliokubaliana na *TBS* ni asilimia 25. Wamekuwa hawapeleki fedha hizo na kufanya wao kujinufaisha binafsi na kupunguza pato la nchi.

Je, Serikali inachukua hatua gani kwa Mawakala hawa?

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hesabu tulizokuwanazo mpaka sasa hivi *TBS* wanapokea asilimia 25 ya fedha zote ambazo zinapatikana kutokana na ukaguzi wa magari. Kwa mwaka jana, tayari zilikuwa zimepatikana Dola za Kimarekani 8,828,040 na *TBS* walipata Dola za Kimarekani 2,207,010 na Mawakala nje ya nchi, wale wanaofanya ukaguzi, walipata Dola za Kimarekani 6,621,030.

Mheshimiwa Naibu Spika, ambacho ningependa kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge, Serikali inaiagiza tena Bodi Mpya ya *TBS* na kwa kutumia nafasi hii, nawaagiza wazipitie upya hizi tozo ambazo zinatolewa, waone kama kiwango cha fedha ambazo tunalipwa *TBS* ni sahihi na kiwango ambacho wanalipwa Mawakala cha karibu asilimia 75 kama kinafaa. Endapo Bodi itatoa mapendekezo Serikalini, tutakuwa tayari kufanya *revision* ili tuhakikishe mapato halisi ya Serikali yanaifikia nchi hii.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tuendelee. Kwa kuwa leo tutakuwa na taarifa za baadhi ya Kamati za Fedha, huenda baadhi ya mambo haya yakajitokeza huko mbele. Wizara ya Fedha sasa; Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama.

Na. 93

**Kodi za Wafanyakazi wa Wizara za Muungano**

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA** aliuliza:-

Moja kati ya mapendekezo ya Kamati ya Kujadili Kero za Muungano ni lile la kodi za Watumishi wa Wizara zile za Muungano wanaofanya kazi Tanzania Zanzibar, ziingizwe kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, lakini Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania haijabadilisha Sheria ili utekelezaji uweze kuanza:-

Je, ni lini Serikali italeta Muswada wa Sheria husika Bungeni ili kutunga Sheria itakayowezesha utekelezaji wa jambo hilo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, Kamati ya Pamoja ya Masuala ya Muungano imeshafikia mwafaka kwamba, kodi za Watumishi wa Wizara zile za Muungano wanaofanya kazi Tanzania Zanzibar, ziingizwwe kwenye Mfuko Mkuu wa Hazina wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa jambo hili umeshaanza. Hata hivyo, ni vyema kuelewa kwamba, suala la kodi ya mapato ni la Kikatiba kama ilivyo kwenye Nyongeza ya Kwanza ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977. Aidha, kwa mujibu wa Kifungu cha 81(1) cha Sheria ya Kodi ya Mapato, kinataka mwajiri kuzuwia kodi ya mapato ya wafanyakazi anaowalipa mishahara na mapato mengine yatokanayo na ajira kwa viwango vilivyoainishwa na kuwasilishwa kwa Kamishna wa Kodi ya Mapato Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Serikali mbili kukubaliana, Wizara ya Fedha imeshaandaa Waraka wa Baraza la Mawaziri ili Baraza nalo liridhie mapendekezo ya marekebisho ya Sheria ya Kodi ya Mapato, Sura ya 332. Mara tu baada ya mapendekezo hayo kuridhiwa, Muswada wa Sheria utakuja Bungeni kwa marekebisho.

**MHE. MWANAMRISHO TARATIBU ABAMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda nimwulize swali moja dogo la nyongeza:-

Majibu ya Mheshimiwa Waziri, yamejikita zaidi katika Kodi ya *payee.* Je, kodi ya mapato iliyozuiliwa *(Withholding Tax)* na Kodi ya Faida ya Makampuni nayo inashughulikiwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mwanamrisho Taratibu Abama, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ajenda za Kamati ya Pamoja ya Masuala ya Muungano, makubaliano yamefikiwa kwenye kodi ya *payee* au kodi ya mapato ya watumishi na pia kodi ya *withholding.* Masuala mengine yaliyobakia ya kikodi bado ni ajenda za Kamati hii na zitapatiwa ufumbuzi si muda mrefu unaokuja.

Na. 94

**Utaratibu wa Ulipaji wa Malipo ya Uzeeni Mstaafu Anapopatwa na Matatizo ya Dharura**

**MHE. JUMA SURURU JUMA** aliuliza:-

Serikali imekuwa ikiwalipa Wastaafu pensheni zao kwa utaratibu uliowekwa, lakini pale mstaafu anapopatwa na matatizo ya aina mbalimbali kama vile kuugua na kuuguliwa na jamaa zake hawezi kupata fedha za kumsaidia kutoka kwenye pensheni yake nje ya muda uliowekwa:-

(a) Je, Serikali haioni umuhimu wa kuanzisha utaratibu wa kuwapatia pesa pale wanapofikwa na matatizo ili utakapofika wakati wa malipo yao wakakatwa fedha hizo?

(b) Kama Serikali itaona kuwa utaratibu huo haufai; je, inaweka utaratibu gani mbadala wa kuwasaidia wastaafu hao wanapopata matatizo kama hayo?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Juma Sururu Juma, Mbunge wa Bububu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaona umuhimu mkubwa wa kuanzisha utaratibu wa kuwasaidia Wastaafu pale wanapofikwa na matatizo. Hata hivyo, kutokana na uwezo wa Serikali kimapato kuwa mdogo kukidhi mahitaji yote muhimu, Serikali bado haijaweza kuanzisha utaratibu wa kuwakopesha fedha Wastaafu, kwa ajili ya kuwawezesha kutatua matatizo ya dharura yanayowafika.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kutekeleza Sera ya Wazee ya Mwaka 2003 na Sera ya Afya ya Mwaka 2007, zinazolenga pamoja na mambo mengine, kutoa huduma kwa wastaafu na wazee wote nchini, bila kujali kigezo cha uwezo au kazi aliyofanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Wastaafu, Serikali imeamua kuwalipa mafao yao ya mwezi, kila baada ya miezi mitatu badala ya sita ili kuwapunguzia makali ya maisha. Hata hivyo, Serikali inawashauri watumishi wote kujiunga na mifuko/mitandao mbalimbali ya Hifadhi za Jamii *(Safety Nets)* kama vile Bima ya Afya, *SACCOS,* Akaunti za Watoto kwa ajili ya shule, vikundi vya kufa na kuzikana, vikundi vya akina mama, wazee na vijana, kabla ya kustaafu ili kujikinga na au kujiongezea uwezo wa kuyakabili matatizo yanayoweza kuwakumba mara baada ya kustaafu.

**MHE. JUMA SURURU JUMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kumwuliza maswali mawili ya nyongeza.

(i) Pamoja na Serikali kutekeleza Sera ya Afya Bure kwa Wazee; je, Serikali ina mkakati gani wa ziada wa kuwakinga hawa wazee na maisha hatarishi badala ya kuelekeza Sera ya Afya ya Bure?

(ii) Mheshimiwa Naibu Spika, hadi sasa kuna taasisi nyingi zinazohusiana na ulipaji wa mafao kama Hazina, *PPF, NSSF* na kadhalika; je, ni nani ana wajibu wa kuwatetea wazee hao? Wanastahiki haki zao kuvunjwa iwapo wanalipwa?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. GREGORY G. TEU):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Fedha, naomba nijibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho nimesema ni kigumu Serikali kukifanya kwa sasa ni kutoa fedha pale wazee wanapopata matatizo ya kiafya. Hata hivyo, Serikali kwa kushirikiana na taasisi mbalimbali zisizo za Kiserikali, zinatoa huduma hasa za elimu kwa ajili ya wazee kuishi maisha ya kiafya *(Good Life Style).*

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, kuna programu nyingi za kuwashajihisha mazoezi, wanaita Vitambi Noma. Kuna Programu za Vyakula Bora na elimu kuhusu suala hili. Pia kuna Programu za Ulevi Noma na kuna Programu nazikumbuka nyingine, Fainali Uzeeni, zote zinafanywa katika kuwakinga wazee wasiende kwenye maisha hatarishi. Kubwa pia kwa upande wa Serikali, kwenye matumizi ya vilevi kama sigara au mazao ya tumbaku, Serikali huwa inaongeza kodi kama mkakati wa kuhakikisha matumizi yake yanapunguzwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kulinda haki za wastaafu; *infact* kwenye mwaka 2008, Serikali ilianzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Hifadhi za Jamii. Hii, pamoja na mambo mengine, kazi zake ni kutoa elimu, kutafuta haki, kuainisha mafao kwenye Mifuko hii na pia kubwa ambalo linahitaji kufanywa ni kuongeza wigo wa Watanzania wanaonufaika na hifadhi hizi za jamii, kwa sababu sasa hivi ni chini ya asilimia tano ambao wanafaidika na mifumo hii.

Na. 95

**Mafanikio ya Shirikisho la Mpira wa Miguu**

**MHE. AHMED JUMA NGWALI** aliuliza:-

Shirikisho la Mpira wa Miguu Tanzania *(TFF)* hapo zamani lilijulikana kama *Football Association of Tanzania (FAT)* ambayo ilianzishwa mwaka 1930 wakati ikiitwa *Tanganyika Football Association (TFA)* na ilijiunga na *FIFA* mwaka 1964:-

Je, ni mafanikio gani ya msingi na ya kujivunia yaliyopatikana kwa Shirikisho la Mpira wa Miguu mpaka sasa?

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa ujumla, Shirikisho la Mpira wa Miguu limejitahidi kupata mafanikio ambayo ni ya msingi kabisa katika maendeleo ya mchezo wa Mpira wa Miguu. Mafanikio hayo ni pamoja na:-

(i) Kukuza na kuendeleza mpira wa miguu katika kila kona ya nchi yetu na kuweka muundo wa utawala katika kila ngazi na unaotekelezeka.

(ii) Kuandaa wataalam wa fani za ufundishaji, uamuzi, utawala na tiba ya wanamichezo zaidi ya 10,000. Wataalam hao wamepata mafunzo ya msingi na ya kati tangu nchi yetu ipate uhuru.

(iii) Kuandaa na kuendesha programu mbalimbali ikiwa ni pamoja na mashindano ya timu za vijana, wanawake na watoto kama sehemu ya kuweka msingi bora wa maendeleo ya mchezo wa soka.

(iv) Katika kipindi hicho, Timu ya Taifa iliweza kutwaa Kombe la *"Challenge"* mara tano huku Klabu za Simba na Yanga zikishinda Kombe la Klabu Bingwa Afrika Mashariki mara moja kila moja.

(v) Timu ya Taifa ilifanikiwa kucheza mara moja fainali za Kombe la Afrika na mara moja kwa Timu za Taifa za Wachezaji wa Ligi za Ndani.

(vi) Kujenga na kuimarisha uhusiano mwema kati ya Shirikisho na Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, mafanikio haya si ya kujivunia sana, bado jitihada kubwa inaendelea kufanyika ili kupata mafanikio zaidi katika miaka ijayo.

**MHE. AHMED JUMA NGWALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba niulize maswali mawili ya nyongeza kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa *TFF* ni *Tanzania Football Federation;* na kwa mujibu wa Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara ya 1 na 2, Zanzibar ni sehemu ya Jamhuri ya Muungano

wa Tanzania; na kwa kuwa Katiba ya *TFF* inatambua Mikoa 21 tu ya Tanzania Bara na haiitambui Mikoa mitano ya Zanzibar. Je, Serikali haioni haja ya kuibadilisha jina *TFF* na kuiita *Tanzania Mainland Football Federation (TMFF)? (Makofi)*

(ii) Kwa kuwa *TFF* inasumbuliwa na ugonjwa wa uwoga, kukosa dira, mwono na utamaduni wa kififikra katika mkakati wa kuendeleza soka nchini; na kwa kuwa *TFF* imejihusisha zaidi na kuendeleza migogoro, fitina, majungu na ubinafsi; je, Serikali ina mkakati gani wa makusudi na wa kutekelezeka wa kuendeleza soka nchini?

**NAIBU SPIKA:** Hili la pili Mheshimiwa, kweli chombo kazi yake ni kuendesha migogoro na fitina? Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali, Mbunge wa Ziwani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, swali la kuhusu *TFF* kuwa na Mikoa 21 na kwamba inatambulika zaidi Bara na haishughulikii masuala ya Zanzibarr, kwa hiyo, iitwe *TFF* iwe kama siyo ya Tanzania, isipokuwa imilikishwe tu kwamba ni ya Bara.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi napenda tu nichukue nafasi hii, kwanza; nimweleweshe kabisa Mheshimiwa Ahmed Juma kwamba, *TFF* inashirikiana kwa karibu kabisa na *ZFA* ambayo ndiyo ipo Zanzibar. Kwa kiasi kikubwa, kumekuwa hakuna mtafaruku wowote. Kwa hiyo, hii dhana ya sasa hivi ya kutaka kuleta mgawanyiko kwamba upo na unakithiri siyo dhana sahihi. Ningependa atambue kwamba, *TFF*

inashughulika kwa karibu kabisa na Zanzibar, kwa hiyo, hakuna haja ya kuitambulisha *TFF* kama vile ni ya Tanzania Bara peke yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna ushirikiano wa karibu kabisa baina ya *ZFA* pamoja na *TFF,* kiasi ambacho hata migogoro ambayo ilikuwepo zamani kuna Kamati ambayo imeundwa ya kuhakikisha migogoro hiyo haipo. Timu ya Taifa ikiwa Kambini, wanashirikiana kwa karibu. Wakati wa kushughulikia Makocha mbalimbali, vyote hivyo vinashughulikiwa kwa karibu. Kwa hiyo, kwa dhana hiyo nyingine ya kusema kwamba, iwe ya Tanzania Bara peke yake, mimi nadhani huo siyo mtazamo mzuri na Watanzania watambue kwamba, hakuna hizo tofauti.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni hilo la *TFF* kutawaliwa na migogoro. Mimi nadhani kutawaliwa na migogoro au kazi yake kubwa ni kutatua migogoro; kwanza nikiri tu kwamba, kumekuwa na migogoro ndani ya masuala ya timu za mipira pamoja na vyama vyake. Kazi moja ya *TFF* kama nilivyoeleza katika majibu yangu ya msingi, nimeeleza makubwa tu hapa, tumeweza kuanzisha hata masuala ya timu za mpira wa wanawake, vijana na kumekuwa na mipango tofauti tofauti ya Kitaifa ambayo inasimamiwa na *TFF* wakishirikiana na *FIFA.*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna masuala ya *Glass Root Sports;* kuna masuala ya *FIFA Health*; kuna masuala ya *Sport Inspiration* wakishirikiana na wadau mbalimbali; yote hayo ni majukumu mbalimbali ambayo *TFF* imekuwa ikiyasimamia na sisi kama Taifa kujitahidi kukuza masuala ya mpira.

Sasa suala la kushughulikia migogoro, kama *TFF* ni muhimu pia washughulikie migogoro. Migogoro ikiendelea katika masuala ya mpira basi itashindikana kabisa kukuza masuala ya mpira. Kwa hiyo ni kiasi tu cha kujiweka sawasawa na wadau na wale ambao wanahusika na masuala ya mpira kuhakikisha

kwamba migogoro hailipi, bali inavunja maendeleo yetu ya mpira.

**NAIBU SPIKA:** Tulitendee haki swali la mwisho kwa siku ya leo. Kama mnavyoona muda wetu Waheshimiwa Wabunge, kuna jibu la nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo, kwanza, napenda nipongeze majibu mazuri ya Naibu Waziri. Pili, ningependa kutoa maelezo ya nyongeza kama ifuatavyo:-

Swali la kwanza lilihusu kwa nini Bara inatumia neno Tanzania. Nataka niseme kwamba, kampuni nyingi sana huku Tanzania Bara, tunatumia neno la Tanzania kwa sababu sisi tumeshaachana na neno Tanganyika. Kikubwa, mtuelewe tu kwamba kutumia hili jina ni kwa ridhaa kati ya *ZFA* na *TFF*; hakuna mgogoro wowote baina ya *ZFA* na *TFFA* juu ya utumizi wa hili jina.

Lingine ni nyongeza; yapo maelewano ya kutosha baina ya *TFF* na *ZFA*. Ninakubali huko nyuma palikuwa na kutokuelewana kipindi fulani, Serikali ikafanya jitihada tukawakusanya wenyewe wakaunda Kamati ya Pamoja ya Wajumbe wa pande zote mbili Bara na Zanzibar wakamaliza tofauti zilizokuwepo.

La pili, kwamba *TFF* na *ZFA* kwa pamoja tuliwahi kupeleka ujumbe *FIFA* kwenda kudai au kwenda kupeleka rai kwamba *ZFA* nayo ikubaliwe kuwa Mwanachama wa *FIFA.* Kazi hii tumeifanya pamoja *TFF* na *ZFA.*

Lingine, kwa taarifa ya Bunge lako Tukufu, *TFF* kwa kutambua kwamba, *ZFA* hawawezi kupata misaada *direct* kutoka *FIFA* na kwa kutambua kwamba sisi ni nchi moja, pale

wanapopata misaada kutoka *FIFA* wanaipeleka Zanzibar japokuwa *ZFA* siyo Mwanachama wa *FIFA;* mfano ni fedha iliyopatikana kwenda kukarabati Uwanja wa Michezo Gombani Pemba, zilitolewa *ZFA* kutoka *FIFA.*

*TFF* baada ya kupokea zile fedha kutoka *FIFA* wakaamua kuwapa ndugu zao wa Zanzibar, tukashirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, ukakarabatiwa Uwanja wa Michezo Gombani Pemba.

Kwa hiyo, hata Makamisaa wanaochaguliwa na *TFF* kwenda kufanya shughuli mbalimbali kwa niaba ya nchi yetu, wanachaguliwa kutoka pande zote mbili za Muungano japokuwa *ZFA* bado haijawa Mwanachama wa *FIFA.* Msimamo wa *TFF* ni kuendelea kuungana na wenzetu wa Zanzibar kudai Uanachama wa *FIFA* kwa sababu Zanzibar ikipata Uanachama wa *FIFA,* ile misaada itaongezeka na manufaa katika nchi yetu yatakuwa makubwa kuliko ilivyo sasa.

**T A A R I F A**

**MBUNGE FULANI:** Taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Baada ya kipindi cha maswali nitapokea taarifa. Swali la mwisho kwa siku ya leo linaelekezwa Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa.

Na. 96

**Janga la Njaa kwa Nchi za Pembe ya Afrika**

**MHE. MASOUD ABDALLA SALIM (K.n.y. MHE. SALIM HEMED KHAMIS)** aliuliza:-

Nchi za Pembe ya Afrika zimeathiriwa sana na ukame na njaa ambao haujawahi kutokea katika kipindi cha miaka 60 iliyopita:-

Je, kaulimbiu inayosema "Afrika Moja, Sauti Moja dhidi ya Njaa" inatafsiriwa vipi kwa vitendo ili kukabiliana na janga hili?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salim Hemed Khamis, Mbunge wa Chambani, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Nchi za Afrika, chini ya Umoja wa Afrika, zimeendelea na jitihada zake kwa kutafsiri kwa vitendo kaulimbiu ya "Afrika Moja, Sauti Moja dhidi ya Njaa". Mwitikio huu wa Nchi za Afrika na Jumuiya za Kimatifa ulitokana na hali mbaya ya balaa la njaa iliyozikumba nchi za eneo la Pembe ya Afrika mwaka jana. Nchi hizo ni Eritrea, Jibuti, Somalia na Kenya. Kwa mujibu wa Umoja wa Mataifa, watu milioni 12.5 waliathiriwa na janga la njaa na kati ya hao milioni tatu na laki sita ni Wasomali. Aidha, hadi kufikia Desemba, 2011 watu sita walikuwa wanakufa kila siku; kati ya hao watano ni watoto wadogo. Gharama za kukabiliana na janga hilo la njaa na matatizo na athari zake zilihitajika kiasi cha dola bilioni 2.48 ili kununua chakula, madawa, maji na huduma nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, tarehe 25 Agosti, 2011, Umoja wa Afrika ulichukua hatua ya kuitisha Mkutano Maalum wa Wakuu wa Nchi Wanachama wa Umoja huo ili kujadili na kusaidia kutatua janga hilo la njaa. Mkutano huo ulifanikiwa kutoa ahadi za kuchanga kiasi cha dola 350 milioni. Hadi mwezi Februari, 2012 wakati wa Mkutano wa Kimataifa kuhusu Somalia uliofanyika Mjini London, Jumuiya ya Kimataifa ilikuwa imechangia Dola za Kimarekani 1,480,000,000 na hivyo kuwepo na upungufu wa bilioni moja kama bakaa. Tanzania iliahidi kuchangia kiasi cha Dola za Marekani 200,000 na tani 300 na tumeendelea kushawishi Mataifa mengine kuchangia kila tunapopata fursa ya kukutana nao huko nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kuwa, Tanzania chini ya mwavuli wa *SADC*, inatazamia kusafirisha chakula hicho cha msaada wakati wowote kuanzia sasa baada ya meli ya Afrika Kusini, itakayobeba vyakula vya msaada kutoka Nchi za *SADC* itakapotia nanga nchini kuchukua shehena hiyo. Zoezi hilo lilichelewa kutokana na hali ya usalama kwenye Bahari ya Hindi, Pwani ya Somalia, ambayo kwa sasa imetengemaa kutokana na vitendo vya kiharamia.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina maswali mawili kama ifuatavyo:-

(i) Kwa kuwa Mheshimiwa Waziri amesema kwamba Serikali inatarajia kusafirisha chakula hicho haraka inavyowezekana kupeleka katika nchi ambazo zimeathirika; na kwa kuwa mara nyingi humu ndani Waheshimiwa Wabunge wamekuwa wakilalamika kwamba katika maeneo yao kuna njaa lakini uharaka huo haupatikani: Je, ujasiri huo wa Serikali kupeleka chakula cha msaada kwa nchi za jirani au nchi za nje na wakati sisi wenyewe hatupeleki kwa haraka utaendelea kwa Watanzania waliokumbwa na njaa?

(ii) Ahadi ni deni; mmeahidi kupeleka dola 200,000; ni lini mtazipeleka hizo kunakohusika?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu Spika, jukumu la Wizara ya Mambo ya Nje ni kusafirisha chakula kama miongoni mwa Nchi za *SADC* kukipeleka Somalia meli itakapopiga nanga na wala siyo kwamba tumeharikisha sana; ahadi hii ilitolewa karibu miezi sita iliyopita lakini kutokana na hali ya uharamia kwenye Bahari ya Hindi, Serikali ilishindwa kukisafirisha kwa wakati lakini tutafanya hivyo.

Inapofika humu ndani kwenye maeneo ambayo yamebanwa na balaa la njaa, Wizara ya Kilimo na Wizara

inayohusika na mabalaa ya aina hiyo kama ya njaa, zitakuwa zinafanya kazi zake vizuri kuhakikisha kwamba chakula kwenye maeneo ya balaa hilo la njaa kinafika kama sisi Wizara ya Mambo ya Nje tunavyotaka kukisafirisha chakula hicho kukipeleka Somalia.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Maswali mawili ya mwisho kabisa ya nyongeza yataulizwa na Mheshimiwa Blandes na Mheshimiwa Hamad Rashid.

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Kumbe kulikuwa na swali la pili!

**NAIBU SPIKA:** Lilikuwepo la pili?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Tulikuwa tumeahidi kuchanga dola 200,000, tunamsubiri Waziri wa Mambo ya Nchi za Nje wa Somalia, ambaye ameahidi kuja kuzikusanya hizo pesa na mara atakapofika tutampatia pesa hizo.

**MHE. GOSBERT B. BLANDES:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa mara nyingi inapotokea janga la njaa katika nchi jirani hasa Sudan, Kenya na hata na Somalia, wakati huo wananchi hususan wa Mkoa wa Kagera na hasa Karagwe, wanakuwa na chakula cha kutosha na cha ziada lakini hawaruhusiwi kuwauzia wananchi wa nchi hizo ambazo zimeathirika. Je, Serikali inatoa kauli gani kwa Wananchi wa Mkoa wa Kagera kupeleka vyakula kama hivyo inapotokea janga la njaa?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA KIMATAIFA:** Mheshimiwa Naibu spika, ni kweli kabisa kwamba, kwa takwimu zilizotolewa na ukweli ulipo ni kwamba, katika nchi zote za Afrika Mashariki na zile za kwenye Pembe ya

Afrika, nchi pekee ambayo ilikuwa na unafuu wa chakula katika msimu wa mwaka 2011/2012 ni Tanzania. Tulishazalisha zaidi na tunadhani kwamba tutazalisha zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani ni suala la utaratibu tu, kama tunavyotambua ni kwamba, wenzetu majirani wakipata majanga ya njaa, wananchi wetu wanao wajibu wa kuwasaidia. Ninadhani ni suala tu la utaratibu wa Serikali pamoja na mikoa inayohusika, kujipanga na kujaribu kufumba macho kwa nchi jirani zinazoathirika. Kwa sababu ni tatizo la kweli na kwa kauli hii suala hili nadhani Serikali tutalifanyia kazi kwa kuwasiliana na wenzetu wa mikoa ya jirani ili pale inapotokea kama kweli kuna janga la aina hii ambalo linawaathiri wenzetu, Serikali ichukue hatua ya kuweza kupeleka chakula kwenye nchi jirani zinazoathirika na chakula na tulikuwa tunafanya hivyo nyuma na sioni kwa nini tusiendelee kuwa na utaratibu huo.

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na tathmini iliyofanywa na Jumuiya za Kimataifa juu ya *NDGs,* moja ambalo limeonekana ni athari za maafa mbalimbali yanayotokea. Tumejaribu miradi ya maendeleo inayogharimu kama shilingi trilioni tatu katika kipindi cha miaka kumi iliyopita. Mkutano wa Istanbul juu ya *risk reduction measures* uliamua kwamba kutengenezwe *guidelines* ambazo zitasaidia nchi mbalimbali kupunguza hizi *risk* kutokana na maafa mbalimbali yakiwemo ya njaa, mafuriko na kadhailika. Lini Tanzania itatupatia hizo *guidelines* ili kupunguza haya maafa ambayo yanaweza kupunguzwa na athari zake zikasaidia hasa katika kusaidia miradi ya maendeleo?

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kabisa kwamba katika tathmini ya *Millennium Development Corporation,* miradi yote ya maendeleo itafanyiwa marekebisho na itatathminiwa kwenye *RIO + 20* na mkutano ambao utafanyika Brazil hivi karibuni. Kwenye tathmini ile inayokwenda ambayo Tanzania

tutakuwa sehemu ya *MDG,* Tanzania pamoja na nchi zote za Kusini zitakuwa zinapeleka *paper* ya kujadili maafa au *risk* kama ilivyosemwa, zinazohusu mabadiliko ya hali ya hewa, balaa la njaa na balaa nyingine yoyote ambayo imejitokeza. Kwenye *Millennium Development* tunategemea kutoa tathmini ya kushauri nchi maskini au nchi zinazoendelea, juu ya kitu kinachoitwa *mitigating factors,* yaani namna ya kuzuia na namna ya kujikimu na balaa.

Moja ya mapendekezo tunayoyapeleka kwenye Mkutano wa Millennium na huo ambao utakuwa Brazil ni kupendekeza kwa nchi zile ambazo zina-*draught,* yaani balaa ya kutokuwa na mvua kuwa na mazao yanayostahimili ukame. Orodha ya bidhaa hizo au vyakula hivyo vinavyoweza kustahimili ukame itapelekwa ili kusaidia wenzetu na kuwaambia wajihusishe na kupanda mazao yanayoweza kustahimili ukame kama vile viazi au mihogo. Pamoja na mapendekezo mengi sana ambayo yatasaidia nchi hizi kujaribu kujikinga na balaa mbalimbali na hivyo hivyo kwa kesi ya matetemeko yanayoweza kutokea, hivyo hivyo kwa kesi ya mawimbi ya bahari yanayoweza kuvimeza visiwa vidogo vidogo. Kwa hiyo, mapendekezo yote haya yatakwenda Brazil na kule yatakwenda kutolewa tathmini na baada ya kujadiliwa na kukubalika pale Tanzania itatoa taarifa ya mapendekezo ya namna ya kujiamini dhidi ya matatizo mbalimbali yatakayokuwa yamejadiliwa na dunia ili kuweza kuwawezesha wananchi wetu kuyafuata bila tatizo la aina yoyote.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Idd Azzan ile taarifa.

**MHE. IDDI MOHAMED AZZAN:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii. Ninataka kutoa taarifa tu hasa kuhusu swali namba 95, ambalo liliulizwa na Mheshimiwa Ahmed Juma Ngwali. Mheshimiwa Waziri alijibu katika majibu yake kwamba, Timu ya Taifa ya Tanzania, imechukua Ubigwa wa Afrika Mashariki mara tano, *Challenge Cup*, halafu

akasema Simba na Yanga zimechukua Ubigwa wa Afrika Mashariki mara moja moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, majibu haya siyo sahihi kwa sababu Simba imechukua Ubigwa wa Afrika Mashariki mara sita, Yanga imechukua Ubigwa wa Afrika Mashariki mara tano, Timu ya Taifa ya Tanzania imechukua mara tatu *Challenge Cup;* mwaka 1974, 1994 na mwaka 2011. *(Makofi)*

Kwa hiyo, nilikuwa naomba kutoa taarifa hiyo na nimesikitika kwa majibu ambayo amekuja nayo labda hakuyafanyia uchunguzi wa kina.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba kutoa taarifa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana kwa taarifa hiyo na hapo ndiyo mwisho wa kipindi chetu cha maswali kwa siku ya leo. Sasa wageni walioko Bungeni asubuhi ni wageni wa Mheshimiwa Devota Likokola, ambao ni Sister Alufone Kunegunda Muhagama kutoka Shirika la Waenezi wa Injili wa Roho Mtakatifu kutoka Kenya. Karibu sana Sister, ambaye naambiwa ni dada yake wa Mheshimiwa. *(Makofi)*

Pia yupo Ndugu Monica Ngenzi Mbega, Mbunge Mstaafu na Mwenyekiti wa Bodi ya Vikoba Tanzania. Mheshimiwa Monica Mbega, alikuwa Mbunge mwenzetu hapa na amekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro na sasa ni Mwenyekiti wa Bodi ya Vikoba Tanzania; karibu sana. *(Makofi)*

Wageni wa Waheshimiwa Wabunge ni pamoja na wageni wanne wa Mheshimiwa Catherine Magige, wakiongozwa na Mheshimiwa Anna Agatha Msuya, Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arumeru. Ahsante sana Anna Agatha Msuya, Makamu wa Mwenyekiti wa Halmashauri ya Arumeru, kuna wengine wanajiuliza huyu ni kutoka Chama cha Mapinduzi. *(Makofi)*

Wageni waliopo kwa ajili ya mafunzo ni wanafunzi 20 wa Shahada ya Uzamili wa Fasihi ya Kiswahili kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma *(UDOM).* Karibuni sana wanafunzi wa *UDOM* mliokuja kututembelea. Ninyi ni majirani zetu, kila mkipata nafasi karibuni sana na tunafurahi sana tunapoona Chuo cha *UDOM* kipekee kabisa kinatoa umuhimu wa kipekee kwa somo la Kiswahili ambalo litatuwezesha kutoa Wataalam wa Kiswahili watakaotumika siyo nchini tu lakini hata nje ya nchi yetu. Karibuni sana vijana wetu.

Kwa hatua hii, niwaombe Waheshimiwa Wabunge, ambao hamjatembelea Chuo Kikuu cha Dodoma ni vizuri kufanya hivyo kabla ya kuondoka katika kipindi hiki cha Bunge. Kweli kabisa ningewasihi kutembelea na kuona baadhi ya hivi vitu ambavyo tunavyo katika maeneo yetu; ni chuo cha kujivunia kabisa.

Pia tuna wanafunzi 72 wanaosoma Shahada ya Elimu katika Saikolojia kutoka Chuo Kikuu cha Dodoma. Hawa ni Shahada ya Elimu katika Saikolojia; karibuni sana kama nilivyowaambia wenzenu, Chuo Kikuu cha Dodoma tunakitegemea sana katika kujikita katika kutoa waatalamu wetu wengi sana katika Sekta ya Elimu. Tunawakaribisha sana na tunawapenda. *(Makofi)*

Pia tuna Maafisa wanne kutoka Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar wakiwa wameambatana na Maafisa wanne kutoka TAMISEMI; hii imeandikwa namna gani? Karibuni sana.

Wageni watatu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wakiongozwa na Ndugu Jason Ishengoma; karibuni sana wageni wetu kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Naomba niwatambulishe wageni wa Mheshimiwa Dkt. Titus Kamani, ambao ni wanafunzi 15 kutoka Chuo Kikuu cha

Tiba cha Bugando. Karibuni sana wanafunzi kutoka Bugando Mwanza.

Pia wapo wageni wa Mheshimiwa Said Mtanda, ambao ni Bwana na Bibi Rwegasira; karibuni sana.

Wapo pia wageni wa Mheshimiwa Capt. Mstaafu George Mkuchika, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), ambao ni Ndugu Naumi Ramadhani Pandu, ambaye ni Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Zanzibar. Sasa hii inafafanua vizuri zaidi; Naumi upo?

Ndugu Amour Khamis Bakar, Mkurugenzi wa Sera, Mipango na Utafiti Zanzibar, Ndugu Zuhura Salum Rashid, Afisa Serikali za Mitaa Zanzibar na Ndugu Juma Fhaki Juma, Afisa Mipango. *(Makofi)*

Pamoja na wageni hao kutoka Zanzibar wapo Maafisa wetu kutoka Ofisi yetu ya TAMISEMI Dodoma, naye ni Mkurugenzi wa Uratibu na Tawala za Mikoa, Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Ndugu Kairima Ramadhani, Mkurugenzi Msaidizi Uratibu Tawala za Mikoa Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Susan Chekani, Afisa Utumishi Ofisi ya Waziri Mkuu, Ndugu Beatrice Kilometa na Afisa Tawala Ofisi ya Waziri Mkuu (TAMISEMI), Ndugu Asifiwe Makwetta. Karibuni sana. *(Makofi)*

Matangazo ya vikao ni kwamba, Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Katiba, Sheria na Utawala, Mheshimiwa Pindi Chana, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane leo katika Ukumbi Namba 219, Jengo la Utawala, baadaye saa saba mchana.

Mheshimiwa Abdallah Kigoda, Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha na Uchumi, anawaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane Ukumbi Namba 227; wao wamepewa ruhusa

wakutane Ukumbi huo 227, saa tano na nusu, kuna jambo la dharura kidogo.

Mheshimiwa Lediana Mng'ong'o, Mwenyekiti wa Kamati ya Masuala ya UKIMWI, anawaomba Wajumbe wa Kamati yake wakutane katika Ukumbi wa Pius Msekwa C, saa saba mchana.

Mheshimiwa Mahmoud Mgimwa, Mwenyekiti wa Kamati ya Viwanda na Biashara, anaomba Wajumbe wa Kamati hiyo wakutane saa saba mchana katika Ukumbi wa Basement.

Mheshimiwa Angellah Kairuki, anawaomba Wajumbe wote wa *TWPG* kuwa leo saa saba mchana, *New Dodoma Hotel* kutakuwa na Semina ya Waheshimiwa Wabunge Wanawake wote juu ya nafasi ya Wabunge Wanawake katika kujenga mshikamano na Umoja wa Kitaifa ili kudumisha amani na utulivu wa nchi yetu Tanzania. Semina hii imeandaliwa na Shirika lisilo la Kiserikali la *Registered Trustee of the Community Development,* lenye Makao Makuu Jijini Dar es Salaam. Wabunge wote mnaombwa kuhudhuria semina hiyo fupi kwa manufaa ya Taifa letu. Itifaki zote za semina zimezingatiwa. Wabunge wanaume walikuwa wanauliza kwamba nao wanaalikwa kidogo angalau kusimamia semina? (*Kicheko*)

Nimepata taarifa kutoka kwa Mheshimiwa Idd Azzan na Mheshimiwa Mariam Kissangi kwamba, ndugu yetu na Mbunge mwenzetu, MheshimiwaAbbas Mtemvu, amepata ajali mbaya Morogoro, saa 12.15 leo asubuhi, ambapo gari lake limegongwa na lori na kupinduka na gari limeharibika vibaya. Tunashukuru Mungu kwamba, Mheshimiwa Abbas Mtemvu na dereva wake, wamepata matibabu Morogoro wapo salama na sasa hivi wanaelekea Dar es Salaam kwa ajili ya kuangalia afya zao vizuri zaidi. Wamepata majeraha kiasi, tuendelee kuwaombea ili wapate nafuu.

Naomba nimsimamishe Mheshimiwa Henry Shekifu. Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Henry Shekifu ametuletea ofisini hati zinazosomeka ifuatavyo: *"The California State Christian University has conferred upon Henry Shekifu in formal recognition of understand ability, achievements and influence in his devoted service to humanity, the Honorary Degree of Doctor of Philosophy in Humanity."* Kwa hiyo, ninamtambulisha rasmi kwenu Waheshimiwa sasa kwamba tuendelee kumtambua Mheshimiwa Henry Shekifu kwamba ni Dkt. Henry Shekiffu. Kwa niaba ya Waheshimiwa Wabunge wote, naomba kukupongeza sana kwa heshima hiyo. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, wakati tunaendelea na kikao cha asubuhi hii, kulikuwa na mvua inaendelea huko nje na baadhi ya maeneo yamekuwa yanapata matatizo ya *leakage,* tume-*take note* ya jambo hili. Niwahakikishie kabisa kwamba, taarifa zimeshapelekwa *TBA,* ambao ndiyo wanaohusika na jengo hili. Kama mnavyojua, masuala ya ukarabati wa jengo hili mpaka sasa bado hayapo chini ya mikono ya Bunge, yaani yapo Serikalini.

Kwa hiyo, tumepeleka taarifa *TBA* ili kwa haraka iwezekanavyo marekebisho yafanyike ili pasiendelee kutokea uharibifu kwenye viti vyetu na *microphones* kutokana na *leakage* inayotokea katika baadhi ya maeneo kwenye paa letu.

Katibu, hatua inayofuata.

## MWONGOZO WA SPIKA

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, endelea Mheshimiwa Kangi.

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru.

Naomba mwongozo wako chini ya Kanuni ya 68(7), inayosema: "Hali kadhalika Mbunge anaweza kusimama wakati wowote ambapo hakuna Mbunge mwingine anayesema na kuomba mwongozo wa Spika kuhusu jambo ambalo limetokea Bungeni mapema ili Spika atoe ufafanuzi kama jambo hilo linaruhusiwa au haliruhusiwi kwa mujibu wa kanuni na taratibu za Bunge na majibu ya Spika yatatolewa papo hapo au baadaye kadiri atakavyoona inafaa."

Mheshimiwa Naibu Spika, jana wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, anajibu swali la *TBS* lililouliza kwa nini hawajachukua hatua kwa Mtendaji Mkuu wa *TBS,* Ndugu Ekelege, alisema kwamba, anashukuru taarifa ya *CAG* imeshafika ofisini kwake na kwamba inafanyiwa kazi. Baadaye Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara aliposimama kutoa majibu ya nyongeza kwa nini hajachukua hatua, alisema kwamba, hawezi kuchukua hatua kwa sababu Ripoti ya *CAG* hajaiona na haijafika kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, na leo pia wakati Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara anajibu maswali hayo hayo ya *TBS,* ameendelea kusema kwamba, Ripoti ya *CAG* imeshatoka na hivyo inawezekana leo tukaendelea kuzungumzia hayo mambo. Sasa nashindwa kuelewa huko *TBS* kuna nini kauli mbili za Serikali zinapingana! Naomba mwongozo wako; Bunge hili na heshima yake lichukue kauli ya nani; ya Waziri au Naibu Waziri? Naomba mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante, tutalitolea mwongozo wake. Mheshimiwa *Chief Whip.*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli jana Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara, alisimama na sisi tumesikia majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri na nimesikia vilevile hoja ya Mheshimiwa Nyerere ndiyo maana ninaye hapa. Nilikuwa napata ufafanuzi aliousema ingawa utatoa

mwongozo wako lakini nataka nikuahidi kwamba, Ofisi ya Waziri Mkuu itakusanya vielelezo vyote hivi na maelezo yote ya wahusika na kuyatolea taarifa hapa Bungeni. *(Makofi)*

Naomba tuachiwe Ofisi ya Waziri Mkuu, tutafanya kazi ya kuja kutoa taarifa ya uhakika baada ya kupata nyaraka zote hizo na bahati nzuri nyaraka ambazo Mheshimiwa ame-*volunteer* kutupa alikuwa ananipa maelezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba utupe muda. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Chief Whip* ni katika Bunge hili, yaani katika Mkutano huu wa Bunge au?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Toa mwongozo wako lakini mimi nimeahidi tutaleta taarifa.

**WABUNGE FULANI:** Lini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Nilichoomba ni kwamba, kutokana na mkanganyiko wa majibu na kutokana na vielelezo hivi inaonekana watu wengi wanajua hii habari siyo Taarifa ya *CAG* peke yake.

Hapa kuna Taarifa ya *CAG* lakini kuna watu binafsi ambao wana maelezo tofauti na ya ziada, mojawapo ni Mheshimiwa Mbunge ambaye yuko hapa naye ana maelezo ya ziada ya Taarifa za *CAG*. Ofisi ya Waziri Mkuu itakusanya taarifa zote hizo na kuja kutoa taarifa ya uhakika hapa Bungeni.

**WABUNGE FULANI:** Lini?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Naomba kwa heshima yako utupe muda tuje tutoe Bunge lijalo.

**WABUNGE FULANI:** Aaah!

**MWONGOZO WA SPIKA**

**MHE. PETER J. SERUKAMBA**: Mwongozo wa Spika.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Taarifa ya Mwenyekiti wa Kamati.

**NAIBU SPIKA:** Sijakupa nafasi, kuna mtu alisema mwongozo? Mheshimiwa Peter Serukamba.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, mwongozo wa Spika, Kanuni ya 68.

Ambacho Mheshimiwa Kangi Lugola ameuliza ilikuwa ni suala rahisi sana; ameuliza tuamini kauli ya nani; ya Naibu Waziri ama ya Waziri? Kwa hiyo, nilitegemea *Chief Whip* angekuja kutuambia tuamini kauli ya nani. Ndiyo kilichoulizwa hapa lakini maelezo hayo mengine yote angeyaleta baadaye.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto Kabwe.

**MHE. KABWE Z. ZITTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni za Bunge, Bunge lako Tukufu limeipa majukumu Kamati yangu kushughulikia masuala yote yanayoshughulika na masuala ya umma na suala ambalo limekuwa likizungumzwa hapa jana na leo, Kamati yangu imekuwa ikilifanyia kazi kwa takriban miezi minane sasa. Niliunda Kamati Ndogo ambayo ilifanya kazi na ilikamilisha Taarifa yake tukaiwasilisha kwa Spika na Spika tayari ameifikisha Taarifa ile ofisi ya Waziri Mkuu kwa maelekezo ya Kibunge.

Ninaomba Serikali ilete taarifa ya utekelezaji kwa maelezo ambayo Spika ameyapeleka Ofisi ya Waziri Mkuu ili jambo hili liweze kwisha kwa sababu linachukua muda mrefu bila sababu yoyote ya msingi, linaipotezea muda Taifa.

Kwa hiyo, Waziri wa Nchi, atakapokuwa analeta Taarifa yake na ninaomba kwa sababu leo tutajadili Taarifa za Kamati za Kifedha za Bunge, Kamati ya *PAC* imeshughulikia jambo hili na Kamati ya *POAC* imeshughulikia jambo hili pia. Kwa hiyo, ni vizuri Serikali ikajiandaa kwamba ikatoa taarifa yake ndani ya kipindi hiki na ndani ya mkutano huu ili jambo hili tuweze kulimaliza mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, ahsanteni sana. Niseme kwamba, bado mtuachie jambo hili, Meza tutalichukulia kwa umuhimu wake baada ya kuwa tumezungumza na upande wa Serikali kwa sababu ni jambo ambalo linatuchukulia muda bila sababu za msingi sana. Kwa hiyo, ahadi yangu ni kwamba, nitamfahamisha Mheshimiwa Spika na kwa pamoja tutajitahidi sana katika kipindi cha Bunge hili jambo hili lipate jawabu ambalo linaeleweka vizuri zaidi siyo kwa Wabunge tu lakini vilevile kwa Wananchi wa Tanzania, kwa sababu ni jambo ambalo linatupaka matope bila sababu hata moja. *(Makofi)*

Katibu, tuendelee.

## HOJA ZA KAMATI

### Kamati ya Hesabu za Serikali *(PAC)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama *Order Paper* yetu inavyoonesha kwamba leo tuna mawasilisho ya Kamati zetu tatu; tutaanza na Kamati ya Hesabu za Serikali ya Mheshimiwa Cheyo, itafuata Kamati ya Serikali za Mitaa ya

Mheshimiwa Daktari Lyatonga Mrema na tutamalizia na Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma. Kila Mwenyekiti nitampa nusu saa kuwasilisha taarifa ya Kamati yake.

Waheshimiwa Wabunge, lakini niwaambie mapema kwamba, wamejiorodhesha wengi kweli kuchangia taarifa hizi tatu, mpaka sasa hivi ninavyoongea na ninyi wamejiandikisha Wabunge 53 kuchangia, jambo ambalo ni jema na la afya tu pia ni jambo zuri. Kwa jinsi hiyo, Meza imepanga kwamba, mjadala wa Kamati hizi utaendelea kama ambavyo imekuwa ada siku za nyuma, tutaufanya kwa siku mbili, yaani leo na kesho. (*Makofi*)

Moja kwa moja sasa naomba nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali.

**MHE. JOHN M. CHEYO – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Ibara ya 96(1) na (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na kwa kuzingatia kifungu cha 114(15) cha Kanuni za Bunge, Toleo la Mwaka 2007, naomba kuwasilisha Taarifa ya kazi za Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kipindi kilichoanzia Aprili, 2011 hadi Aprili, 2012. Aidha, katika kipindi hicho Kamati ilijadili Hesabu za Serikali za mwaka wa fedha wa 2009/2010.

Mheshimwa Spika, Kamati hii hujadili Hesabu za Serikali kwa kuzingatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ambayo huwasilishwa Bungeni mwezi Machi kila mwaka kwa kuzingatia Sheria ya Fedha *(Public Finance Act No.6)* kama ilivyorekebishwa Mwaka 2004, ambayo inasisitiza kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu hufanya kazi yake ya ukaguzi wa Hesabu kwa niaba ya Bunge. Naomba kununukuu kifungu Na. 31(1) cha sheria hiyo:-

*"The Controller and Auditor General shall on behalf of the National Assembly examine, inquire into and audit the*

*accounts submitted to him under section 25 of this Act and perform any other functions which he is authorized to perform by or under this Act."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimwa Spika, aidha, Sheria ya Ukaguzi wa Umma *(The Public Audit Act, 2008)* inatoa pia madaraka kwa Kamati za Bunge za Kiuchunguzi, kwa niaba ya Bunge zima, kujadili Taarifa za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na kisha Kamati hizo kutoa Taarifa zake Bungeni. Naomba kunukuu kifungu cha 38(1) na (2) cha Sheria hiyo kama ifuatavyo:-

"38 (1) *The Public Accounts Committee, Local Authority Accounts Committee, Parastatal Organisations Committee shall discuss the reports of the Controller and Auditor General after they have been tabled in the National Assembly.*

*(2) Upon the completion of hearing the Parliamentary Oversight Committees shall prepare and submit to the National Assembly reports which may include comments and recommendations."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijawasilisha taarifa ya Kamati, naomba nitumie fursa hii kuwashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu ambao uliwateua kwa mujibu wa Kanuni ya 113(3) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, kwa ushirikiano wao na kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kipindi chote cha mwaka mmoja. Aidha, niseme kwamba ni jambo la kushukuru sana kuwa na Wajumbe wenye moyo wa kujitolea usio na kikomo, wepesi wa kuelewa mambo, ushirikiano wa dhati na uadilifu wa kuigwa kama unaoonyeshwa na wajumbe wa Kamati hii. Hivyo basi, kwa heshima kubwa naomba kuwatambua kwa kuwataja majina kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa John Momose Cheyo, Mwenyekiti; Mheshimiwa Zaynab Matitu Vulu, Makamu Mwenyekiti;

Mheshimiwa Asha Mshimba Jecha, Mheshimiwa Lucy Fidelis Owenya, Mheshimiwa Yahya Kassim Issa, Mheshimiwa Ali Keisy Mohamed na Mheshimiwa Hezekiah Ndahani Chibulunje, Mheshimiwa Dunstan Daniel Mkapa, Mheshimiwa Mhonga Said Ruhwanya, Mheshimiwa Abdul Jabir Marombwa, Mheshimiwa Vincent Josephat Nyerere, Mheshimiwa Thuwayba Idriss Muhamed, Mheshimiwa Mendrad Lutengano Kigola, Mheshimiwa Stephen Julius Masele na Mheshimiwa Faida Mohamed Bakari. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati kwa mujibu wa Nyongeza ya Nane, Fasili ya 11 chini ya Kanuni ya 115(2) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2007, majukumu ya kikanuni ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ni haya yafuatayo:-

(a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali yaliyoainishwa katika taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

(b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali; na

(c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Wizara za Serikali kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa msingi wa kanuni hii kila Afisa Masuhuli anawajibika kufika mbele ya Kamati ya *PAC* na kutetea utekelezaji wa bajeti ya fungu lake na ikionekana kuna matumizi mabaya ya fedha, basi huweza kuadhibiwa kwa kuzingatia Kanuni zilizotengenezwa na Waziri wa Fedha chini ya Sheria ya Fedha *(Public Finance Act, No.6 of 2001),* Sehemu ya Pili zikieleza uwajibikaji wa Maafisa Masuhuli kwa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)*, nanukuu:-

*"Every Accounting Officer shall be personally and pecuniary responsible and accountable for the collection and receipt of all revenue or for all disbursements of expenditure in his vote, and shall be answerable to the Public Accounts Committee (PAC)."*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu iliendelea kutekeleza majukumu haya kwa kuzingatia Kanuni na Sheria zote zinazosimamia matumizi ya fedha za umma. Tunaishukuru Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kushirikiana vizuri na Kamati, na vilevile kwa kuandaa mafunzo mahsusi kwa Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati zinazosimamia fedha za umma yaliyokuwa na lengo la kuwajengea uwezo wa kuhoji na kutoa ushauri kwa Serikali kwa kuzingatia mapendekezo yaliyotolewa kwenye Taarifa za Ukaguzi wa Thamani *(Value for Money Audit Reports)* ambazo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameanza kuzitoa. Aidha, mpaka sasa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ametoa taarifa saba za ukaguzi wa thamani na Kamati ya *PAC* imeijadili taarifa tatu kati ya hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati vile vile inapenda kumshukuru Mhasibu Mkuu wa Serikali kwa kuandaa mafunzo ya *"IPSAS (Accrual Basis of Accounting)"* kwa ajili ya Waheshimiwa Wajumbe wa Kamati yangu. Mafunzo yaliyokuwa na lengo la kuwaelimisha Waheshimiwa Wajumbe kuhusu matumizi sahihi ya Kanuni za kihasibu za Kimataifa katika ufungaji wa Hesabu za Serikali yaani *"IPSAS – Accrual Basis of Accounting"* ambazo zinategemewa kuanza kutumika katika ufungaji wa Hesabu za Serikali Kuu. Aidha, mpaka sasa bado Hesabu za Serikali Kuu zinafungwa kwa kutumia *"IPSAS – Cash Basis of Accounting"*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ili kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi, Kamati yangu inalazimika kufanya ziara za kikaguzi katika maeneo kadhaa yenye ulazima ili kuweza kupima ufanisi

wa matumizi ya fedha za umma. Kwa kufanya hivyo, Kamati inakuwa katika nafasi nzuri ya kusimamia matumizi ya fedha za umma hasa kwenye miradi pamoja na upatikanaji wa tija katika matumizi hayo. Aidha, pamoja na Kamati yangu kufanikiwa kutembelea na kukagua baadhi ya miradi inayosimamiwa na Wizara mbalimbali bado mpaka sasa tunakabiliwa na changamoto ya kushindwa kwenda kukagua Balozi zetu hasa kwa zile ambazo zimeonesha kuwa na matumizi mabaya ya fedha au miradi kushindwa kutekelezwa kutokana na sababu mbalimbali. Hivyo, Kamati yangu inaendelea kusisitiza umuhimu wa kuwezeshwa kifedha ili iweze kwenda kukagua Balozi hizo hasa katika mwaka wa ukaguzi unaofuata.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii ina sehemu sita yaani, sehemu ya kwanza ni utangulizi, sehemu ya pili ni masuala ya ujumla yatokanayo na ukaguzi, sehemu ya tatu ni taarifa maalum kuhusu ukaguzi wa ubora wa magari na bidhaa zitokazo nje ya nchi. Sehemu ya nne ni mapitio ya baadhi ya mafungu na ziara za ukaguzi; sehemu ya tano ni maoni na mapendekezo ya Kamati na sehemu ya sita ni hitimisho.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nianze kwa kuwasilisha mambo ya jumla ambayo yamejitokeza wakati Kamati yangu ilipokuwa ikijadili mafungu mbalimbali ya Hesabu:-

| **Mwaka wa Fedha** | **2009/10** | **2010/11** | **2011/12** |
|---|---|---|---|
| Bajeti Nzima | 9,392,107,175, 984 | 11,609,557,000,000 | 13,526,000,000,000 |
| Fedha za Ndani zilizoidhinishwa kwenye Bajeti | 5,459,632,720,867 | 9,156,649,000,000 | 8,330,700,000,000 |
| % ya Bajeti Nzima | 58.2% | 78.8% | 61.6% |
| Fedha za Nje zilizoidhinishwa kwenye Bajeti | 3,932,474,455,117 | 2,452,908,000,000 | 5,195,300,000,000 |
| % ya Bajeti Nzima | 41.8% | 31.2% | 38.4% |

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, uwajibikaji katika matumizi ya fedha za wahisani (Parallel Accountability. Bajeti ya Serikali inategemea fedha za Wahisani kutoka nje kwa wastani wa asilimia 40 kila mwaka kama inavyoonekana kwenye jedwali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali huwajibika kwa Wahisani kutoka nje kwa kupitia utaratibu uliowekwa baada ya makubaliano ya pande zote mbili yaani Serikali *(the Excutive)* na Wahisani *(Development Partners)* ambao unahusisha Wahisani hao kupima ufanisi katika usimamizi wa fedha za Umma ikiwa ni pamoja na zile zinazotolewa na Wahisani, kwa kutumia vigezo vilivyowekwa *(Public Financial Management (PFM) Performance Measurement Indicators)* ambavyo Serikali haina budi kuvifikia kama ina lengo la kuendelea kupata fedha za Wahisani. Aidha, utaratibu huu ulioanzishwa na *"The Public Expenditure and Financial Accountability (PEFA) Initiative"* huishia kwa Wahisani hao kutoa *"PEFA Reports"* inayoonesha kiwango cha ufanisi wa mifumo ya Serikali inayosimamia matumizi ya fedha za umma kwa kuzingatia Sheria ya Fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfumo wa uwajibikaji unaokubalika duniani katika kusimamia matumizi ya fedha za misaada ni ule unaotumia Taasisi za ndani kama Bunge na Kamati zake pamoja na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kusimamia matumizi ya fedha hizo. Kwa upande wa Tanzania, *"The General Budget Support (GBS) Group"* ambao ndio wanaotoa kiasi kikubwa cha fedha za nje (Angalia Jedwali hapo chini), wamejaribu kufanya vikao na Kamati za Bunge zinazosimamia fedha za umma (*PAC, POAC and LAAC*) pamoja na Kamati ya Fedha na Uchumi. Kwa lengo la kutupa taarifa zinazohusu mapato na matumizi ya fedha za Wahisani ili Kamati hizi ziweze kusaidia katika kusimamia matumizi ya fedha hizo na vilevile kwa lengo la kulitaarifu Bunge sababu za fedha za Wahisani kuchelewa au kutotolewa.

| Mhisani *(External Assistance)* | Kiasi kilichotolewa mwaka 2009/2010 |
|---|---|
| General Budget Support | 1,212,101,028,546 |
| Basket Funds | 600,564,470,177 |
| Projects including D-Funds | 580,590,858,927 |
| **Jumla Kuu** | **2,393,256,357,650** |

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imekuwa hailishirikishi Bunge katika kujadili yaliyomo katika *"PEFA reports"* na kwa Bunge kukosa taarifa hizi kumezorotesha kwa kiasi fulani usimamizi wa matumizi ya fedha za umma na hivyo kufanya Bajeti kutotimiza malengo yaliyowekwa *(Unperforming Budget)*. Kamati inasisitiza kuwa ili tuweze kukamilisha mzunguko wa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ni muhimu kwa Serikali kushirikiana na Bunge katika kujadili hizi *"PEFA reports"*. Hivyo, Serikali ianzishe utaratibu utakaowezesha Wahisani kuwasilisha *"PEFA Reports"* kwa Bunge na kisha Bunge kufanya majadiliano na Serikali kuhusu taarifa hizo kwa lengo la kuondoa mapungufu yanayotukabili au kujitokeza katika mchakato mzima wa kuandaa, kutumia na kusimamia Bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) ni Ofisi ya Kikatiba kama inavyotamkwa katika Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Aidha, Sheria ya Ukaguzi wa Umma Na. 11 ya mwaka 2008 kifungu cha 13 kinarejea uhuru wa *CAG* na kifungu cha 24 (1) cha Sheria hiyo. Naomba kunukuu:-

*"The Controller and Auditor General shall employ, appoint, promote and control discipline of such number and categories of officers and employees of such qualifications as may be considered necessary to assist him in the performance of the functions, carrying on responsibilities and the exercise of his powers".*

Mheshimiwa Naibu Spika, kifungu kidogo cha (4) cha kifungu namba 24 kinasema: *"The Controller and Auditor General shall on advice of the relevant authorities, determine remuneration of officers appointed pursuant to subsection (1)."*

Mheshimiwa Naibu Spika, utekelezaji wa sheria zilizotajwa juu pamoja na mamlaka iliyotamkwa kikatiba na kisheria kama nilivyoeleza hapo juu hali halisi katika utekelezaji haiendani na matakwa ya Sheria ya Ukaguzi na kanuni zake. Moja ya vikwazo ni kifungu cha 24(2) cha Sheria ya Ukaguzi ambacho kinasema pamoja na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kupewa madaraka ya kuajiri, kwa mujibu wa kifungu 24(2) utekelezaji wa wajibu huo wa ajira ya watumishi utafanyika kufuatana na Sheria zinazotawala ajira ndani ya Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, zifuatazo ni athari ambazo *CAG* anazipata kwa kutokuwa huru katika masuala yahusuyo ajira ya Watumishi wa Ofisi yake:-

(a) Ofisi ya *CAG* kushindwa kuajiri Watumishi wa kutosha kila mwaka kukidhi mahitaji ya Ofisi na ya kazi kutokana na mawanda *(scope)* ya ukaguzi kupanuka siku hadi siku;

(b) Kushindwa kuwalipa Watumishi mishahara yenye kuvutia na yenye uwiano na kazi nzito na kubwa ya kudhibiti rasilimali za umma hivyo kukabiliwa na hatari ya kushindwa kuwavutia watumishi wazuri kwenye soko la ajira;

(c) Kushindwa kuwa na bajeti huru *(Independent budget)* inayokidhi mahitaji ya msingi kama vile kupanga mishahara bora ya wafanyakazi, kujenga majengo yake Dar es Salaam na kila Mkoa ili kuondoa mgongano wa maslahi na kuwafanya wakaguzi wawe *more objective* katika maamuzi yao; na

(d) Kushindwa kutimiza matakwa ya Taasisi Simamizi za Ukaguzi wa Umma *(Supreme Audit Institutions)* za Afrika na dunia *(AFROSAI-E* na *INTOSAI)* zinazotaka nchi wanachama kutekeleza masharti yaliyoridhiwa katika makubaliano ya Lima na Mexico ikiwa ni pamoja na lile la *CAG* kuwa na uhuru wa kutawala Ofisi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali amejitahidi sana kulifuatilia suala hili tangu mwaka 2009 kwa kuwasiliana na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhusu changamoto za Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi; Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuhusu mapendekezo ya Muundo Mpya wa Mshahara kwa watumishi wa Ofisi ya Taifa ya ukaguzi na Katibu Mkuu Kiongozi kuhusu mapendekezo ya uboreshaji wa mishahara ya wakaguzi. Lakini mpaka sasa walichofanikiwa ni kubadilisha ngazi za mishahara kutoka *TGS* na kuwa *SAI-S*, mabadiliko ambayo hayabadilishi kiwango cha mshahara anachopaswa kupata Mkaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto kubwa iliyopo hivi sasa ni Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi kuwalipa watumishi wake viwango vya mishahara ambayo inaendana na umuhimu wa kazi wanazozifanya. Hivyo, ili kumwezesha *CAG* kuwa na uhuru wa kuajiri na kupanga maslahi ya Watumishi wake, kuna umuhimu mkubwa wa Bunge kuishawishi Serikali kuhusu yafuatayo:-

(i) Kukubali umuhimu wa Ofisi ya *CAG* kuwa huru kama Katiba na Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008 zinavyoelekeza; na

(ii) Kukifanyia marekebisho kifungu Na 24(2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ili *CAG* awe huru katika masuala yanayohusu ajira na maslahi ya Watumishi wa Ofisi yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Bajeti ya Serikali. Moja ya mambo muhimu katika kuhakikisha uwajibikaji ni utekelezaji

wa bajeti. Mchakato wa bajeti kuanzia mijadala yake hadi inapopitishwa umeonekana kuwa na changamoto kadhaa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Bajeti kuchelewa kuanza kutumika. Mjadala kwa ajili ya bajeti kupitishwa na Bunge unafanywa katika kipindi cha mwezi Juni hadi Agosti kila mwaka, wakati Sheria ya Matumizi *(Appropriation Act)* inaanza kutumika kuanzia tarehe 1 Julai kila mwaka. Hii ina maana kwamba, utekelezaji wa bajeti unaanza katikati ya mwezi Septemba kila mwaka na kwa mantiki hiyo, katika kipindi cha kati ya tarehe 1 Julai hadi katikati ya mwezi Septemba, majukumu muhimu ya Serikali hasa Shughuli za maendeleo hayafanyiki kutokana na kutokuwepo kwa bajeti iliyopitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, upitishaji wa bajeti Bungeni huanza kwa kujadili bajeti ya Taifa ambayo pia hupitishwa kabla ya kuanza kujadili fungu moja moja la bajeti hiyo. Utaratibu huu unaufanya mchakato mzima wa bajeti uonekane kama ni *rubber stamping* tu kwani Bunge linakuwa tayari limepitisha bajeti ya Taifa ambayo kimsingi ndio inayojumuisha bajeti za fungu moja moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia changamoto hizo mbili, Kamati inashauri Serikali kujadiliana na Bunge kuhusu uwezekano wa kubadili mzunguko wa bajeti ya Taifa ili kuruhusu mabadiliko ya tarehe za majadiliano kukamilika kabla au ifikapo tarehe 30 Juni ya kila mwaka ili kuipa Serikali muda wa kutosha kutekeleza mipango yake. Vivyo hivyo, Bunge liangalie uwezekano wa majadala wa Wabunge kuhusu bajeti kuanza kwa kujadili bajeti za fungu moja moja na bajeti ya Taifa iwe ya mwisho kujadiliwa. Aidha, kwa kuzingatia kwamba bajeti za nchi za Afrika Mashariki husomwa siku moja, Serikali iwasiliane na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuwianisha mabadiliko yoyote yanayoweza kutoa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti isiyo na uhalisia. Pamoja na kwamba bajeti kwa ujumla hupitishwa na Bunge bado Serikali mara nyingi haitekelezi bajeti kama ilivyopitishwa. Sehemu kubwa ya Bajeti za Wizara, Idara na Wakala hupunguzwa ili iendane na hali halisi ya mapato ya Serikali. Kamati iliweza kubaini suala hili baada ya kupitia Wizara kama zinazooneshwa kwenye jedwali lifuatalo:-

| Wizara/Idara/Wakala | Wizara ya Kazi na Ajira | Wizara ya Maji |
|---|---|---|
| Fedha iliyoidhinishwa 2009/10 | 17,081,779,503 | 237,434,788,860 |
| Fedha iliyotolewa 2009/10 | 11,186,626,325 | 179,206,119,583 |
| Fedha isiyotolewa 2009/10 | 5,895,153,178 | 58,228,679,277 |

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini kuwa kuidhinisha shughuli ambazo hazitaweza kugharamiwa ndiko kunakosababisha kuwepo kwa madeni makubwa hasa katika ujenzi wa barabara, utoaji huduma na matumizi kwa shughuli zisizo katika mpango. Kwa mfano, Idara ya Jeshi la Polisi peke yake ilikuwa ina madeni yenye thamani ya Sh.17,122,418,239 kufikia Juni, 2010. Vivyo hivyo, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii mpaka kufikia mwezi Machi 2012, deni la *MSD* ni Sh. 42,502,444,399 na kufanya Zahanati na Vituo vya Afya kukabiliwa na upungufu mkubwa wa dawa, vifaa tiba na wataalam wa afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ni madeni ambayo Wizara nyingi huenda nayo katika mwaka wa fedha unaofuata na hivyo kusababisha bajeti ya mwaka unaofuata kutokuwa halisia kwani sehemu kubwa hutumika kulipa madeni hayo, ikizingatiwa kwamba imekuwa ni nadra sana madeni hayo kukasimiwa katika bajeti zinazofuata. Aidha, Kamati inashauri kuwa Kamati za Bunge za kisekta zitaarifiwe juu ya madeni hayo na vile vile madeni hayo yawe yanaoneshwa kwenye vitabu vya bajeti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilibaini pia kuwepo kwa matumizi ambayo hayakuwemo katika bajeti iliyopitishwa na Bunge. Mathalani, Serikali imekuwa ikitumia fedha nyingi katika kuratibu shughuli za Maonyesho ya Kitaifa kama Sabasaba, Nane Nane na Utumishi. Katika kupitia Hesabu za Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Kamati ilibaini kuwa kwa mwaka 2009/2010, Wizara ilitumia fedha za matumizi ya kawaida za jumla ya Shilingi bilioni 1.101 kwa ajili ya kuratibu shughuli za Maonyesho ya Nane Nane na ujenzi wa Jengo la Nane Nane. Hii ni Wizara moja tu na imetumia fedha zote hizo ambazo hazikuwa kwenye bajeti iliyoidhinishwa na Bunge kwa Maonyesho ya Nane Nane tu wakati bado kuna maonyesho mengine ambayo Wizara hushiriki kila mwaka.

Kamati inaona kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kufanya tathmini ya fedha ambazo hutumika kwa shughuli za maonyesho tu kwa mwaka na iangalie pia ni kiasi gani ambacho hakikukasimiwa kwenye bajeti hutumika katika shughuli hizo. Aidha, lengo la Kamati si kuzuia kufanyika kwa maonesho ila kuna umuhimu wa kwanza kuhakikisha Bunge linapopitisha Bajeti liwe linajua kuwa ni kiasi gani cha fedha kitatumika kwa maonyesho tu na pili ikionekana ni fedha nyingi zinatumika kwa shughuli hizo, basi Serikali inaweza kuamua kufanya maonyesho kila baada ya miaka miwili kwa kadri Bajeti itakavyoruhusu na kwa kuzingatia vipaumbele vya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Akaunti kuu ya malipo ya Serikali ilifungwa ikiwa na nakisi *(Bank Overdraft)* ya Sh.1,331,073,630,470.30 kutoka Benki Kuu ya Tanzania hii ni kutokana na jumla ya mapato ya Sh.7,928,122,248,611 dhidi ya matumizi ya jumla ya Sh.8,522,395,969,190 na kusababisha nakisi ya jumla ya Sh.594,273,720,579. Hivyo, mwisho wa mwaka 2009/2010, nakisi ilifikia jumla ya Sh.1,331,073,630,470.30. Aidha, nakisi hii haikujumuishwa katika taarifa ya deni la Taifa kwa kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni, 2011, hivyo wakati wa

kupitisha Bajeti ya mwaka wa fedha wa 2010/2011, Bunge halikuwa na taarifa kamili ya nakisi hiyo.

Kamati ilipohoji fedha zilizotumika katika kuendesha mfuko wa kukwamua wananchi kiuchumi maarufu kama "Mabilioni ya JK" iliambiwa kuwa fedha zilizotumika Shilingi bilioni 21.63 kwa mwaka 2009/2010 ni sehemu ya nakisi hiyo kutoka Banki Kuu hivyo hazikuwa katika Bajeti iliyopitishwa na Bunge.Kamati inasisitiza kuwa mifuko yenye manufaa kwa wananchi kama huu ni vema Bunge likapewa taarifa wakati wa kupitisha Bajeti ili fedha zitengwe kwa kuzingatia Sheria ya fedha. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa Mfuko huo uwe rasmi na usimamiwe na Afisa Masuuli anayeeleweka tofauti na ilivyo sasa haieleweki ni nani anasimamia mfuko huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na kuwepo na matumizi yaliyo nje ya Bajeti, Kamati yangu inaliomba Bunge kuangalia uwezekano wa kuiagiza Serikali kurekebisha Sheria ya Fedha ili Mlipaji Mkuu wa Serikali awe na uwezo wa kufanya maamuzi na sio kushauri tu hasa katika kukataa kufanya matumizi yaliyo nje ya Bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na yale yasiyo na ulazima. Aidha, ni vema Bunge likasimamia kwa karibu zaidi matumizi ya Bajeti kwa kuhakikisha kuwa matumizi yote ambayo yako nje ya Bajeti ni lazima yapate idhini ya Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ambalo limekuwa ni tatizo sana ni ucheleweshwaji wa kutolewa fedha zilizoidhinishwa na Bunge, hasa fedha za miradi ya maendeleo. Pamoja na kwamba fedha za maendeleo zimekuwa zikitolewa pungufu, bado kuna ucheleweshaji mkubwa wa kutoa hata hizo kidogo ili ziendane na mipango ya Wizara na Idara mbalimbali za Serikali. Katika mwaka wa fedha wa 2009/2010, Wizara ya Nishati na Madini ilipokea sehemu ya fedha zake za maendeleo kiasi cha shilingi 14,676,876,796 tarehe 26/5/2010, siku 34 kabla ya mwaka kuisha, vivyo hivyo Wizara ya Ujenzi mpaka kufikia tarehe 30/2/2012 miezi minne kabla ya mwaka

wa fedha kuisha imepokea jumla ya Sh.384.8 billioni tu kati ya Sh. 1.2 trillioni zilizoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Wakati huo huo Wizara ina deni la kulipa Makandarasi la jumla ya Sh. 331 billioni, deni ambalo halitofautiani sana na fedha zilizotolewa mpaka sasa hivyo kuashiria kuwa utekelezaji wa miradi ya ujenzi umesimama na kwa yale madeni wanayodaiwa basi gharama za kuyalipa zinaongezeka maradufu.

Muhtasari wa bajeti iliyoidhinishwa kwa ajili ya matumizi ya maendeleo katika Mafungu ya Wizara na Idara za Serikali

| Mwaka | 2008/2009 | 2009/2010 |
|---|---|---|
| Bajeti iliyoidhinishwa(Sh.) | 2,268,306,465,161 | 3,004,100,724,639 |
| Fedha halisi zilizotolewa (Sh.) | 1,635,263,360,853 | 2,299,010,652,135 |
| Tofauti (Sh.) | 633,043,104,308 | 705,090,072,504 |

Mheshimiwa Naibu Spika, matatizo ya kuchelewa kutolewa kwa fedha ama kutolewa pungufu hutokana na utegemezi wa kibajeti. Kama tunavyofahamu Wahisani pia wanakabiliwa na matatizo ya kiuchumi yanayosababisha wao kusuasua sana katika kutoa fedha wanazoahidi. Kwa mwaka wa ukaguzi wa 2009/2010, Serikali ilipokea asilimia 61 sawa na Sh.2,393,256,357,651 kati ya Sh.3,932,474,455,117 tulizoahidiwa na Wahisani ambazo ziliwekwa kwenye bajeti ya mwaka husika. Kamati inaendelea kusisitiza kuwa ni vema Serikali ikaanza kutenga fedha za ndani kwa ajili ya miradi yote muhimu ya maendeleo. Tumewahi kufanya hivyo kwa baadhi ya miradi kama miradi ya barabara, maji ya Ziwa Victoria kwenda Shinyanga na tukapata matokeo mazuri. Suala la msingi ni kuhakikisha tunaongeza wigo wa mapato, tunasimamia vema vyanzo vyetu vya mapato na kuelekeza fedha za ndani kwenye vile vipaumbele muhimu kwa mwaka husika. Tukifanya hivi tutapunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la utegemezi na tutafanikiwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi ya bajeti bila kufuata vipaumbele. Kwa kuzingatia hali ya kifedha ya nchi yetu kila mwaka, kiasi kidogo cha mapato tunachokusanya na kupokea kutoka kwa wadau wa maendeleo hugawanywa kidogo kidogo kukidhi shughuli zilizopangwa. Kwa kufanya hivyo mipango ya maendeleo imekuwa haitekelezeki kwa wakati au kutotekelezeka kabisa. Kamati inaishauri Serikali kuzingatia kikamilifu utekelezaji wa vipaumbele kama vilivyoainishwa katika mpango mkakati wa maendeleo wa miaka mitano *(National Strategic Plan 2011-2016)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukusanyaji mdogo na upotezaji wa mapato. Mapato yanayopatikana kutoka vyanzo vya ndani ni muhimu sana kuikwamua nchi yetu katika utegemezi wa kibajeti. Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni 2010 inaonesha kuwa Mamlaka ya Mapato *(TRA)* nchini ilishindwa kufikia lengo la ukusanyaji mapato kwa asilimia nane ambayo ni sawa na Sh. 391,408,136,001 baada ya kukusanya Sh.4,637,513,963,999 wakati makadirio yalikuwa Sh.5,028,922,100,000. Aidha, Kamati imebaini kuwa sababu zinazofanya *TRA* ishindwe kufikia malengo ya ukusanyaji mapato ni:-

Ukosefu wa uwajibikaji katika kukusanya mapato. Mpaka wakati Kamati inapitia hesabu za Mamlaka ya mapato Tanzania jumla ya Sh.181,274,438,700 pamoja na dola za Kimarekani 47,255,244 zilikuwa hazijalipwa kwa *TRA* toka kwa wadaiwa mbalimbali kutokana na jitihada ndogo zilizowekwa na mamlaka hiyo katika ukusanyaji wa mapato. Kamati yangu inashauri kuwa ili kuboresha ukusanyaji wa mapato na kupunguza utegemezi wa kibajeti kuna umuhimu wa Serikali kuhakikisha kuwa fedha zote zinazohitajika kukusanywa kisheria, zinakusanywa. Aidha, hatua kali za kisheria zichukuliwe kwa watu binafsi, taasisi na makampuni yanayokwepa kulipa kodi kwa makusudi ili kujinufaisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa *TRA* inakabiliwa na kesi nyingi Mahakamani za madai ya kodi zenye thamani ya Sh.13,246,481,632.32 ambazo mpaka sasa hatujui hatma yake na endapo *TRA* itashindwa basi Serikali itapata hasara yenye thamani hiyo. Aidha, Kamati inashauri kwamba *TRA* itumie makampuni binafsi ya kisheria *(outsource legal services)* ili kuwaongezea nguvu wanasheria wa *TRA* na kuweza kukabiliana na kesi hizo kwa mafanikio zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwepo wa udanganyifu na mianya ya ukwepaji kulipa kodi kumeisababishia Serikali hasara ya Sh.15,431,444,821.13 na dola za Kimarekani 2,610,818.50 ambazo *TRA* inataka kuleta Bungeni kwa ajili ya hasara hiyo kufutwa kwenye vitabu vyake vya hesabu. Hiki ni kiasi kikubwa sana kupotea. Kamati inashauri Serikali kuchukua hatua kali kwa Watumishi wanaosababisha hasara hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na *TRA* kukabiliwa na changamoto nyingi zinazopelekea kushindwa kufikia malengo ya ukusanyaji mapato, bado Serikali kupitia Wizara na Taasisi zake ina vyanzo vingi na vizuri vya mapato lakini tatizo limekuwa ni ubunifu mdogo wa vyanzo vya mapato, ukosefu wa uwajibikaji hasa katika kufuatilia mapato yatokanayo na vyanzo vilivyopo na ukiukwaji au kutozingatia sheria zinazosimamia fedha.

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivi kwa sababu Kamati ilibaini kuwa Wizara ya Maliasili na Utalii kwa mwaka wa fedha wa 2009/2010 ilipoteza jumla ya Sh.874,853,564 baada ya kufanya maamuzi ya upendeleo ya kutoa kiwango cha chini cha mrabaha wa mazao ya misitu kuliko kiwango cha sheria ya misitu *(Cap 323)* na Kanuni za Misitu za mwaka 2007 bila kibali cha mamlaka husika. Vivyo hivyo, mikataba isiyo na tija iliyoingiwa na Wizara ya Nishati na Madini hasa katika sekta ya madini, visima vya gesi, nishati ya *uranium* inaikosesha Serikali mapato mengi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaishauri Serikali iangalie upya mikataba iliyoingia kwenye sekta hizo na vilevile iondokane na mtazamo potofu kuwa anayegundua sehemu ambapo madini, gesi, au mafuta ndiye anayetakiwa kuchukua asilimia kubwa ya mapato, wakati rasilimali hizo ni za wananchi na Serikali ndiyo inayopaswa kutetea haki zao. Serikali ihakikishe inapata zaidi ya asilimia 50 ya mapato yatakayopatikana kutoka kwenye rasilimali zake bila kujali aliyegundua uwepo wa rasilmali hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo pamoja na kukabiliwa na tatizo la kuwa na madai makubwa dhidi ya Shirikisho la mpira wa mguu Tanzania *(TFF)* kufuatia Shirikisho hilo kushindwa kupeleka mgawanyo wa mapato yanayotokana na makusanyo ya viingilio vya mlangoni katika viwanja. Aidha, Wizara iangalie uwezekano wa kuanzisha Chuo cha Michezo *(Sports Academy)* ambacho kitafundisha wanamichezo wenye vipaji ambao wataweza kupata fursa ya kununuliwa na kuwa wachezaji wa kulipwa nje ya nchi na hivyo kuliongezea Taifa mapato kwa kuongeza fursa za uwekezaji kwenye michezo na kukuza sekta ya utalii.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu matumizi mabaya ya fedha za Serikali. Katika upande wa matumizi ya fedha za umma kumekuwa na mapungufu mengi. Kamati yangu imebaini kuwa sehemu kubwa ya mapungufu hayo yanatokana na kutozingatiwa kwa Sheria ya Manunuzi ya mwaka 2004. Kwa mwaka wa ukaguzi 2009/2010 manunuzi yaliyofanywa bila kufuata matakwa ya kifungu cha 45 cha Sheria ya Manunuzi ya Umma yalikuwa Sh. 50,685,371,565.58 kama inavyoonekana kwenye Jedwali hapo chini.

| Na. | FUNGU | WIZARA/IDARA/WAKALA/SEKRETARIETI ZA MKOA | KIASI (SH.) |
|---|---|---|---|
| 1. | 23 | Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali | 49,433,343,399.58 |
| 2. | 99 | Wizara ya Mifugo na Uvuvi | 320,871,938 |
| 3. | 81 | Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza | 54,424,314 |
| 4. | 50 | Wizara ya Fedha | 373,184,960 |
| 5. | 34 | Wizara ya Mambo ya Nje na Uhusiano | 212,897,447.23 |
| 6. | 91 | Tume ya Kudhibiti Madawa ya Kulevya | 40,748,400 |
| 7. | 29 | Idara ya Magereza | 358,394,154 |
| 8. | 82 | Sekretarieti ya Mkoa wa Ruvuma | 11,654,400 |
| | | **JUMLA** | **50,685,371,565.58** |

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu katika manunuzi umeonekana katika mafungu mengi na kwa mantiki hiyo tunaishauri Serikali kuchukua hatua za makusudi kurekebisha hali hiyo kwani fedha nyingi zaidi katika bajeti ya Serikali huenda katika sekta ya manunuzi. Aidha, Kamati inazitaka taasisi za ununuzi kuweka mpango wa mwaka wa manunuzi ili kuepuka manunuzi ya dharura na kupata thamani ya fedha, kupunguza gharama za matumizi na kupata manunuzi sahihi kwa njia ya Wazabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na suala la kutozingatia Sheria ya Manunuzi, kumekuwepo na udhaifu katika mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu za malipo. Kamati yangu imesikitishwa na kuwepo kwa hoja zenye thamani ya Sh.362,026,933,382.25 zilizohusu malipo yenye nyaraka pungufu. Ila ilibainika kuwa baada ya hoja kutolewa nyaraka hizo hupatikana baadaye na hoja hufungwa pindi mkaguzi anaporidhika. Aidha, mara nyingi nyaraka hizo hupatikana pindi Wizara zinapoitwa na Kamati ya *PAC*. Kamati inashauri Serikali kuweka watumishi wenye sifa zinazostahili na kutengeneza sera ya utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu hasa kwa njia ya kielektroniki ili kuhakikisha uwepo wa utunzaji kumbukumbu endelevu Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kumekuwa na matumizi yasiyo na ulazima, mathalan Kamati ilibaini kuwa hadi kufika tarehe 30 Juni, 2010, Serikali Kuu peke yake ilikuwa inamiliki

magari yenye thamani ya Sh.5,092,449,965,734 na bado Serikali imeendelea kununua magari zaidi. Mwendelezo wa ununuzi wa magari ya gharama kubwa huongeza gharama za uendeshaji wa magari, matumizi ambayo si ya lazima sana kwa Serikali yenye uchumi mdogo uliozidiwa na madeni.

Mheshimiwa Naibu Spika, matumizi mengine yasiyo na ulazima yalifanya na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii na Wizara ya Ujenzi ambazo zimekuwa zikipangisha kwa gharama kubwa kwa sababu ya kutomiliki majengo ya kutosha kwa ajili ya Ofisi. Jedwali hapo chini linaonyesha kodi inayolipwa na Wizara hizo baada ya kupangisha.

| | **Kodi ya pango kwa mwezi** | **Kodi ya Pango kwa mwaka** |
|---|---|---|
| Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii | 38,000,000 | 456,000,000 |
| Wizara ya Ujenzi | 40,000,000 | 480,000,000 |

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kwa mwaka 2009/2010, kumekuwa na malipo kwa watumishi hewa ya jumla ya Sh.1,842,607,565.29. Malipo haya yalifanyika kwa watumishi waliofariki, waliostaafu na kufukuzwa kazi. Kamati imeendelea kusisitiza kwa Maafisa Masuuli wa kila fungu kuhakikisha kuwa kumbukumbu sahihi za watumishi walio chini yao zinawekwa ili kuondokana na tatizo hili. Aidha, Kamati imejulishwa na Menejimenti ya Utumishi wa Umma kuwa Serikali imeanza kutumia mfumo maalum wa malipo ya mishahara kwa njia ya kielektroniki utakaosaidia kuweka kumbukumbu za watumishi wote wa Serikali. Mfumo huo unasimamiwa na Menejimenti ya Utumishi wa Umma ambayo imewapa Waajiri na Maafisa Usimamizi Rasilimali Watu, uwezo wa kuingiza taarifa za kiutumishi katika mfumo huo kwa lengo la kurahisisha na kuharakisha zoezi la kuwaingiza watumishi wapya kwenye mfumo wa malipo ya mshahara *(payroll system)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kulitaarifu Bunge kuwa baada ya Kamati yangu kutoa Bungeni pendekezo la

Serikali kuimarisha udhibiti wa mfumo wa malipo ya mishahara kwa lengo la kudhibiti ubadhirifu, Menejimenti ya Utumishi wa Umma ilifanya uchunguzi wa watumishi hewa na walibainika kuwepo 3.921 na hivyo ushauri wa Kamati kuokoa jumla ya Sh.10,000,000,000 ambazo zingeendelea kupotea. Kamati inapongeza juhudi zilizofanyika ila inasisitiza Serikali kupitia mfumo mpya wa kielektroniki wa malipo ya mishahara kuhakikisha inasimamia uadilifu wa Waajiri na Maafisa Usimamizi Rasilimali Watu waliopewa dhamana ya kuingiza majina ya watumishi kwenye *payroll*.

Mheshimiwa Naibu Spika, umiliki wa ardhi na majengo ya Serikali. Baada ya Kamati kujadili Hesabu na kukagua mali za Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Balozi zetu ilibaini kuwa Taasisi nyingi hazina Hatimiliki za ardhi na Majengo inayomiliki. Kwa mfano, Chuo cha Michezo cha Malya kinachomilikiwa na Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo; ardhi na majengo yanayomilikiwa na Balozi zetu zilizopo London, Nairobi na Maputo. Kamati inaishauri Serikali kupitia Wakala wa Majengo *(TBA)* kuhakikisha kuwa umiliki wa ardhi na majengo kwa Wizara, Idara, Wakala, Sekretarieti za Mikoa na Balozi zetu unarasimishwa. Ni vema Serikali itamke bayana kisheria kuhusu mmiliki wa viwanja na majengo ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu ilipitia Hesabu za Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa na mimi kupata fursa ya kukagua viwanja na majengo yanayomilikiwa na Balozi zetu zilizopo Washington *DC*, New York na London.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubalozi uliopo New York unamiliki jengo la zamani la ghorofa tano lililonunuliwa mwaka 2009 kwa thamani ya US$ 24.5 milioni ambalo limepangishwa kwa wapangaji ambao karibu mikataba yao inakwisha. Jengo hilo linahitaji kufanyiwa ukarabati utakaogharimu US$ 3.0 milioni ili ghorofa ya nne na ya tano iweze kutumika kama Ofisi za Ubalozi wa Tanzania kwenye Umoja wa Mataifa na ghorofa

zilizosalia zipangishwe kwa faida ili ziweze kuongeza mapato kwa Serikali yanayokadiriwa kuwa US$1.2 milioni kwa mwaka. Mpaka sasa Kamati haijapata taarifa ya utekelezaji wa maombi hayo ya Ubalozi kwa Wizara husika. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuhakikisha inakarabati jengo hilo kwa lengo la kulipangisha ili kuongeza mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubalozi uliopo Washington DC unamiliki majengo mawili (Jengo la zamani na Jengo jipya la Ubalozi) ambayo yote yanahitaji ukarabati. Jengo jipya linahitaji kukarabatiwa ili Ubalozi uweze kupangisha ghorofa tatu ambazo hazitumiki kwa shughuli za kiofisi na Jengo la zamani linahitaji kukarabatiwa ili litumike kama nyumba ya kufikia wageni wa Serikali ya Tanzania wanaokwenda huko kwa shughuli za Kitaifa au kupangisha Taasisi za Kimataifa ambazo zimeonesha nia ya kutaka kukodisha jengo hilo. Ubalozi uliwasiliana na Wizara kuhusu ukarabati wa majengo hayo na kutoa kibali cha kuyapangisha ambapo mpaka sasa ukarabati huo haujafanyika. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha ukarabati wa majengo hayo unafanyika na kukubaliana na mapendekezo ya kupangisha majengo hayo kwa faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ubalozi uliopo London, Uingereza unamiliki majengo ambayo yamechakaa na viwanja kadhaa ambavyo Serikali imeshindwa kuviendeleza. Miongoni mwa viwanja hivyo, ni kiwanja namba 19 *Denewood Road*, *N6 4AQ* ambapo baada ya kubomolewa nyumba iliyokuwepo mwaka 2007 hapajajengwa jengo lingine. Kamati inashauri Serikali ifanye maamuzi ya haraka ya kujenga kwenye viwanja visivyoendelezwa na kukarabati majengo yote yaliyochakaa kwa lengo la kuyapangisha kwa faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ishirikiane na Wizara ya Fedha, Wakala wa Majengo *(TBA)* na Mifuko ya Hifadhi ya jamii *(PPF, NSSF, PSPF, GEPF, NHIF* na *LAPF)* katika kuhakikisha

kuwa Serikali kupitia Balozi zake inatumia fursa zilizopo kwenye nchi hizo kama ya kutumia *mortgage financing* kukarabati na kujenga majengo na kisha kupangisha kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali. Aidha, Serikali ikasimishe kwa *TBA* mamlaka ya kuingia mikataba ya kibiashara yenye lengo la kukarabati, kujenga na hatimaye kupangisha majengo yaliyo chini ya Balozi zetu kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati yangu inakabiliwa na changamoto ya kushindwa kujadili Hesabu na kukagua mali zilizo chini ya Balozi zetu kutokana na ufinyu wa bajeti, Kamati inaliomba Bunge lako Tukufu kuangalia uwezekano wa Kamati hii kwa kushirikiana na Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuwezeshwa kibajeti ili ziweze kutembelea na kukagua Hesabu na mali za Balozi zetu hasa majengo kwa kuanzia na nchi za Uingereza, India, Ujerumani, Sweden, Urusi na Japan. Aidha, kwa kufanya hivyo Bunge lako litaweza kuona hali halisi ya majengo na mali za Serikali katika Balozi zetu na kuishauri Serikali ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa maalum kuhusu ukaguzi wa magari yaliyotumika unaofanyika nje ya nchi pamoja na ukaguzi wa bidhaa nyingine. Mwezi Aprili 2009, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali *(PAC)* iliwasilisha taarifa yake Bungeni iliyokuwa na mapendekezo kadhaa ambayo hatimaye yalipitishwa na kuwa maazimio ya Bunge. Aidha, moja kati ya mapendekezo hayo lilikuwa la kuitaka Serikali, kupitia Sheria yake ya Ukaguzi wa Viwango vya Ubora wa Bidhaa, kuhakikisha inasitisha utaratibu wa kukagulia magari nje ya nchi *(pre-shipment inspection)* na kuanza utaratibu wa kukagua magari yote baada ya kutoka bandarini na mipakani yaani *post-shipment inspection*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa taarifa hiyo ya Kamati iliyopitishwa na Bunge, utaratibu wa *post-shipment inspection* ungemlazimu anayeleta gari nchini kulipia ushuru

wa gari lake kama itakavyoamuliwa na *TRA* na baada ya kutoa gari hilo bandarini, lingekaguliwa kwanza na *TBS* ili kuhakikisha limefikia viwango vilichowekwa ndipo lipate usajili. Kamati ilisisitiza kuwa utaratibu huo ungeongeza mapato kwa *TBS* na Serikali zaidi ya ule wa kutumia Wakala nje ya nchi kwa maana *TBS* huingia gharama kubwa katika usimamizi na Serikali kwa ujumla hupoteza kiasi kikubwa cha fedha za kigeni *(externalized foreign currency)* na kuwanufaisha Wakala waliopo nchi za nje. Mathalani, Taarifa ya *TBS* ilionesha kuwa tangu mwaka 2002 hadi tarehe 30 Juni, 2011, fedha za kigeni zilizokusanywa kutokana na tozo za magari nje ya nchi ni jumla ya US$17,141,675.1, kati ya hizo mapato ya wakala ni US$14,103,302 na mapato ya *TBS* ni US$3,038,373.1 tu. Hivyo, kwa kuzingatia takwimu hizo, kama utaratibu wa kukagua magari yaliyotumika ungefanyika ndani ya nchi basi Serikali ingekusanya jumla ya US$17,141,675.1 (Tshs.27,598,097,000) badala ya US$ 3,038,373.1 (Tshs.4,891,781,000) tu zilizokusanywa kama mapato kupitia tozo za ukaguzi wa magari na Shirika la *TBS*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mapendekezo hayo kuridhiwa na kupitishwa na Bunge mwaka 2009, Serikali kupitia Wizara ya Viwanda na Biashara inayosimamia Shirika la Viwango la Taifa *(TBS)* haikubadilisha utaratibu wa kukagua magari yaliyotumika nje ya nchi ambao unaonesha kuanza kutumika tangu mwaka 2002 kabla hata kipengele cha kusimamia utaratibu huo *(pre-shipment verification conformity to standards)* hakijawekwa kwenye Sheria hiyo ya Viwango. Marekebisho ya Sheria ya Viwango ya mwaka 1975 yaliyofanywa mwaka 2009 ndio yaliiruhusu *TBS* kusimamia utaratibu huo, kabla ya hapo Shirika la *TBS* lilitumia utaratibu huo bila ya Sheria na Bunge lililetewa Muswada wa Marekebisho hayo bila ya kuambiwa gharama kamili ya kuendesha utaratibu huo na kujikuta linahalalisha maovu yaliyokuwa yakiendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Wizara kutotekeleza azimio la Bunge, Kamati iliamua kujiridhisha kwanza kuhusu faida na hasara za kukagulia magari nje ya nchi. Kwa masikitiko makubwa, Kamati ililazimika kukutana mara tatu na Afisa Masuuli wa Wizara hiyo kwa sababu alishindwa kujibu hoja ya kukaidi azimio la Bunge na vilevile kugoma kutoka takwimu ambazo Kamati na Wakaguzi walihitaji kwa lengo la kufanya uchunguzi na kuishauri Serikali ipasavyo. Katika kikao cha mwisho ambacho kilihudhuriwa pia na Wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma, Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara na Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Afisa Masuuli wa Fungu hilo aliagizwa kuandaa taarifa itakayoainisha yafuatayo na kisha kuipeleka kwa Wakaguzi kwa uhakiki kabla ya Alhamisi tarehe 2 Februari, 2012:-

(i) Idadi kamili ya magari yaliyoingizwa nchini na kukaguliwa ikiwa ni pamoja na kuainisha thamani ya fedha za kigeni zilizolipwa *(externalized foreign currency)* na kiasi cha mapato kilichokusanywa tangu utaratibu wa kutumia Wakala kukagua magari nje ya nchini uanze.

(ii) Idadi kamili ya bidhaa zilizooneshwa kwenye Taarifa ya awali ya *CAG* (iliyojadiliwa tarehe 27 Januari, 2012) kama bidhaa zilizokaguliwa na *TBS* na kutofikia viwango ingawa hakuna ushahidi kuwa bidhaa hizi zilidhibitiwa kuingia nchini.

(iii) Utaratibu mzima wa kukagua bidhaa zingine ukiacha magari pamoja na gharama ambazo *TBS* inaingia katika utekelezaji wa utaratibu huo *(externalised foreign currency)* na mapato yaliyopatikana kwa miaka mitano (5) ya nyuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Aprili, 2012, Kamati ilipokea taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi maalum wa Shirika la Viwango Tanzania ambayo imebainisha yafuatayo:-

(i) Idadi kamili ya magari yaliyokaguliwa na Wakala kwa kipindi cha kuanzia 2002/2003 mpaka 2010/2011 ilikuwa ni magari 167,379 na ilitofautiana na ile iliyosemwa awali na *TBS* ambayo ni magari 155,591 (tofauti ya magari 11,787).

(ii) Thamani ya fedha za kigeni zilizolipwa *(Externalization of foreign currency)* kuanzia mwaka 2002/2003 mpaka 2010/2011 ya jumla ya *USD* 17,141,675 ambapo kati ya hizo mapato ya *TBS* ni *USD* 3,038,374 na mapato ya wakala ni 14,103,301 ilitofautiana na uhakiki uliofanywa na ofisi ya *CAG* kwani kulingana na idadi ya magari 167,379 yaliyokaguliwa jumla ya *USD* 18,348,540 zilipaswa kulipwa *(Externalization of foreign currency)* kati ya hizo, mapato ya *TBS* ni *USD* 3,446,957.50 na mapato ya wakala ni USD 14,901,582.501.

(iii) Uhakiki umeonesha kuwa kulingana na makubaliano kati ya *TBS* na wakala, gharama ya kukagua gari ni kati ya dola 100 - 200 tofauti na ile iliyotolewa awali na *TBS* ambayo ilikuwa kati ya dola 90 – 200.

(iv) Utoaji wa leseni kwa Wakala hawakuwa na sifa kama ilivyoainishwa kwenye tangazo la *the Guardian* la tarehe 26/11/2006.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia taarifa hiyo ya *CAG*, Kamati inaishauri Serikali kufanya yafuatayo:-

(i) Serikali imuwajibishe Afisa Masuuli wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa sababu zifuatazo:-

(a) Kwa kushindwa kutekeleza azimio ya Bunge la kusitisha utaratibu wa kukagulia magari nje ya nchi na badala yake kukagulia ndani ya nchi.

(b) Kwa kushindwa kusimamia Shirika la Viwango *(TBS)* mpaka limesababisha Serikali kupoteza jumla ya *USD* 18,348,540 *(Externalization of foreign currency)*.

(c) Kwa kuliletea Bunge marekebisho ya Sheria ya Viwango vya Ubora bila kulieleza hasara ambayo inaweza kusababishwa kwa kuendelea kukagulia magari na bidhaa nyingine nje ya nchi.

(ii) Kamati inalishauri Bunge kuunda Kamati Maalum itakayoshirikiana na Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma *(POAC)* kwa ajili ya kufanya uchunguzi zaidi kuhusu ukaguzi wa magari na bidhaa nyingine unaofanywa na Shirika la Viwango (TBS).

(iii) Wizara ilete Muswada Bungeni wa kukifanyia marekebisho kifungu cha 4(1)(s) cha Sheria ya Viwango ili kiweke bayana kuwa ukaguzi wa magari na bidhaa nyingine zitokazo nje ufanyikie ndani ya nchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, matokeo ya ukaguzi kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2010 yanaonesha kutoboreka kwa hati zilizotolewa kwa Serikali Kuu na Taasisi zake ikilinganishwa na mwaka uliopita kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:-

| **Category of entities** | **Unqualified Opinions** | | **Qualified Opinions** | | **Adverse Opinions** | | **Disclaimer of Opinion** | | **Total** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| F/Y | 2008/2009 | 2009/2010 | 2008/2009 | 2009/2010 | 2008/2009 | 2009/2010 | 2008/2009 | 2009/2010 | 2008/2009 | 2009/2010 |
| MDAs | 46 | 42 | 5 | 13 | 1 | 1 | - | - | 52 | 57 |
| RAS | 18 | 12 | 2 | 7 | 1 | 1 | - | 1 | 21 | 21 |
| Embasies/Missions | 27 | 29 | 4 | 2 | 1 | - | - | - | 32 | 31 |
| **Total** | **91** | **83** | **11** | **22** | **3** | **2** | **-** | **-** | **105** | **108** |
| **Average** | **87%** | **77%** | **10%** | **20%** | **3%** | **2%** | **NIL** | **1%** | **100%** | **100%** |

Mheshimiwa Naibu Spika, ingawa kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2011, matokeo ya ukaguzi yameonesha kuboreka kwa hati zilizotolewa kwa Serikali Kuu na Taasisi zake

ukilinganisha na mwaka 2009/2010 kama inavyoonekana katika jedwali hapo chini:-

| **Mwaka** | **2009/2010** | | **2010/2011** | |
|---|---|---|---|---|
| | **Idadi** | **%** | **Idadi** | **%** |
| Hati zinazoridhisha | 54 | 70 | 69 | 85 |
| Hati zenye shaka | 20 | 26 | 12 | 15 |
| Hati zisizoridhisha | 2 | 3 | - | - |
| Hati mbaya | - | - | 1 | 1 |
| **Jumla** | **77** | | **81** | |

Mheshimiwa Naibu Spika, sababu zilizopelekea matokeo ya hati za ukaguzi kuboreka ni zifuatazo:-

(a) Bunge kupitisha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ya mwaka 2008 ambayo imemwongezea uhuru *CAG* wa kufanya ukaguzi kwa ufanisi zaidi. Vile vile uwepo wa Kanuni za Bunge ambazo ndizo zinazipa mamlaka Kamati za Bunge kusimamia matumizi ya fedha za Serikali.

(b) Kazi nzuri inayofanywa na Kamati za Bunge katika kuwashauri Maafisa Masuuli kwa lengo la kupunguza hoja za ukaguzi.

(c) Uwepo wa ushirikiano mzuri kati ya Kamati ya *PAC* na *CAG* na vile vile ushirikiano mzuri kati ya Kamati ya *PAC* na Maafisa Masuuli wasikivu wenye nia ya kuhakikisha kunakuwa na matumizi mazuri ya fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kupitia na kuchambua Hesabu za Fungu 22- Deni la Taifa; Hesabu za Fungu 23 – Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, pamoja na Hesabu za Majumuisho ya Kitaifa, Kamati yangu iliweza kubaini changamoto zifuatazo:-

Kwanza, udhibiti wa Deni la Taifa. Deni la Taifa katika kipindi kilichoishia tarehe 30 Juni 2010 limeongezeka kutoka

Sh.7,621,286,730,034 mwishoni mwa mwaka wa fedha 2008/09 hadi kufikia Sh.10,503,806,011,885 ambalo ni ongezeko la asilimia 39.27. Tatizo lilipo ni kwamba wakati Deni la Taifa likiongezeka kwa asilimia 39.27, uchumi wa nchi *(GDP growth rate)* umeongezeka kwa wastani wa asilimia 6.5 tu tangu mwaka 2006/2007 mpaka 2009/2010. Hii inamaanisha kwamba Serikali haiko katika nafasi nzuri ya kulipa deni hilo pindi wakati wa kulipa utakapowadia. Aidha, mgawanyo wa deni hilo ni kama inavyoonekana katika jedwali hapa chini:-

| Aina ya Deni | 2006/07 | 2007/08 | 2008/09 | 2009/10 |
|---|---|---|---|---|
| Deni la Nje | 3,642,591,417,989 | 4,601,657,485,229 | 5,386,646,362,543 | 7,747,903,803,161 |
| Deni la Ndani | 1,832,420,666,865 | 1,875,794,357,188 | 2,234,640,367,491 | 2,755,902,208,703 |
| Jumla ya Deni | 5,475,012,084,854 | 6,477,451,842,417 | 7,621,286,730,034 | 10,503,806,011,885 |
| Ongezeko la Deni | (1,763,861,798,060) | 1,002,439,757,563 | 1,143,834,887,617 | 2,882,519,281,851 |
| Badiliko la deni la nje | (%)-24% | 26% | 17% | 44% |
| Badiliko la deni la ndani | (%)25% | 2% | 19% | 23% |
| Badiliko la deni lote | (%) -24% | 18.31% | 17.66% | 39.27% |
| GDP real rate | 5.8% | 7.3% | 7.1% | 6% |

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifahamishwa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kuwa mpaka tarehe 30 Juni, 2011, deni la Taifa limefikia kiasi cha shilingi trilioni 14.4 na hakuna malipo ya deni hilo yaliyofanyika mpaka sasa. Kwa mwelekeo huu wa Deni la Taifa, Kamati yangu inaishauri Serikali kuwa makini katika shughuli zake za kiuchumi kwa kuweka uwiano wa kukuza uchumi ambao utaweza kuleta tija kwa Taifa na kulipa madeni yote kwa wakati yanapofikia muda wa kulipwa. Pia

kuna haja ya kuongeza wigo wa vyanzo vya ndani vya mapato na kuwa makini katika kutumia fedha za umma kwa kukwepa matumizi ambayo hayana ulazima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu inaendelea kusisitiza umuhimu wa Serikali kuwa na Taasisi moja ambayo itashughulikia madeni yote ya Taifa na pia pawepo na *database* moja ili kuweza kuwa na kumbukumbu sahihi ya madeni yaliyolipwa, yanayoendelea kulipwa na yale yasiyolipwa. Kamati ilipewa taarifa kuwa mpango wa kuwa na taasisi moja inayoshughulikia Deni la Taifa bado haujakamilika ila Serikali kupitia mpango wake wa maboresho ya Deni la Taifa *(Tanzania Government Debt Management Reform and Capacity Building Plan)* imeanza mchakato wa kuanzisha Idara mpya ndani ya Wizara ya Fedha ambayo itashughulikia Deni la Taifa ili kuongeza ufanisi katika kushughulikia madeni tofauti na ilivyo sasa ambapo Deni la Taifa hushughulikiwa na idara mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhika baada ya kuona zoezi la kuwa na *Single Unified Database* ya Deni la Taifa linaendelea vizuri ambapo kwa sasa Wizara ya Fedha imeanza kutoa taarifa za deni la Serikali na Benki Kuu inatoa taarifa za deni la nje na la Sekta binafsi. Kilichobaki sasa ni kuunganisha *database* hizo mbili za deni la Taifa kwenye *server* moja ili taarifa za Deni la Taifa zipatikane kiurahisi kutoka kwenye chanzo kimoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipewa taarifa kuwa bado uongozi unaendelea kulifanyia kazi suala hilo na kama Idara ya kushughulikia Deni la Taifa itaanzishwa haraka iwezekanavyo basi ndiyo itakayosimamia *database* ya Deni la Taifa inayoanzishwa. Kwa kuzingatia hatua hizo zilizochukuliwa baada ya Kamati kutoa mapendekezo hayo kwenye taarifa yake ya mwaka jana, Kamati inaendelea kusisitiza kwa Serikali kukamilisha mapema mpango wake wa kuanzisha Idara ya usimamizi wa Deni la Taifa na single unified database ya Deni

la Taifa ili Deni la Taifa liweze kusimamiwa kwa karibu na kudhibiti ongezeko lake ambalo haliendani na ukuaji wa uchumi wa nchi yetu.

Pili, utoaji wa dhamana za Serikali kwa mikopo ya Mashirika ya Umma na Taasisi binafsi uliozidi kiwango. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010, Serikali ilikuwa na madeni yaliyoingiwa kwa njia ya udhamini yanayofikia Sh.711,804,989,096 ambayo ilikuwa ni sawa na dhamana ya asilimia 96.8 ya mikopo yote. Haikuweza kufahamika ni kwa jinsi gani Serikali ilikuwa ikidhamini zaidi ya kiwango kinachotakiwa kama inavyoelekezwa katika Kifungu Na. 13(1)(b) cha Sheria ya Mikopo ya Serikali, Misaada na Udhamini ya Mwaka 1974 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004. Nanukuu:-

"…Kiwango cha juu kabisa ambacho Serikali inaweza kudhamini deni hakitazidi asilimia 70 ya fedha zilizokopwa…". Kamati ilibaini kwamba dhamana hizo hazikuwa na rehani halisi, hii inaweza kusababisha Serikali kujiweka hatarini kwa kuwa na dhamana ya kiasi kikubwa cha mikopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipewa taarifa na Mlipaji Mkuu wa Serikali kuwa Serikali imeamua kusimamisha kwa mwaka mmoja utoaji wa dhamana na mikopo kwa idara za Serikali na kuendelea kutoa kwa makampuni ya kibiashara kwa lengo la kufanya tathmini ya athari zilizosababishwa na udhamini wa Serikali na kisha kuangalia uwezekano wa kurekebisha Sheria ya Mikopo ya Serikali, Misaada na Udhamini ya Mwaka 1974 kama ilivyorekebishwa mwaka 2004 ili utoaji wa dhamana za Serikali uwe na tija. Kamati inapongeza uamuzi huo ila inasisitiza uwepo wa *ceiling* ya *Goverment exposure* kwa mikopo inayodhamini. Aidha, ni vema Serikali ikaunda idara au taasisi itakayosimamia dhamana za Serikali ili kuepuka dhamana hizo kuwa madeni ya Serikali.

Tatu, ufungaji wa Hesabu za Serikali Kuu kwa kutumia *IPSAS Acrual Basis of Accounting*. Serikali Kuu bado inatumia

*IPSAS Cash Basis of Accounting* katika ufungaji wake wa Hesabu na hii imekuwa ni mojawapo ya sababu zilizosababisha Hesabu za Majumuisho kupata Hati yenye Mashaka kwa miaka ya 2007/2008 na 2008/2009 na kupata Hati Chafu kwa mwaka 2009/2010. Kamati ilipomhoji Afisa Masuuli wa Fungu husika aliitaarifu Kamati kuwa Fungu hilo litaendelea kupata Hati yenye Mashaka mpaka Serikali itakapokamilisha mchakato wa kuandaa Daftari la Kudumu la Mali za Serikali. Hivyo, Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inakamilisha mchakato wa kuunda Daftari hilo ambalo uundwaji wake utasaidia Serikali kuanza kufunga hesabu kwa kutumia *IPSAS Accrual Basis of Accounting* na hatimaye tuweze kuwa na *Financial Statements* za Hesabu za Serikali nzima na Fungu husika liweze kupata Hati Safi.

Nne, ushirika wa Serikali na Taasisi binafsi *(PPP)*. Uwekezaji katika Ushirika wa Serikali na taasisi binafsi *(PPP)* si madhubuti unaweza kuisababishia Serikali kubeba mzigo mzito wa gharama kubwa ambazo zingeweza kuepukika. Serikali imekuwa ikibeba mzigo mkubwa kama kulipa mishahara ya wafanyakazi wa wawekezaji binafsi na kulipa mikopo ya iliyochukuliwa na wawekezaji binafsi, mifano ni pamoja na *Songas*, *TRL Limited, IPTL Limited* na *Kiwira Coal Mines Limited*. Kamati ilihoji mkataba wa *Songas* na Serikali ambao ulikuwa na makubaliano kuwa Serikali ikope kwa niaba ya *Songas* na faida itakayotengenezwa na *Songas* itumike kulipa deni hilo lakini hadi kufikia tarehe 30 Juni 2010, deni hilo lilifikia Sh.238,267,694,761 ikimaanisha kuwa *Songas* haijaweza kutengeneza faida ambayo ingelipa deni hilo na riba ya deni hilo inazidi kuongezeka. Kamati ilimuagiza Mlipaji Mkuu wa Serikali kuhakikisha anaangalia upya mikataba ya aina hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu masuala yaliyojitokeza katika taarifa tatu za ukaguzi wa ufanisi zilizotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kamati ilijadili taarifa tatu za ukaguzi wa ufanisi kati ya saba ambazo zimetolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Taarifa

zilizojadiliwa zinahusu afya ya uzazi chini ya Afisa Masuuli wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii; ukaguzi wa shule za sekondari chini ya Afisa Masuuli, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na usimamizi wa miradi ya ujenzi chini ya Afisa Masuuli, Wizara ya Ujenzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu ukaguzi wa ufanisi wa afya ya uzazi chini ya Afisa Masuuli, Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii. Ukaguzi wa ufanisi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulilenga kuangalia kama Wizara ya Afya na Ustawi wa jamii inasimamia, inafanya tathmini mbalimbali, inatoa elimu ya afya na kuandaa mgao wa fedha katika shughuli zinazohusiana na huduma ya afya ya uzazi kiuwekevu, kitija na kiufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu baada ya kujadili taarifa hiyo inatoa ushauri ufuatao kwa Wizara husika:-

(i) Wizara kuhakikisha kwamba inasimamia ipasavyo kiwango cha huduma ya afya ya uzazi. Hii ni pamoja na kuwa na mipango kwa ajili ya kufuatilia afya ya wajawazito; kutambua masuala muhimu yanayohusiana na afya ya wajawazito kwa kuzingatia tathmini ya vitu hatarishi; kuweka malengo kuhusiana na masuala muhimu ya afya ya uzazi yanayotakiwa kufikiwa katika ngazi tofauti tofauti na kuboresha mfumo wa kuchukulia taarifa za huduma ya afya nchini.

(ii) Wizara kutoa mwongozo wa kutosha kwa vituo vya afya kuhusiana na huduma za afya kuhusu elimu ya afya ya uzazi ambazo zinapaswa kutolewa kwa wananchi. Hii ni pamoja na kuandaa mpango wa kuelimisha wananchi; kuwa na ratiba toshelezi kwa ajili ya utoaji wa elimu ya afya ya uzazi kwa watu na kutoa taarifa sahihi na toshelevu inayohusiana na afya ya uzazi.

(iii) Wizara kuhakikisha kuwa mara kwa mara, inafanya tathmini ya vipengele vya mfumo wa afya vinavyohusiana na afya ya wajawazito. Hii ni pamoja na kuandaa mpango wenye mlengo wa vitu hatarishi utakaotumika kutathmini huduma za vituo vya afya nchini, kutoa viwango kwa vituo vya huduma ya afya kwa ajili ya kupima huduma za kliniki kwa wajawazito na uhifadhi wa kumbukumbu za afya ya uzazi, kutathmini taratibu za kitabibu juu ya msingi wa kupima afya, mafanikio ya mipango ya elimu, tathmini ya kiwango cha rasilimali katika vituo vya afya, kuchukua hatua dhidi ya vituo visivyofanya kazi vizuri juu ya masuala ya afya ya uzazi na kutathmini kiwango cha mawasiliano ya matokeo ya tathmini ya huduma ya vituo vya afya.

(iv) Wizara kuhakikisha kuwa kuna bajeti sahihi kwa ajili ya kutenga fedha za afya ya uzazi. Hii ni pamoja na kuweka vigezo vya mgao wa bajeti katika kuamua kiasi cha fedha zitakazotengwa kwa ajili ya masuala ya afya ya uzazi na kuweka utaratibu wa ufuatiliaji wa bajeti iliyotumika katika huduma za afya ya uzazi.

(v) Wizara isimamie kwa karibu huduma za afya ya uzazi kwa lengo la kupunguza vifo vya wajawazito ikiwa ni pamoja na kupeleka watoa huduma ya afya ya kutosha kwenye vituo vya afya.

(vi) Wizara ihakikishe kunakuwa na chumba cha mapumziko katika kila Zahanati au kituo vya Afya ambacho wajawazito wataweza kukitumia kwa ajili ya kusubiria huduma.

(vii) Wizara ifanye utafiti kuhusu sababu za ongezeko la wajawazito kujifungua kwa njia ya upasuaji.

(viii) Wizara iangalie uwezekano wa kuleta Muswada Bungeni utakaokuwa na kipengele kitakachofanya utaratibu wa kuorodhesha au kutoa taarifa za vifo vya wazazi uwe ni wa lazima kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu ukaguzi wa ufanisi juu ya ukaguzi wa shule za sekondari chini ya Afisa Masuuli, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi. Ukaguzi wa ufanisi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulilenga kupima kama idara ya ukaguzi wa shule inatimiza azma yake ya kulinda elimu bora ya mafunzo katika shule za sekondari.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati baada ya kujadili taarifa hiyo inatoa ushauri ufuatao kwa Wizara na Serikali kwa ujumla:-

(i) Idara ya ukaguzi katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ichukue mtazamo wa matatizo zaidi, itengeneze mfumo wa kutafiti na kuongeza ufuatiliaji na kutathmini matokeo mabaya ya shule. Vipaumbele lazima vitolewe ili kuboresha uongozi wa shule na kuwataka wakaguzi waangalie sababu za ufaulu duni wa wanafunzi.

(ii) Kutokana na udhaifu wa Idara ya Ukaguzi wa Shule, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi iainishe vipaumbele vya idara. Aidha, suala la kuongeza ubora wa utoaji elimu ya hisabati na sayansi liwe moja ya vipaumbele vya Idara hiyo.

(iii) Wizara iweke mfumo mzuri wa mawasiliano ya taarifa za ukaguzi wa shule ili iweze kutumia taarifa hizo kufanya maboresho katika mifumo ya kusimamia ubora wa elimu itolewayo kwa wanafunzi.

(iv) Wizara ihakikishe kuna mfumo mzuri wa kufuatilia mipango ya Idara ya ukaguzi wa shule. Aidha, tathmini ya mafanikio ya Idara katika kukuza matokeo ya masomo ya hisabati na sayansi ifanyike mara kwa mara.

(v) Wizara ihakikishe kuwe na taratibu za kisheria ambazo zitafuatwa katika kubadilisha mitaala tofauti na ilivyo

sasa ambapo mitaala imekuwa ikibadilishwa mara kwa mara bila kufanya tathmini ya kutosha ya tija itakayopatikana.

(vi) Wizara itenge fedha za kutosha kwenye bajeti ya idara ya ukaguzi ili idara hiyo iweze kutimiza mipango na malengo yake kila mwaka. Aidha, fedha za wakaguzi zipelekwe Wilayani badala ya kuwa Makao Makuu.

(vii) Serikali inashauriwa kuwekeza zaidi kwenye elimu ya msingi kama inavyofanya kwenye elimu ya juu. Aidha, tathmini ifanyike kuhusu tija inayopatikana kwa Serikali kutumia fedha nyingi kwa mtihani wa kidato cha pili.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu ni ukaguzi wa ufanisi juu ya usimamizi wa miradi ya ujenzi wa barabara chini ya Afisa Masuuli wa Wizara ya Ujenzi. Ukaguzi wa ufanisi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ulilenga kuangalia kama Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara (*TANROADS*) wameweza kutambua matatizo ya ucheleweshaji wa miradi, ongezeko la gharama za ujenzi na matatizo ya ubora wa kazi katika usimamizi wa kazi za ujenzi wa barabara kwa lengo la kupunguza matatizo hayo kwa kutumia rasilimali zilizopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati yangu baada ya kujadili taarifa hiyo inatoa ushauri ufuatao kwa Wizara na Serikali kwa ujumla:-

(i) Wizara ya Miundombinu na *TANROADS* ziboreshe mchakato mzima wa shughuli za mwanzo za miradi, kama vile kutimiza masharti ya mkopo na taratibu za manunuzi.

(ii) *TANROADS* iwe na bajeti ya mradi mzima yenye udhibiti imara katika kipindi chote cha mradi. Kwa kila mradi, ni muhimu kuweka wazi wajibu na majukumu kati ya wahusika mbalimbali ili kudhibiti muda, gharama na masuala ya ubora. Aidha, kuna haja ya kuchukuliwa hatua ili kuongeza uwezo wa

*TANROADS* katika kutambua na kusimamia mapungufu yanayoweza kujitokeza.

(iii) Wizara na *TANROADS* waboreshe utunzaji wa kumbukumbu na kuanzisha daftari la kutunzia rekodi za utendaji wa wakandarasi na washauri kwa kila mradi wa barabara.

(iv) Wizara na *TANROADS* zinapaswa kuchukua hatua za makini ili kupunguza ongezeko la muda na gharama kwa kuendelea na jitihada zake za kuboresha uratibu wa taasisi za kutoa huduma (mfano, *TANESCO, DAWASCO*) na wahusika wengine ambao wanashiriki katika maeneo ya ujenzi wa barabara.

(v) Wizara na *TANROADS* zinapaswa kuwaajiri wataalam wenye uwezo, taaluma na uadilifu kwa ajili ya ufuatiliaji na ukaguzi wa miradi hata kama zitaendelea kushirikisha washauri kwa ajili ya kufuatilia utekelezaji wa miradi mbalimbali.

(vi) Serikali ihakikishe kuwa Wizara na *TANROADS* wanakuwa na uongozi wenye uwezo unaohitajika wa kusimamia kazi zake.

(vii) Wizara na *TANROADS* inapaswa kuamua juu ya kiwango cha usimamizi kwa wakandarasi. Kuna hatari ya *TANROADS* kujihusisha sana na majukumu ya wakandarasi. Hii inaweza kudhoofisha na kuvuruga utekelezaji majukumu kwa wakandarasi na usimamizi kwa upande wa *TANROADS*.

(viii) Wizara na *TANROADS* inapaswa kuweka bayana majukumu ya washauri wanaowatumia. Kwa mfano, kama kampuni ya ushauri inahusika katika kazi ya usanifu, ni vyema kufafanua katika mkataba kwamba kampuni itawajibika kulipa gharama zitakazosababishwa na mapungufu yake.

(ix) Serikali ifanye tathmini ya uwezekano wa kuweka wazi kwa umma maamuzi, mikataba na nyaraka muhimu za ujenzi wa barabara. Nyaraka za usanifu na ukaguzi wa mwisho zaweza kuwa wazi baada ya kukubaliwa na wahusika.

(x) Serikali itoe maelekezo ya wazi kwa *TANROADS* juu ya jinsi ya kusimamia washauri. Hii ni pamoja na kuunda Tume ya kufanyia marekebisho yenye lengo la kuziimarisha Wizara na *TANROADS* kwa kuzingatia uadilifu, taaluma, mikakati ya kiutendaji na masuala ya uwazi na uwajibikaji.

(xi) Serikali na *TANROADS* zichukue hatua za makusudi za kuboresha hatua za awali za utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha kuwa usanifu unaboreshwa ili ulingane na hali halisi na kuepuka mabadiliko yasiyo ya lazima yanayofanywa wakati wa ujenzi. Wizara ya Ujenzi na *TANROADS* zinapaswa kuweka utaratibu wa kupitia na kurekebisha usanifu na makadirio ya miradi baada ya kuandaliwa na washauri kabla ya ujenzi.

*(xii)* *TANROADS* iboreshe usimamizi wa mradi na mfumo wa udhibiti wa ubora ili kuepuka ucheleweshaji, kuongezeka kwa gharama na kulazimika kufanya ukarabati wa barabara muda mfupi tu baada ya kuanza kutumika.

(xiii) Wizara ya Ujenzi na Wakala wa Barabara Tanzania *(TANROADS)* watoe ripoti yenye tathmini ya ubora wa mfumo unaotumika kusimamia shughuli zote za ujenzi wa miradi ya barabara na kisha kutumia tathmini hiyo kuboresha mfumo uliopo ili Serikali iweze kudhibiti kupata tija kwenye miradi yake ya ujenzi wa barabara.

(xiv) Wizara iwape kipaumbele Wakandarasi na Washauri wa ndani hasa katika utoaji wa zabuni za kazi za ujenzi wa barabara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inapongeza hatua iliyofikiwa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali

kutoa taarifa za ukaguzi wa ufanisi na Kamati kuzijadili. Aidha, Kamati ingependa kuliomba Bunge lako Tukufu kuhakikisha kuwa taarifa zote zinazotolewa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ziwe zinaletwa Bungeni na kujadiliwa na Kamati zako kwa kuzingatia Kanuni za Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ziara za ukaguzi zilizofanywa na Kamati. Katika mwaka wa fedha wa 2011/2012 Kamati ilifanya ziara za kukagua thamani ya kazi katika maeneo yafuatayo:-

(i) Mradi wa maji wa Ziwa Victoria (Kahama-Shinyanga *Water Project*).

(ii) Mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Manchira, lililopo Mugumu, Serengeti.

(iii) Ujenzi wa Bwawa la Habiya lililopo katika Wilaya ya Itilima, Simiyu.

(iv) Ujenzi wa barabara ya Bariadi-Lamadi, Mkoa wa Simiyu.

(v) Ujenzi wa barabara ya Ndundu-Somanga, Mikoa ya Lindi na Pwani.

(vi) Miradi ya umeme kwa njia ya gesi Mkoa wa Mtwara.

(vii) Viwanja vya ndege Mikoa ya Lindi na Mtwara.

(viii) Ujenzi wa jengo lenye ghorofa 18 kwenye kiwanja namba 45 na 46 kilichopo Mtaa wa Chimara, Dar es Salaam uliofanywa na Wakala wa Majengo *(TBA)* kwa kuingia ubia na Mwekezaji *M/S Royale Orchard Inn*.

Mheshimiwa Naibu Spika, maoni na mapendekezo ya Kamati. Baada ya kupitia Hesabu zilizokaguliwa za Wizara, Mikoa na Idara zinazojitegemea, Kamati yangu imebaini mapungufu kadhaa katika baadhi ya mafungu, mafanikio katika mafungu mengine na changamoto kwa mafungu mengi. Kama nilivyoeleza katika sehemu zilizotangulia, bado Serikali ina changamoto kubwa katika kuhakikisha kuwa fedha za umma zinatumika vema, kwa matumizi yaliyokusudiwa lakini pia kwa kufuata sheria na taratibu zilizowekwa. Kamati yangu ina maoni na mapendekezo yafuatayo:-

Kwanza, Serikali kuhakikisha inaweka utaratibu wa kujadili na Bunge taarifa zitolewazo na wahisani *(PEFA reports)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza kuwa ili tuweze kukamilisha mzunguko wa uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma ni muhimu kwa Serikali kushirikiana na Bunge katika kujadili *PEFA reports*. Hivyo, Kamati yangu inapendekeza Serikali kuanzisha utaratibu utakaowezesha Wahisani kuwasilisha *PEFA Reports* kwa Bunge kupitia Waziri wa fedha na kisha Bunge kufanya majadiliano na Serikali kuhusu taarifa hizo kwa lengo la kuondoa mapungufu yanayotukabili au kujitokeza katika mchakato mzima wa kuandaa, kutumia na kusimamia Bajeti ya Serikali.

Pili, kuimarisha Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kutokuwa huru katika masuala yanayohusu ajira na maslahi ya Watumishi wake, Kamati inaliomba Bunge kuishawishi Serikali yafuatayo:-

(a) Kukubali umuhimu wa Ofisi ya *CAG* kuwa huru kama Katiba na Sheria ya Ukaguzi Na. 11 ya mwaka 2008 zinavyoelekeza; na

(b) Kukifanyia marekebisho kifungu Na 24 (2) cha Sheria ya Ukaguzi wa Umma ili *CAG* awe huru katika masuala yanayohusu ajira na maslahi ya Watumishi wa Ofisi yake.

Tatu, kuboresha utekelezaji wa Bajeti ya Serikali.

(a) Bajeti kuanza kutumika kwa wakati. Kamati ingependa kuishauri Serikali ifanye majadiliano na Bunge kuhusu uwezekano wa kubadili mzunguko wa bajeti ya Taifa ili kuruhusu mabadiliko ya tarehe za majadiliano kukamilika kabla au ifikapo tarehe 30 Juni ya kila mwaka ili kuipa Serikali muda wa kutosha kutekeleza mipango yake. Pia, Bunge liangalie uwezekano wa mjadala wa Wabunge kuhusu bajeti kuanza kwa kujadili bajeti za fungu moja moja na bajeti ya Taifa iwe ya mwisho kujadiliwa. Aidha, kwa kuzingatia kwamba bajeti za nchi za Afrika Mashariki husomwa siku moja, Serikali iwasiliane na nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kuwianisha mabadiliko yoyote yanayoweza kutokea.

(b) Kupunguza tatizo la ucheleweshaji na utoaji wa fedha pungufu. Ili kupunguza matatizo ya utoaji fedha pungufu na ucheleweshaji wa utoaji fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwenda kwa Wizara na idara mbalimbali za Serikali kwa ajili ya utekelezaji wa majukumu yao, Kamati inaendelea kushauri kuwa kasma zote muhimu za maendeleo zitengewe fedha za ndani ama zile za nje zenye uhakika, kutokana na uzoefu kuwa fedha zinazoahidiwa hazipatikani kwa muda muafaka katika mwaka husika wa fedha na wakati mwingine kutotolewa kikamilifu.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Kamati pia inashauri Serikali kutoingiza katika makisio ya bajeti ile mihadi ya fedha kutoka kwa Wahisani ambayo haijathibitisha upatikanaji na badala yake fedha hizo zinapotolewa na Wahisani ni ndipo Serikali ilete *Supplementary Budget* Bungeni kwa ajili ya kuidhinishwa. Kwa kufanya hivyo Serikali itaepuka kuwapa

wananchi matumaini ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo isiyotekelezeka.

(c) Ni kupunguza matumizi ya kuratibu Maonyesho ya Kitaifa. Kamati inaona kuna umuhimu mkubwa kwa Serikali kufanya tathmini ya fedha ambazo hutumika kwa shughuli za maonyesho ya Kitaifa kama Saba Saba, Nane Nane na Utumishi kwa mwaka na pia iangalie kiasi cha fedha ambacho kinatumika kwenye maonesho hayo lakini hakikukasimiwa kwenye bajeti ya Wizara na Idara za Serikali. Aidha, Serikali iwe wazi kuhusu kiasi cha fedha kitakachotumika kuratibu shughuli za Maonyesho wakati Bunge linapitisha Bajeti ya Taifa.

(d) Ni kudhibiti matumizi yaliyo nje ya bajeti na yasiyo na ulazima. Kufuatia uwepo na matumizi yaliyo nje ya Bajeti, Kamati yangu inaliomba Bunge kuiagiza Serikali kurekebisha Sheria ya Fedha ili Mlipaji Mkuu wa Serikali aongezewe uwezo wa kisheria utakaomwezesha kufanya maamuzi ya kudhibiti matumizi yaliyo nje ya bajeti iliyoidhinishwa na Bunge na yale yasiyo na ulazima. Aidha, ni vema Bunge likasimamia kwa karibu zaidi matumizi ya Bajeti kwa kuhakikisha kuwa matumizi yote ambayo yako nje ya Bajeti ni lazima yapate idhini ya Bunge. Kazi hiyo ya kusimamia matumizi ya Bajeti inaweza kufanywa na Kamati ya Bunge ya Fedha na Uchumi au kwa kuanzisha Kamati ya Bunge ya Bajeti *(Parliamentary Budget Committee)* kama ilivyo kwa Mabunge mengine yaliyoanzisha Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inashauri Wizara zote kutenga fedha kwenye bajeti zake za kila mwaka kwa lengo la kujenga majengo ya Wizara hizo ambayo yatatumika kama Ofisi badala ya kuendelea kupangisha na kulipa kodi kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali ifanye tathmini ya gharama zinazotumika katika ununuzi wa magari ya Serikali nje ya nchi hasa Japan kwani huuzwa kwa bei kubwa mno tofauti na mtu binafsi anaponunua. Aidha, hata mchakato wa

kuagiza huchukua muda mrefu na kusababisha gharama za ununuzi. Kamati inashauri Serikali kuingia kwenye *forward exchange rate contracts* inapofanya ununuzi wa magari kwa lengo la kudhibiti kupanda kwa gharama kunakotokana na kuyumba kwa sarafu yetu. Aidha, ni vema pia Serikali ikafanya tathmini ya gharama zinazotumika katika matumizi ya kila siku ya magari yote ya Serikali kwa lengo la kupunguza gharama hizo.

Nne, ni kuongeza mapato ya Serikali. Kufuatia Serikali kushindwa kufikia malengo iliyojiwekea katika ukusanyaji wa mapato, Kamati inapendekeza kuwa:-

(a) Serikali ipunguze misamaha ya kodi kwa kadri itakavyowezekana na iongeze wigo wa kodi kwa kuhusisha sekta isiyo rasmi.

(b) Mamlaka ya mapato iongeze jitihada katika kuhakikisha bajeti zake za makusanyo ya mapato zinakuwa za uhalisia zaidi.

(c) Mfumo wa uangalizi na udhibiti wa ndani katika Mamlaka ya Mapato unapaswa kuimarishwa ili kuhakikisha kuwa marejesho ya mapato na malipo ya kodi vinapitiwa kwa makini ili kubaini udanganyifu na mianya ya ukwepaji kodi kwa lengo la kuongeza mapato yatokanayo na kodi na kuzuia matumizi mabaya ya fedha za Serikali.

(d) Serikali inashauriwa kuchunguza sababu zilizofanya *TRA* ishindwe kukusanya kiasi kilichokadiriwa katika bajeti yake na kwa kushauriana na *TRA* ije na hatua madhubuti zitakazoondoa tatizo hilo la kutofikia malengo katika ukusanyaji mapato. Aidha, ni vema Serikali kwa kupitia *TRA* kuangalia upya sheria inayosimamia ukusanyaji wa mapato kwa lengo la kuainisha vyanzo vya mapato ambavyo *TRA* inatakiwa kukusanya kodi na kuangalia ni vipi ambavyo havijaanza

kutumika na vilevile kuongeza vyanzo vingine ambavyo havimo kwenye sheria hiyo kwa lengo la kuongeza mapato.

(e) Serikali kupitia *TRA* iongeze ukusanyaji mapato katika vyanzo vifuatavyo ambavyo Kamati inaona bado hatukusanyi kodi ya kutosha kutokana na sababu mbalimbali; Migodi ya madini, Rasilimali ya Gesi, *Uranium*, Makampuni ya Simu, sekta ya uvuvi na sekta ya kilimo na mifugo.

Tano, kuimarisha usimamizi na umiliki wa ardhi na majengo ya Serikali. Kufuatia Serikali kutokuwa na kumbukumbu za kutosha kuhusu mali zake na vile vile haina hatimiliki za majengo na viwanja vingi inavyomiliki. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inathaminisha mali zake na inakamilisha kwa haraka iwezekanavyo uanzishaji wa daftari la mali za kudumu za Serikali *(Fixed Assets Register)* ambalo litajumuisha vile vile mali za Serikali zilizopo nje ya nchi kwenye Balozi zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia uwepo wa usimamizi usioridhisha wa mali za Serikali zilizo chini ya Balozi zetu, Kamati inashauri Serikali yafuatayo:-

(a) Kufanya maamuzi ya haraka ya kujenga kwenye viwanja visivyoendelezwa na kukarabati majengo yote yaliyochakaa kwa lengo la kuyapangisha kwa faida.

(b) Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa ishirikiane na Wizara ya Fedha, Wakala wa Majengo *(TBA)* na Mifuko ya Hifadhi ya jamii *(PPF, NSSF, PSPF, GEPF, NHIF* na *LAPF)* katika kuhakikisha kuwa Serikali kupitia Balozi zake inatumia fursa zilizopo kwenye nchi hizo kama ya kutumia *Mortgage financing* kukarabati na kujenga majengo na kisha kupangisha kwa lengo la kuongeza mapato ya Serikali.

(c) Mamlaka ya Majengo *(TBA)* ipewe mamlaka ya kuingia mikataba ya kibiashara yenye lengo la kukarabati,

kujenga na hatimaye kupangisha majengo yaliyo chini ya Balozi zetu kwa lengo la kuongeza mapato yake.

(d) Serikali ilete Bungeni Muswada unaotamka bayana kuhusu mmiliki wa viwanja na majengo ya Serikali.

Sita, udhibiti wa madeni na mihadi ya Serikali. Kufuatia kuwepo kwa madeni na mihadi yenye thamani ya Shs.1,637,290,544,945 hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2010, Kamati yangu inashauri Serikali ijiepushe kuingia katika mihadi huku ikijua hakuna fedha zilizotengwa kwa ajili ya matumizi hayo na madeni hayo yawe yanaonyeshwa kwenye makisio ya bajeti ya mwaka unaofuata ili Bunge lijue kabla ya kuipitisha bajeti hiyo. Aidha, ni muda muafaka sasa kwa Serikali kufikiria kuchukua hatua kali kwa Maafisa Maasuli watakaoshindwa kuzingatia mfumo wa bajeti unaosisitiza dhana ya fedha taslimu.

Saba ni uzingatiaji wa Sheria ya Manunuzi na udhibiti wa matumizi yasiyo ya lazima. Kamati inapendekeza kuwa Sheria ya Manunuzi, Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na mapendekezo ya *CAG* katika eneo hili yazingatiwe kikamilifu.

Nane, uboreshaji wa ukaguzi wa ubora wa magari na bidhaa zitokazo nje ya nchi unaofanywa na *TBS*. Kamati inapongeza maamuzi ya Bunge yaliyofanywa mwaka jana ya kusitisha utaratibu wa kukagulia magari nje ya nchi *(pre-shipment inspection)* na kuitaka *TBS* kuanza utaratibu wa kukagua magari yote baada ya kutoka bandarini na mipakani yaani *post-shipment inspection*. Kufuatia azimio hilo kutotekelezwa, Kamati inashauri ifuatavyo:-

(i) Serikali imwajibishe Afisa Masuuli wa Wizara ya Viwanda na Biashara kwa sababu zifuatazo:-

(a) Kwa kushindwa kutekeleza azimio la Bunge la kusitisha utaratibu wa kukagulia magari nje ya nchi na badala yake kukagulia ndani ya nchi.

(b) Kwa kushindwa kusimamia Shirika la Viwango *(TBS)* mpaka limesababisha Serikali kupoteza jumla ya *USD* 18,348,540 *(Externalization of foreign currency)*.

(c) Kwa kuliletea Bunge marekebisho ya Sheria ya Viwango vya Ubora bila kulieleza hasara ambayo inaweza kusababishwa kwa kuendelea kukagulia magari na bidhaa nyingine nje ya nchi.

(ii) Bunge kuunda Kamati maalum itakayoshirikiana na Kamati ya Bunge ya Mashirika ya Umma *(POAC)* kwa ajili ya kufanya uchunguzi zaidi kuhusu ukaguzi wa magari na bidhaa nyingine unaofanywa na Shirika la Viwango *(TBS)*.

(iii) Wizara ilete Muswada Bungeni wa kukifanyia marekebisho kifungu cha 4(1)(s) cha Sheria ya Viwango ili kiweke bayana kuwa ukaguzi wa magari na bidhaa nyingine zitokazo nje ufanyikie ndani ya nchi.

Mhesimiwa Spika, kutokana na ziara zilizofanywa, Kamati inatoa maoni na ushauri ufuatao:-

(i) Kuhusu Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria "Kahama-Shinyanga *Water Project*, Kamati iliridhishwa na utekelezaji wa mradi huu kwa sababu ilikuta shughuli zote za mradi zimekamilika na mradi ulikuwa umeanza kutoa huduma ya maji kwa Mkoa wa Shinyanga na Mji wa Kahama. Aidha, Mradi huu unao uwezo wa kuzalisha kiasi cha mita za ujazo 80,000 kwa siku kwa sasa. Kamati inaishauri Serikali yafuatayo kuhusu mradi huu:-

(a) Mradi huu ni wa Kitaifa ambao umeigharimu Serikali zaidi ya Sh.250 bilioni. Kamati inashauri Serikali ihudumie

uendeshaji wa mradi huu mpaka mradi utapoweza kujiendesha baada ya kuunganisha watumiaji wengi zaidi katika Mikoa ya Shinyanga, Tabora na Singida. Aidha, kuendesha mradi huu kwa kutegemea wakazi wa Shinyanga mjini na Kahama ni kuwapa mzigo mkubwa ambao hawezi kumudu wa kulipa gharama kubwa za maji.

(b) Mpaka sasa ni asilimia 38% tu ya uwezo wa uzalishaji wa mradi ndiyo unaotumika na maji yanayotumika ni aslimia 50 tu ya maji yanayozalishwa. Kamati inashauri ili kuwe na tija katika matumizi ya mradi, Serikali ipanue wigo wa matumizi ya maji hayo kwa kuyasafirisha hadi mikoa na miji mingine ya jirani ili kuongeza kiwango cha matumizi.

(c) Kamati inashauri Serikali kuimarisha usambazaji wa maji katika vijiji vya jirani ili kuwawezesha na wao kupata huduma hiyo muhimu.

(ii) Kuhusu mradi wa Ujenzi wa Bwawa la Manchira lililopo Mugumu, Serengeti uliyoigharimu Serikali jumla ya Sh. 10,193,037,924.60, Kamati inashauri Serikali kuwa bei ya maji iwe ndogo ili kumwezesha mwananchi wa kawaida kumudu kutumia huduma hii muhimu na Serikali ipanue mradi wa usambazaji wa hudumu hii ya maji ya bwawa ambao uambatane na usafishwaji na utiaji wa dawa katika maji hayo ili yaweze kuwa safi na salama.

(iii) Mradi wa Bwawa la Habiya uliopo Itilima, Simiyu ulikadiriwa kutumia jumla ya sh.1,245,805,620. Mradi ulikadiriwa kukamilika ndani ya miezi minne na nusu na kazi za ujenzi zilianza tarehe 16.7.2009. Mpaka siku Kamati ilipotembelea mradi huu (tarehe 1 Juni, 2011) Mkandarasi alikuwa ameshalipwa Jumla ya Sh.337,353,598 ambazo ni sawa na asilimia 27.08 ya gharama ya mkataba, na mkataba ulikuwa umefikia asilimia 42. Hivyo Kamati inaishauri Serikali kupanga bajeti ya kutosha kwa miradi inayoianzisha na kutoa fedha hizo kwa wakati ili iwe na tija, Bajeti ya miradi yote ya mabwawa

ihusishe pia gharama za miundombinu ya kusambazia maji hayo kwa wananchi na ukadiriaji wa fidia kwa wananchi walio katika eneo la mradi uzingatie thamani halisi ya mali zilizopo katika eneo hilo ili kuondoa malalamiko yanayotolewa na wananchi kwa kunyimwa haki yao.

(iv) Kuhusu ujenzi wa barabara ya Bariadi-Lamadi Mkoani Simiyu mpaka sasa ujenzi wa barabara hiyo haujakamilika na Mkandarasi aliyepewa kazi hiyo hayupo kwenye eneo la ujenzi. Wizara ya Ujenzi iliiambia Kamati kuwa waliposhindwa kumlipa fedha zote ndipo aanze kazi Mkandarasi aligoma kuendelea na sasa Wizara, *TANROADS* na Mkandarasi huyo wako kwenye mazungumzo kuhusu kuanza ujenzi huo. Aidha, Kamati haikufurahishwa na kitendo za Mkandarasi huyo kupewa kazi zaidi ya moja wakati hana uwezo wa kifedha. Kamati inashauri Serikali kuhakikisha inaongeza juhudi za kuwaongezea uwezo Makandarasi wetu wa ndani (Watanzania) na kisha kuwapa kazi za ujenzi.

(v) Kuhusu ujenzi wa barabara ya Ndundu-Somanga inayounganisha Mikoa ya Lindi na Pwani, yenye urefu wa kilomita 60 mpaka sasa barabara hiyo haijakamilika na magari hukwama mara kwa mara ingawa ilitegemewa iwe imekamilika tangu Oktoba 2011. Sababu tulizoelezwa ni kwamba Mkandarasi hana fedha za kutekeleza mradi kutokana na *TANROADS* kuchelewa kumlipa deni lake la US$ 4,000,000. Kamati inaishauri Serikali kutoa fedha za miradi hasa ya ujenzi kwa wakati na Wizara isiingie mikataba wakati haina uhakika wa fedha. Aidha, *TANROADS* iendelee kusimamia ujenzi wa barabara hiyo ili ikamilike mapema isije kuendelea kuongeza gharama za ujenzi.

(vi) Kamati ilikagua Mradi wa Umeme kwa njia ya gesi Mkoani Lindi uitwao Somanga *Fungy*. Mradi ulianza mwaka 2005 na una uwezo wa kuzalisha *MWs* 7.5 kwa kutumia gesi inayochukuliwa kutoka bomba kuu linalosafirisha gesi kutoka Songosongo hadi Dar es Salaam. Lengo la mradi huu ni kutoa

huduma ya umeme kwa Wilaya za Mkuranga, Rufiji, Kilwa na Kibiti. Mpaka sasa maeneo yanayopata umeme ni Kilwa Wilayani pamoja na wanakijiji wachache walio karibu na barabara maana gharama za kuvuta umeme kwa aliye karibu na nguzo ni Sh.70,000 wakati kwa yule aliye mbali inabidi anunue nguzo kwa Sh.300,000 hivyo wanakijiji wa kawaida hawawezi kumudu gharama hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na hilo umeme unaotumika ni chini ya MW moja. Kamati, imethibitisha kuwa umeme unazalishwa wa kutosha, lakini hautumiki ipasavyo. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali kupitia *TANESCO* ifidie baadhi ya gharama za kuingiza umeme kwa wananchi ambao wana nia ya kuweka umeme katika nyumba zao lakini hawana uwezo wa kununua nguzo na vile vile Serikali itumie nishati ya gesi kwa ajili ya kupunguza uhaba wa nishati ya umeme unaoikabili nchi yetu.

(vii) Kamati ilitembelea mradi wa gesi uliopo Mnazi Bay, Mtwara. Mradi huo una visima vya gesi vinne ambapo kimoja tu ndio kinachofanya kazi. Umeme unaotolewa na kisima hiki ni *MWs* 18. Kama visima vyote vinne vingekuwa vinafanya kazi basi mradi huo ungeleta tija kubwa ambapo wawekezaji wangeweza kuanzisha viwanda vya mbolea, saruji na kufua umeme wa kutosha. Hivyo, Kamati inaishauri Serikali ifanye maamuzi haraka ya kuendeleza mradi huo ili visima vyote vifanye kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kutumia fursa hii kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati kuhusu Hesabu zilizokaguliwa za Wizara na Idara za Serikali kwa mwaka wa fedha 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mara nyingine naomba kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wenyeviti wa Bunge kwa kuendelea kuliongoza Bunge kwa uadilifu mkubwa. Nawatakia baraka za Mwenyezi

Mungu katika kuendelea kuitekeleza kazi nzito na muhimu tulizowakabidhi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa moyo na uadilifu mkubwa. Aidha, nawapongeza kwa kushiriki kikamilifu katika maandalizi ya Taarifa hii na kunipa heshima ya kuiwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza kazi zake, Kamati ilikuwa ikisaidiwa na Maafisa Waandamizi kutoka Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Idara ya Usimamizi wa Mali za Serikali na Kamishna wa bajeti. Nawashukuru sana kwa mchango wao wa kitalaam.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Daktari Thomas D. Kashillilah kwa kuiwezesha Kamati hii kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, nampongeza Katibu wa Kamati hii Ndugu Mathew Kileo kwa kuratibu shughuli zote za Kamati kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naliomba Bunge lako Tukufu lipokee Taarifa hii na kuijadili na hatimaye lipitishe mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali. Ahsante sana Mheshimiwa Cheyo tunakushukuru sana.

Mheshimiwa ulisimama kwa ajili ya Mwongozo ni wakati wako sasa.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako kutokana na taarifa ambayo ilikuwa ikisomwa sasa hivi na Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali kwamba mpaka sasa hivi hatunayo hapa, katika kusoma kwake alikuwa akituambia turejee maelezo ambayo yeye hakuweza kuyasoma.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa kwa *observation* hiyo. Nikiri kwamba tumegundua kwamba Waheshimiwa Wabunge hamna vitabu hivi ambavyo Mwenyekiti amekuwa akisoma muhtasari wake na nina nakala zake hapa. Ni jambo ambalo linashangaza sana ndio maana vijana wangu mezani hapa nimekuwa nikiwatoa mmoja baada ya mwingine sijui ni nani anayeshikilia hili jambo ili msipate mapema.

Kwa hiyo, tuwiane radhi lakini katika muda mfupi sana ujao mtapata vitabu hivi. Kwa kweli ni kosa ambalo halipaswi kutokea kwa Taasisi kama ya kwetu. Nawaomba tuendelee lakini tutapata katika muda usiokuwa mrefu kuanzia hivi sasa. Nimeshatuma watu wangu naamini ikibidi nitamtoa hata Katibu aliyebaki hapa na yeye vile vile afuatilie huko huko. Kwa kuwa wananisikia nimwombe Katibu wa Bunge awaambie vijana wake walete ripoti zinazosomwa hapa mara moja.

Naomba nimwite Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati za Serikali za Mitaa, Mheshismiwa Daktari Augustine Lyatonga Mrema.

**MHE. DKT. AUGUSTINE L. MREMA – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 114 (15) ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007, naomba kuwasilisha Bungeni Taarifa ya Mwaka ya

Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 120 ya Kanuni za Bunge (2007), muundo wa Taarifa hii upo katika sehemu kuu tatu. Yaani Sehemu hii ya utangulizi, sehemu ya pili inayohusu matokeo ya Ziara na Mahojiano ya Kamati na sehemu ya tatu ambayo inahusu Hoja ama Mapendekezo ya Kamati kuhusu masuala yaliyobainika.

Katika sehemu ya tatu, mapendekezo yatawasilishwa kama Hoja za Kamati kwa mujibu wa Kanuni ya 54(2) ili kuliwezesha Bunge lako Tukufu kuwa katika nafasi nzuri zaidi ya kuijadili na kuiasili (*adopt*) taarifa na hivyo kuyafanya mapendekezo kuwa Maazimio ya Bunge kwa Serikali. Kwa msingi huo, Kamati inataraji kuwa Serikali itawasilisha Bungeni majibu ya kina kuhusu hoja hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati hii ina wajumbe kumi na tano wafuatao:-

Mheshimiwa Daktari Augustino L. Mrema, Mwenyekiti; Mheshimiwa Idd M. Azzan, Makamu Mwenyekiti; Mheshimiwa Maida Abdalah, Mjumbe; Mheshimiwa Abdul R. Mteketa, Mjumbe; Mheshimiwa Godfrey W. Zambi, Mjumbe; Mheshimiwa Hasnain M. Murji, Mjumbe; Mheshimiwa Joseph R. Selasini, Mjumbe; Mheshimiwa Kafulila D. Zacharia, Mjumbe; Mheshimiwa Kuruthum J. Mchuchuli, Mjumbe; Mheshimiwa Omary A. Badwell, Mjumbe; Mheshimiwa Riziki S. Lulida, Mjumbe; Mheshimiwa Subira Khamis Mgalu, Mjumbe; Mheshimiwa Susan L.A. Kiwanga, Mjumbe; Mheshimiwa Tauhida C. Galos Nyimbo, Mjumbe na Mheshimiwa Zabein M. Mhita, Mjumbe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huduma ya mawasiliano, ushauri kuhusu shughuli na taratibu za Kibunge, uandishi wa taarifa na mihtasari, utafiti na uchambuzi wa masuala

mbalimbali ilitolewa na Katibu wa Kamati Ndugu Mswige Dickson Bisile akisaidiwa na Ndugu Waziri Kizingiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, hadidu za rejea za msingi kwa ajili ya Kamati hii ni majukumu yake ya Kikanuni ambayo yameainishwa katika Nyongeza ya Nane, Fasili Ndogo ya 12 ya Kanuni za Bunge, Toleo la 2007 kuwa ni:-

(a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za Serikali za Mitaa yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

(b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati ili kuondoa matatizo hayo.

(c) Kutoa mapendekezo na ushauri kwa Serikali za mitaa kuhusu matumizi mazuri ya fedha ili kuhakikisha kwamba tatizo la matumizi mabaya ya fedha linapungua katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati yamekuwa yakitekelezwa kwa njia kuu mbili ambazo ni mahojiano (mezani) kupitia Taarifa zilizokaguliwa za mapato na matumizi ya kila mwaka ya Halmashauri na kwa njia ya ziara za ukaguzi wa thamani na ukaguzi wa ufanisi katika utekelezaji wa miradi. Wakati mahojiano Mezani yamekuwa yakifadhiliwa na Ofisi ya Bunge, Ziara za Ukaguzi wa miradi zimekuwa zikifadhiliwa na Mradi wa Maboresho katika Usimamizi wa fedha za Umma (*Public Finance Management Reform Programme, PFMRP*) kupitia Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu mahojiano mezani. Hii ni mbinu kongwe, imekuwa ikitumiwa siyo tu na Kamati bali pia na vyombo mbalimbali vya kiuchunguzi duniani. Ni mbinu inayookoa gharama kwani wahusika (Halmashauri) huishia kuandaa majibu ya Hoja za Ukaguzi na

kuyawasilisha kwa watumiaji *(LAAC)*. Mbinu hii imekuwa ikitumiwa na Kamati tangia ilipoanzishwa, fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli za Kamati zimekuwa zikitengwa kwa ajili ya kukidhi mbinu hii. Katika Fungu 42, zimekuwa zikitengwa fedha kwa ajili ya kuiwezesha Kamati kufanya vikao Dodoma, Dar es Salaam au Zanzibar, siyo kufanya ziara za ukaguzi wa thamani (*Value for Money Audit*) na Ukaguzi wa Ufanisi (*Performance* Audit) katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Kwa upande wa pili, mbinu hii ni ya kizamani huangalia zaidi majibu na ukweli ulio katika maandishi kuliko majibu na ukweli halisi uliopo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hivyo, kwa watumishi ambao ni wataalam wa kuandika lakini hawana sifa ya kuwa wakweli na waaminifu, mbinu hii inaweza kutumiwa kumlaghai mtumiaji wa taarifa kwa sababu inaonesha ukweli ulio katika maandishi na siyo ukweli ulio katika mradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, Ukaguzi wa Thamani na Ukaguzi wa Ufanisi ni mbinu za kisasa ambazo zimeasiliwa (*adopted*) katika Ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa njia ya ukaguzi wa thamani, Kamati au Mkaguzi hujiridhisha papo hapo uwiano uliopo kati ya majibu yanayotolewa na mtekelezaji wa mradi na uhalisia wa mradi anaouona. Wakati katika Ukaguzi wa Ufanisi (*Performance Audit*) Kamati au Mkaguzi hujiridhisha na namna kazi ilivyofanyika kwa kuzingatia miongozo na matumizi ya mradi husika kwa jamii husika.

Hivyo, kwa kutumia mbinu hizi, ni rahisi kupima tija itokanayo na matumizi halisi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo nchini. Na ni rahisi pia kwa Kamati kuepuka kudanganywa. Hizi ni mbinu sahihi zaidi kutumiwa na Kamati inayosimamia nidhamu ya matumizi ya fedha za umma hasa fedha ambazo matumizi yake yalishafanyika miaka kadhaa iliyopita. Mbinu hizi humwezesha Mkaguzi kujiridhisha na kilichotendeka ama kinachoendelea

kutendeka. Mbinu zote mbili hutekelezwa kwa upana zaidi kwa njia ya ziara.

Kwa upande wa pili, mbinu hizi ni ghali kifedha na muda kwani zinahitaji muda na fedha kwa ajili ya kutafiti hali halisi ya mahali pa ukaguzi, kusafiri, kutunza kumbukumbu, malazi na kadhalika wakati wa kufanikisha ukaguzi wa miradi. Hata hivyo, wahenga walisema *vizuri ni gharama!*

Ni maoni ya Kamati kwamba, kwa kuwa *CAG* naye kwa sasa ameanza kutilia maanani zaidi Ukaguzi wa Thamani na Ukaguzi wa Ufanisi, Kamati za Bunge nazo ziwezeshwe ili zijikite zaidi katika Ukaguzi wa aina hii ili kujiridhisha na tija itokanayo na kodi za wananchi na kuimarisha nidhamu ya matumizi ya kodi hizo Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamekuwepo na maboresho kadhaa katika utendaji wa Kamati hasa katika maeneo matatu yafuatayo:-

(a) Halmashauri kuhojiwa kwa kuzingatiwa uzito wa hoja za Ukaguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali Kamati ilirithi kutoka kwa watangulizi wake utaratibu wa kuzitaka Halmashauri zilizopo katika kila Mkoa kuwasilisha Taarifa za Hesabu zao mbele yake. Kufuatia ongezeko la Idadi ya Halmashauri nchini ambalo haliwiani na uwezo wa muda na fedha za uendeshaji wa shughuli za Kamati, imeonekana kuwa ni vema Kamati ikajikita katika kuzihoji Halmashauri ambazo maoni ya wakaguzi yamebainisha kuwa zina matatizo zaidi katika matumizi ya fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, rai ya Kamati ni kwamba Halmashauri isipoitwa mbele yake katika mwaka fulani wa fedha isibweteke kwani ratiba inaweza kubadilishwa wakati

wowote na Halmashauri yoyote ikaitwa kulingana na taarifa za kiuchunguzi zinazoweza kuwa zimepatikana katika muda huo.

Pili, kutoziita baadhi ya Halmashauri kunatakiwa kuwa kichocheo kwa Ofisi za Makatibu Tawala wa Mikoa, Mabaraza ya Madiwani, Watendaji wenyewe, na wananchi kwa ujumla kuwa Wazalendo, waaminifu na waangalizi madhubuti wa fedha na mali za umma. Kamati inatambua umuhimu wa watumishi wa umma katika Halmashauri na inasisitiza kwa watumishi hao kujijengea sifa za kuaminika katika matumizi ya fedha za umma kwa manufaa ya umma. Inawapongeza wale wote waliopo katika nafasi zao na kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

(b) Kupungua kwa Idadi ya Maafisa Wanaohudhuria Vikao.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali Wakuu wa Idara, Sehemu na Vitengo katika kila Halmashauri walikuwa wanahudhuria vikao vya uwasilishaji wa Taarifa za Halmashauri kwenye Kamati. Kitaalam tathmini ya Kamati imebaini kuwa utaratibu huu unazigharimu Halmashauri kiasi kikubwa sana cha fedha kwa ajili ya kukamilisha zoezi hilo. Aidha, ilibainika pia kuwa utaratibu huu ni kinyume na miongozo ya kisheria (Sheria ya Fedha za umma, 2001, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982 na Hati ya Makubaliano ya fedha za Serikali za Mitaa, 1997) kuhusu Maafisa wawajibikaji katika Taarifa za fedha katika taasisi za umma.

Kwa tathmini hiyo, Kamati imeweka utaratibu kwamba katika kuwasilisha Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Halmashauri, Afisa Masuuli wa kila Halmashauri ataambatana na Mweka Hazina, Afisa Mipango (Mchumi), Mkaguzi wa Ndani na Mhandisi wa Ujenzi wa Wilaya. Katibu Tawala wa Mkoa na Wastahiki Mameya au Waheshimiwa Wenyeviti wa Halmashauri Watakuwepo katika Vikao hivyo kwa ajili ya kusaidia kutoa Maelezo ambayo Kamati itaona inafaa. Kwa

kutumia utaratibu huu mpya, siyo tu kwamba gharama za uwasilishaji wa Taarifa zitapungua lakini pia Maafisa Masuuli watajengewa umahiri katika kuielewa na kuielezea miradi ya maendeleo inayotekelezwa katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pia utaratibu huu mpya utawezesha timu ya Wataalam kadhaa wenye madaraka kamili katika idara zao kuendelea kuwepo katika maeneo yao ya kazi wakati wa vikao vya Kamati vikiendelea. Awali Wakuu wa Idara zote, Vitengo na Sehemu walikuwa wanahudhuria uwasilishaji wa Taarifa kwenye Vikao vya *LAAC* hivyo kuleta ombwe la maamuzi katika Halmashauri kwa muda wote waliokuwa katika uwasilishaji.

(c) Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo kupewa kipaumbele.

Mheshimiwa Naibu Spika, miradi ya maendeleo hutekelezwa kwenye maeneo ya watu siyo vitabuni. Hivyo, Kamati inaona ni vema kutumia muda wake mwingi katika kujiridhisha na utendaji wa Serikali katika kutekeleza miradi hiyo kwa kufanya ziara za ukaguzi wa miradi hiyo kuliko kutumia muda mwingi kukagua vitabu mezani bila kuiona miradi yenyewe. Bila ya ukaguzi wa miradi itakuwa ni vigumu kwa Kamati kuliletea Bunge Taarifa zenye ushahidi kuhusu ufanisi na tija itokanayo na matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri.

Kadhalika hoja hii inapata nguvu kutokana na ukweli kwamba Taarifa zinazowasilishwa mbele ya Kamati ni zile ambazo matumizi yake yalikwisha fanyika miaka kadhaa iliyopita. Hivyo, ni vema kuona matumizi haya kwa kuikagua miradi iliyotumia fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika hili, maoni ya Kamati ni kwamba pawepo sasa na dhamira ya makusudi ya Serikali na Bunge lako Tukufu kutenga fedha kwa ajili ya Kamati za fedha

za umma na Kamati za Bunge kwa ujumla kufanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo ili kujionea uhalisia au ukweli uliopo katika utekelezaji wa miradi hiyo. Hapa dhana ya Bunge kuisimamia Serikali katika kutekeleza sera zake kwa wananchi itaweza kukamilika na kuleta tija. Kamati inashukuru kwamba hata Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ameliona hilo na ameanza kuwa madhubuti zaidi katika kufanya Ukaguzi wa thamani (*Value for Money Audit*) na Ukaguzi wa ufanisi (*Performance Audit*) katika miradi mbalimbali

(d) Kuimarika kwa uhusiano baina ya Kamati na wadau.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa inatambua umuhimu wa mawasiliano kati yake na wadau wengine mathalani Kamati zingine za Bunge ndani ya Tanzania na nje ya Tanzania katika nchi marafiki, Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, Wizara mbalimbali hususani TAMISEMI na Wizara ya Fedha na Uchumi, Asasi za Kiraia, Waandishi wa Habari, vyuo, watafiti mbalimbali na kadhalika. Uhusiano wetu na taasisi hizo katika kupokea Taarifa zilizotafitiwa kwa ajili ya kuimarisha utendaji wa Halmashauri zetu uko wazi. Tunawakaribisha sana ilimradi watazingatia Sheria, Kanuni na taratibu za Kibunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika sehemu ya kwanza imeelezwa kwa kifupi kuhusu Wajibu wa Kamati kuwasilisha kila mwaka taarifa ya utendaji kazi wake Bungeni, Majina ya wajumbe wa Kamati, majukumu ya msingi ya Kamati na maboresho yaliyofikiwa katika utendaji wa Kamati. Sehemu ya pili ya taarifa hii itaeleza kwa uchache mambo mbalimbali yaliyobainika wakati wa Ziara za Kamati na wakati wa kujadili taarifa za Halmashauri mezani. Maelezo yaliyopo katika sehemu ya pili ndiyo yatakayosaidia kimsingi kuunda na kuwasilisha hoja au mapendekezo ya Kamati katika sehemu ya tatu ya taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili inahusu uchambuzi kuhusu ruzuku ya maendeleo katika Halmashauri, usimamizi wa ruzuku hiyo na matokeo ya mijadala ya taarifa za ukaguzi na ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, ni uchambuzi kuhusu ruzuku ya maendeleo katika Halmashauri. Kwa ujumla, mfumo wa utoaji wa ruzuku kwa Serikali za Mitaa nchini ni mzuri kwani unaiwezesha Serikali Kuu kujua mgawanyo wa fedha za umma kwa Halmashauri zote. Mgawanyo huu huridhiwa na Bunge kupitia katika vikao mbalimbali. Hivyo, ni mfumo ambao unaruhusu kujua wahusika na kipindi cha uhusika wao katika utoaji, upokeaji na utumiaji wa ruzuku hiyo. Kamati inaona dosari zilizopo ni katika kasi ya kupeleka fedha zilizoidhinishwa na Bunge kwenye Halmashauri, uwazi na uwajibikaji wa watendaji katika Mfumo huo ili uweze kuleta tija inayotarajiwa.

Aidha, chini ya mfumo huu, ruzuku ya maendeleo katika Serikali za Mitaa nchini hutolewa kupitia Mfuko wa Ruzuku ya Maendeleo ya Serikali za Mitaa, yaani *the Local Government Development Grant (LGDG)*. Katika Mwaka wa Fedha 2009/2010, jumla ya shilingi 2,274,157,800,000 zilitengwa na Serikali Kuu kama ruzuku ya maendeleo na matumizi ya kawaida kwa Halmashauri zote 133 nchini. Kati ya kiasi hicho, shilingi 1,617,270,700,000 milioni zilikuwa ni kwa ajili matumizi ya kawaida (*Recurrent Expenditure*) wakati shilingi milioni 656,887,000,000 zilikuwa ni kwa ajili ya shughuli za maendeleo. Kwa mgawanyo huu maana yake ni kwamba, Serikali inaziwezesha Halmashauri kula zaidi kuliko kuzalisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mgawanyo wa ruzuku kwa namna hii, ni vigumu zaidi kuona maendeleo ya uhakika katika Halmashauri zetu. Kwa sababu fedha za uzalishaji ni kidogo kuliko zile za matumizi ya kawaida. Matokeo yake itazidi kuwa vigumu kuona maendeleo na ukuaji halisi wa uchumi vijijini. Hivyo, tutegemee zaidi ongezeko la uhamiaji wa watu

kutoka vijijini kuja mijini kwa matumaini ya kupata huduma bora za jamii mijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, ni kuhusu matokeo ya taarifa za ukaguzi na ziara za Kamati. Kwa njia ya taarifa na Ziara za Ukaguzi wa thamani na ufanisi, Kamati iliweza kubaini matatizo sugu yafuatayo yenye kuashiria ama kuchangia matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri:-

Moja, udhaifu katika ukusanyaji wa mapato ya Ndani ya Halmashauri. Udhaifu huu unasababishwa na sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(a) Udhaifu katika mipangilio ya Halmashauri katika kukusanya mapato kutokana na kiasi kidogo cha utaalam na teknolojia katika kutathmini unyumbufu wa vyanzo vya mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu huu ulidhihirika baada ya Kamati kubaini kuwa makadirio ya Halmashauri nyingi kukusanya mapato yao kwa mwaka siyo halisia (*unrealistic annual own source revenue collection estimate*s). Kamati ilipobaini udhaifu huu, ilizipangia baadhi ya Halmashauri kiasi cha kukusanya kwa mwaka na zikatimiza (mfano, katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010, Hanang iliagizwa kukusanya 450 milioni ikakusanya 650 milioni) wakati mipango yao haikuwa ya kufikia kiasi hicho. Hii inatoa picha kwamba mipango ya baadhi ya Halmashauri kuhusu ukusanyaji wa mapato haya siyo halisia. Suala la mipango kutokuwa halisia nalo linastahili uchunguzi kadri muda utavyoruhusu.

(b) Mikataba na miradi isiyo na tija. Uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba kuwepo kwa Mikataba na miradi ya maendeleo isiyofanyiwa upembuzi yakinifu wa kisheria au kimapato kunachangia sana udhaifu wa mapato ya ndani ya Halmashauri hizi.

Mikataba mingi ya Halmashauri na mawakala wa kukusanya mapato ya ndani inanufaisha zaidi mawakala kuliko Halmashauri zenyewe. Kwa mfano:-

(i) Mkataba wa Ukusanyaji ushuru wa maegesho ya magari katika maeneo yasiyo rasmi kati ya Jiji la Dar es Salaam (2005 - 2013). Katika Mkataba huo, ilikubalika kwamba Jiji liwe linapata mgao wa shilingi 50,500,000/= kila mwezi kwa muda wote huo bila ya kujali ongezeko la magari mjini. Kamati inaipongeza Halmashauri ya Jiji kwa kuona tatizo hilo kisha kuuhuisha Mkataba husika. Ni vema Halmashauri zingine zikaona uwezekano wa kuhuisha Mikataba ya ukusanyaji wa mapato ambayo inaziingiza hasara.

(ii) Katika Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni kulikuwa na Mkataba wa manunuzi ya trekta za kuzoa taka. Katika manunuzi hayo, Manispaa ilimlipa Mzabuni kiasi cha shilingi milioni 55.6 zaidi ya kiasi stahiki.

(iii) Upo Mkataba usioeleweka kati ya Manispaa ya Kinondoni na Mwekezaji *M/S Oysterbay Villas Limited* kuhusu umiliki wa jengo usiokuwa na ukomo. Jengo hilo limekamilika lakini mpaka sasa Halmashauri haipati gawio lolote!

(iv) Upo Mkataba wenye utata pia katika ujenzi wa vyumba vya madarasa katika shule ya Sekondari ya Ananasifu. Mradi mmoja una mikataba miwili yenye kiasi tofauti cha fedha na waingia Mkataba tofauti kwa upande wa Halmashauri ya Manispaa ya Kinondoni. Mkataba mmoja unaonesha gharama za mradi ni shilingi milioni 800 wakati mwingine unaonesha gharama za ujenzi wa mradi ni shilingi milioni 500.

Mheshimiwa Naibu Spika, ipo miradi ambayo inatekelezwa katika Halmashauri ikiwa ni hasara kwa Halmashauri zenyewe. Kwa mfano, mnamo mwaka 2004 Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam (Jiji, Temeke, Kinondoni na Ilala) zilikubaliana kuanzisha mradi wa pamoja

wa machinjio katika maeneo ya Gongo la Mboto. Katika mradi huo Halmashauri zilichangia jumla ya shilingi 2, 009, 265, 976/= kutokana na mapato yao ya ndani.

Wabia wengine katika mradi huo walikuwa ni Kampuni ya *R&M* kutoka Malayasia Kampuni ya *East African Meat (EAMEATCO)*. Kamati haikuweza kubaini mara moja namna wabia hao walivyopatikana na kiasi walichochangia kwenye mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu mradi haujawahi kufanya kazi hata siku moja! Lakini fedha zilizochangwa zimetumika. Swali hapa ni zimetumikaje na zimetumiwa na nani?

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, Mipango ya kibabe ya Serikali Kuu katika vyanzo vya mapato vilivyoko kwenye Halmashauri. Kamati inaona kuna namna mbalimbali ambazo maamuzi ya Serikali Kuu yanachangia katika udhaifu huu. Kwa mfano:-

(i) Kuingia kwa Mamlaka ya Mapato nchini *(TRA)* katika kukusanya kodi ya majengo katika Halmashauri za Manispaa. Maelezo ya watendaji wa Manispaa zilizofanyiwa majaribio ya utaratibu huu ni kwamba haufai kuendelea. Ni utaratibu uliodidimiza zaidi mapato ya Halmashauri hizo kuliko kuyaongeza.

(ii) Kuchelewa kupeleka ama kutopeleka kabisa gawio linalotokana na mauzo ya nje ya korosho ghafi katika Halmashauri zinazotegemea korosho kama chanzo kikuu cha mapato. Suala hili limewahi kutolewa kwenye Taarifa ya Mwaka ya Kamati (2008/2009) japokuwa Serikali haikutoa majibu kabisa.

(iii) Kuuzwa kwa mali za Halmashauri bila mawasiliano na ushauriano na Halmashauri zenyewe. Kwa mfano, katika Mwaka 2008 Serikali Kuu iliuza nyumba za

Manispaa ya Temeke zilizopo Masaki pasipo mawasiliano na Manispaa husika.

(iv) Kukumbatia vyanzo mbalimbali vya mapato (ushuru wa minara ya simu, usajili wa zahanati, kodi ya ardhi na kadhalika) katika maeneo ya Halmashauri. Vyanzo vingi vya mapato ambavyo serikali Kuu imeziachia Halmashauri ni vile ambavyo uzalishaji wake kwa mwaka siyo imara *(unstable sources of revenue*) kama vile ushuru wa kuzoa taka na ushuru wa mazao. Aidha, vyanzo hivyo vina usumbufu mkubwa sana katika ukusanyaji.

Mbili, mishahara kwa watumishi hewa. Tatizo hili bado linaendelea. Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya *CAG* kwa mwaka wa fedha ulioishia 30, Juni, 2010 unaonesha kuwa kiasi cha shilingi 583,221,297 kililipwa kama mishahara kwa watumishi hewa.

Kiasi hicho cha mishahara kwa watumishi hewa kwa mwaka huo kingetosha kuchangia ujenzi wa vyumba 194 vya madarasa katika Mpango wa Maendeleo ya shule za Msingi (MMEM) ambapo shilingi milioni tatu hutolewa na Serikali kwa kila darasa. Maoni ya Kamati ni kwamba, Bunge liitake Serikali kutoa Taarifa ya Mpango Mkakati wa Halmashauri katika kushughulikia tatizo hili kabla halijakomaa na kuwa sugu zaidi.

Tatu, manunuzi yasiyozingatia taratibu. Pamoja na kuwepo kwa miongozo mbalimbali ya Kisheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma (2004), inashangaza kuona kwamba bado matatizo ya malipo yasiyokuwa na hati, malipo yenye nyaraka pungufu na manunuzi bila ya taratibu sahihi tenda. Katika mwaka ulioishia 30 Juni, 2010, jumla ya shilingi zisizopungua bilioni nane zilibainika kutumika katika manunuzi yasiyokuwa na nyaraka na yenye nyaraka pungufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, shaka ya Kamati katika hali kama hii inakuwa ni kujiuliza kama kweli fedha hizo zililipwa kwa

ajili ya huduma zilizotolewa kwa manufaa ya wananchi. Kwa mtazamo wa Kamati, hivi ni viashiria vya kupungua kwa nidhamu ya matumizi ya fedha za umma ndani ya Serikali.

Nne, udhaifu katika kusimamia utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Udhaifu huu, ulibainika katika Ziara za Kamati kwenye Halmashauri mbalimbali. Miradi mbalimbali ya maendeleo hutekelezwa kwa viwango hafifu au kwa kuchelewa au haitekelezwi kabisa kwa sababu mbalimbali ikiwa ni pamoja na:-

(a) Mara nyingine Serikali Kuu haipeleki kwa wakati ruzuku kwa ajili ya kutekeleza miradi hiyo;

(b) Mara nyingine Serikali Kuu haipeleki kiasi chote cha ruzuku iliyoombwa kwa ajili ya utekelezaji wamiradi husika; na

(c) Kukosekana kwa usimamizi wa kitaalam wa miradi husika.

Kwa mfano, katika ujenzi wa bweni la Ukombozi katika shule ya Wasichana ya Kipok Wilayani Monduli, kiasi cha shilingi milioni 14 kilitolewa kwa Mkandarasi pasipo Mhandisi wa Wilaya kufanya ukaguzi wa kazi iliyofanyika. Aidha, Katika Halmashauri ya Wilaya ya Monduli, shilingi milioni 16 zililipwa zaidi kwa Mzabuni aliyesafirisha chakula cha njaa bila ya kufanya marekebisho kwenye Mkataba wa awali wa malipo hayo.

Mara nyingine katika baadhi ya Halmashauri baadhi ya miradi hutekelezwa pasipo hata Mabaraza ya Madiwani kujua miradi hiyo inavyotekelezwa. Kwa mfano, ujenzi wa Bwawa la Oldonyosambu kwa ajili ya kunyweshea mifugo katika Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. Bwawa hili limegharimu kiasi cha shilingi milioni 92 lakini ubora wa kazi ni wa kutia shaka. Lipo pia suala la ujenzi wa daraja katika barabara ya Kosovo – Orarashi, Wilayani Monduli. Katika barabara hii, Madiwani

hawafahamu ni nani aliyejenga daraja hilo kati ya Halmashauri na Mkandarasi binafsi, *Big Game*.

Sanjari na maelezo hayo hapo juu, imebainika pia kupitia ziara za Kamati kwamba katika baadhi ya Halmashauri fedha za ujenzi wa shule za sekondari za Kata zinapelekwa katika Mabaraza ya Madiwani badala ya Bodi za Shule husika. Utaratibu huu ni kinyume na misingi ya utawala bora na mgawanyo wa majukumu. Mabaraza ya Madiwani ni vyombo vya kusimamia utekelezaji wa Mipango ya Serikali katika Halmashauri siyo vyombo vya utendaji. Hali hii ikiachwa iendelee, itakuwa ni vigumu kwa Madiwani kujitathmini na kujikosoa pale wanapokosea. Hali hii ilibainika katika Manispaa ya Arusha Kamati ilipofanya ukaguzi wa ujenzi wa maabara katika Shule ya Sekondari ya Naura.

Tano, watumishi wabadhirifu kuhamishiwa sehemu nyingine ndani ya Serikali. Ziara za Kamati zimetoa mwanga kwamba ipo tabia ya Serikali kutochukua hatua dhidi ya ubadhirifu wa fedha na mali za umma. Kamati imejiridhisha kutoka katika Halmashauri mbalimbali kwamba watuhumiwa wa ubadhirifu wamekuwa wakihamishwa na kupelekwa katika sehemu mbalimbali ndani ya Serikali za Mitaa na, au Serikali Kuu badala ya kuchukuliwa hatua za kisheria. Mifano michache ni kama ifuatavyo:-

(a) Ndugu Materu aliyekuwa Afisa kilimo na Mifugo *(DALDO)* amehamishiwa katika Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Lindi akitokea Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa. Lakini ameacha matumizi mabaya ya fedha za miradi ya kilimo huko Kilosa.

(b) Ndugu Elly Jese Mlaki alihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Babati lakini akiwa ameacha masuala mengi yasiyofaa katika matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri ya Wilaya Kishapu. Kadhalika Ndugu Emmanuel Masele aliyekuwa Mweka Hazina katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu alihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Rombo;

huku Afisa mipango wa Wilaya hiyo akihamishiwa Halmashauri ya Wilaya ya Ngara.

Sita, Wakuu wengi wa Idara Kukaimu. Tatizo la Watumishi kukaimu nafasi za Ukuu wa Idara katika Halmashauri mbalimbali nchini linazidi kukua na kuchangia ulegevu katika kusimamia maamuzi mbalimbali na matumizi ya fedha za umma nchini. Ni tatizo linalopunguza kasi ya wanaokaimu kuwajibika ipasavyo katika maamuzi wanayoyasimamia. Mifano dhahiri ipo kutokana na yaliyojili katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, Monduli na Jiji la Arusha na kadhalika.

Kamati imebaini kuwa sababu kubwa ya Wakuu wengi wa Idara kukaimu inatokana na utaratibu wa Serikali kwamba ili mtumishi aweze kuwa Mkuu wa Idara, sharti, pamoja na sifa zingine, awe na uzoefu usiopungua miaka saba kazini. Lakini katika mtazamo mwingine, inawezekana kwamba umakini wa Wizara husika kuratibu nafasi za utumishi katika Serikali za Mitaa ukawa na ulegevu kiasi cha kushindwa kung'amua haraka uwepo wa tatizo hili na madhara yake.

Saba, tofauti ya kiasi cha matumizi katika taarifa zinazokwenda kwa *CAG* na *LAAC*. Taarifa za Hesabu za Mwisho za Halmashauri (*final statements of accounts*) katika mwaka fulani wa fedha ndizo zinazotumiwa na *CAG* kutoa aina ya Hati ya Ukaguzi (*Qualified, Unqualified, Adverse or Disclaimer Audit Certificate*). Katika hali ya kawaida, maudhui ya taarifa hizi (kimapato na matumizi) hayapaswi kutofautiana na yale yaliyomo kwenye taarifa zinazowasilishwa mbele ya *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, imekuwa ni vigumu sana kwa Kamati kuziacha tofauti hizi zikishamiri bila ya kutaka majibu ama ufafanuzi wa Serikali. Hivyo, ni maoni ya Kamati kwamba Bunge lako Tukufu litake sasa maelezo ya kina ya Serikali kuhusu tofauti hizi na zinavyosababishwa. Jedwali lifuatalo

linaonesha baadhi ya mifano iliyobainika katika uchambuzi wa Taarifa za Halmashauri kwa Mwaka wa Fedha wa 2009/2010:-

**Jedwali Na 1. Tofauti za Mapato au Matumizi ya Halmashauri katika taarifa zinazowasilishwa kwa CAG na LAAC**

| **Na.** | **Halmashauri** | **Mwaka wa Fedha** | **Kiasi cha Matumizi kilichooneshwa kwenye Taarifa zilizowasilishwa kwa *CAG* (*Final Accounts*)** | **Kwenye Taarifa zilizowasilishwa *LAAC*** | **Maelezo H/Shauri kwenye kuhusu tofauti** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mtwara-M/ndani | 2009/10 | 9.3 Bil | 6.3 Bil | - |
| 2 | Tandahimba | 2009/10 | 12.1 Bil | 7.9 Bil | - |
| 3 | Kigoma (Man) | 2009/10 | 9.1 Bil | 5.2 Bil | - |
| 4 | Handeni | 2009/10 | 14.5 Bil | 12.1 Bil | - |
| 5 | Temeke (Man) | 2009/10 | 29.3 Bil | 38.5 Bil | - |
| 6 | Ilala (Man) | 2009/10 | 52.7 Bil | 50.2 Bil | - |
| | **JUMLA** | | **127 Bil** | **120.7 Bil** | **-** |

Nane, ruzuku ya miradi ya maendeleo kutopelekwa kwa wakati. Katika ziara za Kamati ilibainika kwamba baadhi ya miradi ya mendeleo katika baadhi ya Halmashauri haikutekelezwa kwa wakati ama imetekelezwa chini ya viwango. Miongoni mwa sababu ni kwamba Serikali Kuu haikupeleka ruzuku kwa wakati na kwa kiasi stahiki. Mara nyingi kutopeleka fedha kwa wakati na kwa kiasi stahiki kumezisababishia Halmashauri kubadili matumizi ya fedha hizo au kuzitumia pasipo mtiririko mzuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, tatu, ukaguzi maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Mnamo tarehe 9 Machi, 2012, *CAG* aliwasilisha Bungeni Taarifa ya Ukaguzi Maalum katika Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu.

Taarifa imewataja vinara wa ubadhirifu huu kuwa ni Ndugu Muhidin Mohamed (Mweka Hazina), Walugu Mussa (Mtunza fedha wa Halmashauri), Ndugu Boniface Nkumiming na Mhandisi wa Halmashauri Ndugu Leonard Mashamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ajabu zaidi ni kwamba matukio ya ubadhirifu wa fedha hizi yanawagusa watumishi wa Benki ya *NMB,* Tawi la Manonga, Shinyanga kwa kulipa fedha bila kuzingatia taratibu. Jedwali lifuatalo linatoa picha ya ubadhirifu huo kwa kuonesha mifano michache tu:

**Jedwali Na. 2. Matukio ya Ubadhirifu wa Fedha za Umma Kishapu**

| Na. | Aina ya Ubadhirifu | Kiasi cha Fedha katika Ubadhirifu | Mwaka wa Fedha Uliohusika | Rejea |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Malipo yenye shaka kutokana na mapungufu ya nyaraka na udhaifu katika usimamiziwa mikataba na miradi | 4.2 Bil | 2008/9-2009/10 | NAOT |
| 2 | Uhamisho wa fedha bila idhini ya DED na kuzitumia kinyume na malengo | 1.6 Bil | 2009/10 | NAOT |
| 3 | Uhamisho wa fedha ambao haukufika kwenye akaunti zilikokuwa zinahamishiwa | 1.95 Bil | 2009/10 | NAOT |
| 4 | Malipo kwa Walipaji wasiofahamika | 689.5 mil | 2009/2010 | NAOT |
| 5 | Manunuzi ya mafuta ya magari (pertroli na dizeli)kwa matumizi yasiyofahamika | 42.1 Mil | 2008/9- 2009/10 | NAOT |
| 6 | Hati za Malipo ambazo hazikuidhinishwa | 221.8 Mil | 2009/10 | NAOT |
| 7 | Kutotekelezwa kwa Miradi 14 ya maendeleo kutokana na ubadhirifu wa fedha | 532.4 Mil | 2007/8 - 2009/10 | NAOT |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8 | Ubadhirifu katika mradi wa Uwekezaji (DASIP) | 200.1 Mil | 2007/8 – 2009/10 | NAOT |
| 9 | Uhamisho wa fedha bila idhini | 119.7 Mil | 2009/10 | NAOT |
| 10 | Hundi zilizoghushiwa | 502.1 Mil | 2007/8 & 2008/9 | NAOT |
| 11 | Matumizi ya fedha kinyume na Malengo yaliyokusudiwa | 766.5 Mil | 2009/10 | NAOT |
| 12 | Uhamisho wa fedha kwenda kwenye akaunti zisizofahamika | 452.3 Mil | 2009/10 | NAOT |

Mheshimiwa Naibu Spika, nne, ni taarifa maalum ya udhaifu katika ukusanyaji wa mapato ya ndani katika Halmashauri kwa ujumla. Uwezo wa kujitegemea kifedha wa Halmashauri hauridhishi, kuna utegemezi uliokithiri. Kwa wastani, uwezo wa Halmashauri zote nchini kujitegemea ni wa asilimia 10, kiasi ambacho ni sawa na 3-5% ya matumizi yote ya Serikali katika Mwaka 2009/2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu huu umewahi kuzungumziwa katika Taarifa ya Mwaka ya Kamati hii kwa hesabu zilizoishia 30 Juni, 2009. Lakini pia ni suala ambalo limewahi kufanyiwa utafiti wa kina kabisa na Taasisi zingine kama vile *REPOA*. Tafiti hizi zimeonesha kuwa uwezo wa Halmashauri zetu kupanga, kubuni, kurekodi na kusimamia kwa umadhubuti ukusanyaji wa mapato yao ya ndani uko chini sana. Taarifa hii ya *CAG*, 2011, imedhihirisha udhaifu huu, sababu zake na imetoa maoni juu ya namna ya kuupunguza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na dondoo zingine, kinaonesha uwezo wa kujitegemea kwa kila Halmashauri kwa Halmashauri zote 144 zilizokaguliwa katika mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, kutokana na udhaifu uliopo katika ukusanyaji wa fedha hizo, zaidi ya 75% ya Halmashauri hazina taa za barabarani na zina kiwango cha chini cha usafi wa mazingira.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya mwisho ni maoni na mapendekezo ya Kamati. Baada ya maelezo ya kina kuhusu matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Halmashauri, naomba kuwasilisha hoja kumi na nne (14) za Kamati. Hoja hizi ndiyo maoni na mapendekezo ya Kamati na naliomba Bunge lako Tukufu kuyajadili na kuyaafiki kwa lengo la kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa nchini:-

KWAKUWA, ruzuku ya Serikali Kuu ni muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri;

NA KWA KUWA, matokeo ya ziara za Kamati yamedhihirisha kwamba ruzuku hii haipelekwi kwa wakati na kwa kiasi kinachostahili hivyo kuchangia udhaifu katika matumizi yake na utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kuwa Bunge likubali:-

(a) Kuishauri Serikali kuwa iwe na uhalisia katika bajeti yake kuu *(realistic budget)*. Uhalisia huu utasaidia kuwepo kwa uwiano kati ya kiasi cha fedha kinachopangwa na kuidhinishwa na Bunge kwa ajili ya Serikali za Mitaa na kiasi halisi cha fedha kinachopelekwa huko.

(b) Kuishauri Serikali kupeleka ruzuku hiyo kwa wakati na kwa kiasi kinachostahili kwenye Halmashauri.

(c) Kuitaka Serikali kuwasilisha kila mwaka Bungeni Taarifa ya fedha zinazoidhinishwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za maendeleo katika Halmashauri ikiwianishwa na kiasi cha fedha ambazo zinakuwa zimepelekwa kwenye Halmashauri hizo katika mwaka husika.

(d) Kuishauri Serikali (HAZINA) kuanzisha utaratibu wa kuwa na mwakilishi ambaye ni Afisa Bajeti Serikali za Mitaa

kwenye Vikao vya *LAAC*. Mwakilishi huyo atasaidia kutoa ufafanuzi wa baadhi ya masuala yanayohusu upelekaji wa ruzuku kwenye Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo hoja hii itakubalika na kuungwa mkono, itaongeza uwezekano wa Halmashauri kutekeleza mipango yao kwa wakati na matokeo yake yataliwezesha Bunge kuwa katika nafasi nzuri ya kupima ufanisi na nidhamu ya Halmashauri katika kusimamia matumizi ya ruzuku hiyo.

KWA KUWA, makusanyo ya fedha za ndani za Halmashauri ni muhimu kuziwezesha Halmashauri kulipia gharama za matumizi mbalimbali kama vile kuchangia miradi mbalimbali ya maendeleo vijijini, usafi kwenye miji, operesheni za ulinzi, taa za barabarani na kadhalika;

NA KWA KUWA, udhaifu katika kukusanya fedha hizo una athari hasi kwa huduma zilizotajwa na unachangia ongezeko la utegemezi wa Serikali Kuu kwa Wafadhili wa nje;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge likubali kuitaka Serikali:-

(a) Kuandaa na kusimamia Mpango Mkakati Maalum wa Miaka Mitano kwa ajili ya kuhimiza na kukuza jitihada za Halmashauri kuongeza juhudi za kubuni na kusimamia ukusanyaji wa mapato kutoka kwenye vyanzo mbalimbali;

(b) Kutathmini kwa pamoja (kulingana na mazingira ya kila Halmashauri) vyanzo vipya vya mapato;

(c) Kutoa taarifa ya tathmini ya ufanisi uliotokana na kuitumia Mamlaka ya Mapato nchini *(TRA)* kukusanya kodi ya majengo katika Halmashauri za Manispaa mbalimbali nchini;

(d) Kuona uwezekano wa kuziachia Halmashauri baadhi ya vyanzo vya mapato vilivyoko kwenye maeneo yao (mfano ushuru wa minara ya simu na usajili wa zahanati binafsi). Lakini pia kuongeza asilimia ya mgawo wa mapato kwa Halmashauri (kwa mapato ambayo yanakusanywa na Halmashauri na kupelekwa Serikali Kuu); na

(e) Kutoa maelezo na kisha ufumbuzi wa suala la nyumba za Halmashauri ya mbalimbali ilizouza. Mfano ukiwa ni nyumba tatu za Manispaa ya Temeke zilizokuwa katika maeneo ya Masaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja hii ikiungwa mkono na kupata utekelezaji madhubuti itasaidia kutoa msukumo wa kuziwezesha Halmashauri kupunguza utegemezi kwa Serikali Kuu.

KWA KUWA, utafiti wa Kamati umebaini kuwepo kwa maelekezo ya Serikali na miongozo ya kisheria inayokinzana kuhusu ushuru wa mauzo ya korosho ghafi *(Cashewnut Export Levy)* kwa Halmashauri husika (Mfano, Sheria Na. 18 ya Bodi ya Korosho, 2009) inataka asilimia 65 ya ushuru wa korosho ghafi kupelekwa kwenye Mfuko wa Wakfu wa Kuendeleza Zao la Korosho, Marekebisho ya Mwaka 2006 ya Sheria ya Fedha Kifungu 10A(2) yanataka ushuru huo kugawanywa miongoni mwa Halmashauri zinazozalisha korosho.

Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, 1982 haitoi ufafanuzi wowote kuhusu utozaji wa kodi ya usafirishaji wa korosho ghafi nje ya nchi; wakati baadhi ya maelekezo ya Serikali yanataka ushuru huo uelekezwe kwenye upatikanaji wa pembejeo),

NA KWA KUWA, kukinzana kwa miongozo na maagizo hayo kumechangia kwa kiasi kikubwa Halmashauri husika kukosa mapato yatokanayo na mauzo ya korosho hizo,

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kuwianisha miongozo na maelekezo hayo mara moja ili kuondoa utata wa kutokupeleka gawio la ushuru huo kwa Halmashauri husika.

KWAKUWA, Taarifa ya Ukaguzi Maalum wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu, (2011) imeonesha kiasi cha ubadhirifu, maeneo ya ubadhirifu, sababu za ubadhirifu, vipindi vya ubadhirifu, athari za ubadhirifu na wahusika katika ubadhirifu huo;

NA KWA KUWA, mpaka sasa hakuna hatua zilizochukuliwa dhidi ya wahusika kwa lengo la kukomesha ubadhirifu huo;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge likubali kuitaka Serikali kutoa maelezo ya kuridhisha ni kwa nini ubadhirifu huu uliachwa ukishamiri kwa miaka mitatu mfululizo (2007/2008- 2009/2010) bila ya wahusika kuchukuliwa hatua za kisheria.

Mheshimiwa Naibu Spika, taratibu hazikatazi kumtumia *CAG* kama shahidi maalum endapo suala hili litapelekwa Mahakamani. Shida iliyopo hapa ni Serikali kuonekana inawakumbatia wahusika kwa kisingizio cha uchunguzi unaendelea. Nini kinachunguzwa badala ya kupeleka kesi Mahakamani na kumwita *CAG* kutoa ushahidi? Bunge linaombwa kuikubali hoja hii na kutaka utekelezaji kutoka kwa Serikali.

KWA KUWA, tatizo la ulipaji wa mishahara kwa watumishi hewa linaendelea kufuja mapato ya Serikali (583.2 milioni katika mwaka wa fedha wa 2009/2010) kwa kuikosesha miradi mingine fedha za utekelezaji;

NA KWA KUWA, mishahara hii hulipwa na watu wanaojulikana kwa watu wasiojulikana au wasiokuwepo kabisa;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge likubali kuitaka Serikali kuwasilisha Bungeni Taarifa Maalum ya namna tatizo hili linavyoshughulikiwa kwa lengo la kuliondoa kabisa. Lakini pia Serikali iwasilishe hapa Bungeni Taarifa Maalum ya namna wahusika walivyochukuliwa hatua za kisheria. Hii ni kwa sababu tatizo hili limekuwa likisemwa na *CAG* na *LAAC* kwa muda mrefu sasa na linaathiri matumizi ya fedha za umma.

KWA KUWA, uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba mnamo mwaka 2004, Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam (Ilala, Kinondoni, Temeke na Jiji la Dar es Salaam) zilisaini Mkataba wa pamoja kwa ajili ya Mradi wa pamoja wa Kiwanda cha Nyama;

NA KWA KUWA, upande wa pili wa Mkataba ulikuwa ni Kampuni ya *R & M* kutoka Malaysia na mpaka sasa Mradi huo haujawahi kufanya kazi;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza Bunge likubali kuitaka Serikali:-

(a) Kutoa maelezo Bungeni juu ya uwepo wa Mkataba wa mradi huo na kiasi cha fedha/ mali ambayo kila Halmashauri ilichangia;

(b) Kutoa maelezo kuhusu nani alikuwa mkusanyaji wa michango hiyo na alikuwa akiiweka wapi;

(c) Maelezo haya yaweke bayana kampuni ya *R & M* kutoka Malaysia na *EAMEATCO* zilipatikanaje na zilikuwa na nafasi gani katika Mradi au Mkataba huo; na

(d) Kutoa maelezo kuhusu namna Halmashauri za Mkoa wa Dar es Salaam zilivyofaidika na mradi huo ikiwa ni pamoja na hatma ya fedha au mali ambazo Halmashauri hizo zilichangia katika Mradi huo.

KWA KUWA, uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba baadhi ya watumishi wanaohusishwa na matukio ya kibadhirifu wamekuwa wakihamishwa kutoka kituo walichofanya ubadhirifu kwenda kwenye kituo kingine kwa maelezo kwamba wanapisha uchunguzi;

NA KWA KUWA, uhamisho huu hautofautiani na nia ya kusambaza ubadhirifu nchi nzima badala ya kuukomesha;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali:-

(a) Kutoa maelezo ya kuridhisha ni kwa nini baadhi ya watuhumiwa wa ubadhirifu katika Halmashauri hawachukuliwi hatua za kisheria badala yake wanahamishwa vituo vya kazi; na

(b) Kutoa ufafanuzi ni kwa namna gani kumhamisha mtuhumiwa wa ubadhirifu kwenda kituo kingine cha kazi kunatumika kama mbinu ya kukomesha tabia za kibadhirifu kwa mhusika.

KWA KUWA, njia mojawapo katika kubaini mapato na kudhibiti matumizi ni kufanya manunuzi kwa kutumia hati maalum za malipo ya Serikali;

NA KWA KUWA, kuendelea kuwepo kwa mapato ama malipo bila hati ni kiashiria cha mwanya wa upotevu wa mapato na uwepo wa matumizi holela yenye kutia shaka Serikalini (malipo yasiyokuwa na hati shilingi bilioni 2.4 katika Mwaka wa Fedha wa 2009/2010);

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge liitake Serikali kueleza sababu za kuwepo kwa tatizo hili na Mkakati wake katika kulidhibiti.

KWA KUWA, imebainika katika uchunguzi wa Kamati kwamba mojawapo ya sababu zinazosababisha kuwepo kwa Wakuu wa Idara wengi wanaokaimu nafasi zao za kazi katika Halmashauri ni utaratibu wa Serikali kuweka kigezo cha watumishi hao kutimiza miaka saba ya uzoefu kazini;

NA KWA KUWA, imebainika pia kwamba utaratibu huu wa kukaimisha una madhara hasi katika kusimamia kwa dhati mikakati ya Serikali na matumizi bora ya fedha za umma (Rejea Taarifa ya Ukaguzi Maalum Kishapu);

KWA HIYO BASI, Bunge linaombwa likubali kuishauri Serikali ione uwezekano wa kulegeza sharti la uzoefu wa miaka saba badala yake iwe miaka mitatu ili isaidie kupunguza tatizo la kukaimu na madhara ya kukaimu katika usimamizi na matumizi bora ya fedha za umma katika Halmashauri.

KWA KUWA, uchunguzi wa Kamati umebaini kwamba upo ulegevu katika usimamizi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri;

NA KWA KUWA, ulegevu huu umejidhihirisha kwa namna ambayo baadhi ya miradi hutekelezwa chini ya viwango, mingine haitekelezwi kabisa, wakati mingine haitekelezwi kwa wakati lakini malipo yanakuwa yamekwishafanyika;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge likubali kuishauri Serikali:-

(a) Kuandaa na kutekeleza Mpango Maalumu wa kuwaelimisha Madiwani na wananchi kwa ujumla juu ya umuhimu wao katika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maendeleo;

(b) Kuwaelimisha Madiwani kwamba wao siyo watendaji na hivyo siyo jukumu lao kusaini mikataba ya miradi ya maendeleo na wazabuni kwa niaba ya Halmashauri; na

(c) Kuzisimamia Halmashauri kwa ukaribu zaidi kwa lengo la kuimarisha ufanisi.

KWA KUWA, uchunguzi wa Kamati umebaini kuwa katika baadhi ya Halmashauri, mathalan, Halmashauri ya Jiji la Arusha, fedha za ruzuku ya maendeleo *(LGCDG)* kwa ajili ya shule za Sekondari za Kata zinapelekwa katika Mabaraza ya Kata badala ya Bodi za Shule;

NA KWA KUWA, Mabaraza ya Kata yanapaswa kuwa vyombo vya uangalizi wa matumizi ya fedha hizo kuliko kuwa vyombo vya utendaji;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge likubali kuishauri Serikali kuwa badala ya kupeleka fedha hizo kwenye Mabaraza tajwa zipelekwe kwenye Bodi za Shule ili kuimarisha utawala bora katika Mabaraza hayo. Kama Bodi za shule hizo hazijaundwa basi iwe sehemu ya ushauri huu kwamba shule zote ambazo tayari zimekwishaanza kudahili wanafunzi ziunde Bodi kwa ajili ya usimamizi wa shughuli zao.

KWA KUWA, ni wajibu wa Kikatiba na Kisheria kwa *CAG* kufanya Ukaguzi katika hesabu za Serikali;

NA KWA KUWA, Taarifa Tatu za Ukaguzi alizoziwasilisha Bungeni kwa ajili ya Mwaka wa fedha wa 2009/2010, zimeisaidia sana Kamati kupata picha halisi ya nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri;

KWA HIYO BASI, Kamati inaliomba Bunge likubali kuishauri Serikali kuongeza bajeti na Watumishi wa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi ili Ofisi hiyo iweze angalau kila mwaka kuwasilisha Bungeni Taarifa za Kaguzi Maalum na Ukaguzi wa thamani *(VFM)* wa Halmashauri angalau tano kwa ajili ya kulipa Bunge

picha pana ya yanayojiri katika matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri nchini.

KWA KUWA, Taarifa za Hesabu za mwisho wa mwaka za kila Halmashauri (*Final Accounts)* ndizo zinazotumiwa na *CAG* kutoa aina ya Hati ya Ukaguzi na maoni ya ukaguzi;

NA KWA KUWA, imebainika katika uchunguzi wa Kamati kwamba kiasi cha fedha za matumizi yanayooneshwa katika Taarifa hizi kinatofautiana na yale yanayooneshwa kwenye Taarifa zinazowasilishwa na Halmashauri hizo hizo kwenye vikao vya *LAAC;*

KWA HIYO BASI, Bunge linaombwa likubali kuitaka Serikali kutoa maelezo kwa nini Taarifa zinazowasilishwa kwenye Kamati zinatofautiana na Taarifa zinazowasilishwa kwa *CAG* hasa katika kipengele cha matumizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila ya kutoa maelezo ya kuridhisha katika jambo hili, Kamati itabakia na mashaka kwamba kuna matumizi yasiyofaa katika fedha hizo.

KWA KUWA, taarifa za mwisho wa mwaka wa Hesabu za Halmashauri (*Final Accounts*) zinawasilishwa kwa *CAG* miezi mitatu (Mwezi Septemba kila Mwaka) baada ya Mwaka husika wa fedha kufungwa wakati Taarifa za mapato na matumizi na utekelezaji wa maoni ya ukaguzi huletwa na Halmashauri kwa takribani miezi tisa baada ya mwaka husika wa fedha kufungwa;

NA KWA KUWA, muda wa miezi tisa utazisaidia Halmashauri kujibu hoja zote za ukaguzi kwa kina;

KWA HIYO BASI, Kamati inapendekeza kwamba Bunge likubali kuitaka Serikali (Halmashauri) kuwasilisha kwa *CAG* Taarifa za Hesabu za mwisho wa mwaka *(final Accounts*) na Taarifa kwa ajili ya vikao vya *LAAC* kwa wakati sawa (kuanzia

Hesabu za 2010/2011). Lakini pia pawekwe Kanuni za adhabu kwa Halmashauri ambayo itashindwa kutimiza sharti hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, endapo hoja hii itaafikiwa na kutekelezwa ipasavyo itazisaidia Halmashauri kujiandaa kikamilifu kuwasilisha taarifa zao kwa mujibu wa Ratiba ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya changamoto zinazoikabili Kamati katika utekelezaji wa majukumu yake ni pamoja na:-

(a) Ufinyu wa muda na fedha. Changamoto hii inatokana na ukweli kwamba Kamati (z) inafanya kazi kwa muda wa siku sitini kwa mwaka ambapo ndani ya siku hizo kuna siku za Jumamosi na Jumapili na siku za sikukuu mbalimbali. Hivyo kwa uhakika kabisa ni kwamba, Kamati inafanya kazi kwa muda wa siku arobaini tu (40) kwa mwaka. Huu ni muda mdogo sana kwa Kamati za Bunge kuweza kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Aidha, kiasi cha fedha zinazotengwa hakitoshi kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Hakuna fedha zinazotengwa kwa ajili ya shughuli za ukaguzi wa miradi ya maendeleo. Kwa maana hiyo endapo Program ya Usimamizi wa fedha za Umma *(PFMRP)* ambayo inafadhili ziara za Kamati itasitishwa, Kamati haitaweza kupata ushahidi wa hali halisi iliyopo katika miradi ya maendeleo katika Halmashauri.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, lipo tatizo la Serikali kutojibu hoja za Kamati. Kwa mfano, hoja zote zilizotolewa na Kamati katika Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za mwaka wa fedha ulioishia 30 Juni, 2009 hazikujibiwa kabisa.

(c) Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa za Halmashauri kuchelewa kufika kwa *CAG* na *LAAC*. Kisheria, Halmashauri zinapaswa kuwasilisha taarifa zao za mapato na matumizi ya

mwaka kwa *CAG* miezi mitatu baada ya mwaka husika wa fedha kufungwa. Ni kwa kutumia taarifa hizi ambapo Mkaguzi Mkuu hutoa mapendekezo na aina ya Hati ya Ukaguzi kwa Halmashauri husika. Baada ya Mapendekezo na Hati kutolewa ndipo *CAG* huwasilisha Bungeni (Mwezi Aprili kila Mwaka) Taarifa ya Kazi (Ukaguzi) alioufanya.

Baada ya Taarifa ya Ukaguzi kuwasilishwa Bungeni ndipo Kamati huanza kuzitaka Halmashauri kuwasilisha taarifa za mapato na matumizi yao Bungeni. Kimsingi, hizi ni taarifa za majibu ya Halmashauri kutokana na hoja za ukaguzi. Katika hatua hiyo, Kamati imebaini kwamba Halmashauri nyingi zinafanya uzembe, haziwasilishi taarifa zao kwa *CAG* na kwenye Kamati kwa wakati hivyo kusababisha mabadiliko yasiyo ya lazima kwenye Ratiba ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuchukua fursa hii kutoa shukrani zangu kwako kwa namna ambavyo umekuwa ukitoa miongozo mbalimbali ya kusaidia ufanisi katika utendaji wa Kamati. Nawashukuru sana Wajumbe wote wa Kamati yangu kwa kutekeleza majukumu yao kwa ustadi mkubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, namshukuru sana Katibu wa Bunge Daktari Thomas D. Kashililah na Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Charles Mloka kwa ufafanuzi wa mambo mbalimbali ya uendeshaji wa shughuli za Kibunge kila tulipowahitaji. Aidha, naomba kutumia fursa hii kumshukuru Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Watumishi wake kwa Taarifa za Ukaguzi zinazoisaidia Kamati kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Shukrani zaidi kwa nchi wahisani wa Mfuko wa Maboresho katika matumizi ya fedha za umma *(PFMRP)* kwa kutuwezesha kufanya ziara za ukaguzi wa miradi, shukrani kwa Ofisi ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na HAZINA kwa ushirikiano wao wakati wote wa Vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Kamati, natumia fursa hii kumpongeza Katibu wa Kamati Ndugu Mswige Dickson

Bisile pamoja na Msaidizi wake Ndugu Waziri Kizingiti na Watumishi wote wa Bunge kwa ushirikiano wao kwa wakati wote ambao Kamati ilihitaji utaalam wao.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa hii imebainisha matatizo sugu yaliyobainika katika matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri zetu katika kipindi cha mwaka wa fedha wa 2009/2010. Dhidi ya matatizo hayo mapendekezo kadhaa yametolewa kama suluhisho. Ni vema Serikali ikajipanga vema kwa ajili ya kutekeleza ushauri huo bila ya kuhitaji usimamizi mkubwa wa Kibunge. Kutokana na uchambuzi uliofanyika, ni vema pia Halmashauri zikaitambua nafasi yao katika ujenzi wa uchumi na maendeleo ya Taifa hili. Halmashauri zilisaidie Taifa kufika mahali ambapo Watanzania walioko Mijini watapenda kuhamia Vijijini kwa sababu ya kuboreshwa kwa huduma za jamii vijijini.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

**MHE. ZABEIN M. MHITA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mrema, ahsante sana kwa taarifa hiyo nzuri ya Kamati yako ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Tunakushukuru sana. Waheshimiwa Wabunge kabla hatujaendelea niwaombe tu Waheshimiwa Mawaziri na Manaibu Mawaziri, wataalam kutoka Ofisi ya Vitambulisho vya Taifa wako Msekwa A, chumba namba sita wanaomba mfike pale kwa ajili ya kuchukuliwa alama za vidole na wataalam hao. Mkiwakosa itabidi kuwatafuta. Sasa naomba nimwite Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Mheshimiwa Zitto Kabwe atupatie taarifa ya Kamati ya Bunge anayoisimamia.

## Taarifa ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Juni 30, 2010

**MHE. KABWE Z. ZITTO – MWENYEKITI WA KAMATI YA HESABU ZA MASHIRIKA YA UMMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami napenda kuwapongeza watu wote waliochaguliwa jana kuwa Wabunge katika Bunge la Afrika Mashariki. Lakini pili, kwa niaba ya Chama changu, napenda kuwashukuru nyote kwa moyo mmoja kabisa kwa kura ambazo mlitupatia, hazikutosha, lakini imedhihirisha kabisa kwamba kuna watu wengi ambao siyo wa Chama chetu ambao wametupatia kura. Tunawashukuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote, napenda kukushukuru kwa kunipa fursa hii muhimu ya kuwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu, pamoja na mambo mengine, maoni na mapendekezo ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma *(POAC)* juu ya Hesabu, ufanisi wa Mashirika ya Umma na utekelezwaji wa Sera ya Ubinafsishaji Nchini.

Maoni na Mapendekezo haya ni kufuatia uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, juu ya Mashirika mbalimbali ya Umma nchini kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2010 na pia kutokana na Taarifa ya Msajili wa Hazina *(The Treasury Notes)* kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2011 pamoja na ziara za ukaguzi wa ufanisi katika baadhi ya miradi inayotekelezwa na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, majukumu ya Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma yameainishwa katika Sehemu ya Tatu ya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Bunge Toleo la mwaka 2007 chini ya Kanuni ya 115 kifungu cha 13 katika fasili ndogo (a) hadi (e) kama ifuatavyo: -

(a) Kushughulikia taarifa za kila mwaka za Hesabu zilizokaguliwa za Mashirika ya Umma;

(b) Kuainisha maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za Umma;

(c) Kufuatilia mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati;

(d) Kufanya tathmini ya ufanisi wa Mashirika ya Umma; na

(e) Kufuatilia utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza majukumu yake, Kamati ya Bunge ya Hesabu za Mashirika ya Umma imetumia nyenzo zifuatazo:-

(a) Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 kama ilivyofayiwa marekebisho mara kwa mara na hasa kuhusu mamlaka ya Bunge na Kamati zake;

(b) Kanuni za Bunge (Toleo la Mwaka 2007);

(c) Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (kwa mwaka ulioishia 30 Juni, 2010);

(d) Sheria ya Manunuzi ya Mwaka 2004, Sheria ya Fedha za Umma ya Mwaka 2001, Sheria ya Ukaguzi wa Umma na Sheria iliyoanzisha kila Shirika husika;

(e) Taarifa za Msajili wa Hazina kama Mwenye hisa Mkuu katika Mashirika yote ambapo Serikali imewekeza;

(f) Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa za kila Shirika kwa mwaka wa fedha unaojadiliwa ikiambatanishwa na

majibu ya hoja za Ukaguzi kutoka katika Manejimenti ya kila Shirika husika;

(g) Taarifa za kitafiti kutoka maeneo mbalimbali juu ya mambo yanayogusa majukumu ya Kamati na;

(h) Ziara za Ukaguzi wa Ufanisi na Tathmini katika zoezi zima la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Taarifa ya Msajili wa Hazina kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2011 ulibaini kuwa kwa kipindi hicho Serikali imekuwa ikimiliki hisa katika Mashirika ya Umma na Kampuni binafsi zenye Jumla ya Thamani ya Sh. 10,275,149,624,561.50. Aidha, jumla ya Mashirika ya Umma 234 yaliwasilisha taarifa za Hesabu zilizokaguliwa kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 30 2010.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Msajili wa Hazina, ilibainika kuwa jumla ya Mashirika ya Umma 11 hayakuwasilisha Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa kwa Msajili wa Hazina ili taarifa hizo zijumuishwe kwenye taarifa kuu ya mwaka. Mashirika hayo ni:-

*(a) Agency for Developmen;*

(b) Chuo cha Ardhi Morogoro;

(c) Hifadhi ya Taifa ya Chakula;

*(d) National Housing Building Research Institute*;

*(e) Public Procurement Appeals Tribunal*;

*(f) Social Security Reguratory Authority*;

*(g) Tanzania Official seeds Certification Agency*;

(h) *Tanzania Revenue Appeals Board*, na

(i) *Tengeru Community Development Training na Tume ya UNESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama tulivyoainisha hapo juu, hadi kukamilika kwa mwaka wa fedha wa 2010/2011 Serikali ilikuwa imewekeza kiasi cha Sh.10,275,149,624,561.50 katika Mashirika ya Umma. Mtiririko wa gawio kutokana na uwekezaji wa Serikali Katika Mashirika ya Umma kwa miaka miwili mfululizo ulikuwa kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji wa Serikali kwenye Mashirika ya Umma, mwaka 2009/2010, mtaji uliowekezwa ni Sh. 7,760,783,352,713.95 na gawio lililopatikana ni Shilingi bilioni 40.6. Mwaka 2010/2011, mtaji uliowekezwa ni Sh. 10,275,149,624,561.50 na gawio lililopatikana ni Shilingi bilioni 28.7. Tofauti ni Shilingi bilioni 11.8.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma yalichangia mapato Serikalini kutokana na gawio, mikopo, riba na michango mingine. Gawio kutoka Mashirika ya Umma lilipungua kutoka Shilingi bilioni 40.6 mwaka 2009/2010 mpaka shilingi bilioni 28.7 mwaka 2010/2011. Pungufu ya gawio hili kwa miaka miwili ya fedha ni Shilingi bilioni 11.8 sawa na asilimia 29.2 ambapo Serikali ilikuwa imekusudia kukusanya Jumla ya shilingi bilioni 51.4.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa Kamati ulibainisha sababu za msingi za kushuka kwa gawio toka kwenye Mashirika ya Umma kwenda Serikalini, sababu kubwa ikiwa ni kushuka kwa makusanyo ya mikopo na gawio kama inavyofafanuliwa katika jedwali lifuatalo: -

**Jedwali Na. 2**

**Mapato ya Serikali kutoka kwenye Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha 2009/2010 na 2010/2011:**

| Na. | Aina ya Mapato | Mwaka | Kiasi | Asilimia ya pungufu/ Ongezeko |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Makusanyo Mengineyo (*Remittences*) | 2009/2010 | Bilioni 14.0 | 52.6% sawa na pungufu ya Shilingi bilioni 7.4 |
| | | 2010/2011 | Bilioni 6.6 | |
| 2. | Makusanyo toka kwenye mikopo na riba *(loans and interest)* | 2009/2010 | Bilioni 11.4 | 79.5% sawa na pungufu ya Shilingi bilioni 9.1 |
| | | 2010/2011 | Bilioni 2.3 | |
| 3. | Makusanyo toka kwenye gawio (*Dividend*) | 2009/2010 | Bilioni 15.1 | 30.9 % sawa na ongezeko la Shilingi bilioni 4.6 |
| | | 2010/2011 | Bilioni 19.8 | |

Mheshimiwa Naibu Spika, gawio na michango mingine *(remittances)* kwenda Serikalini, inategemea sana utendaji wa Mashirika ya Umma kwa mwaka husika. Kupungua kwa gawio linalotokana na michango mingine na madeni na riba kutoka Mashirika ya Umma kwenda Serikalini ni ishara kuwa baadhi ya Mashirika ya Umma yamepungua ufanisi na hivyo kushindwa kulipa madeni yake yaliyochukuliwa chini ya udhamini wa Msajili wa Hazina na pia baadhi ya madeni ambayo Serikali ilitoa udhamini kupitia kwa Msajili wa Hazina.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kumtaka Msajili wa Hazina aimarishe usimamizi wa Mashirika ya Umma ili yafanye kazi kwa ufanisi na kutoa faida kwa Taifa. Kamati inasisitiza kwamba Ofisi ya Msajili wa Hazina iwe makini inapotoa Udhamini wa mikopo kwa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Mashirika ya Umma kwa vipindi vilivyoishia 30 Septemba, 2009; 31 Desemba, 2009 na Juni 30, 2010 jumla ya Mashirika ya Umma 170 yaliwasilisha Taarifa za Hesabu zao kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa ajili ya ukaguzi ambapo taarifa za Mashirika 122 sawa na 71.7 % ya taarifa zote zilizowasilishwa zilikaguliwa na kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi uliofanywa na Kamati kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2010 ilibainika kuwa jumla ya Mashirika ya Umma 92 yalipata hati safi za Ukaguzi *(Unqualified opinion)* ikiwa ni sawa na 75.4% ya kaguzi zote; kaguzi 12 (9.8%) zilipata hati safi yenye masuala ya msisitizo; kaguzi 10 (8.2%) zilipata hati yenye shaka; kaguzi saba (5.8%) zilipata hati zenye shaka zenye masuala ya msisitizo ambapo Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alishindwa kutoa maoni ya ukaguzi kwa shirika moja (0.8%) na hakuna shirika lililopata hati mbaya/chafu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, alishindwa kutoa maoni ya ukaguzi na hivyo kutoa *adverse opinion* kwa Shirika la Masoko Kariakoo, sababu kubwa ikiwa ni Shirika hilo kutoweka kumbukumbu ya mali zake, thamani halisi ya mali hizo na pia kutokuwepo kwa Bodi ya Wakurugenzi kwa mujibu wa Sheria iliyoanzisha Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilichukua hatua stahili za kuwasiliana na Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa ambayo ni Wizara mama ya Shirika husika ili kupata ufumbuzi wa uteuzi wa Bodi mpya ambayo italisimamia Shirika na kuhakikisha mali za Shirika zinakuwa salama. Hata hivyo, hadi sasa Kamati imejiridhisha kuwa Bodi haijateuliwa na hakuna taarifa iliyotolewa.

**Jedwali Na.3 Mchanganuo wa Hati za Ukaguzi**

| Mashirika | Hati safi | Hati safi yenye masuala ya msisitizo | Hati zenye Shaka | Hati zenye shaka zenye Msisitizo | Kushindwa kutoa Hati |
|---|---|---|---|---|---|
| 122 | 92 | 12 | 10 | 7 | 1 |
| 100% | 75.4% | 9.8% | 8.2% | 5.8% | 0.8% |

Mheshimiwa Naibu Spika, kumekuwa na ongezeko kubwa la Taasisi za Umma na Mashirika ya Umma katika kupata hati safi za ukaguzi. Ongezeko hili kimsingi pamoja na mambo mengine linatokana na juhudi za Bunge lako Tukufu kwa ushirikiano mkubwa na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi katika kuimarisha usimamizi wa mapato na matumizi katika Mashirika ya Umma, hali ambayo imeimarisha uwajibikaji na uwazi wa kutosha. Orodha kamili ya kila Shirika na Hati iliyopatikana vimeambatishwa kama kiambatisho Na. 1 cha Taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya Ukaguzi wa Umma namba 11 ya Mwaka 2008, inampa Mamlaka Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kukagua Hesabu za Mashirika ya Umma baada ya kuwasilishwa kwake kwa mujibu wa Sheria hiyo. Kamati imebaini kuwa kumekuwapo na mwenendo usioridhisha kwa baadhi ya Mashirika ya Umma kukiuka matakwa hayo ya kisheria ya kupeleka Taarifa ya hesabu zao kwa *CAG* ili zikaguliwe kwa muda muafaka na hivyo kukwamisha utendaji wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa upande mmoja na pia usimamizi wa Bunge kupitia Kamati zako kwa upande mwingine. Sababu kubwa za ucheleweshaji huu ni pamoja na kutokuwepo kwa Bodi za Wakurugenzi na pia Menejimenti za Mashirika kutokujibu hoja za Wakaguzi kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha 2009/2010, Mashirika yafutayo hayakuzingatia Sheria hiyo:-

- Bodi ya Utalii Tanzania *(TTB),* ambayo imekuwa bila Bodi ya Wakurugenzi kwa zaidi ya miaka mitatu hadi Bodi mpya ilipoteuliwa mwezi Machi, 2012;

- Kituo cha Chakula na Lishe Tanzania *(TFNC);*

- *Tanzania Governement Freight Agency (TGFA),* na

- Kampuni ya Mbolea Tanzania *(TFC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ngazi ya Kamati, Taarifa za Mashirika 67 kati ya Taarifa za mashirika 122 zilizokaguliwa zimejadiliwa kikamilifu na hatua kadha wa kadha zenye lengo la kuimarisha matumizi bora ya fedha za Umma zilichukuliwa katika maeneo yote ambayo yalibainika kutokuwa misingi ya matumizi bora ya fedha za Umma. Hii ni sawa na 78.2% ya Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya uchambuzi wa kina wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2010 na kwa kuzingatia hoja mahsusi za ukaguzi kwa kila Shirika la Umma lililofika mbele ya Kamati, maeneo yafuatayo yaligundulika kuwa na matumizi yasioridhisha na yenye shaka ya fedha za Umma;

Mheshimiwa Naibu Spika, katika uchambuzi wa Taarifa ya Hesabu za Mashirika mbalimbali ya Umma, Kamati imebaini kuwa, maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za Umma yanahusisha ukiukwaji mkubwa wa Sheria ya Manunuzi ya Umma na kanuni zake. Ukiukwaji huu wa Sheria na Kanuni za Manunuzi ya Umma kwa namna moja ama nyingine unaisababishia Serikali hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria ya manunuzi ya Umma na kanuni zake ni mwongozo mkuu wa kusimamia manunuzi ya Umma, ambao ni sharti Mashirika ya Umma yazingatie, na kwa kufanya hivyo, fedha za Umma zinakuwa zimeokolewa. Kwa mfano, Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* ambalo kwa mwaka mmoja wa fedha tu linafanya manunuzi yenye thamani kati ya Shilingi bilioni 300 hadi Shilingi bilioni 600 (kwa mfano, mwaka wa fedha 2009/2010 *TANESCO*, walifanya manunuzi ya kiasi cha shilingi bilioni 258). Fedha hizo ni nyingi sana, hivyo ni muhimu msisitizo na hatua za kisheria zikaendelea kuchukuliwa kwa Taasisi zote ambazo zinakiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma na kuisababishia Serikali hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mifano ya wazi kuhusiana na upotevu wa fedha za Umma kutokana na kutozingatiwa kwa Sheria ya manunuzi ya Umma inaweza kuelezwa kwa ufasaha kutokana na mifano mahsusi ifuatayo:-

- Shirika la Ugavi wa Umeme *(TANESCO)* lilitumia Shilingi Bilioni 1.8 ukilinganisha na Shilingi milioni 65 zilizokuwa zimepangwa katika bajeti ya ukarabati wa gati mojawapo katika kituo cha bwawa la Mtera. Ongezeko hilo la gharama za manunuzi kwa ajili ya ukarabati, ni kiasi kikubwa na Kamati haikuridhika na majibu ya Menejimenti, hivyo kuagiza uchunguzi wa ndani ili kubaini uhalisia wa manunuzi hayo *(internal investigation on cost increase)*

- Chuo Kikuu Kishiriki cha Mkwawa *(MUCE)* kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2010 kilishindwa kuthibitisha kwa wakaguzi wa hesabu uwepo wa vifaa vilivyonunuliwa vyenye thamani ya Shilingi milioni 267 ikiwa ni pamoja na madawa ya maabara hivyo kupelekea chuo kupata Hati yenye shaka ya Ukaguzi *(qualified audit opinion)* kutokana na kukiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma.

- Aidha, kwa Chuo hiki Kikuu kishiriki cha Mkwawa, licha ya Kamati kubaini na kupata nyaraka kadhaa zikionyesha malipo kwa watumishi hewa, pia Kamati ilibaini malipo ya fedha kutoka Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu, yaliyokuwa yanalipwa kwa wanafunzi hewa. Hatua zilizochukuliwa ni pamoja na kuunda Kamati ndogo ambayo inaendelea na uchunguzi wa upotevu wa fedha hizo na pia kuviarifu vyombo vya dola kama TAKUKURU kufanya uchunguzi wa kina.

- Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania *(TCRA)* pia ilikiuka Sheria ya Manunuzi ya Umma katika vipengele kadhaa na hasa kwa kufanya manunuzi yenye thamani ya Shilingi milioni 855.96 bila kuzingatia mpango wa manunuzi wa mwaka *(Annual Procurement Plan, APP).* Aidha, Mkaguzi wa Hesabu wa *TCRA* alikuwa ameainisha upungufu kadhaa katika ongezeko la gharama za ujenzi wa jengo la *Mawasiliano Towers*, hivyo Kamati ilimwomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhakiki ongezeko la gharama hizo za ujenzi kuona kama zilipata idhini ya Bodi na Sheria ya Manunuzi ya Umma, na alipofanya hivyo, aliiarifu Kamati kuwa amejiridhisha na ongezeko la gharama za ujenzi na thamani halisi ya jengo na hivyo kuifunga hoja hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma yana Mamlaka kisheria kuingia katika Mikataba mbalimbali kutokana na utendaji wake wa shughuli za kila siku. Kama ilivyoripotiwa katika Taarifa ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2008/2009, eneo la uingiaji na usimamizi wa Mikataba limeendelea kuwa miongoni mwa upungufu mkubwa katika Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2010 Kamati ilibaini kuwepo kwa mkanganyiko mkubwa katika Mkataba ulioingiwa baina ya Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* na Kampuni ya *Star Times*

*International Communication,* kutoka nchini China katika uendeshaji wa Kampuni ilyoundwa kwa pamoja na wabia hao wawili *(Star Media Tanzania Limited).* Kwa mujibu wa makubaliano hayo, *TBC* ina hisa 35% na *Star Times International Communication,* hisa 65% katika kampuni tanzu iliyoundwa. Kwa mujibu wa makubaliano ya kimkataba baina ya wadau hao wawili, inaelezwa kuwa *TBC* watatoa miundombinu kwa ajili ya Kampuni na *Star Times International Communication*, watatoa teknolojia ya uendeshaji wa Kampuni ya ubia.

Mheshimiwa Naibu Spika, upungufu uliobainika katika mkataba baina ya *TBC* na *Star Media* ni kama ifuatavyo: -

(a) Hadi sasa thamani halisi ya uwekezaji katika Kampuni hiyo tanzu bado haujulikani.

(b) Mtambo wa *satelite up link* na baadhi ya vifaa ambavyo ni mali ya *TBC* vinatumika na Kampuni tanzu bila makubaliano, kwa mfano ilibainika kuwa satelite up link inayotumiwa na *Star Media Tanzania Limited* ina thamani ya shilingi milioni 495 na ni mali ya *TBC*.

(c) Tathmini na utoaji wa taarifa ya mali zisizohamishika ambazo zinatakiwa kuingizwa kwenye Kampuni tanzu ya ubia haijafanyika hadi sasa.

(d) Kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2010 kiasi cha fedha kinachofikia shilingi milioni 36 kinachotokana na shughuli za Kampuni Tanzu *(Star Media Tanzania Limited)*, kilikuwa hakionekani katika vitabu vya hesabu za *TBC*.

(e) Ilibainika kuwa Mkataba hauelezi wazi namna mtaji wa Kampuni tanzu utakavyohudumiwa *(Financing Structure)* na wabia hao wawili.

(f) Upungufu mwingine ni kuwa, hakuna mkataba wa kibiashara *(Binding Contract on Commercial Issues)* baina ya wadau hao wawili.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kwa mantiki ya upungufu tajwa hapo juu, Kamati iliamua kufanya kikao cha pamoja baina ya wadau mbalimbali wa Shirika la Utangazaji Tanzania *TBC* mnamo tarehe 23 Mei, 2011 na kuhudhuriwa na Uongozi wa *TBC*, Msajili wa Hazina na Viongozi kutoka Wizara ya Habari, Utamaduni na Michezo, ambapo majadiliano ya kina yalifanyika kuhusu mkataba huo na hasa ukizingatia maslahi ya kifedha ndani ya Mkataba huo ambayo ni miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kazi za Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika majadiliano hayo, upungufu ya kimkataba yaliainishwa na kujadiliwa kwa kina na pande zote na Wizara mama ya *TBC*, iliahidi kufuatilia na kutafuta ufumbuzi wa matatizo hayo, lakini hadi hivi sasa Kamati haijapata maelezo ya hatua iliyofikiwa kuyatatua.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na suala hilo, Kamati ilibaini kuwa, kuna umuhimu wa kuangalia upya namna ya kugharimia utangazaji wa Umma *(financing of Public Broadcasting)* ili kuifanya *TBC* kuwa huru na kutoa wigo sawa kwa vyombo binafsi hasa kwa kuiwezesha *TBC* kuwa kweli ni chombo cha utangazaji cha Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Daktari Manfred Kops ambaye ni Mkurugenzi Mkuu wa *Institute of Broadcasting Economics*, wa chuo kikuu cha Cologne Ujerumani, anabainisha kuwa ni muhimu vyombo vya utangazaji wa Umma vikahudumiwa ipasavyo ili visije kugeuka kuwa vya kibiashara na kuacha kusimamia maslahi ya Umma na badala yake kujikita kwenye kutafuta masoko, hapa ametoa nukuu ya mmoja wa wanahabari waliobobea kuhusu kuhudumia vyombo vya utangazaji wa Umma. Namnukuu:

*"The hidden defects of commercial broadcasting make the effects of commercialization even more harmful, as they might unconsciously and irreversibly change the viewers' and listeners' Programme preferences, and worse, their willingness and capability to participate in political, democratic debates about public affairs. Instead of further commercializing Public broadcasting systems, strengthening of their noncommercial elements would be appropriate, to ensure that the economy is subservient to democracy and that" democratic debate can take place, and then the organization of the economy should result from that debate."* Mwisho wa kunukuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ambavyo imekuwa ikiongelewa na wengi wa Waheshimiwa Wabunge, ni muda muafaka sasa kwa Serikali kutoa fedha za kutosha kwa *TBC* ili iboreshe huduma zake kwa kuwa na vifaa na rasilimali za kutosha na ifanye kazi zake kwa uhuru kwa manufaa ya wananchi wote bila itikadi za kisiasa wala ubaguzi wa aina yeyote ile.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Kamati imebaini upungufu mkubwa na ambao unakwenda kuitia Serikali hasara kubwa, unahusu ukodishaji wa Ndege aina ya *AirBus* uliofanywa na Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL).* Kamati ilibaini kuwa Msajili wa Hazina kwa niaba ya Serikali alitoa dhamana kwa Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL)* mwaka 2007 ili liweze kukodi ndege aina ya *Air Bus* 420 – 214 kutoka kwa Kampuni ya *Wallis Trading* ya Lebanon kwa muda wa miaka sita. Kamati ilitaka kujiridhisha na namna mchakato huo ulivyofanyika na kubaini upungufu mkubwa ufuatao:-

(a) Kwanza kabisa ilibainika kuwa ukodishaji wa ndege hiyo ulifanyika Oktoba mwaka 2007 wakati dhamana ya Serikali kwa *ATCL* ilitolewa tarehe 02/04/2008. Hivyo ni wazi

ndege ilikodiwa kabla ya kutolewa dhamana ya Serikali. Hii ni kinyume kabisa na Sheria inayosimamia utoaji wa dhamana za mikopo Serikalini ya mwaka 1974, kama ilivyofanyiwa marekebisho mara kadhaa, *(The Government Loans, Guarentees and Grants Act of 1974 as it was ammended in the year 2003).*

(b) Mkataba ulitiwa saini kinyume na ushauri wa wataalamu ambao Katika Taarifa yao walisema sio sahihi kukodi Ndege ambayo baada ya miezi sita itatakiwa kufanyiwa matengenezo makubwa "12 *years check*";

(c) Kamati ilibaini kuwa, waliongia Mkataba huo walifahamu kuwa ndege itakayokodiwa italazimika kwenda matengenezo makubwa miezi sita baada ya kuingizwa nchini.

(d) Dhamana ya Serikali iliyotolewa ilikuwa na thamani ya dola za kimarekani 60,000,000 na hadi kufikia 30 Juni, 2011 dhamana hiyo pamoja na riba ni shilingi za kitanzania bilioni 108.

(e) Baada ya ndege kukodiwa, ilibaki mikononi mwa mkodishaji kwa kipindi cha miezi saba toka Mkataba usainiwe mwezi Oktoba, 2007 hadi Mei, 2008 kutokana na kuchelewa kwa dhamana ya Serikali.

(f) Ndege hiyo iliwasili nchini mwezi Mei, 2008 na kufanya kazi kwa miezi sita tu na kutakiwa kupelekwa nchini Ufaransa kufanyiwa matengenezo makubwa yaitwayo "*12 Year Check*".

(g) Mwezi Julai, 2009 ndege ilipelekwa Ufaransa na kukamilika matengenezo lakini haikurudishwa kwa sababu *ATCL* walikosa fedha za kulipia matengenezo, USD 3,009,495.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia hoja zilizojitokeza hapo juu, ni wazi kuwa Serikali italazimika kulipa deni hilo la *ATCL* kwa

sababu lilichukuliwa chini ya dhamana ya Serikali, na ambalo kimsingi limetokana na Watendaji waliotumia Madaraka na wajibu wao vibaya na ambao kwa makusudi wanalifikisha Taifa kwenye hasara kubwa. Ni maoni ya Kamati kuwa, Serikali ichukue hatua madhubuti na stahili kwa watu wote watakaobainika kukiuka Sheria katika kuingia Mkataba huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo imedhihirika kuwa kuna usimamizi usioridhisha wa fedha za Umma ni katika Bodi ya Pamba Tanzania *(TCB).* Katika kuchambua na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Bodi ya Pamba Tanzania kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2010 ilionekana kuwa, Bodi ya Pamba imepata hati yenye Shaka ya Ukaguzi *(qualified audit opinion)* na sababu kubwa iliyosababisha Bodi kupata hati yenye Shaka ya Ukaguzi ni Usimamizi usioridhisha wa fedha za umma zilizotolewa na Serikali ili kunusuru Wakulima wa Pamba kutokana na kuanguka kwa bei ya pamba.

Mheshimiwa Naibu Spika, itakumbukwa kwamba kutokana na mdororo wa uchumi duniani mnamo mwaka 2008/2009, Serikali iliamua kutoa ruzuku kwa wakulima wa Pamba ili kufidia anguko kubwa la Bei kutoka Sh. 460/= kwa kilo hadi Sh. 360/= kwa kilo, hivyo tofauti hiyo ilitolewa kufidia tofauti ya bei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Taarifa ya Mkaguzi wa Nje wa Hesabu za Bodi ya Pamba aliyekagua Hesabu za Bodi ya Pamba kwa niaba ya *CAG*, hadi kukamilika kwa Hesabu za Juni 30, 2010 Jumla ya Sh. 2,472,348,080/= zilikuwa zimelipwa kwa wakulima, lakini hakukuwa na uthibitisho wowote kuwa fedha hizo zimewafikia Wakulima na hata pale Mkaguzi wa hesabu wa Nje wa Bodi ya Pamba, alipojaribu kuchukua baadhi ya Wakulima *(sampling)* na kuwahoji na kwa maelezo yao walikataa kuwa hawajalipwa fedha hizo na pia walionyesha changamoto ya utaratibu uliotumika kulipa fidia.

Mheshimiwa Naibu Spika, hofu ya fedha za kunusuru wakulima wa Pamba kutolipwa ipasavyo, iliongezeka kutokana na kasoro zilizoibuliwa na Mkaguzi wa Hesabu wa Bodi ya Pamba, hasa kutokana na utaratibu uliotumika kuwalipa Wakulima. Katika utaratibu huo, Mkaguzi aliieleza Kamati kuwa Wakulima walikuwa wakipewa fomu za kusaini malipo kupitia kwa Wakala wa Bodi, hivyo kuibua hali ya wasiwasi kuwa kuna uwezekano baadhi ya watu wasiokuwa waaminifu kufaidika na malipo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na upungufu huo mkubwa wa utendaji wa Bodi ya Pamba, Kamati ilibaini pia matumizi ya Shilingi milioni 36 yaliyolipwa kwa Wajumbe wawili wa Bodi ya Wakurugenzi ya Bodi ya Pamba kwa Kuandaa Mpango kazi wa Bodi kinyume na utaratibu wa dhana ya utawala bora na Sheria za Manunuzi ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilishindwa kuendelea kujadili Taarifa ya Hesabu za Bodi ya Pamba kutokana na upungufu uliojitokeza na ilipendekeza kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali afanye Ukaguzi Maalum wa Bodi ya Pamba. Aidha, Kamati inaiomba pia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) kuchunguza malipo yaliofanywa na Bodi ya Pamba kwa Wakulima.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika mbalimbali ya Umma yamekuwa yakianzishwa kwa mujibu wa sheria na matangazo husika ambayo hufafanua maudhui na majukumu ya kuanzishwa Taasisi husika. Pamoja na kuwepo kwa sheria na matangazo hayo, Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya Mashirika ya Umma yameanzishwa, lakini hayatekelezi majukumu yake ya kisheria kwa sababu tu hayapewi fedha uendeshaji na hivyo kupata hoja za ukaguzi zinazotokana na Shirika kutotimiza wajibu wa kuanzishwa kwake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kusisitiza hoja hii, Kamati ilijadili Taarifa ya Baraza la Taifa la Uwezeshaji kiuchumi

*(National Economic Empowerment Council)* ambalo lilianzishwa kwa Sheria Na. 16 ya mwaka 2004 likiwa na malengo makubwa ya kuhakikisha Watanzania wanapata fursa ya kushiriki kikamilifu katika shughuli na umiliki wa uchumi. Lakini kinyume na malengo hayo ya kisheria, Baraza hili limeshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na ufinyu wa bajeti toka Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja kubwa inayoibuliwa na Wakaguzi wa Baraza ni kuwa, halitekelezi majukumu yake ya kisheria na majibu yanayotolewa na Menejimenti ya *NEEC* ni kuwa bajeti haitoshelezi. Ni maoni ya Kamati kuwa Serikali itoe fedha zinazotakiwa (kwa mwaka wa fedha 2012/2013 shilingi bilioni 25.5) ili Baraza la Taifa la uwezeshaji Kiuchumi litekeleze majukumu yake ipasavyo na ikizingatiwa kuwa hiki kitakuwa ndiyo chombo cha msingi cha kuratibu mambo yote yanayohusu uwezeshaji wa kiuchumi kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni vyema Serikali ikaamua kuachana na utaratibu wa kuanzisha Taasisi mpya kila siku kama inashindwa kuziendeleza ipasavyo zile zilizopo na ambazo nyingine zinashabihiana kimajukumu, na kwa bahati mbaya iwapo Mashirika na Taasisi hizo hazitimizi majukumu yake kutokana na ufinyu wa bajeti zinaendelea kuwa *cost centers* kwa Serikali kulipa Mishahara na Fedha za ya matumizi mengineyo *(OC).*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mamlaka za Maji Nchini zimeendelea kukabiliwa na changamoto kubwa ya ufanisi kutokana na kukabiliwa na madeni makubwa yanayotakana na ukusanyaji hafifu wa maduhuli na pia changamoto kubwa ya uchakavu wa miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imetembelea mradi wa upanuzi wa uzalishaji maji wa *DAWASA/DAWASCO* kwenye eneo la Ruvu Chini unaotekelezwa na *Millenium Challenge Account* na kubaini kuwa mradi huo utaongeza uzalishaji wa

maji kwa kiasi cha mita za ujazo 270,000 ila changamoto kubwa inabaki kuwa miundombinu ya usafirishaji maji toka Ruvu Chini ilipo mitambo ya *DAWASA/DAWASCO* kuleta Jijini Dar es Salaam. Ni maoni ya Kamati kuwa ili kuyawezesha Mashirika haya mawili *(DAWASA/DAWASCO)* kutekeleza majukumu yake ipasavyo, ni sharti Serikali ikawa na utaratibu wa kuweka uwiano wa utekelezaji miradi *(consistance)* ili kuwa na tija ya miradi kwa wakati muafaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia ukaguzi wa Kamati katika miradi ya *DAWASCO/DAWASA* na kwa lengo la kuupa mradi wa kuongeza uzalishaji wa maji katika eneo la Ruvu Chini, Kamati inaitaka Serikali itoe fedha kutengeneza miundombinu ya maji ili kuupa mradi msukumo wa kutosha. Aidha, ni vyema Wizara ya Maji ikafanya kazi kwa karibu na Mamlaka za maji ili kwa pamoja walenge kutekeleza miradi yenye manufaa kwa Taifa na ambayo inatekelezeka.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mashirika ya Umma yana jukumu kubwa la kutoa huduma kwa ufanisi kwa wananchi kwa gharama ambayo mwananchi wa kawaida anaweza kuimudu. Kwa muda mrefu huduma kama za umeme, maji na afya zimekuwa zikitolewa na Mashirika na Taasisi za Umma. Tatizo kubwa ambalo limeyakumba Mashirika mengi ya Umma ni ulimbikizaji wa madeni makubwa kwa huduma wanazotoa na pia kutokuwa na mipango ya dhati ya kudhibiti ongezeko hilo la madeni na pia kuwa na mbinu mbadala za kukusanya madeni husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ulimbikizaji huu wa madeni na kutokukusanya madeni ipasavyo kunayapunguzia Mashirika ya Umma uwezo wa kufanya kazi zake ipasavyo. Kwa mfano, hadi kufikia tarehe 31 Desemba, 2010 Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* lilikuwa linawadai wateja wake jumla ya Shilingi bilioni 245 na katika deni hilo Shilingi bilioni 15 zinadaiwa katika Taasisi mbali mbali za Serikali kama Wizara, Idara na Halmashauri za Wilaya. Ni kwa mfano huo tu inadhihirika wazi ni

vigumu kwa Shirika kama *TANESCO* kuongeza ufanisi wakati ikishindwa kukusanya madeni na pia Serikali kushindwa kulipa deni lake kwa *TANESCO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kutokusanya na ulimbikizaji wa madeni limeendelea kuwa tatizo sugu katika Mamlaka za Maji hapa nchini, na hivyo kuzorotesha uboreshaji wa miundombinu na huduma ya maji kutokana na makusanyo hafifu. Hadi kufikia Juni 30, 2010 Mamlaka ya Maji Safi na Maji Taka Arusha ilikuwa inawadai wateja wake kiasi cha Shilingi bilioni 1.0. Mamlaka ya Maji Tanga inadai Shilingi milioni 39.0; Mamlaka ya Maji Mbeya inadai Shilingi milioni 576 na Mamlaka ya Maji Shinyanga inadai Shilingi milioni 576.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inasisitiza kuwa ni muhimu Mashirika husika yakaongeza juhudi za kukusanya madeni hayo na pia inapendekeza kwa Serikali kuangalia njia bora ya kulipia madeni ya Taasisi zake zinazodaiwa na Mamlaka za Maji na pia Shirika la Ugavi wa Umeme ili kuyanusuru Mashirika haya na kuyapa ufanisi wa kutosha.

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji katika miradi mbalimbali ni mojawapo ya jukumu mahsusi lenye kusaidia kuongeza mapato katika Mashirika ya Umma, lakini uwekezaji ni lazima ufanyike katika miradi yenye manufaa na tija kwa Taifa. Baadhi ya Mashirika ya Umma yamekuwa yakifanya uwekezaji bila kufanya utafiti wa kutosha na hivyo kuisababishia Serikali hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inafanya rejea mahsusi ya uwekezaji wa Mfuko wa Akiba ya Wafanyakazi wa Serikali za Mitaa *(LAPF)* katika uwekezaji wake katika Jengo la *Millenium Towers* na hasa ukodishaji wa jengo lililotumika kama *Hotel* ya *Peacock* ambalo hadi sasa mwekezaji alikwishaondoka na hajailipa *LAPF* stahili zake. Aidha, Kamati imebaini kuwa uingiaji wa mikataba kwa ajili ya ukodishaji wa

jengo kwa matumizi ya hoteli haukuwa na manufaa kwa Shirika.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kamati kuwa Mashirika ya Umma ni lazima yafanye upembuzi na uchunguzi wa kina kabla ya kufanya uwekezaji wa aina yoyote ile ili kuhakikisha kuwa fedha za Umma zinawekezwa kwenye maeneo yenye tija. Aidha, ili kutimiza wajibu wa kikanuni wa Kamati. Kamati itaendelea kulishughulikia jambo hili ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati iliunda Kamati ndogo mnamo mwezi Agosti, 2011 ambapo kwa ushirikiano mkubwa wa Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa hesabu za Serikali, walifanya uchunguzi maalum kuhusu Wakala wanaokagua magari yanayoingizwa nchini kwa niaba ya Shirika la Viwango Tanzania, *TBS (kwa mujibu wa kiwango cha ukaguzi TZS 698:2001 – Road Vehicles Code of Practice for Inspection and testing of used Motor Vehicles for road worthiness)*

Mheshimiwa Naibu Spika, uchunguzi huo maalumu ulikamilika na taarifa ilikabidhiwa kwako mnamo mwezi Februari, 2012 ikiwa na uchambuzi wa kina, maoni na mapendekezo kadhaa. Aidha, jambo hili liliendelea kushughulikiwa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali ikiwa imepanua wigo wa kuchunguza fedha zote zinazotokana na ukaguzi wa bidhaa zinazoingizwa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na umuhimu wa jambo hili, Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali ilianzisha pia uchunguzi kwa baadhi ya Vituo vya Ukaguzi na Kamati imepewa Taarifa kuwa uchunguzi huo umekamilika. Ni vyema Bunge likafahamishwa kuhusu utekelezaji wa hoja za uchunguzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wakati Kamati ikiwasilisha taarifa yake ya mwaka 2008/2009, ilikuja na pendekezo mahsusi la kuunda Kamati ndogo ambayo ilishughulikia suala la

Kampuni ya *General Tyre East Africa Limited* ambayo ilikuwa inamilikiwa na Serikali kwa hisa ya asilimia 74.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilifanya kazi yake na kuikabidhi kwako mnamo mwishoni mwa mwaka 2011 ikiwa na mapendekezo ya namna ya kuifufua *GTEAL*. Lakini pia taarifa ilianisha jinsi ambavyo mikopo iliyochukuliwa na *GTEAL* kwa dhamana ya Serikali inavyoweza kurejeshwa. Itakuwa ni jambo jema kama Kamati kupitia Bunge hili itapokea maelezo ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati kwa mwaka 2010 iliwasilishwa mbele ya Bunge lako Tukufu mnamo tarehe 6 Aprili, 2011. Aidha, majibu ya Serikali juu ya hoja za Kamati yaliwasilishwa na Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina. Hata hivyo, kwa lengo la kufuatilia utekelezwaji wa mapendekezo yanayotolewa na Kamati, Kamati yetu imeendelea kufuatilia utekelezaji wa maagizo yake kila mara. Tunatarajia kuwa kwa mujibu wa kanuni za Bunge, Serikali italeta majibu ya hoja za Kamati mbele ya Bunge lako Tukufu ili majibu ya hoja hizo yaweze kujadiliwa kikamilifu kwa lengo la kukamilisha *`Accountability Loop'* na pia katika kuimarisha misingi ya utawala bora.

Mheshimiwa Naibu Spika, bila taarifa ya utekelezaji toka Serikalini, Kazi ya Taarifa za Kamati na za *CAG* inakuwa haina maana, uwajibikaji *(accountability)*, ndiyo msingi mkuu wa kuwepo kwa Bunge na Kamati zake.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Taarifa ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2008/2009, hoja kadhaa ziliibuliwa na Kamati, na baada ya kupokea majibu ya Serikali kuhusu utekelezaji wa hoja hizo, Kamati inaendelea kufuatilia utekelezaji wa baadhi ya hoja ambazo utekelezaji wake haujakamilika ili kuweza kupata ufafanuzi wa kutosha toka Serikalini kwa lengo la kuongeza ufanisi wa Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati imeridhishwa kwa kiasi kikubwa na utekelezwaji wa hoja zifuatazo:-

(a) Hoja ya utekelezaji wa miradi ya Mchuchuma na Liganga itakayoendeshwa kwa ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa *(NDC)* na wawekezaji Binafsi. Kwa kiasi kikubwa Wizara ya Viwanda na Biashara imetekeleza maoni ya Kamati. Hata hivyo, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa leseni za utafutaji makaa ya mawe na chuma zitolewe kwa Mashirika ya Umma pekee.

(b) Hoja nyingine ambayo imetekelezwa kwa kiasi kikubwa ni kuhusu uamuzi wa kutumia mfumo mpya wa malipo ya *concession fees* katika Hifadhi za Taifa ili kuinua mapato ya Serikali. Hoja hii pia ipo katika hatua za utekelezaji japo kumekuwepo na changamoto kubwa za kiutekelezaji.

(c) Kamati imeridhishwa pia na uamuzi wa Serikali kupunguza dhamana za ukopaji kutoka kwenye mifuko ya Pensheni kama ilivyokuwa imependekezwa na Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande mwingine, Kamati inaendelea kufuatilia utekelezaji wa baadhi ya hoja ambazo bado utekelezaji wake siyo wa kuridhisha kwa lengo la kuhakikisha mapendekezo yote ya Kamati yanafanyiwa kazi ipasavyo. Hoja hizo ni kama ifuatavyo:-

(a) Kamati ilipendekeza kufanywe jitihada za dhati kuimarisha Ofisi ya Msajili wa Hazina kwa mujibu wa Sheria ya Msajili wa Hazina *Cap. 418* ili kuipa nguvu na uwezo wa kuyasimamia Mashirika ya Umma ipasavyo, ama vinginevyo, Serikali izingatie mapendekezo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali aliyependekeza kuundwa kwa chombo au Taasisi Maalumu ya kudhibiti na kusimamia utendaji wa Mashirika ya Umma. Hoja hii bado haijatekelezwa kikamilifu kwani hadi sasa kilichopitishwa ni Sheria ya Msajili wa Hazina

lakini kimaudhui na kimantiki Ofisi hii bado haijaanza kujitegemea kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

(b) Hoja ya kuanzishwa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma *(Public Investment Fund)*, jambo hili hadi sasa halijafanyiwa kazi na Serikali ukizingatia ukweli kuwa, Mashirika ya Umma yalianzishwa kwa makusudi makubwa ya kutoa huduma kwa wananchi kwa gharama nafuu, na kwa muda mrefu yamekuwa yakifanya hivyo japo yanakabiliwa na changamoto kubwa. Aidha, kutokana na mantiki kuwa baadhi ya Mashirika yamekuwa yakizalisha ziada kutokana na huduma wanazotoa, kwa mfano mifuko ya Hifadhi ya Jamii, Mamlaka ya Bandari Tanzania, *EWURA, TCRA, SUMATRA*, na hivyo basi Kamati inaendelea kusisitiza juu ya uanzishwaji wa Mfuko huu maalumu ili kusaidia baadhi ya Mashirika ya Umma ambayo ni muhimu kwa uchumi wetu kupata mitaji, kwa mfano *ATCL, NIP (strategic parastatals)* na kadhalika.

(c) Hoja nyingine ambayo utekelezaji wake siyo wa kuridhisha ni kuhusu uteuzi wa Wajumbe wa Bodi za Wakurugenzi katika Mashirika ya Umma. Kwa mfano, katika Bodi ya Utalii Tanzania, Bodi ya Wakurugenzi ilimaliza muda wake kwa zaidi ya miaka miwili, lakini imechukua muda mrefu hadi Bodi mpya kuteuliwa kiasi ambacho kinaweza kuwa na athari za usimamizi wa Menejimenti ya Bodi hiyo. Vile vile Shirika la Ndege Tanzania halina Bodi hadi sasa.

(d) Hoja nyingine ambayo haijafanyiwa kazi ni kuongeza mtaji kwa Shirika la Tija la Taifa *(NIP)* ambacho ni chombo muhimu kinachoweza kulisaidia Taifa katika kuhakisha shughuli zinafanyika kwa tija ikizingatiwa uchache wa rasilimali tulizonazo. Shirika hili ambalo likitumiwa vizuri litapunguza upotevu wa fedha za umma unaofanyika katika nyanja za mafunzo toka kwa Taasisi ambazo baadhi hazina nyenzo na uwezo wa kutoa mafunzo yenye ubora unaotakiwa, halipati ruzuku toka Serikalini ili kujiendesha kwa ufanisi. Kamati ilipendekeza Wizara ya Kazi iingize Mpango kazi wa Shirika

kupatiwa Shilingi bilioni 1.5 ili kulipa uwezo na nyenzo za kufanyia kazi ili liweze kuwa *think tank* ya Taifa katika maeneo ya kuongeza tija na ufanisi.

(e) Hoja ya kuligawanya Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* kuwa Mashirika mawili ili kutoa usimamizi wa kutosha katika Sekta ya Gesi, bado halijafanyiwa kazi na Serikali, hivyo Kamati inaendelea kufuatilia utekelezaji wa hoja hii ili kuliwezesha Taifa kukabiliana na changamoto za Sekta ya Gesi na Mafuta zilizokwishabainika hadi sasa na zile za baadaye. Katika hoja hii, Kamati ilisisitiza marekebisho ili kuwa na Shirika la Mafuta na Gesi *(ambalo linaweza kuitwa Petro Tan)* na Mamlaka ya Mafuta na Gesi *(Petrolium Authority)*. Shirika lifanye Biashara na kuwekeza. Mamlaka itahusika na leseni na Usimamizi wa Sekta ya utafutaji na uzalishaji wa mafuta na gesi na pia kusimamia Mikataba.

(f) Hoja nyingine ni kuhusu mpango maalum wa kulinusuru Shirika la Umeme Tanzania *(TANESCO)* na hali duni ya kifedha ili liweze kukabiliana na changamoto za kuzalisha, kusafirisha na kuuza u meme. Kamati inaona hoja hii bado haijakamilika ikiwa ni pamoja na hoja ya kuliangalia upya Shirika la Umeme na kuona hoja ya kuligawanya ili kupata Shirika la Uzalishaji *(liberalised generation)* na Shirika la Umma la usambazaji na Ugawanyaji *(transmission and distribution).* Kama uamuzi wa haraka wa kufanya mageuzi katika *TANESCO* hautafanyika, ni wazi wataendelea kutumia zaidi ya Shilingi bilioni 245 kununua umeme kutoka kwa wazalishaji binafsi kufuatia mikataba ghali sana na Kampuni binafsi. Hali hii ni mbaya zaidi katika kipindi hiki cha umeme wa dharura. Kamati inataka kupata maelezo ya utekelezaji wa pendekezo hili.

(g) Kamati ilishauri kwamba Shirika Hodhi la yaliokuwa Mashirika ya Umma *(CHC),* lifanywe la kudumu na limiliki hisa zote za Serikali katika Kampuni binafsi ambazo Serikali ina hisa chini ya asilimia 50, hivi sasa Kamati inashindwa kufuatilia

uwekezaji wa hisa za Serikali katika Kampuni binafsi na hivyo wananchi kutokujua hatma ya mali zao kupitia Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2009/2010 Kamati imeendeelea kupima ufanisi kwenye Mashirika ya Umma kwa kuzingatia vigezo vikubwa vifuatavyo:-

(a) Uzingatiaji wa misingi ya utawala bora katika uendeshaji wa Shirika husika *(corporate good governance).*

(b) Kiasi cha mtaji uliowekezwa katika Shirika na namna mtaji huo unavyoweza kuongezeka kutokana na utendaji wa kila siku wa Shirika.

(c) Uzingatiaji wa Sheria na taratibu zinazolianzisha Shirika husika *(compliance with laws).*

(d) Uwezo wa kiuongozi ndani ya Shirika, hasa uwezo wa Watendaji Wakuu na Menejimenti ya Shirika.

(e) Kutojihusisha kwa namna yoyote kwa Shirika au watumishi wa Shirika katika masuala yanayohusiana na rushwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kufanya rejea katika andiko la kitabu kinachofahamika kama *Next Steps Team, Ofice of Public Services, Cabinet Office, United Kingdom,* waandishi mabingwa katika tathmini ya Ufanisi wa Sekta ya Umma Ndugu Jeremy Cowper na Daktari Martini Samuels wanabainisha kuwa tathmini ya ufanisi wa Sekta ya Umma unapimwa kwa vigezo vifuatavyo:-

- Upimaji wa ufanisi wa Shirika au Taasisi kwa malengo yaliyo wazi *(objectively assesment of Performance);*

- Kuainisha maeneo muhimu yanayohitaji maboresho;

- Kuangalia Taasisi na Mashirika mengine namna yalivyotekeleza mipango ya mabadiliko kuelekea ufanisi na mwisho; na

- Kufanya majaribio kuona iwapo mbinu zinazotumika kuleta ufanisi zinatoa matunda yaliyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya kwanza ya ufanisi wa Mashirika ya Umma yanayomilikiwa na Serikali kwa asilimia 100, imefanyika kwa kuzingatia kigezo cha mapato ya Shirika kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni, 30, 2010 na Desemba, 2010 *(Income turn over),* Mashirika kumi yaliyozalisha mapato mengi na kiasi cha mapato ni kama ifuatavyo:-

**Jedwali na 3:**

**Faida *(Income turn over)* iliyopatikana kwa Mashirika tisa ya Umma yanayofanya biashara na kutoa huduma**

| Na. | Shirika | Mwaka wa fedha | Mapato |
|---|---|---|---|
| 1. | Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) | 30 Juni, 2010 | 40,462,263,480 |
| 2. | Reli Assets Holding Corporation | 30 Juni, 2010 | 10,261,012,039 |
| 3. | Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) | 30 Juni, 2010 | 5,431,451,354 |
| 4. | Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) | 30 Juni, 2010 | 4,439,885,000 |
| 5. | Kilimanjaro Airport Development Company (KADCO) | 31 Desemba, 2010 | 514,364,000 |
| 6. | Twiga Bancorp Limited | 31 Desemba, 2010 | 472,396,000 |
| 7. | Shirika la Magazeti la Serikali (TSN) | 31 Desemba, 2009 | 322,061,475 |
| 8. | Shirika la Posta Tanzania (TPC) | 31 Desemba, 2010 | 144,892,423 |

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa madhumuni ya kuliarifu Bunge lako Tukufu juu ya ufanisi wa Mashirika ya Umma, Kamati ilifanya tathmini ya Ufanisi katika baadhi ya Mashirika ya Umma

ambayo sio ya kibiashara na kuangalia faida iliypatikana kama ifuatavyo:-

**Jedwali na 4:**

**Faida iliyopatikana kwa Mashirika kumi ya Umma yanayotoa huduma na hayapati ruzuku ya Serikali**

| Na. | Shirika | Mwaka wa fedha | Mapato |
|---|---|---|---|
| 1. | Mfuko wa Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF) | 30 Juni,2010 | 207,987,134,000 |
| 2. | Mfuko wa Pensheni wa Mashirika ya Umma (PPF) | 30 Juni,2010 | 97,625,924,000 |
| 3. | Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Serikali za Mitaa ( LAPF) | 30 Juni,2010 | 90,480,644,002 |
| 4. | Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) | 30 Juni ,2010 | 63,772,740,000 |
| 5. | Mfuko wa Pensheni wa Watumishi Serikali (GEPF) | 30 Juni, 2010 | 18,692,844,000 |
| 6. | Mfuko wa Pensheni wa Watumishi wa Umma (PSPF) | 30 Juni, 2010 | 16,293,556,000 |
| 7. | Mamlaka ya Elimu ya Ufundi Stadi (VETA) | 30 Juni, 2010 | 16,086,732,000 |
| 8. | Mamlaka ya udhibiti wa mawasiliano Tanzania (TCRA) | 30 Juni, 2010 | 14,304,397,000 |
| 9. | Bodi ya Bima za amana ( DIB) | 30 Juni, 2010 | 10,642,254,839 |
| 10. | Mamlaka ya udhibiti wa Nishati na Maji (EWURA) | 30 Juni, 2010 | 7,511,452,000 |

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tathmini hiyo inayotoa picha halisi ya ufanisi wa baadhi ya Mashirika ya Umma, ni maoni ya Kamati kuwa usimamizi wa dhati wa Mashirika ya Umma upewe msukumu wa kutosha. Aidha, Serkali iendelee na juhudi za kutosha katika uwekezaji wa Mashirika ya Umma ambayo yanatoa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, zoezi la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma lilianza kutekelezwa hapa nchini mwanzoni

mwa miaka ya 1990 likiwa na lengo kubwa la kuiondoa Serikali katika kufanya biashara moja kwa moja, kutoa nafasi ya kukua kwa Sekta Binafsi na zaidi kuimarisha utendaji wa yaliokuwa Mashirika ya Umma ili badala ya kupokea ruzuku kutoka Serikalini, basi Mashirika husika yafanye kazi na kuzalisha kwa tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wanataaluma wa Uchumi, Ndugu Sunita Kikeri, John Nellis na Mary Shirley katika andiko lao lenye kichwa cha habari, *Privatization, The Lessons of Experience, World Bank, June 1992*, wanaelezea hoja muhimu nane zinazoweza kuufanya ubinafsishaji ulete matokeo stahili. Hoja hizo nane ambazo zilitakiwa kuzingatiwa ipasavyo wakati wa ubinafsishaji wa Viwanda na Mashamba ya bidhaa za Kilimo ni kama ifuatavyo:-

(a) Ubinafsishaji unatakiwa kufanyika kama sehemu ndogo tu ya mpango mkubwa wa mageuzi ya kiuchumi ukilenga kuleta ufanisi. Aina hii ilifanyika katika nchi za New Zealand, UK na Chile. Kwa kutumia mbinu hii, masoko huru yalifunguliwa na kutoa nafasi kwa Sekta binafsi kukua na kuweka kanuni za kuwalinda walaj.

(b) Uandaaji wa Kanuni za kudhibiti soko ili kuhakikisha kuwa wadau wote ikiwa ni pamoja na Serikali, walionunua viwanda na wananchi wa kawaida wote kwa pamoja wanakuwa chini ya kanuni za udhibiti ili kuepuka *monopolies*.

(c) Nchi inaweza kutumia mbinu ya kukodisha Menejimenti na siyo kuuza mali za Shirika husika na ikaendelea kupata faida za ubinafsishaji (mfano Kampuni ya usambazaji maji ya *Ivory Coast*).

(d) Ubinafsishaji unatakiwa kufanyika baada ya kufanyika tathmini ya kina na kujipa muda wa kutosha badala ya kutekeleza zoezi hilo kwa kasi bila utafiti wa kina.

(e) Ubinafsishaji lazima ufanyike kwa uwazi *(transparency)* ikizingatiwa kuwa uwazi ndio msingi wa maendeleo ya kiuchumi na kisiasa.

(f) Kabla ya ubinafsishaji, Serikali inatakiwa kuandaa mpango mkakati wa kulinda jamii yake ili isipate shida kutokana na zoezi la ubinafsihaji *(developing a social safety net).*

(g) Serikali lazima iwe na mbinu mbadala katika kukabiliana na changamoto za ubinafsishaji ili kuleta matokeo bora, kwa mfano kama kuweka mpango wa kugawana hisa katika Shirika badala ya kukabidhi umiliki wa Shirika kwa mwekezaji kwa asilimia mia moja *(flexibility on privatization tactics).*

(h) Uimarishaji wa ukuaji wa sekta binafsi katika uchumi huru mchanganyiko *(free* market *economy)* ni jambo la muhimu ili kuufanya ubinafsishaji kutoa matokeo stahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka wa fedha 2009/2010, Kamati iliamua kufanya tathmini ya utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma kwa kuchagua Sekta ndogo ya Mashirika ya Umma yaliokuwa yakijishughulisha na uzalishaji wa bidhaa za Kilimo na baaadhi ya Mashamba ya bidhaa za Kilimo. Kamati kwa kushirikiana na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja Ofisi ya Shirika Hodhi la yaliyokuwa Mashirika ya Umma *(CHC)* kwa pamoja walichagua maeneo mahususi na kuyatembelea na hivyo kutoa tathmini ya utekelezaji wa zoezi hilo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza lililoshughulikiwa na Kamati ni kutembelea Viwanda vya Korosho vilivyobinafsishwa katika Mikoa ya Lindi na Mtwara ili kuona iwapo utekelezwaji wa Sera ya Ubinafsishaji umefikia malengo yaliokusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Korosho cha Likombe kipo mjini Mtwara na kilijengwa mwaka 1980 kwa kutumia teknolojia ya Kijapani. Kwa Mwaka 2004, kiwanda kiliuzwa kwa kampuni ya *Micronix System Limited* kwa bei ya Shilingi milioni 100 ambayo alikwishalipa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda hakijawahi kuzalisha tangu kilipobinafsishwa mwaka 2004. Mwekezaji hajafanya ukarabati wowote wa mashine zilizokuwepo kiwandani ila amenunua mashine nne mpya za upakiaji ambazo ni *mixing, packing, drying* na *humidifier machines.* Sehemu kubwa ya mashine za zamani zimeharibika na kulundikwa sehemu moja na mwekezaji anadai kuwa teknolojia yake imepitwa na wakati na hivyo hazifai kwa matumizi tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya Kamati kutembelea eneo la Kiwanda 19/03/2012 ilibainika kuwa Mwekezaji amekodisha sehemu ya ghala kwa kampuni binafsi ambayo inaendesha zoezi la kutunza korosho kwa mtindo wa stakabadhi ghalani na pia amekodisha sehemu ya Kiwanda kwa Kampuni ya Olum ambayo inafanya shughuli za Ubanguaji wa Korosho kwa kiasi kidogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kamati kuwa zoezi la ubinafsishaji katika Kiwanda hiki halikufanikiwa, na mwekezaji tayari amekwishavunja makubaliano ya Mkataba wa Mauzo kwa kuchelewa kuwekeza. Ni muhimu sasa kwa Serikali kuchukua hatua stahili kuhusiana na Masharti ya Mkataba yaliyovunjwa na Mwekezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Korosho cha Mtama kipo Lindi Vijijini na kilijengwa mwaka 1978 kikiwa na uwezo wa kubangua tani 5,000 za korosho kwa mwaka. Kiwanda kiliuzwa kwa kampuni ya *Lindi Farmers Company Limited* mwaka 2005 kwa bei ya Shilingi milioni 30.0 ambayo amekwishalipa. Hadi kinabinafsishwa, kiwanda kilikuwa katika

hali nzuri na kwamba yalihitajika matengenezo madogo madogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kutembelea kiwanda hiki, kwa kiasi fulani Kamati imeridhika na namna mwekezaji alivyofanya ukarabati mkubwa uliogharimu kiasi cha Shilingi milioni 890. Kiwanda kipo katika hali nzuri na mitambo yote inafanya kazi. Mwekezaji alieleza kuwa wamechelewa kuanza uzalishaji kutokana na ukosefu wa fedha kwa ajili ya kuendesha kiwanda. Hata hivyo, wanatarajia kuanza uzalishaji mwezi Juni, 2012 kwa kuwa wamefanikiwa kupata fedha na kwa sasa wameshanunua tani 10 za korosho na mafuta ya kuchomea korosho.

**Mwonekano halisi kwa njia ya picha**



**Sehemu ya kuchambulia korosho**



Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Korosho cha Lindi kipo mjini Lindi na kilijengwa kuanzia mwaka 1977 kwa kutumia teknolojia ya Kiitaliano na kilikuwa na uwezo wa kubangua tani 10,000 za korosho kwa mwaka.

Kiwanda kilifanyiwa majaribio mwaka 1978 na kuendelea kufanya kazi hadi mwaka 1996, kiliposimama. Mwaka 2004 kiwanda kiliuzwa kwa kampuni ya *Bucco Investment Holdings Limited* kwa bei ya shilingi milioni 50.0.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji alitakiwa kuwekeza kiasi cha Dola za Kimarekani 600,000 kwa ajili ya ukarabati wa kiwanda. Mwekezaji amefanya ukarabati kwa gharama ya Shilingi milioni 250.

Maeneo yaliyofanyiwa ukarabati ni *boiler*, mashine za kukatia korosho na *grading*. Kiwanda kimesimama kwa kukosa mtaji wa uendeshaji. Ni maoni ya Kamati kuwa Mwekezaji

amevunja Mkataba wa Mauzo kwa kushindwa kufufua kiwanda.

**Mwonekano katika picha**





Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Korosho Newala II kipo Wilaya ya Newala Mkoa wa Mtwara. Ujenzi wake ulianza mwaka 1977 na kukamilika mwaka 1980 kwa kutumia tekinolojia ya kijapani na kilikuwa na uwezo wa kubangua tani 10,000 za korosho kwa mwaka. Kiwanda kilifanya kazi kwa muda wa mwaka mmoja na kisha kusimama kutokana na uhaba wa korosho ghafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2004 kiwanda kiliuzwa kwa kampuni ya *Micronix Sytems Ltd.* kwa bei ya Shilingi milioni 75.0. Mwekezaji alikwishalipa fedha zote na kukabidhiwa kiwanda. Hadi wakati kiwanda hiki kinabinafsishwa, sehemu kubwa ya kiwanda ilikuwa katika hali nzuri ukiacha matengenezo ya sehemu kadhaa kutokana na kukaa kwa muda mrefu bila ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulingana na Mpango wa Uwekezaji, Mnunuzi alitakiwa kuwekeza kiasi cha Dola za Marekani milioni 3.64 katika ukarabati wa kiwanda kwa kipindi cha miaka mitano kuanzia mwaka 2006 mpaka 2010 kama

ilivyoainishwa kwenye Mkataba wa Mauzo. Mwekezaji alieleza kuwa amewekeza kiasi cha Shilingi milioni 150 katika ukarabati wa kiwanda kwa kununua mashine za kutumia teknolojia ya mkono. Ukarabati huo ulifanyika mwaka 2009. Mashine za zamani zimekusanywa na kulundikwa sehemu moja kwa kile mwekezaji anachodai kuwa teknolojia yake imepitwa na wakati.

**Mwonekano katika picha**





Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha Korosho Newalla I kipo mjini Newala, mkoa wa Mtwara, kando ya barabara

iendayo Masasi. Kiwanda kilijengwa mwaka 1976 na kufanyiwa majaribio mwaka 1981 na hakikufanya kazi baada ya majaribio ya awali. Kiwanda hiki kilijengwa kwa mitambo ya teknolojia ya Kiitaliano yenye uwezo wa kubangua tani 10,000 kwa mwaka.

Aidha, kwa maelezo ya Uongozi wa Shirika Hodhi la yaliokuwa Mashirika ya Umma *(CHC),* mwaka 2004 kiwanda kiliuzwa kwa kampuni ya *Agrofocus Limited* kwa bei ya Shilingi milioni 75.0. Mwekezaji alikwishakamilisha malipo.

Hadi wakati kinabinafsishwa, mitambo na mashine ya kiwanda vilikuwa katika hali nzuri ukiacha sehemu chache za umeme na mikanda ya kusafirishia korosho. Aidha, majengo ya kiwanda yalikuwa katika hali nzuri isipokuwa sehemu kadhaa za paa ambazo zilihitaji ukarabati ili kuzirejesha katika hali ya kawaida.

Mwekezaji amewekeza kiasi cha Shilingi milioni 718.0 katika ukarabati wa kiwanda. Mashine zote zimekarabatiwa na zinafanya kazi. Kiwanda kipo katika hali nzuri, mazingira ni safi na majengo yote yamepakwa rangi.

Mashine pia zipo katika hali nzuri. Mwekezaji amefanya kazi nzuri kulingana na Mkataba wa Mauzo.

**Mwonekano katika picha**

Mashine zikiwa katika hali nzuri





Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya tathmini, Kamati haijaridhishwa kabisa na zoezi la ubinafshishaji wa Mashirika ya Umma katika Sekta Ndogo ya Viwanda vya Korosho (Mamlaka ya Korosho). Viwanda vyote vya kubangua korosho vilivyojengwa kwa Mkopo wa Benki ya Dunia vyenye thamani ya Dola milioni 284 havifanyi kazi. Wawekezaji waliovinunua wamevigeuza kuwa maghala ya kuhifadhia korosho na nchi inaendelea kupata hasara kubwa kwa kusafirisha korosho ghafi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tathmini ya ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma ilifanyika pia katika mashamba na viwanda vya zao la Mkonge vilivyobinafsishwa ili kupata picha halisi ya utekelezwaji wa Sera ya Ubinafsihaji katika eneo hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitembelea baadhi ya Viwanda na Mashamba ya bidhaa za Katani yaliyobinafsishwa na kuandaa tathmini ifuatayo ambayo inatokana na hali halisi ya kiwanda au shamba:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Shamba la Mkonge la Gomba *(Gomba Sisal Estate)* lipo katika Wilaya ya Korogwe Mkoani

Tanga na lina ukubwa wa hekta 4,562 zikiwa zimegawanywa katika makundi matatu ambayo ni Gomba hekta 1,623, Mwenga hekta 1,008 na Mswaha hekta 1,931. Shamba hili lilibinafsishwa mwaka 1998 kwa kampuni ya *Gomba Agricultural Industries Ltd.*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwekezaji alianza kupanda mkonge mpya aliponunua shamba mwaka 1998, hadi ilipofikia mwaka 2011 jumla ya hekta 1,516.88 zilikuwa tayari zimepandwa mkonge. Kwa sasa mwekezaji ana mpango wa kupanda hekta 100 kwa mwaka. Shamba lipo katika hali nzuri na uwekezaji wa zaidi ya Shilingi bilioni 1.6 umefanyika. Kamati imeridhika na utekelezaji wa Sera ya Ubinafsishaji katika shamba hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilipewa taarifa kuwa uzalishaji umekuwa ukiongezeka kutoka wastani wa tani 516 mwaka 1998 mpaka wastani wa tani 889.95 mwaka 2011. Uzalishaji mkubwa wa tani 915 ulionekana mwaka 2008. Kupungua kwa uzalishaji baada ya mwaka 2008 ulitokana na mtikisiko wa uchumi wa dunia. Mkonge mwingi huuzwa nje ya nchi na kiwango kidogo huuzwa hapa nchini katika kiwanda cha *TANCORD* na nyingine huuzwa kwa kampuni ya *Mohammed Enterprises Ltd.*

Mheshimiwa Naibu Spika, *Hale Sisal Estate* lipo katika Wilaya ya Korogwe Mkoani Tanga na lina ukubwa wa hekta 4,180 ambapo kati ya hizo, hekta 315 ni eneo la kiwanda, barabara, makazi, milima na sehemu chepe chepe. Eneo linalobaki la hekta 3,865 ndilo linalofaa kwa kilimo cha mkonge. Eneo linalofaa kwa kilimo cha mkonge ni hekta 3,865 kati ya hizo ni hekta 1,136 ambazo ni sawa na asilimia 29.4 ya eneo lote la shamba ndizo zilizopandwa mkonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ilitembelea shamba hili na kuona kuwa, Korona zote mbili zipo katika hali nzuri na zinatumia aina mbili ya teknolojia za usindikaji. Korona ya asili

kwa ajili ya singa ndefu na korona ya *hammer mill* ambayo hutoa singa fupi kwa ajili ya rojorojo, karatasi na *composites.* Majengo na miundombinu ya barabara kwa sehemu kubwa ni ya kuridhisha. Pia kuna mradi wa *Bio-gas* unaozalisha umeme kutokana na mabaki ya zao la mkonge.

**Mradi wa bio gas katika shamba la Hale**



Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaamini kwa dhati kuwa Sera ya ubinafsishaji imefanikiwa kwa kiasi kikubwa katika mradi huu, na endapo zoezi la tathmini ya mafanikio na changamoto za ubinafshaji litafanyika ipasavyo, basi wawekezaji wa aina hii waendelee kupata msukumo na msaada wa Serikali ili kuongeza tija na uzalishaji kwa manufaa ya uchumi wa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Amboni Sisal Estate* lipo katika Wilaya ya Tanga Mkoani Tanga na lina ukubwa wa hekta 3,851. Shamba lilikuwa linamilikiwa na Kampuni ya *Amboni Plantations Limited*. Mwekezaji *(Amboni Plantations Limited)* aliliweka dhamana shamba hilo kwa ajili ya kupata mkopo kutoka benki ya *Stanbic,* hata hivyo alishindwa kuulipa. Mwaka

2007 benki ililichukua shamba hilo na kuliuza kwa kampuni ya *Segera Estates Limited*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba hili lilinunuliwa na kampuni ya *Sagera Estates Limited* mwaka 2007. Sehemu kubwa ya shamba lilikuwa imechukuliwa kwa matumizi mbalimbali. Mfano, baadhi wa wahanga wa mafuriko yaliyotokea mwaka 1971, walihamishwa kutoka sehemu zilizoathirika na kupelekwa katika eneo la shamba hili na kuunda kijiji cha Mafuriko. Hali ya uvamizi wa shamba ilizidi kuongezeka ambapo zaidi ya hekta 2,200 zimevamiwa na kuna vijiji zaidi ya sita vyenye wakazi zaidi ya 3,000. Huduma za kijamii kama vile shule, Kanisa, Msikiti na shughuli ya kiuchumi kama vile kilimo, uchimbaji wa kokoto, viwanda vya kutengeneza chokaa zinapatikana ndani ya shamba lililovamiwa. Kwa sasa shamba limebakiwa na ukubwa wa hekta 1,651 na hakuna mkonge wowote shambani ila kuna vichaka, majani marefu na miti.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kiwanda cha *Tancord (1998) Limited* kilifunguliwa mwaka 1965 kwa lengo la kuzalisha bidhaa za mkonge. Serikali kupitia iliyokuwa Tume ya Rais ya Kurekebisha Mashirika ya Umma *(PSRC)* iliamua kuuza hisa zote za kampuni ya *MGC* kikiwemo kiwanda hiki kwa Kampuni ya Katani limited mnamo mwaka 1998. Bei ya ununuzi ilikuwa ni Dola za Kimarekani 858,339 ambapo mnunuzi amekwishalipa zote.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutathmini ubinafsishaji wa kiwanda hiki, imebainika kuwa, jumla ya Dola za Kimarekani milioni 21 zilitakiwa kuwekezwa kwa kipindi cha miaka 10 kuanzia mwaka 2007. Mpaka sasa jumla ya Dola milioni 12 zimewekezwa ambazo ni sawa na 57% ya makubaliano ya mkataba. Uwekezaji mkubwa umefanyika katika ukarabati na ununuzi wa mashine mpya, ukarabati wa mifumo ya maji na umeme, ununuzi wa magari, ukarabati na ujenzi wa majengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuonyesha ufanisi wa ubinafsishaji kwenye kiwanda hiki, jumla ya tani 11,089 zimeweza kuzalishwa kwa kipindi cha miaka mitatu kuanzia mwaka 2009 ambazo ni wastani wa tani 3,696 kwa mwaka. Uwezo wa kiwanda ni kuzalisha tani 60,000 kwa mwaka. Hivyo uzalishaji halisi (tani 3,696) ni sawa na 6% ya uwezo wa kiwanda. Uzalishaji huu mdogo ulisababishwa na uchache wa upatikanaji wa singa kutoka kwa wazalishaji wa mkonge, soko na upatikanaji wa umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Bombuera Sisal Estate* lina ukubwa wa hekta 2,370 na lipo Wilaya ya Korogwe Mkoani Tanga. Shamba hili, ni moja ya mashamba yaliyouzwa kwa *Chavda Group* mwaka 1998 ambapo mwekezaji alitumia Hati Miliki ya shamba kupata mkopo ambao haukutumika kwa kusudi la kuendeleza shamba iliyopelekea kulitelekeza. Hivyo, shamba hilo lilishikiliwa na Benki ya *CRDB* mpaka mwaka 2002 lilipouzwa kwa Kampuni ya *AMC Arusha Limited.*

Mheshimiwa Naibu Spika, hali ya shamba ni mbaya, kwani hakuna shughuli zozote za kufufua kilimo cha mkonge. Sehemu kubwa ya shamba imevamiwa kwa kujengwa nyumba za kudumu na kulima mazao ya msimu na ya kudumu. Aidha, Kamati imebaini kuwa, Korona iliuzwa kwa amri ya Mahakama baada ya mwekezaji kushindwa kulipa madeni yaliyotokana na madai mbalimbali. Hii ilisababishwa na uzalishaji kusimama kutokana na miundombinu ya umeme kuibiwa. Aidha, nyumba nyingi za wafanyakazi katika shamba hilo zimeharibika.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Kwafungo Sisal Estate* lipo katika Wilaya ya Muheza Mkoani Tanga na lina ukubwa wa hekta 2,310. Shamba hili ni moja ya mashamba yaliyouzwa kwa *Chavda Group* mwaka 1998 ambapo mwekezaji alitumia Hati miliki ya shamba kupata mkopo ambao haukutumika kwa kusudi la kuendeleza shamba, hivyo shamba hilo bado linashikiliwa na Benki ya *CRDB*.

Mheshimiwa Naibu Spika, shamba limetelekezwa na hakuna mkonge. Pia wanavijiji wamevamia na kulima mazao ya msimu na ya muda mrefu. Ni maoni ya Kamati kuwa kuna ulazima wa Serikali kuangalia upya matatizo ya shamba hilo ili kutekeleza vyema sera ya ubinafsishaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Ubena Zomozi Sisal Estate* liliuzwa kwa Kampuni ya *Highlands Estates Ltd*. mwaka 2007. Shamba liko katika Wilaya ya Bagamoyo Mkoa wa Pwani na lina ukubwa wa hekta 4,227. Shamba liko katika hali nzuri na upandaji mkonge mpya unaendelea. Jumla ya hekta 499 zimepandwa mkonge ambayo ni sawa na 12% ya eneo lote la shamba. Hekta tano zimepandwa maembe, na hekta 57 ni shamba kwa kwa ajili ya ufugaji wa ng'ombe wa nyama.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kamati kuwa ubinafshishaji wa baadhi ya Viwanda vya Katani hasa *Hale Estate* umefanikiwa kwa kiasi kikubwa na hivyo kuishauri Serikali iendelee kutafuta masoko zaidi ya bidhaa za Katani na bidhaa nyinginezo kama *biogas*, na kadhalika. Hali kadhalika wakulima wadogo wawezeshwe ili kushiriki kikamilifu katika kilimo cha mkonge kupitia mashamba yaliyobinafsishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya mjadala wa maudhui na uchambuzi wa Taarifa hii hapo awali, Kamati ina maoni na mapendekezo mahususi yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ni maoni ya Kamati kuwa Ofisi ya Msajili wa Hazina bado inatakiwa kuimarisha usimamizi katika Mashirika ya Umma kwa niaba ya Serikali. Aidha, Kamati inaamini kuwa iwapo Mashirika ya Umma yatasimamiwa vyema, yana nafasi kubwa ya kusaidia ukuaji wa pato la Taifa na uchumi wa nchi kwa ujumla.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa katika uchumi mchanganyiko *(mixed economy)*, ambao Sekta binafsi haijakuwa sana na hivyo kuihitaji Sekta ya Umma

katika kutengeneza miundombinu na mazingira bora ya uchumi, ni wajibu wa Serikali kwa kupitia Mashirika ya Umma kuendelea kutoa baadhi ya huduma za muhimu kwa wananchi wake kwa gharama nafuu zaidi bila kulenga kupata faida kubwa. Ni kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni kuwa huduma za afya, pensheni kwa wazee, huduma za nishati na uinuaji wa kiuchumi kwa wananchi wa kawaida zitabaki kutegemea kwa kiasi kikubwa  Mashirika ya Umma hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuzingatia kanuni za kudumu za Bunge Toleo la mwaka 2007, naomba kuwasilisha mapendekezo ya Kamati kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati imebainisha kuwa Mashirika mengi ya Umma hayana mitaji ya kutosha kujiendesha, na kwa kuwa kutokuwepo kwa mitaji kunasababishwa zaidi na kutokuwepo kwa Mfuko wa Uwekezaji wa Umma *(Public Investment Fund)*, kwa hiyo, Kamati inaendelea kupendekeza  kuwa Mfuko wa uwekezaji wa Umma uanzishwe mara moja ili kwa utaratibu utakaoonekana unafaa, baadhi ya Mashirika ya Umma yenye kupata faida, yaanze kuweka fedha katika mfuko huo ili kusaidia Mashirika ya Umma yasiyokuwa na mitaji ila ni *strategic* kwa Taifa letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati imebaini viashiria vya Fedha za kufidia wakulima wa Pamba kutokana na anguko la uchumi duniani, kutowafikia walengwa  kupitia kwenye Bodi ya Pamba Tanzania, na kwa kuwa viashiria hivyo vinatokana na ukaguzi wa hesabu za Bodi kwa mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2010 ambao umeonyesha kuwa baadhi ya walengwa wa fedha za kunusuru bei ya Pamba wamekiri kutopewa fedha hizo na hivyo Mkaguzi kutoa hati yenye shaka kwa Bodi ya Pamba. Kwa hiyo, Kamati inapendekeza kuwa, Kamati inapendekeza kuwa Bodi ya Pamba, iliyopo sasa hivi, ivunjwe na iundwe upya. Aidha,

Kamati inaitaka Serikali ifanye ukaguzi na uchunguzi maalumu ili kubaini iwapo fedha za kufidia anguko la bei ya pamba ziliwafikia walengwa kama ilivyokusudiwa na kisha kuchukua hatua stahili kutokana na uchunguzi huo na Bunge lipewe Taarifa ya matokeo ya uchunguzi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa katika tathmini yake ya viwanda vilivyobinafsishwa vya ubanguaji Korosho, imebainika kuwa baadhi ya wawekezaji wamekiuka kwa makusudi mikataba ya uendeshaji wa Viwanda hivyo, na kwa kuwa kwa kufanya hivyo wamesababisha Taifa kuendelea kusafirisha korosho ghafi kwenda Nje ya Nchi na hivyo kuondoa fursa ya wakulima kupata faida ya kutosha na kupunguza ajira nchini, kwa hiyo, Kamati inapendekeza kuwa Serikali ichukue uamuzi wa kuvirejesha viwanda vyote vya kubangua Korosho vilivyobinafsishwa na wawekezaji wake kushindwa kuviendeleza ili kuona namna bora ya kuwekeza kwenye ubanguaji wa korosho ikiwa na pamoja na Serikali kusisitiza umuhimu wa kuuza Korosho iliyobanguliwa Nje ya Nchi kwa kuwajengea uwezo wakulima wa kubangua Korosho.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati imebaini kuwa Bodi ya Madawa Tanzania *(MSD)* inatumia takribani siku 21 ili kukamilisha mchakato wa kuondoa dawa bandarini, na kwa kuwa ucheleweshaji huo unaathiri usambazaji wa dawa hapa nchini kwa wakati muafaka na muda mwingine kusababisha dawa kuharibika kabla ya kuwafikia walengwa na hivyo kusababisha hoja kadhaa za Ukaguzi wa Hesabu, Kamati inapendekeza kuwa Bodi ya Madawa ianze mchakato wa kuwa na ghala maalum (*bonded ware house)* ili kurahisisha utoaji wa dawa bandarini mapema iwezekanavyo na zikaguliwe huko na Mamlaka zinazodhibiti ubora kama Shirika la Viwango la Tanzania *(TBS)* na Mamlaka ya Chakula na Dawa *(TFDA).* Kamati inapendekeza kwa Serikali kupitia Wizara ya Fedha na *TRA* kuharakisha jambo hili kabla mwaka wa fedha haujakamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Kamati imebaini na kuthibitisha ukosefu wa mitaji ya kutosha na uwekezaji mdogo wa Serikali katika baadhi ya Mashirika ya Umma ili yatekeleze mipango mikakati muhimu kwa manufaa ya Umma na baadhi ya Mashirika hayo ya Umma ni yale ambayo ni chachu ya maendeleo ya Taifa *(strategic Parastatals)*, na kwa kuwa ukosefu wa fedha na mitaji unazorotesha juhudi za Taifa letu kupata maendeleo. Kwa hiyo, Kamati inapendekeza kuwa Serikali itoe bajeti ya kutosha kwa Mashirika yafuatayo:-

Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi *(NEEC)* ambalo linahitaji kiasi cha Shilingi bilioni 25.5 kutekeleza majukumu yake ya kisheria, Shirika la Tija la Taifa *(NIP)* na Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* ili Mashirika haya yaweze kutekeleza mipango yake ipasavyo ambayo mingi imelenga kuinua maisha ya Watanzania wa kawaida waweze kushiriki shughuli za kiuchumi ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Taifa linakabiliwa na changamoto kubwa zinazohusiana na shughuli za usimamizi wa Nishati ya Gesi asilia na Mafuta na hasa uchimbaji na usimamizi wa mapato yatokanayo na gesi asilia, na kwa kuwa tunalo Shirika la Umma la Mafuta na Petroli *(TPDC)* ambalo ndilo lenye jukumu la kuendeleza Sekta hiyo hapa nchini, na kwa kuwa Shirika hilo linakabiliwa na changamoto kubwa ikiwamo kutojiendesha kwa mujibu wa amri ya uanzishwaji wake *(establishment order)* na hivyo kukwama kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Kwa hiyo, basi Kamati inapendekeza kuanzia sasa Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* lijiendeshe kwa mujibu wa Amri *(order)* ya uanzishwaji wake *(TPDC Establishment Order of 1969* na pia *Public Corporation Act of 1992)* ikiwa ni pamoja na kubaki na fedha zote inazokusanya kama Mashirika mengine *(retention)* badala ya kurudishwa Wizara ya Nishati na Madini. Aidha, Kamati inasisitiza kuwa, Wizara ya Nishati na Madini isiingilie utendaji kazi wa kila siku wa *TPDC* ili Shirika hili lifanye kazi kwa ufanisi, kwa uhuru na kwa misingi ya uanzishwaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa kumedhihirika wazi ukosefu wa ufanisi katika uendeshaji wa Shirika la Ndege Tanzania *(ATCL),* kulikosababishwa na matatizo ya Menejimenti iliyokuwepo na mikataba mibovu (mfano ukodishwaji wa ndege ya *Air bus*), Kamati inapendekeza hatua za kisheria zichukuliwe kwa wote waliohusika na uingiaji wa mikataba hiyo, lakini pia Kamati inapendekeza Serikali ifikirie uundwaji upya wa Shirika la Ndege la Taifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa tathmini ya ubinafsishaji wa Mashamba ya Mkonge imedhihirisha kuwa hali ya mashamba mengi siyo nzuri, kati ya mashamba yote yaliyobinafsishwa, ni mashamba mawili tu ya Mkambara na Mwelya yanayoridhisha kwa namna yanavyohudumiwa. Kamati inaishauri Serikali ifuatilie kwa ukaribu uendelezaji wa mashamba ili sera ya ubinafsishaji iwe na matunda yaliyokusudiwa.

Aidha, ili kuepuka migogoro na wananchi, maeneo ya mashamba yaliyovamiwa na wananchi yaachiwe kwa wananchi hao na mipaka ya mashamba ilindwe ipasavyo, na kwa wawekezaji walioshindwa kuendeleza mashamba ya Mkonge, Serikali iyarudishe na kuyagawa upya ikiwezekana hata kwa Wakulima wadogo. Fikra kwamba Mkonge lazima ulimwe na Wakulima wakubwa imepitwa na wakati. Serikali iwawezeshe wakulima wadogo kupitia Taasisi za Fedha walime Mkonge katika mashamba hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na ongezeko la riba inayotokana na Mkopo ambao Serikali imechukua kutoka kwenye Mifuko ya Hifadhi ya Jamii kugharimia ujenzi wa Chuo Kikuu Dodoma, Kamati inatoa pendekezo mahsusi kwa Serikali kutia saini makubaliano ya mkopo baina yake na Mifuko ya Hifadhi ya Jamii nchini kwa fedha walizotoa kujenga Chuo Kikuu cha Dodoma. Ni vyema ikafahamika kuwa fedha hizi ni mali ya Wanachama na hivyo ni lazima zilindwe ipasavyo.

Itakumbukwa kuwa pendekezo hili limetolewa kwa mara ya tatu mfululizo na Kamati kwenda Serikalini na hadi sasa halijatekelezwa. Kamati inataka kupata maelezo ya Serikali juu ya jambo hili. Kwa hiyo, Kamati inaliomba Bunge liazimie sasa, na kuitaka Serikali kutia saini makubaliano hayo ili madeni ya Mifuko ya Jamii yawe salama kwa mujibu wa Sheria ya Dhamana, Mikopo na Ruzuku. Kamati inasisitiza kuwa madeni ambayo hayana mashaka, yaanze kulipwa mara moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Mkataba baina ya Shirika la Utangazaji Tanzania *(TBC)* na *Star Times International Communication* una upungufu kadhaa ya kisheria na ambao umebainishwa na Mkaguzi wa Hesabu wa *TBC* baada ya kuchambua Mkataba na Taarifa ya Hoja za Ukaguzi, na kwa kuwa upungufu huo unaweza kuwa na athari katika utendaji wa *TBC* kwa siku zijazo; kwa hiyo basi, Kamati inapendekeza kuwa, Serikali iupitie upya Mkataba huo ili kuainisha maeneo ya maboresho.

Aidha, Serikali ifanye utaratibu wa kuangalia namna nzuri ya kutoa fedha kwa uendeshaji wa *TBC* ili kiwe chombo cha utangazaji wa Umma chenye kujiendesha kwa uhuru na kwa maslahi ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuna tatizo kubwa sana la uwekezaji katika ujenzi wa Chuo kikuu cha Dodoma. Mifuko ya hifadhi ya jamii yote ambayo iliikopesha Serikali kwa ajili ya ujenzi wa Chuo Kikuu cha Dodoma haijalipwa, na Serikali imegoma kuingia mkataba, na hali hii inahatarisha fedha za wafanyakazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inaliomba Bunge kuazimia na kuitaka Serikali kwanza kuweka sahihi makubaliano yaliyofikiwa na mifuko yote ya hifadhi ya jamii kuhusiana na ujenzi wa Chuo kikuu cha Dodoma; lakini pili, yale malipo ambayo hayana *queries* hivi sasa, Serikali iyalipe mara moja, vinginevyo wastaafu watakosa fedha za kulipwa,

kwa sababu uwekezaji huu ni wa fedha za wafanyakazi na tulikuwa tunaomba jambo hili Naibu Spika na Wabunge watakapochangia tuhakikishe linatokea haraka iwezekanvyo. Vinginevyo, baadhi ya mifuko kama *PSPF* itakufa na tutashindwa kuwalipa wafanyakazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati inataka Serikali ifanye uchunguzi kuhusiana na mkataba kati ya *TBC* na *Star Times Media* ili tuweze kuhakikisha kwamba *TBC* wanapata haki yao inavyostahili.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa suala zima la ubinafsishaji wa yaliyokuwa mashirika ya umma limekuwa na changamoto kubwa sana, zaidi kutokana na baadhi ya mali za mashirika ya umma kuuzwa kwa bei isiyolingana na thamani, pia mikataba mingi ya ubinafsishaji imekiukwa na wawekezaji; na kwa kuwa kwa kiasi kikubwa zoezi hili halikufanikiwa katika maeneo mengi na kwa kuwa Bunge kama Mwakilishi wa wananchi lingependa kufahamu faida na changamoto za zoezi zima la ubinafsishaji ili Waheshimiwa Wabunge wapate nafasi ya kujadili zoezi hili kwa uwazi.

Waheshimiwa Wabunge ni kwamba mpaka sasa hivi nchi yetu haijawahi kufanya tathmini ya kuweza kujua faida na hasara ambazo tumezipata katika zoezi zima la ubinafsishaji. Hivyo Kamati inapendekeza na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuendesha Uchunguzi Maalum *(inquiry Privatisation Policy in Tanzania)* kwa kushirikiana na Shirika Hodhi la yaliyokuwa Mashirika ya Umma *(CHC)* kushirikiana kwa ajili ya uchunguzi huu. Tunataka hii *public inquiry* iwe wazi na taarifa yake ijadiliwe Bungeni na tuweze kuona ni namna gani ambavyo tutakavyofanya kwa mashirika ambayo yamebakia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa changamoto zinazolikabili Taifa katika Sekta ya Mafuta na gesi ni kubwa na hivyo kuhitaji mkakati wa makusudi wa muda mrefu wa

kukabiliana nazo, na kwa kuwa Mashirika ya Umma ikiwa ni pamoja na Shirika la Maendeleo ya Petroli *(TPDC)* ndiyo wadau wakubwa wa kuhakikisha nchi inanufaika ipasavyo na Sekta ya Gesi na Mafuta, na kwa kuwa Makampuni yanayotafuta mafuta na gesi hapa nchini yamekuwa yakipeleka fedha *TPDC* ili ziweze kutoa mafunzo kwa watumishi ili kuongeza uelewa katika Sekta hiyo.

Kwa hiyo, Kamati inapendekeza kuwa, kuanzishwe Mfuko Maalum *(Trust Fund)* ili fedha zote za mafunzo ziwekwe humo ili kupanua wigo kwa Watanzania wote ambao wangependa kusomea fani za gesi na kutumika kwa watumishi wachache wa *TPDC* na Wizara ya Nishati na Madini na muda mwingine kutumika kwa shughuli zisizo za mafunzo kama ilivyobainishwa na Kamati ya Nishati na Madini. Lengo ni kujenga uwezo zaidi wa nchi yetu tunapoelekea kuwa mzalishaji mkubwa wa gesi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Shirika la ugavi wa Umeme Tanzania *(TANESCO)* linakabiliwa na hali mbaya ya kifedha unaotokana na gharama kubwa ya kununua umeme kutoka kwenye makampuni binafsi (kwa mfano *IPTL* pekee wanalipwa Shilingi bilioni 64.2 kwa mwaka), na kwa kuwa gharama za ununuzi wa umeme ndiyo zinasababisha *TANESCO* iendelee kupata hasara kila mwaka (kwa mfano hasara ya Shilingi bilioni 47.3 kwa mwaka 2009/2010) na hata kuongeza gharama za umeme kwa wananchi, Kamati inapendekeza kuwa, katika muda mfupi baada ya mtambo wa *TANESCO* wa *(Jacobsen)* kuanza kazi waachane na kununua umeme wa gharama kubwa kama ule wa *IPTL*, na katika muda mrefu Kamati inasisitiza kufanyike uwekezaji wa kutosha katika kuzalisha umeme.

Miradi ya Umeme inayopendekezwa kufanywa na Mashirika ya Umeme ipewe kipaumbele sana ili kuwepo na mchanganyiko sawia *(right balance)* kati ya uwekezaji binafsi na ule wa Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa Taarifa za uchunguzi kuhusiana na Shirika la Viwango Tanzania *(TBS)* uliofanywa na Kamati Ndogo ya *POAC* ulikamilika na taarifa kuwasilishwa kwako, na kwa kuwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pia amekamilisha uchunguzi kuhusiana na *TBS* na utekelezaji wa majukumu yake kisheria, Kamati inapendekeza sasa Serikali ilete taarifa ya utekelezaji na majibu ya hoja za taarifa hizo mbili ili Bunge liweze kupata nafasi ya kuzijadili kwa kina na vile vile kuweza kuazimia hatua ambazo zinapaswa kuchukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa ya Kamati imeeleza kwa kina namna Kamati ilivyotekeleza majukumu ya msingi na mfanikio iliyopata katika utekelezaji wa majukumu yake. Napenda kutoa shukurani zangu za dhati kwa watu wote ambao walihusika na utayarishaji wa taarifa hii, kwanza wewe binafsi na Spika na Katibu wa Bunge na Maafisa wa Bunge ambao walihusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia naomba nichukue fursa hii kwa heshima na taadhima kuwatambua Wajumbe wa Kamati yangu, Wajumbe mahiri kabisa, wachapakazi hodari na wazalendo ambao wanafanya kazi ya ziada kuhakikisha kwamba mashirika ya umma yanasimamiwa vizuri. Wajumbe hao ni Mheshimiwa Deo Haule Filikunjombe - Makamu Mwenyekiti, Wajumbe ni Mheshimiwa Felister A. Bura, Mheshimiwa Juma A. Njwayo, Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola, Mheshimiwa Daktari Pudensiana Kikwembe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ile Kamati Ndogo ambayo niliitangaza kuhusiana na uchunguzi wa fedha za mikopo ya wanafunzi Wajumbe wake ni Mheshimiwa Daktari Pudenciana W. Kikwembe, Mheshimiwa Zainab R. Kawawa na Mheshimiwa Alphaxard K. N. Lugola. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Wajumbe wengine ni Mheshimiwa Muhammad Amour Chomboh, Mheshimiwa Aliko

N. Kibona, Mheshimiwa Amina Mohamed Mwidau, Mheshimiwa Jerome D. Bwanausi, Mheshimiwa Ali Kheir Khamis, Mheshimiwa Esther N. Matiko, Mheshimiwa Zainab R. Kawawa, Mheshimiwa Christowaja G. Mtinda, Mheshimiwa Murtaza A. Mangungu na Mheshimiwa Ester A. Bulaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kumshukuru Katibu wa Bunge kwa ushauri wake na *support* yake. Napenda kumshukuru sana Katibu wetu wa Kamati Ndugu Erick Maseke na Msaidizi wake Bibi Halima Laizer na Waandishi wa Taarifa Rasmi za Bunge Ndugu Silvanus Chindandi na Bibi Anne Mng'ong'ose kwa kazi nzuri sana ambayo wanatusaidia katika Kamati yetu. Taarifa hii isingeweza kuwepo hapa bila msaada mkubwa sana vijana wetu hawa ambao wanafanya kazi nzuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutumia fursa hii kuishukuru Benki ya Dunia kupitia Mradi wa Urekebishaji wa Usimamizi wa Fedha za Umma *Public Finance Management Reform Programme* kwa kifupi *(PFMRP)* kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza ziara mbalimbali za kukagua na kutathimini ufanisi wa Mashirika ya Umma inayotekelezwa na kuratibiwa na Ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

Kwa mara nyingine tena napenda kuwashukuru watalaam kutoka ofisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwenyewe Ndugu Ludovick Uttoh *(CAG)* kwa kazi nzuri sana ambayo wanaifanya, Ofisi ya Msajili ya Hazina *(TR)* na Maafisa kutoka Shirika Hodhi linaloshughulikia madeni na mali ya yaliyokuwa Mashirika ya Umma *Consolidated Holdings (CHC)* kwa ushirikiano mkubwa waliotuonesha katika kuhakikisha Kamati hii inatekeleza wajibu wake ipasavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza kwa umakini sana japo kwa masikitiko kutokana na ubadhirifu ambao umeonekana katika

Kamati hii, lakini naamini kabisa sote kwa pamoja tunaweza kufanya kazi ili kuweza kuhakikisha kwamba tunayarekebisha mashirika yetu na tunajenga nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja.*(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Zitto Kabwe - Mwenyekiti wa Kamati ya Mashirika ya Umma kwa taarifa ya Kamati.

Waheshimiwa Wabunge, sasa tumepokea taarifa zote tatu, lakini kwa kweli kwa masikitiko makubwa Wabunge hamjapata nakala ya taarifa hizi mpaka sasa. Kila niliyemtuma kufuatilia hakuweza kurudi kuniletea jibu. Kwa hiyo, nami nipo kama ninyi, sina majibu. Lakini niwahakikishie *by* saa 1.00 tutakaporudi hapa tutakuwa na nakala mkononi. Nitawaomba tu wale ambao mtakuwa mnachangia kwa wakati huo, basi mjipange kwa kuzipitia kwa haraka iwezekanavyo. Nitahakikisha zinapatikana katika muda siyo mrefu mara tu baada ya kuahirisha shughuli hizi. Kwa sababu zipo na zilikwishachapishwa na zinapatikana. Kwanini haziingii hapa ndani? Ndiyo swali ambalo kwa kweli linasikitisha.

**KUHUSU TAARIFA**

**MHE. MURTAZA A. MANGUNGU:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nikupe taarifa kwamba nakala hizi zipo kwenye *pegion hall,* mimi binafsi nimezikuta, ninazo zote tatu na nimezikuta kwenye *pegion*.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Tuta-*sort out* hii *confusion.* Kuna madai kwamba baadhi ya Wajumbe wa Kamati ndiyo waliowekewa kwenye *pegion hall.* Kuna baadhi wanasema ziliwekwa jana kwa Wabunge wote; maneno ni mengi sana,

lakini nawahakikishia tutakutana ofisini tuta-*sort out* hii *problem* na saa 11.00 kila mmoja atakuwa na nakala kwa jambo hili ili mjadala huu uweze kuwa wa maana. Tunaomba Katibu kosa hili lisitokee tena. Ikiwekwa Mezani leo kesho yake inagawiwa humu Ukumbini, siyo siku moja kabla. Hapana.

Waheshimiwa Wabunge, baada ya maelezo hayo, niseme kwamba kulitokea taarifa asubuhi kwamba Mbunge mwenzetu, Waziri wa Ujenzi - Mheshimiwa John Magufuli alipata homa ghafla akapelekwa hospitali ya Mkoa wa Dodoma akawa amelazwa, ni kweli. Bahati nzuri Waziri Mkuu alipata nafasi ya kukimbia mara moja na kuona hali yake, walipompima pale wakaona *pressure* iko juu, lakini kwa sasa tunavyoongea *pressure* imeshuka ila bado ana tatizo kidogo la kichomi upande wa kushoto. Tunamtakia vile vile aendelee kupata matibabu mema na ahueni haraka.

Waheshimiwa Wabunge, waliojiandikisha hapa wanakaribia 70 kuchangia katika Kamati hizi tatu. Kwa hiyo, tutakapoanza saa 11.00 jioni tutaanza moja kwa moja na wachangiaji kadri ambavyo orodha yetu itakuwa imebandikwa ukutani. Kwa hiyo, nitaomba tuwahi ili shughuli yetu ya uchangiaji ikianza tuwe pamoja. Kwa hatua hiyo, naomba sasa kusitisha shughuli za Bunge hadi leo saa 11.00 jioni.

*(Saa 6.54 Bunge lilifungwa Mpaka Saa 11.00 jioni)*

*(Saa 11.00 jioni Bunge lilirudia)*

*Naibu Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alikalia Kiti*

**NAIBU SPIKA:** Sasa tunaanza na uchangiaji na kwa kweli kwa sababu orodha yetu ni ndefu niwaambie kabisa Waheshimiwa Wabunge kwamba kama mtu hatakuwepo, itakuwa ni vigumu sana kumrudia. Kwa hiyo, ni vizuri kuwa

makini. Mchangiaji wetu wa kwanza ni Mheshimiwa Luhaga Mpina.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nataka tu kupata mwongozo wako. Ukiangalia hizi ripoti tatu zilizoletwa leo ni muhimu sana kwa maendeleo ya nchi yetu. Muda tulionao ni kidogo sana ili kuweza kupata nafasi watu wote kuchangia. Nikasema hivi isingekuwa tuone uwezekano wa kupunguza muda ili tuweze kupata watu wengi zaidi waweze kuchangia?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, wazo ni zuri. Nina wachangiaji 64, mimi binafsi peke yangu siwezi kuliamulia. Labda niwahoji dakika ngapi mnadhani inafaa?

**WABUNGE:** Dakika 10.

**NAIBU SPIKA:** Dakika 10, mtaweza kuchangia kwa dakika 10. Ngoja Makatibu wangu wanishauri hapa kwa haraka haraka. Sasa tufanye hivi Mheshimiwa Luhaga Mpina yeye atafaidika na zile dakika 15 aanze wakati tukiangalia utaratibu mwingine. Mheshimiwa Mpina endelea.

**MHE. LUHAGA J. MPINA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mada hii. Alichokizungumza Mheshimiwa Serukamba ni kile ambacho nilikiombea mwongozo juzi kwamba Bunge halichunguzi kwa makini na kujadili ripoti zinazotoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Hii inatokana na kwamba Kamati ya Uongozi mnatupangia muda mfupi sana wa kujadili taarifa hizi muhimu huku mkijua umuhimu wake. Bahati mbaya sana katika Kamati ya Uongozi hata wale Wenyeviti wa Kamati husika kwa maana ya Mwenyekiti wa Kamati ya *POAC*, Mwenyekiti wa *PAC* pamoja na Mwenyekiti wa *LAAC* wamo kwenye Kamati ya Uongozi, lakini wanakubali Kamati hizi

kujadiliwa kwa masaa kitu ambacho siyo haki kulitendea Bunge hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Kanuni ya 94 mpaka 107 kanuni katika namna ya utungaji wa Sheria za Fedha Kanuni hizi zimesema dhahiri kwamba utaratibu wa kujadili hotuba ya Bajeti ya Serikali itakuwa ni muda usiozidi siku tano. Lakini kujadili bajeti za Wizara imesema bayana kwamba ni muda usiozidi siku 50 lakini ilipofika kwenye kupokea, sasa ule utekelezaji wa bajeti yenyewe kanuni hizi zimekaa kimya. Hapo ndiyo udhaifu ulipoanza kwa sababu leo hii Taarifa ya *CAG*, Taarifa ya Kamati muhimu ya Hesabu ya Mashirika ya Umma, Taarifa ya Hesabu za Serikali, Taarifa ya Hesabu za Serikali za Mitaa mpaka ipangiwe muda na Kamati ya Uongozi kwa jinsi wao wanavyoona inafaa. Huu muda siyo wa kuamini hivyo tena.

Mheshimiwa Naibu Spika, napendekeza kwamba sasa tuwe na utaratibu maalum kanuni zetu tuzifanyie marekebisho ili ziruhusu Taarifa ya *CAG*, Taarifa ya Kamati ya *PAC*, Taarifa ya *LAAC* zipewe muda wa kutosha kujadiliwa hapa Bungeni, ikiwezekana tuwe na Bunge Maalum la wiki mbili la kujadili taarifa hizi tu na mapendekezo yake. Hapo ndipo tutakapofikia pazuri kuliko hivi tunavyofanya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haina mantiki Bunge lako linakaa siku 55 hapa kujadili bajeti, fedha za Watanzania tunazipeleka kule, zinakwenda kutumika halafu tunakuja hapa hatuna muda tena wa kupitia uhalali wa matumizi haya. Hiyo siyo haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende kwenye suala zima la mapendekezo yenyewe sasa ya Kamati, pendekezo la Kamati ya *LAAC* pendekezo namba 3.1.4 ya Kamati ya *LAAC* ambalo linasema pamoja na pendekezo hilo kuitaka Serikali kutoa maelezo ya kuridhia kwa nini iliacha ubadhirifu ukashamiri kwa miaka mitatu bila wahusika kuchukuliwa hatua?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwenye taarifa za *CAG* ya mwaka 2009/2010 na taarifa ya mwaka 2010/2011, Halmashauri inayozungumzwa ya Kishapu zimetumika fedha vibaya jumla ya Shilingi bilioni 5.5 na bado inaelezwa kwamba kuna mishahara hewa iliyolipwa zaidi ya Shilingi bilioni 583 na taarifa ya mwaka huu pia inaonyesha zaidi ya Shilingi milioni 200 na kitu zimetumika kulipa watumishi hewa.

Fedha nyingi za Halmashauri ukipitia zile taarifa za Mkaguzi zimepotea, watu wanafanya malipo bila vielelezo, taratibu za matumizi zinakiukwa, malipo hewa, mradi hewa, watu wanalipwa mamilioni ya fedha, ushahidi umeorodheshwa miaka mitano, nimesoma miaka mitano ya taarifa za *CAG* zikionyesha wizi mkubwa unaofanywa na watendaji kule kwenye Halmashauri; Halmashauri ya Meatu baada ya kuona uchunguzi wa Kamati Ndogo ya Julai - Desemba mwaka 2010 ilibainika mamilioni ya fedha yamepotea. Taarifa hizi zililetwa kwa Waziri mhusika wa TAMISEMI lakini mpaka leo ninavyozungumza mwaka mmoja umepita hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa.

Sasa kutokana na hali hii na tabia hii sasa ambayo imekithiri kwa watendaji wa Serikali kutokuchukua hatua na kwa nini hawachukui hatua? Hawachukui hatua kwa sababu wale wabadhilifu wa fedha za umma wanashirikiana nao. Hawachukui hatua kwa sababu ya kulindana kwa misingi ya undugu. Hawachukui hatua kwa sababu ya kuogopa baadhi ya mafisadi ambao wanaogopa kuwa-*attack*. *(Makofi)*

Sasa kama hali ndiyo iko hivyo, haiwezekani Bunge lako Tukufu tunakaa hapa kujadili fedha za Watanzania, tumeziidhinisha, zinakwenda kule kuliwa tu halafu watu tuliowapa mamlaka hawachukui hatua. *(Makofi)*

Mimi nasema na ninaongeza katika pendekezo hilo la kuchukua hatua hizo zilizopendekezwa na Kamati katika hilo pendekezo namba 3.1.4. naliomba Bunge lako Tukufu liridhie

kwamba imfungulie mashtaka Waziri anayehusika na TAMISEMI na imuunganishe na hawa wabadhirifu wa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, siyo hali ya kawaida mabilioni ya Watanzania yanatafunwa halafu tunakuja hapa tunasema maneno watu hawachukui hatua. Pia tulete sasa mapendekezo mengine kwamba tuweke fedha, tufanye mabadiliko makubwa katika sheria yetu ya fedha tuweke sheria nyingine, tuongeze kifungu kingine ambacho kitawachukulia hatua kali Watendaji wa Serikali na mamlaka zinazohusika ambao wanatakiwa kuchukua hatua kwa Watendaji walioko chini yao hawachukui hatua, tuwabebeshe mzigo huo wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la Kamati ya *POAC* la 7.2.2 ambalo linasema kwamba ufanyike uchunguzi maalum ili kubaini endapo fedha za kufidia anguko la bei ya pamba kama zilifidiwa kwa walengwa, Taarifa ya *CAG* inasema wazi kwamba Sh. 2,474,348,080/= hazikuthibitishwa malipo yake. Taarifa hii ni ya mwaka 2009/2010. Sasa leo ni miaka miwili imepita Serikali au Wizara husika, au Watendaji husika au Bodi husika bado imeshindwa kuthibitisha matumizi haya kama ni kweli yalifanyika kwa watu waliokuwa wanadai. Lakini hapa nilipo ninayo malalamiko ya makampuni ambayo yalifanya malipo ya Shilingi 80 kama nyongeza kwa wakulima ambayo ni zaidi ya Shilingi bilioni 6.3 yanadai haya makampuni mpaka leo hayajalipwa fedha hizo.

Kama nilivyozungumza kwamba yapo makampuni kama *NGS Investment Company Limited* na wenzake wanadai Shilingi bilioni 6.3. kutoka Bodi ya Pamba ikaguliwe, inadaiwa Shilingi bilioni 2.4 kwamba imeshindwa kuthibitisha uhalali wa malipo yake, mpaka leo haijathibitisha hilo na Kamati inaendelea kulalamika, na Kamati ya *POAC* siyo mara yake ya kwanza kuendelea kulalamikia suala hili. Mimi sikubaliani na pendekezo ambalo limetolewa na Kamati ya Mashirika

walilolitoa wakisema kwamba uchunguzi maalum ufanyike ili kubaini. Miaka miwili bado tunazungumza uchunguzi maalum ufanyike! Mimi naomba tufanye mabadiliko hapa, tuseme tuwaagize sasa wale waliohusika kufuja hizo fedha za umma wakamatwe, washitakiwe na wafilisiwe kufidia mali ya wananchi hawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini bado Serikali ifidie hizo fedha za Makampuni halali yaliyofanya kazi halali ya kuongeza hawa wakulima kuwanusuru kwa kuwaongezea bei yao ya pamba. Hilo lifanyike mara moja kwa sababu walifanya kwa nia njema.

Serikali ilisema ongezeni shilingi 80, sisi kama Serikali tutafidia. Matokeo yake, wajanja wachache wamezifuja fedha hizo. Kosa ni la nani? Makampuni yale yafidiwe, wale akina *NGS Investment Company Limited* wafidiwe fedha zao. Lakini kwa sababu hawa watumishi waliosababisha hasara hii tunao na wapo na wanapatikana, fedha hizi wazilipe na wachukuliwe hatua nyingine za kisheria. Lakini kikubwa wafilisiwe kufidia mali ya Watanzania walioifuja.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anaendelea kuwa hana uhuru pamoja na kuja na sheria ya *The Public Audit Act, 2008* na marekebisho yaliyofanywa na Sheria Na. 5 na Na. 15 ya mwaka 2010, bado mkaguzi wetu hajawa na mamlaka halali ya kuweza kufanya kazi zake sawa sawa. Kwa nini nasema hajawa na mamlaka halali ya kufanya kazi? Bado kifungu cha Sheria ya Fedha ya mwaka 2001, kifungu cha 23, bado Wizara zote zinataka kwamba ifikapo tarehe 30 Juni, fedha zote ambazo bado hazijatumika zinatakiwa ziende Hazina. Lakini sheria hiyo bado haijazingatia umuhimu wa Ofisi Nyingine kama *CAG*.

Kitendo cha *CAG* kuondolewa fedha ifikapo tarehe 30 Juni, kunakwamisha mpango kazi mzima wa shughuli za ukaguzi na hivyo kumkwaza kutokuendelea na ukaguzi.

Ukaguzi mwingine unachelewa, lakini licha ya kuchelewa, kaguzi nyingine hazifanyiki kabisa kwa sababu ya fedha hizo zinapokuwa zimerudishwa. Bado sheria haijazingatia kwamba unaporudisha fedha zile: Je, fedha hizi ulizileta muda gani? Fedha zinaletwa mwezi wa Nne, wa Tano halafu tarehe 30 Juni, unasema zirudishwe. Huu siyo utaratibu mzuri. Ni vizuri tukazipitia sheria zetu vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Sheria zetu kama nilivyozungumza katika kifungu hicho kinachohusu kurudisha fedha za umma muda unapokuwa umefika, lakini kingine ni kwamba kitendo cha *CAG* kulazimika kwamba taarifa zake za fedha anapomaliza ukaguzi wake lazima uchunguzi uende kwa Mkurugunzi wa Mashitaka. *CAG* ni *independent,* tuna-*clear* kwamba ni *independent.* Lakini Mkurugenzi wa Mashitaka siyo *independent,* tumfanye Mkurugenzi wa Mashitaka wa Nchi hii pia awe *independent* kama ilivyo nchi nyingine ili kwamba inapotoka kwa Mkaguzi Mkuu wa Serikali, basi kusiwepo na ile kuoneana haya. Inapokwenda kwa Mkurugenzi Mkuu wa Mashitaka, ambayo yeye bado hayuko *independent,* yuko chini ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, wakati mwingine anashindwa kuchukua hatua stahili zinazotakiwa kwa ajili ya wafujaji wa fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ni suala zima la viongozi wetu. Tumesema muda mrefu na Serikali imekuwa ikiahidi malipo ya viongozi walioko chini, Waheshimiwa Madiwani, Waheshimiwa Wenyeviti wa Vijiji, Serikali imekuwa ikitoa ahadi za mara kwa mara kwamba itarekebisha malipo ya viongozi hawa. Kwa masikitiko makubwa katika bajeti iliyopita tuliahidiwa kwamba viongozi hawa wangeweza kurekebishiwa malipo yao ifikapo Desemba ya mwaka huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa tunavyozungumza, Wenyeviti wa Vijiji, Waheshimiwa Madiwani bado hawajarekebishiwa posho zao, bado hawajaanza kulipwa posho zao kulingana na kazi wanazofanya. Tuliongea kwa

uchungu kuwa viongozi hawa ndiyo hawa wanaokwenda kusimamia hii miradi ya maendeleo, ndio hao wanaokwenda kusimamia fedha tunazoziidhinisha kila siku kwenda katika Halmashauri. Lakini malipo yao yameendelea kuwa madogo.

Mheshimiwa Diwani kumlipa Sh. 120,000/=, yaani Sh. 4,000/= kwa siku hata mwanafunzi anayesoma shule leo chuoni analipwa Sh. 7,500/= kwa siku. Hili haliwezi likandelea kukubalika. Madiwani wetu walipwe stahili zao zinazotakiwa kulipwa ili waweze angalau kumudu maisha yao. Huwezi ukampa mtu jukumu kubwa la kusimamia fedha zote zile halafu usimpe nguvu ya kufanya kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nimetoka familia ya wachungaji. Mchungaji cha kwanza anatakiwa apewe chakula cha kutosha ili aweze kuwalinda wale mifugo na kuwachunga salama na kuwarudisha salama. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Luhaga Mpina tunakushukuru sana kwa kutuanzishia mjadala. Sasa narudi kwenye mwongozo ambao ulikuwa umeulizwa na Mheshimiwa Peter Serukamba na mimi nautolewa ufafanuzi ufuatao kwa kutumia kanuni ya 150 ambayo inasomeka kama ifuatavyo:-

Kwa idhini ya Spika, kanuni yoyote inaweza kutenguliwa kwa madhumuni mahsusi baada ya Waziri, Mwanasheria Mkuu wa Serikali au Mbunge yeyote kutoa hoja kwa ajili hiyo.

Hoja ya kutengua Kanuni za Bunge haitahitaji kutolewa taarifa. Kwa mamlaka hayo basi, na kwa busara ya uendeshaji bora ili kutoa nafasi kwa Waheshimiwa Wabunge zaidi kuchangia hoja hii ambayo mngependa kuizungumzia, naamua kwamba muda wa kuchangia utakuwa dakika 10, utazungumza baada ya dakika saba kengele ya kwanza itapigwa na baadaye dakika tatu mwishoni itapigwa ya kumalizia dakika 10.

Kwa hiyo, naomba kila mmoja ajitahidi kwenda kwenye mada moja kwa moja bila kupoteza muda. Naomba nimwite Mheshimiwa Michael Lekule Laizer, tunaanza zile dakika zetu 10.

**MHE. MICHAEL L. LAIZER:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia taarifa ya Kamati zote tatu. Kwanza, nampongeza *CAG* pamoja na watu wa Ofisi yake. Nawapongeza Wenyeviti wote watatu kwa taarifa nzuri walizotusomea leo asubuhi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, mimi naona suala hili ni kubwa na ni zito. Nadhani ni zito hata zaidi ya kupitisha bajeti. Kwa sababu bajeti tunapopitisha ni fedha ambazo tunakisia tunadhani kwamba zitakusanywa. Hizi tunazozizungumzia leo ni fedha zimekusanywa zikaliwa siyo fedha ambazo zimekwishakusanywa tayari zimeliwa kwa njia nyingi. Kinachonisikitisha ni taarifa za kila mwaka, Wenyeviti wanatoa taarifa, *CAG* analeta taarifa, ni upotevu wa fedha, ni malipo hewa, ni manunuzi ambayo hayako, ni wizi kila na Serikali inakaa kimya.

Kama mnaona taarifa hizi kwamba ni za uongo, kwa nini msilete taarifa yenu ya kukanusha kwamba hakuna mishahara hewa? Hakuna mambo ya ununuzi, Serikali inakaa kimya na fedha za wananchi zinaliwa kila siku hakuna miradi inayoendelea kijijini, hakuna fedha zinazokwenda Halmashauri, halafu tunakaa kila siku kuwaimbia Serikali wanakuwa kama wameweka nta kwenye masikio hawasikii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, leo mimi ningetegemea kwamba Waziri wa Fedha angekuwepo hapa kwa sababu hizi fedha tunazozungumzia zimetoka ofisini kwake. Lakini anaona kwamba ni kitu cha kawaida, tumezoea. Hivi Wabunge tunakuja hapa kufanya nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama shughuli yetu ni kuisimamia Serikali na wameboronga, wamekula fedha za

wananchi, tunafanya nini? Kama ni kukataa kupitisha bajeti ndiyo kazi yetu, kama tunaweza kukataa kupitisha bajeti ya fedha ambazo tunakadiriwa kwamba zitakusanywa na hizi zote zilizoliwa tunakaa kuwaambia Serikali hawasikii, mimi ningeomba Wabunge wenzangu, hizi taarifa tungekataa mpaka utekelezaji wake ufanyike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tuambiwe fedha zote za malipo hewa zinakwenda wapi. Hivi malipo hewa si kuna mtu anayetoa? Kwa nini wananyamaza? Miradi ambayo ipo chini ya kiwango, inajulikana, mali za Serikali zinauzwa, Halmashauri ya Longido gari imeuzwa ambayo Afisa amepeleka gari *garage*, imetengenezwa kwa milioni 11 ameweka tairi mpya, kabla Halmashauri haijalipa hizo fedha, barua ikaja kwamba huyu Afisa amenunua hiyo gari kwa shilingi 1,490,000/=, halafu Halmashauri inadaiwa shilingi milioni 11 kwa gari hilo, eti kibali kimetoka Wizara ya Fedha kwamba huyo Afisa ameuziwa hiyo gari. Halafu bado Halmashauri ilipe gari ambayo yeye ndiyo amejitengenezea na kujiuzia.

Mheshimiwa Naibu Spika, wizi kama huo na Serikali wanajua, nimewaeleza, Halmashauri tumeisimamisha hiyo gari na tumeichukua ni mali ya Halmashauri aende kutushitaki. *(Makofi)*

Ndugu zangu, hapa tunacheza, kuna Wabunge wenzangu ambao wapya sidhani kama fedha zimewahi kwenda kwenye Halmashauri zao tangu waingie hapa Bungeni, hakuna kazi za miradi ya maendeleo inayoendelea. Kwa hiyo, mimi naona Serikali sijui niseme nini, sijui Serikali wamechoka au wanafanya makusudi kwa sababu naumia, miradi ya maendeleo isipoenda na fedha zinakusanywa, tunaona majumba yanaendelea kujengwa na hao maafisa na ninyi mnaona.

Kwa hiyo, fedha za wananchi zinavyokwenda tunaziona, mnaona katika Halmashauri zenu majengo yanaendelea,

nyumba za watumishi zinajengwa zao wenyewe, wananunua magari, ni matajiri, lakini Serikali inakaa kimya.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu ukaguzi, Waziri Mkuu ametuma tume, nilifurahi sana nilipoona tume imetumwa na Waziri Mkuu imekwenda kuangalia miradi na imethibitisha kwamba miradi ni mibovu, wamekuja wameleta hiyo taarifa, hiyo taarifa haikufanyiwa kazi na Halmashauri walifurahi kweli kwamba Serikali leo imeamka, lakini hiyo taarifa imezimwa. Kwa hiyo, nasema hapa sijui Wabunge wenzangu mtaongea nini kwa sababu kila Mbunge akisimama hapa ni kilio. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nazungumza kwa uchungu kwa fedha za wananchi ambazo zinaliwa na sio kwamba hazionekani, inajulikana kabisa. Mbona Serikali inapotaka kupitisha *budget review* wanaleta hapa? Hizi fedha zote zinazokosekana ambazo haziendi kwa Halmashauri, Halmashauri imepangiwa fedha, lakini hazikwenda, kwa nini wasilete taarifa kwamba hizo fedha hazikupatikana kwa ajili hii na hii na hii? Nakumbuka Halmashauri ya Longido tulipangiwa au tuliomba bajeti ya shilingi bilioni 11 na ni bilioni nne tu pamoja na mishahara. Hiyo bilioni nne ni pamoja na mishahara, hakuna fedha za maendeleo.

Kwa hiyo, ndugu zangu hapa tunazungumza na Serikali, tunawauliza Serikali, lakini nasikitika kwamba hawakuona umuhimu, hawakuona kwamba jambo hili ni muhimu. Kwa sababu Waziri wa Fedha angekuwepo ili atujibu haya yote, hizi fedha zimetoka Hazina. Tunazungumza kila siku, tunaondoka hapa hakuna kinachofanyika. Hatupati *feedback* ya nini tulichoiambia Serikali. Leo watuambie kwa hili wasinyamaze kama miaka mingine, watujibu. Kwa nini mnalipa mishahara hewa mpaka leo?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, huu muda kwanza ni mfupi, ingekuwa ni heri kuongeza siku tuzungumze, tuiambie

Serikali kuliko kumpunguzia Mbunge muda. Nakushukuru kwa nafasi uliyonipa. *(Makofi)*

**MHE. ALPHAXARD K. N. LUGOLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

Kwanza nashukuru Wenyeviti wa Kamati zote tatu za mahesabu kwa ripoti nzuri walizozitoa na labda niseme tu mambo ambayo napenda kuyaongea jioni ya leo ni mambo mazito yakihusu Wizara ya Fedha, lakini kwa bahati mbaya na kwa kusikitika Waziri muhusika hayupo, lakini Naibu wake yupo, nadhani atafikisha ujumbe au kwenye *Hansard.(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ripoti ya Mahesabu ya Mashirika ya Umma kuna kipengele ambacho ningependa nianze nacho kinachozungumzia tatizo sugu katika nchi hii la Wizara ama Serikali kuyaingilia Mashirika ya Umma katika shughuli za kiutendaji na katika kuyaingilia, wanayaingilia katika maslahi binafsi na sio katika maslahi ya Taifa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoa mifano mingi humu, Wizara ya Nishati na Madini wanavyoingilia *TPDC* na tumependekeza wawaache wawe huru ili wafanye shughuli zao. Wizara ya Fedha imekuwa ikiingilia kwa kiasi kikubwa Mashirika ya Umma, hususani Shirika Hodhi la Mashirika ya Umma yaani *CHC. (Makofi)*

Napenda Wabunge wenzangu mnielewe, napenda Serikali yangu inielewe, mimi ni Mbunge wa CCM, mimi ni Mjumbe wa Kamati ya Kudumu ya Hesabu ya Mashirika ya Umma, nina fursa kubwa ya kuchungulia ndani ya Mashirika ya Umma katika hesabu, nina fursa ya kuangalia ubinafsishaji unavyokwenda, ndugu zangu Wabunge naomba mnielewe ili msikilize jinsi Wizara ya Fedha inavyotafuna nchi hii kwenye Mashirika ya Umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Waziri, katika ripoti hii ya *CAG,* imeonyesha namna gani Wizara ya Fedha na hususan Waziri mwenyewe Mheshimiwa Mkulo alivyoweza kuingilia Shirika la *CHC* katika uuzaji wa mali za Serikali. Kwanza tuna *plot* namba 10 pale *Nyerere road,* Waziri Mkulo, yeye mwenyewe aliamua kwa kuishinikiza *CHC* wauze *plot* hiyo kwa *Mohamed Enterprises Company Limited* kitendo hiki kikamfanya *DG* wa *CHC* kutokubaliana na Mheshimiwa Mkulo, lakini la pili tulikuwa na Shirika la Umma linaitwa *Tanzania Motor Service Company* kwa ajili ya uagizaji wa magari, walikuwa na mali na majengo pale *Ali Hassan Mwinyi road plot* namba 24, lakini *CHC* walipoamua kuuza jengo lile kwa Murad Sadick kwa shilingi bilioni 1.3 akalipa *deposit* ya asilimia 10 kwa *CHC* baadae cha kushangaza *DG* wa *CHC* akapata barua ikimuagiza asitishe mara moja kuliuza jengo hilo kwa Murad Sadick, lakini baadaye nini kilitokea; ni kuandikiwa barua kwamba waanzishe mazungumzo na Murad Sadick ya kutoendelea kuuza jengo hilo na hapo Murad Sadick alisema amepata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waziri Mkulo akawaambia wafanye mazungumzo, mazungumzo yaliendaje? Mazungumzo Mwenyekiti alikuwa ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Fedha Ndugu Ramadhan Khijjah ndiye aliyefanya mazungumzo wakubaliane kwamba badala ya kununua lile jengo, sasa wamkubalie kumlipa milioni 964 na sio bilioni 3.9 ambazo Murad alikuwa anataka.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nini kilitokea? Na nchi hii ujue inavyotafunwa. Katibu wa Wizara aliidhinisha kwamba malipo haya yafanyike haraka iwezekanavyo na Wizara yenyewe ndiyo ilifanya malipo hayo na sio *CHC* na wakati ule tulikuwa tunaenda kwenye uchaguzi. Ni lini Wizara imehusika katika kuuza mali ambapo kuna Shirika ambalo linahusika na kuuza mali? *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakumbushe ni Waziri Mkulo aliyeleta Azimio la Bunge kwa kuifuta *CHC* ili kazi zake zifanywe na Msajili wa Hazina. Niliwatahadharisha kwamba wanaifuta *CHC* kwa sababu wanataka kuficha madhambi haya, leo tumeona ubadhirifu unafanywa na Wizara ya Fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hakuishia hapo, alipoona Wabunge mmekataa *CHC* isifutwe, alienda kule akamsimamisha kazi Mtendaji Mkuu wa *CHC,* alienda kule akavunja Bodi ya *CHC* ambayo ilihoji kwa nini amekuwa akishinikiza mambo ambapo Bodi haikuhusishwa na hakuishia hapo, alirudi Bungeni hapa akasema wale wanaochangia kwamba *CHC* isifutwe wamehongwa ili waitetee *CHC. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, alikuwa ni Mwenyekiti Mheshimiwa Kabwe Zitto, napenda niwarejeshe Waheshimiwa Wabunge, aliamua kuweka rehani Ubunge wake endapo Waziri Mkulo atathibitisha kwamba amehongwa au Kamati ya Mashirika ya Umma tumehongwa na alimuomba na yeye aweke rehani Uwaziri wake, lakini kwa sababu alijua alitaka kuiogopesha Kamati ya Mashirika ya Umma ndiyo sababu leo ninamtaka Waziri Mkulo ama afute kauli yake ya kwamba tulikuwa tumehongwa na aweze kumsafisha Mwenyekiti Mheshimiwa Kabwe Zitto. *(Makofi)*

Mheshismiwa Naibu Spika, Wizara ya Fedha inaangamiza nchi. Ninaomba Wizara hii Waheshimiwa Wabunge tuitazame vizuri, tusipoitazama vizuri nchi hii itaangamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niende *TBS* nigusie kidogo. Hivi *TBS* hawa bado mnasubiri nini? Watanzania wanakufa, matairi yasiyo na viwango yanauwa Watanzania, mbolea zisizo na viwango zinauwa Watanzania, mafuta ya ndege yasiyo ya viwango yanauwa Watanzania, nina wasiwasi hata ndege ambayo haikuruka Kigoma inawezekana ilikuwa na tatizo la mafuta ya kuchakachuliwa.

Pale Moshi pale, Mheshimiwa Rais gari lake liliuziwa mafuta ya kuchakachuliwa na leo tunatumia mafuta ya ndege ambayo yako mtaani yamechakachuliwa. Nakuomba Mungu uepushe ndege ya Rais isiweze kuwa na mafuta haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulikwenda kule Hong Kong hakuna cha makampuni, tulienda Hong Kong tumepelekwa ofisi ambazo sio za kweli na mwenyewe Charles Ekelege akajibu kwamba ametudanganya, tukaenda Singapore hapakuwa na ofisi, nilikasirika kutokana na kudhalilishwa nikijua Mwibara hakuna madawati, hakuna walimu, nyumba za walimu hakuna, lakini tunachezea fedha za Watanzania kwenda kuangalia makampuni ambayo hayapo. Nilidhalilika na nilitamani kumpiga ngumi lakini kwa sababu nimeokoka sikuweza kufanya hivyo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huyu Ekelege analindwa, Bonny Mwaitege ambae ni mwimbaji wa injili aliwahi kusema ukitaka kujua huyu ameokoka angalia matendo. Vitendo vinavyofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara, vinaonyesha dhahiri kwamba wanamlinda Ekelege na taasisi ya *TBS.* Ekelege kusema kwamba Wabunge walienda kutalii ni matendo yake yanayoonyesha kwamba Ekelege analindwa na Serikali katika utendaji wake wa Shirika la Viwango na ana dharau Bunge na sio kwamba amewadharau Wabunge walioenda Hong Kong pamoja na Singapore.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie na Bodi ya Pamba. Mzee wangu aliwahi kumponyesha mtu mmoja kumnyoa kichwa alikuwa na chawa, kufua nguo zake zilikuwa na chawa, akaamini afya yake itaimarika, lakini kumbe kule nyumbani, nyumba yake ilikuwa na papasi, viroboto na kunguni afya yake haikuimarika. Wakulima hata kama mvua itanyesha, watapata pembejeo, watapata pesa nzuri, lakini ndani ya Bodi ya Pamba kuna papasi, kuna kunguni, kuna

viroboto wakulima wa pamba wataendelea kuwa maskini na pamba haitawatajirisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Bodi ivunjwe na *special audit* ifanyike ili tuweze kujua wahusika wote wachukuliwe hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. LUCY P. OWENYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Napenda nishukuru Kamati zote tatu na Wenyeviti kwa kutoa hotuba zao vizuri. *(Makofi)*

Aidha, napenda niungane na Kamati ya *PAC* kwa kutoa ushauri kwamba Ofisi ya *CAG* inafanya kazi katika mazingira magumu kwa kutokuwa na wafanyakazi wa kutosha, kwa hiyo tumeishauri Serikali ifanye marekebisho katika Sheria ya Ukaguzi Namba 11 ya mwaka 2008 katika kifungu 24(2) kwamba wawe huru ili waweze kutafuta wafanyakazi wao wenyewe na waweze kurekebisha maslahi ya wafanyakazi wa Ofisi ya *CAG.*

Mheshimiwa Naibu Spika, na mimi naomba nizungumzie kidogo kuhusu *TBS.* Mimi nimekuwa ni Waziri Kivuli katika Wizara ya Viwanda na Biashara tangu mwaka 2005, tumekuwa tukizungumzia suala la ukaguzi wa magari nje ya nchi. Mpaka leo hii nimeshukuru Kamati ya *POAC* iliunda tume, wakaenda kule wanakokagua na wakakuta kwamba ofisi ni hewa. Sasa sisi kama Kamati tumehoji; hawa wanaokagua magari wamepokea zaidi ya bilioni 27, lakini Serikali imepata bilioni nne tu tunauliza bilioni 15 zimekwenda wapi? Tunataka majibu ya kina na nashukuru Mheshimiwa Waziri leo asubuhi amesema kwamba watakagua na tunataka Serikali itujibu kwamba zile bilioni 15 zimekwenda wapi kwa sababu tuna shida nyingi, shida za madawati, shida za dawa na kadhalika.

Kwa hiyo, tunaomba Serikali itueleze shilingi bilioni 15 zimekwenda wapi na waliopelekea tukakosa fedha wawajibishwe kama Kamati inavyosema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bidhaa ambazo hazikidhi viwango, katika Jumuiya ya *East Africa, KBS* yaani *Kenya Bureau of Standard* na *Tanzania Bureau of Standard* wana makubaliano kwamba kuna baadhi ya bidhaa ambazo zikiingia Tanzania zikiwa zimeshachekiwa kule Kenya zikija Tanzania hazina haja ya kuchekiwa tena, lakini *TBS* walicheki wakakuta kuna baadhi ya vifaa ambavyo vikija Tanzania havikidhi viwango. Mfano halisi katika ripoti ya *CAG* kuna kampuni ambayo inaitwa *Yana Tyres,* inaleta matairi ambayo hayakidhi viwango, yanaingia ndani ya nchi na yapo sokoni, hii ni hatari kwa sababu *accident* zinatokea nyingi matairi yanapasuka, kwa hiyo, ni suala la kuliangalia sio matairi tu hata vyakula.

Mheshimiwa Naibu Spika, *Unilivers* wanaleta vyakula kama *Blue Band* na kadhalika na watumiaji wanavitumia, tunaona magonjwa ya kisukari, magonjwa ya *pressure* yanazidi, pengine *cancer* zinazidi, tunazidi kulalamika kwa nini magonjwa ambayo yamezidi kutokea kwenye nchi yetu lakini unakuta ni baadhi ya hivi vyakula vinaingia nchini na bado vinakuwa kwenye masoko na havichukuliwi hatua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu bajeti ya maendeleo kwenye Wizara, Wizara nyingi zimekuwa zikipewa bajeti za maendeleo kwa hisia tu, unakuta bajeti wanazoziomba sio wanazozipata, mfano halisi ni bajeti ambayo Wizara ya Maji imepewa, wao waliomba kiasi cha shilingi bilioni 17.3 wakapewa bilioni 11 pungufu ya bilioni tano sasa ukiangalia pungufu yote hii ina maana baadhi ya shughuli za maendeleo hayafanyiki halafu tunalalamika kwamba shughuli za maendeleo hazifanyiki, kumbe unakuta ile pesa aliyopewa ni kwa hisia tu na siyo ile fedha halisi. Kwa hiyo, tunaomba Serikali ihakikishe kwamba inatafuta vyanzo ambavyo tunaweza

tukawa na bajeti ambayo ni asilia badala ya kutegemea wahisani ambao na wenyewe wana wana matatizo ya kiuchumi huko walipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baadhi ya matatizo ambayo tumeyaona ni kuhusu Deni la Taifa. Deni la Taifa linazidi kukua kutoka trilioni 10 mpaka trilioni 14 na hakika mpaka sasa hivi litakuwa limeshapanda zaidi ya trilioni 14 zinaweza zikafika hata trilioni 20. Lakini inabidi tuangalie mipango yetu, kupanga ni kuchangua. Tunakuwa na deni kubwa, umaskini unazidi kuwepo. Sasa hivi ni jambo la kusikitisha, umaskini walio nacho wanakuwa nacho, maskini wamezidi kuwa maskini. Kuna sehemu ambazo kule Mburahati tumefika kiasi ambacho mtu yupo nyumbani anashindwa kununua dawa ya mswaki, anachukua mswaki wake anaenda dukani anawekewa dawa ya shilingi kumi, hii ni aibu kwa nchi yenye rasilimali, kwenye nchi yenye madini. *(Makofi)*

Lakini tunashindwa jinsi gani ya kuhakikisha kwamba *TRA* wanaweza wakakusanya kodi za kutosha ili tuweze kuzitumia na wananchi wetu waweze kufaidika na rasilimali zao walizonazo kwenye nchi yao, ni aibu na ni jambo la kusikitisha. Naomba sana Serikali ipange na tujue ni nini tunachokitaka katika vipaumbele vyetu. Siyo kwamba kutumia pesa kwa matumizi ambayo si ya lazima, unakuta Serikali inanunua magari mengi sana na magari ya aghali sana ambayo yanahitaji *service* kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, unakuta gari, shangingi moja kuifanyia *service* siyo chini ya shilingi milioni mbili, unakuta wanaenda kufanya kwenye sherehe za Kitaifa. Mfano sherehe za Nanenane, Wizara moja tu ya Afya imetumia zaidi ya shilingi bilioni 1.1 kwa ajili ya maadhimisho ya Nanenane. Wananunua *t-shirt,* wananunua kofia, wananunua suti, za nini wakati tuna shida nyingi ambazo zipo mbele yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lazima tuangalie ni jinsi gani tunaweza kupangilia mipango yetu ili tuweze kuwasaidia watu wetu ambao wapo kwenye matatizo na wanazidi kuwa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niongelee kidogo kuhusu Shirika la *Air Tanzania (ATC).* Ni jambo la kusikitisha, tumeongea mara nyingi sana kuhusu hili Shirika la *Air Tanzania.* Mimi naomba hao waliopelekea wakaenda wakakodi ndege ya *Airbus* ambayo ni 420214 walijua kabisa ndege ile ilikuwa inatakiwa kufanyiwa *service* kubwa *VA twelve years check.* Miezi sita tu baada ya miezi sita ndege ile imepelekwa kwenda kufanyiwa *twelve year's check, twelve year's check* ina maana ndege inaende kufanyiwa *overhaul* yaani kila kitu, ni kama inaenda kuwekewa injini mpya, kila kitu ni lazima kiwe kipya, kwa hiyo, walijua. Kwa hiyo, ile ndege sasa hivi imeenda kuwekewa kila kitu kipya. Deni limebaki Tanzania, ndege haipo Tanzania. Je, ile ndege ipo wapi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni miaka mingapi tangu ile ndege ipelekwe huko wapi sijui Ufaransa kutengenezwa. Tunataka Serikali itujibu. Ni nani wanahusika na ubadhirifu huu? Ni nani atakayelipa deni hili? Inatia uchungu sana.

Mimi naomba ni-*declare* kabisa, mimi ni mdau wa utalii, tunaenda tunauza utalii, mtu anasema anataka kuja Tanzania. Sasa anakuja mpaka Tanzania hebu niambie nitafikaje Kigoma? Nitafikaje Kilimanjaro? Hata ile *connection* ya ndani hatuna. Lakini kwa sababu tulikuwa tumeanza na ndege tisa, sasa hivi tumebaki na ndege mbili. Maskini wa Mungu ndege moja nayo imeharibika tena huko Kigoma, Waziri atueleze wana mikakati gani ya kuhakikisha kwamba tuna Shirika ambalo litafanya kazi na sisi tuweze kujivunia kama wenzetu wanavyojivunia Kenya.

Sasa hivi inatia aibu sana unaenda mahali unasema wanataka kuja Tanzania, inabidi uende Kenya ukaanze ku-

*negotiate* jinsi ya kuja Tanzania. Ni aibu na sisi tuna rasilimali za kutosha. Kama ni suala la kununua ndege au la kukodisha ndege tunaweza ku-*lease* ndege. Ndege yenyewe imeenda kuwa *leased* nasikia ni dola 325 kwa mwezi. Sijui kama huo mkataba bado tunalipa hilo deni la dola 325 kwa mwezi Mheshimiwa Waziri? Nafikiri utatujibu wakati wa kujumuisha. Tunataka tujue hizi fedha ni nani anazilipa na mtawezaje kuzilipa, maana yake Shirika lina madeni kibao. Lakini bado tunaenda kuingia mikataba ambayo haina tija kwa Taifa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kwa kweli inasikitisha na naomba kabisa wakati wakijumuisha Mawaziri watueleze wana mikakati gani ya kuhakikisha kwamba Shirika letu la *Air Tanzania* linafanya kazi na hiyo *Airbus* watairudisha kule Lebanon na kama bado wanaendelea kulipa hizo dola 325 kwa siku.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lucy Owenya. Mheshimiwa Magdalena Sakaya, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso. Mheshimiwa Magdalena Sakaya.

**MHE. MAGDALENA H. SAKAYA:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kunipa nafasi nami niweze kuchangia kidogo kwenye Taarifa za Kamati hizi za *oversight* tatu.

Kwanza niungane na wenzangu kwamba kwa kweli muda ambao tunapewa kujadili fedha za walipa kodi, fedha za wanyonge, zinazotafunwa bila utaratibu hautoshi Mheshimiwa Naibu Spika, tunaomba utaratibu ubadilike, hii ni kugawa pesa bila kuzifuatilia. Haiwezekani *CAG* anaripoti zaidi ya tatu, nne kubwa kiasi hiki, kuna ripoti tatu zimewasilishwa hapa, leo na kesho, Wabunge wengi wana mawazo tofauti. Serikali inayapataje?

Kwa hiyo, utaratibu huu naomba ubadilike kwa sababu ni kutotendea haki Watanzania hela zao zinapoliwa bila utaratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe pongezi kwa Kamati zote tatu za *oversight,* Wenyeviti wao pamoja na Wabunge wote ambao ni Wajumbe wa Kamati hizo kwa taarifa nzuri sana. Kwenye ripoti ya *CAG* cha kwanza ambacho kimenisikitisha kati ya mapendekezo 12 yaliyotolewa na *CAG* kwa mwaka 2010/2011 ni pendekezo moja tu lililofanyiwa kazi mpaka juzi mwezi wa tatu. Hii ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitaki kushughulikia matatizo ya fedha kwenye nchi hii. Kila mwaka *CAG* anakuja na ripoti, anatoa mapendekezo mengi, hayafuatiliwi, kwa hiyo, matatizo yanarudia mwaka baada ya mwaka kwa sababu Serikali yenyewe haioneshi nia ya dhati. Inakuwaje ndani ya mwaka mmoja pendekezo moja tu kati ya mapendekezo 12 siyo aibu? Hebu Serikali ione aibu, haiingii akilini kabisa. Yote haya yanagusa fedha za walipa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Serikali yenyewe ione aibu kwamba haiwatendei Watanzania haki ihakikishe kwamba mapendekezo yanafanyiwa kazi ili angalau fedha ambazo zinaibiwa ziweze kupona kwa ajili ya kusaidia Watanzania ambao wanakufa maskini. Pendekezo moja limefanyiwa kazi, mapendekezo mawili yamefanyiwa kazi *partially,* mapendekezo tisa hayaguswa kabisa, *shame! (Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la mishahara hewa. Kila mwaka tukae hapa tujadili mishahara hewa. Hivi anayetoa hii mishahara ni nani? Na kwa nini hatua hazichukuliwi? Haiwezekani milioni 792.2 ziendelee kutafunwa kila mwaka tunakuja na *data* mpya, hakuna hatua na wakati Watanzania wanakufa maskini, hawana huduma, hawana maji, hawana barabara, hawana elimu, tunakwenda wapi?

Haiwezekani, hapa lazima Serikali ituambie inafanya nini, tunataka majibu sahihi kesho wakati wa ku-*wind up. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mapendekezo mengi yanatolewa na Kamati, yanatolewa na *CAG* hayafanyi kazi. *CAG* amesema kwamba ukaguzi wa ndani uongezewe *support* tuongeze ofisi, tuongeze wakaguzi. Lakini bado matatizo tunaendelea kuona yanakuwepo. Tatizo sijui linakuwa wapi? Ametoa mapendekezo, Kamati imetoa mapendekezo, *Accounting Officers* na *Head of Department* wa Halmashauri wawajibike kwa matatizo yoyote yanayotokea ndani ya Halmashauri zao kwenye maeneo yao ya kazi, hakuna kinachofanyika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuongeza Ofisi za Ukaguzi maeneo mbalimbali ya Wilaya zetu ili kurahisisha kazi za ukaguzi wa fedha za walipa kodi, kwenye suala la ukaguzi kwa kweli linatia huruma, linatia aibu, tunaomba sana Serikali jamani iwajibike kwa hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni suala la usimamizi mbovu wa mapato kwenye Halmashauri zetu. Kwenye ripoti ya *CAG* jumla ya vitabu 682 vya kukusanya mapato kutoka kwenye Halmashauri 36 havikuonekana. Vitabu 682 hatujui vilikuwa na hela kiasi gani *can you imagine* kwamba Halmashauri ambazo zina Watendaji, ina Mkurugenzi, kila Idara ina Mkuu wa Idara, ina watendaji mpaka ngazi ya chini, vitabu vimekwenda wapi? Kwa nini vitoke viachwe pale kwa ajili ya ukaguzi, huu ni wizi. Hatuwezi kukubaliana na hali hii. Tunaomba Serikali iwajibike, tujue hizo Halmashauri vitabu ambavyo havikuonekana vimekwenda wapi? Fedha ambazo zimepatikana kwenye hivyo vitabu zimekwenda wapi? Kwa sababu havikuonekana kwenye akaunti ndiyo maana Mkaguzi Mkuu hakuviona, haviwezi kufanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwaka 2010/2011 jumla ya Halmashauri 47 zilikusanya fedha kiasi cha shilingi 4,227,984,618.

Fedha hizo hazikufikishwa kwenye Halmashauri husika. Jamani bilioni nne ni hela ya kutosha kujenga hata maabara kwenye shule zile za Kata lakini zinaliwa tu hivi hivi bila huruma. Hebu tuone aibu kwa haya masuala yanayotokea kila siku na kila mtu anasimama hapa hakuna hatua, hakuna *action* Watanzania wanaendelea kufa maskini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kukosekana kwa udhibiti wa usimamizi wa fedha kumesababishia kiasi cha shilingi 8,332,985,540 kutofika kwenye Halmashauri zilitoka kwa walipa kodi. Hizi ni *data* ambazo zipo kwenye ripoti ya *CAG.* Tunataka Serikali ituambie hizi fedha ambazo zimelipwa na walipa kodi mbalimbali hazijafika kwenye Halmashauri husika, zimeishia wapi hapa katikati?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli taarifa hizi ambazo tunazisoma kila siku *data* zinazotolewa na *CAG* hatua hazichukuliwi, inatia huruma. Suala lingine ambalo linaumiza na kila siku linazungumziwa ni suala la kuhamisha watumishi wabadhirifu. Kila mwaka tunasema, ni kwa nini anapoiba pesa ya mlipa kodi, pesa ya mnyonge, asiwajibishwe? Nataka Serikali itujibu kesho kwani adhabu ya kumhamisha mtumishi kutoka kwenye Halmashauri moja ya Kishapu kumpeleka Halmashauri ya Rombo, hiyo ni aibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mtu ametafuna hela za walipa kodi, badala umwachishe kazi na afungwe, mnaenda kumpeleka aendelee kwenda kutafuna hela kwingine huko. Huu ni wizi wa hela za walipa kodi. *(Makofi)*

Mimi naomba Wabunge wenzangu tuungane, tutunge sheria kama nchi nyingine kama mtu amekula hela za wanyonge, tuweke sheria tumpige risasi hadharani. Haiwezekani Watanzania waendelee kuteseka na wengine wanaendelea kula fedha zao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni suala la manunuzi yasiyofuata utaratibu. Jamani Wabunge tumetunga Sheria ya Manunuzi ya Umma, lakini katika Halmashauri karibu zote ripoti inasema hawatumii utaratibu wa manunuzi ya umma, wanajinunulia wanavyotaka na tunajua asilimia kubwa ya pesa ya walipa kodi zinakwenda kwenye manunuzi kwenye Halmashauri zetu. Kwa nini Sheria ya Manunuzi haifuatwi na kwa nini Serikali haifuatilii na nini sasa kifanyike kuhakikisha sheria tuliyoitunga Wabunge inafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, udhaifu wa Serikali mimi ninaona kabisa udhaifu wa Serikali unasababisha watumishi kutokuwajibika, kufanya wanavyotaka, kutafuna hela za walipa kodi *simply* kwa sababu hawachukuliwi hatua, ya kuzungumza ni mengi muda ni kidogo..

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine la kusikitisha watumishi wa benki wamefikia hatua ya kushiriki na watumishi wa Halmashauri kutafuna hela za wananchi, fedha za miradi. Tumeona ripoti inasema pesa nyingi zinatoka kwa njia isiyoeleweka kwenye makubaliano kati ya watumishi wa benki, mtumishi wa Halmashauri inatoka kisirisiri inakwenda kuliwa, miradi haiendi. Katika Halmashauri miradi yote imesimama, shule zipo nusu nusu, watoto wanateseka, miradi ya maji inaliwa. Leo tunaangaika, haiwezekani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mambo haya kwa nchi ambayo tunasema ni nchi ya amani, nchi ambayo inawajibika, Serikali ambayo ni sikivu hayatakiwi kuendelea kusikika kila siku. Serikali ichukue hatua, kwa kweli inatia aibu. Haipendezi kwa sababu nchi hii ni maskini sana na watu wenyewe wanajitoa sana. Kodi ambazo zinatafunwa kila siku ambazo tumezitaja hapa na zingine zipo huku ni nyingi, nina imani kila mmoja atasoma na ataona ni hela za wanyonge.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo wakiwa wanalipishwa kule vijijini hata kuku anakamatwa ili mradi alipe anachotakiwa.

Hata ni kulipia shule wengine wanafungwa. Yapo maeneo wanawekwa kwenye Ofisi ya Kijiji hata siku mbili, tatu kwa sababu wameshindwa kutoa mchango wa shule. Leo pesa zinatafunwa na wajanja wachache na Serikali imenyamaza.

Mheshimiwa Naibu Spika, inasikitisha, inaumiza, inatia uchungu. Hatutendei Watanzania haki, tunaomba Serikali ichukue hatua. Serikali iamke na isaidie Watanzania waweze kuondokana na umaskini.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Magdalena Sakaya. Sasa Waheshimiwa Wabunge nawaletea Mbunge mpya kabisa Mheshimiwa Cecilia Paresso. *(Makofi)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Ahsante Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kufika hapa pia shukrani za dhati kwa wazazi wangu, mume wangu na familia yangu kwa ujumla. Pia napenda kutoa shukrani kwa viongozi wangu Wakuu wa Chama na wanachama wote kwa ushirikiano wao. *(Makofi)*

Aidha, nawashukuru viongozi wangu wa CHADEMA Karatu yakiwemo mabaraza ya vijana, wazee, wanawake, madiwani wenzangu wa Karatu na Madiwani wote Tanzania nzima. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kupongeza chama changu kwa kuendelea kujenga imani kwa wananchi na hivyo kuongeza uwakilishi katika kazi za Bunge na Halmashauri na pia kwa ushindi wa uchaguzi katika Jimbo la

Arumeru Mashariki. Kwa pamoja tuendeleze falsafa ya nguvu ya umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia kuchukua fursa hii kutoa pole kwa misiba iliyoipata nchi hii kwa kuondokewa na Wabunge wawili Mheshimiwa Regia Mtema na Mheshimiwa Jeremiah Sumari, Wabunge wawili wa Baraza la Wawakilishi, watumishi wa Bunge na Watanzania wote ambao wametutangulia mbele ya haki, Mungu azilaze roho zao mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichangie taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Niwapongeze Wenyeviti waliowasilisha Kamati hizi na nakubaliana na Kamati kwa wazo walilolitoa la kuweza kupunguza gharama ambayo inaipata Halmashauri kwa kuwaita watendaji wengi kuja kuhakikiwa na Kamati wakati Kamati inahakiki Halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda kuungana na Kamati kwamba waweze kukagua zile zenye uzito wa hoja. Lakini pia ni vema Serikali iweze kuiwezesha Kamati hii kwa maana kwamba Halmashauri 133 nchini. Lakini ufanisi wa demokrasia na kuweka wazi ni vigumu kukwepa gharama. Ni vyema Serikali iweze kuiwezesha Kamati hii iweze kukagua Halmashauri zote nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu inaonyesha kwamba mfano kwa mwaka 2009/2010 Halmashauri 29 zimekaguliwa nchini na ikapata *unqualified opinion* lakini ukienda mwaka 2010/2011 Halmashauri hizo hizo 29 zimetoka kuwa *unqualified* na kwenda *qualified* na moja ikipata *adverse.* Sasa ni vema Serikali iweze kuona umuhimu wa kuiwezesha Kamati hii na kukagua Halmashauri zote isiangalie tu Halmashauri baadhi ambazo zina uzito fulani wa hoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye suala la uchambuzi wa ruzuku katika Halmashauri, fedha za miradi ya ruzuku ya maendeleo zinachelewa mno. Serikali inazichelewesha fedha hizi hazifiki kwa wakati, hatujui uzembe unakuwa wapi? Ni vema Serikali ichukue nafasi yake iweze kuziwezesha Halmashauri. Wakati mwingine utalaumu tu Halmashauri lakini kama Serikali haijaweza kuiwezesha Halmashauri, Halmashauri haiwezi kufanya kitu chochote. Mfano kwa mwaka huu wa fedha Halmashauri haikuweza kupata fedha za miradi ya maendeleo kwenye robo ya kwanza wala robo ya pili. Fedha zimekuja kwenye robo ya tatu ambapo tunaelekea mwisho wa bajeti. Sasa je, watatekelezaje miradi ile iliyokusudiwa? Ni vema Serikali iweze kutekeleza haya na kuona mfumo nzuri wa udhibiti wa mapato wa matumizi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia unatakiwa unapochangia unaniangalia mimi. Naona unaangalia sana chini hapo. Endelea tu Mheshimiwa. *(Kicheko)*

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Nashukuru Mheshimiwa Naibu Spika, nafikiri nitazoea tu taratibu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka niongelee kwamba Serikali ni vema iweke mfumo imara wa kudhibiti matumizi katika Halmashauri zetu. Halmashauri zetu zimekuwa na matumizi makubwa hasa kwenye uendeshaji wa magari, utengenezaji wa magari, ununuzi wa vipuri, matumizi yamekuwa makubwa mno. Sasa ni vema Serikali iweke mfumo mzuri wa udhibiti. Utakuta mfano Kata X ameenda Mkuu wa Idara labda ya Maji. Kata hiyo hiyo X anaenda Mkuu wa Idara ya Maendeleo ya Jamii. Kata X hiyo hiyo anaenda Mkurugenzi, lakini kumbe ingewezekana wakapanga safari hiyo hiyo moja kwenye hiyo Kata X wakapunguza kuliko kila mtu kwenda na gari lake. *(Makofi)*

Sasa ni vema Serikali ione ni namna gani na ituletee taarifa ni namna gani itaweka mfumo mzuri wa udhibiti. Ukienda kwenye suala la mikataba, mikataba mingi inayoingiwa na Halmashauri na mawakala imekuwa kama siri, Mabaraza ya Madiwani hayana fursa nzuri ya kuangalia mikataba hii. Ni vema sasa Mabaraza ya Madiwani kabla ya mkandarasi au wakala yeyote kuanza kazi ni vema Mabaraza ya Madiwani yaweze kupitia mikataba hii na iwe ya uwazi na wao wenyewe waridhie ndipo wakala husika au mkandarasi aweze kutekeleza yale ambayo yapo katika mkataba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukienda kwenye vyanzo vya mapato, Serikali Kuu imenyang'anya vyanzo vingi vya mapato ndani ya Halmashauri na ndio maana Halmashauri zote zimekuwa tegemezi, Halmashauri inasubiri fadhila ya Serikali Kuu, sasa sijui ile dhana ya kupeleka madaraka Serikali za Mitaa iko wapi? Je, ni kwa maneno? Ni kwa nini isiende kwa vitendo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali za Mitaa zimenyang'anywa vitu vingi. Mfano waliahidi kurudisha leseni za biashara kuanzia Januari, Halmashauri zetu zingeweza kukusanya leseni za biashara, lakini mpaka leo utekelezaji huo haupo; sasa Serikali ituambie ni lini watazipa mamlaka kamili Serikali za Mitaa ziweze kuwa na mamlaka kamili ya ukusanyaji wake wa mapato na kuamua mambo yao bila kuingiliwa kwa kiasi kikubwa na Serikali Kuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la watumishi wabadhirifu. Mara nyingi kwa sababu nilikuwa Diwani, naona kule chini, tunaona tu kwenye suala la Wakuu wa Idara, mfano Mkuu huyu wa Idara ameharibu anahamishiwa Halmashauri nyingine, lakini kule kuna tatizo la Watendaji wa Kata na Watendaji wa Vijiji. Mtendaji wa Kijiji anaharibu, anakula fedha za michango, anahamishiwa kijiji kingine badala ya kumwajibisha pale alipo; anahamishiwa kijiji kingine,

hachukuliwi hatua, matokeo yake kunakuwa kuna migogoro mikubwa sana kati ya Watendaji wa Vijiji na Wajumbe wa Halmashauri ya Serikali za Vijiji. Sasa Serikali ituambie kwamba kwa hawa pia ni lazima wawe wanachukuliwa hatua palepale kuliko kuhamisha tatizo. Bora kutibu tatizo kuliko kulihamisha tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kuchangia suala la mfumo wa utoaji wa taarifa kwa Madiwani. Mfumo huu umekuwa ni mbovu, hauwawezeshi Madiwani kupata ule uhalisia. Ni vema sasa Serikali, ione mfumo mwingine mpya ambao utakuwa ni rahisi kwa Madiwani. Tunaelewa kwamba Madiwani wetu wengi Tanzania bado wana elimu ndogo, wana uelewa mdogo, lakini hawapewi mafunzo ya kutosha na Wizara husika; sasa ni vema ukawepo utaratibu wa taarifa hizi kusomeka kwa urahisi na kusimamia kile wanachokiona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusema kuwa ni vema pia Serikali iweze kuangalia utaratibu wa vikao vya Mabaraza ya Madiwani, vinakaa baada ya miezi mitatu, kwa nini angalau isiwe hata baada ya miezi miwili ili waweze kusimamia? Kuna vitu vingine vinahitaji maamuzi ya Mabaraza ya Madiwani, lakini maamuzi yale yanachelewa mpaka usubiri miezi mitatu, mitatu. Sasa ni vema pia Serikali ione utaratibu huu na iweze kuubadilisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Madiwani wamekuwa na kilio kikubwa sana kwenye posho. Kabla sijaingia hapa nililisikia suala hili na Serikali iliahidi, lakini mpaka leo mpaka kesho, hakuna utekelezaji. Waziri aksimama baadaye naomba atuambie kwamba ni lini posho za Madiwani zitabadilishwa na isiwe posho na iwe mishahara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. DAVID Z. KAFULILA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi ya kuchangia hoja ya Hesabu za Serikali jioni hii ya leo. *(Makofi)*

Awali ya yote, kabla sijaanza kuchangia niseme tu kwamba kwanza ninaishukuru Serikali kwa kulifanya Jimbo langu la Kigoma Kusini kuwa Wilaya rasmi kwa ajili ya kusogeza maendeleo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapozungumza hoja za ukaguzi kwa kiasi kikubwa, kwa uzoefu mdogo ambao nimeupata tangu mwaka 2011 mpaka sasa na nikisoma taarifa za Mabunge yaliyopita, inaoeneka kwamba hoja hizi zinafanana. Kwamba yale yale yaliyokuwa yakifanyika mwaka 2004 yanaonekana kwamba ndio yaleyale yamefanyika mwaka 2005, yaleyale yanafanyika mwaka 2006, 2007, 2008, 2009 na 2010. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, inaelekea kwamba kuna tatizo la msingi ambalo inahitajika Serikali kutazama upya. Nimeona nianze kwanza na utangulizi huo kabla sijaja kwenye hoja mahsusi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ningependa kuchangia hoja ya ubinafsishaji; kama kuna eneo ambalo nchi hii imeuzwa, kama kuna mchakato ulifanywa wa kuuza Taifa hili ni mchakato wa ubinafsishaji. Watu wamezungumza maeneo mengi sana kuhusu hasara ambazo tumezipata kwenye ubinafsishaji, lakini mimi nitatoa mfano mmoja tu wa Mgodi wa Chumvi Uvinza; huu mgodi ni mgodi ambao nimekuwa nikiufuatilia hata kabla sijawa Mbunge, mgodi huu una uwezo wa kuzalisha chumvi kwa zaidi ya miaka 800 kwa utafiti uliofanywa na Kampuni ya Ujerumani mwaka 1927. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mgodi huu ulijengwa kwa fedha za Waitaliano miaka ya wakati wa Uhuru, lakini umekuja kuuzwa kwa shilingi milioni 900; mwekezaji kauziwa mgodi huu

kwa shilingi milioni 900, akalipa 10% ambayo ni milioni 90 na mwekezaji yule akabadilisha *plant* moja, sio kubadilisha, akang'oa mitambo ya *plant* moja ambayo inazalisha chumvi kwa kutumia umeme, akauza nchini Iran kwa thamani ya bilioni 4.5. Amenunua kwa milioni 900, akaomba alipe 10% kwanza, lakini bado mitambo aliyoing'oa ameuza nchini Iran kwa bilioni 4.5.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii haiwezekani. Haya ndio mambo ambayo yanawafanya watu walalamike. Haya ndio mambo ambayo yanaongeza hasira. Wafanyakazi waliokuwa wakifanya kazi kwenye mgodi ule kwa miaka 30 mpaka 40, kuna watu wamelipwa mafao ya shilingi 200,000/= unaweza ukadhani maigizo, lakini kuna watu wamefanya kazi katika mgodi ule miaka 20, miaka 30, wamelipwa kuanzia shilingi 200,000/= mpaka shilingi 1,200,000/=.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndio mambo ambayo yanatufanya tukasirike. Naomba kukazia Azimio la Kamati ya *POAC;* tunahitaji mchakato wa ubinafsishaji upitiwe upya. Ni muhimu mikataba yote iwekwe hadharani, wekeni kwenye mitandao watu wawe wanasoma tu. Kama mikataba mmekwishakuingia, kuna sababu gani ya kuendelea kuifanya kuwa siri? *(Makofi)*

Mimi nimekwenda kuomba Ofisi ya Bunge wanipatie Mkataba huu wa Mgodi wa Chumvi, wakauomba Serikalini, ikachukua muda kupatikana. Lakini hata ulipopatikana, ninausoma chini ya ulinzi; Mbunge, nasoma Mkataba chini ya Ulinzi, duuh! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii nchi ni ya akina nani? Mimi nilidhani sisi Wabunge ndio waamuzi wa nchi. Sasa inawezekanaje mimi kama Mbunge nasoma mkataba chini ya ulinzi, hivi raia wa kawaida akitaka kuuona huu mkataba unaohusu rasilimali za nchi yake itakuwaje? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba jambo hili liweze kutazamwa vizuri. Nchi yetu ina uwezo, tatizo kubwa na ugonjwa mkubwa ambao tunao ni namna ya kusimamia hicho kidogo ambacho kinapatikana; mbali ya kushindwa kusimamia namna ya kukusanya, lakini hata hicho kidogo ambacho kinapatikana, tunashindwa kukisimamia. Kuna matumizi mabaya mno, watu ni vijana wanaingia Serikalini anafanya kazi miaka mitatu anajenga ghorofa. Mimi nashangaa, mimi Mbunge, mbona hata nyumba sina? Watu wanafanya kazi *TRA* pale, miaka mitatu miaka minne, ni matajiri wakubwa; hawakusanyi kodi. Nimewahi kuwaambia hapa wanatufanyia usanii kwamba wanaonesha kwamba tunakadiria kukusanya kiasi hiki, halafu tumekusanya kiasi hiki, kwa hiyo tumezidi kwa asilimia hizi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukweli ni kwamba nchi hii haikusanyi kodi. Nimepata kuwaambia kwamba mwaka 2005 tulikuwa tunakusanya kwa mwezi bilioni 260 wakati *exchange rate* ya dola kwa *Tanzanian Shillings* ilikuwa shilingi 1,000/=. Kwa sarafu iliyo imara kama dola, tafsiri yake ni kwamba mwaka 2005 tulikuwa tunakusanya dola milioni 260. Lakini mpaka sasa tunakusanya bilioni 435, ukipeleka ukiangalia kwa pesa za madafu utahisi kwamba tunakwenda mbele sana. Lakini ukipeleka kwenye sarafu iliyo imara kama dola unaona kwamba tulikusanya dola milioni 260 mwaka 2005 leo tunakusanya dola milioni 235 mwaka 2011/2012, kwa hiyo, bado kuna tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho ningependa kuzungumzia suala zima la umaana wa bajeti na Bunge. Bado Bunge hili, mchezo tunaoufanya wa kukaa hapa kujadili bajeti hauna maana yoyote. Angalia mfano mmoja, Wizara ya Miundombinu bajeti iliyopita hii ambayo tunamalizia walipitishiwa *1.2 trillion,* (bilioni 1200) lakini mpaka mwezi wa pili wamepewa bilioni 380, na wakati wana madeni ya bilioni 330. Kwa hiyo, ni sawasawa na kwamba hiyo bajeti yote haikufanya kazi yoyote isipokuwa ililipa deni tu. Sasa kuna maana gani

ya kukutana kwa ajili ya kupanga bajeti kama mwenendo wa bajeti uko namna hii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nashauri kwamba ni muda muafaka sasa tuanzishe *a Budget Office* ya Bunge. Bunge liwe na *Budget Office* ambayo ita-*monitor.* Isiwe kwamba tukishapitisha mwaka wa fedha, tunakuja kukutana tena mwaka mwingine wa fedha; hii ni hasara kubwa, kuna umuhimu wa kuwa na *Budget Office* ambayo ita-*monitor* hatua kwa hatua kila siku, kila mwezi inakuwa inafanya *monitoring* ya yale ambayo tuliyapitisha.

Mheshimiwa Naibu Spika, inawezekana kabisa hapa, tukifanya utafiti mdogo kwenye hizi Wizara ambazo tunakubaliana kwamba tulizipa fedha katika mwaka wa fedha uliopita katika mwaka wa fedha huu ambao unakwenda kumalizika, kuna baadhi ya Wizara utakuta zimepata 40%, 30% zingine 10%, sasa maana ya kupanga ni nini?

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha ipo, hii nchi ina fedha na haiwezekani nchi ambayo ni ya tatu kwa dhahabu katika Afrika, bado tujadili bajeti ya kasungura kadogo, haiwezekani. Nchi ambayo ni ya 11 kwa mito mingi duniani, nchi ambayo kwa gesi inazidi kupaa, wanakadiria kwamba huenda miaka nane ijayo tukawa miongoni mwa nchi chache kabisa mbili, tatu kwa gesi nyingi duniani. Inawezekanaje bado tunapanga bajeti za kimaskini? Hii ni nchi ambayo ilipaswa kuwa *a donor country,* hii ni nchi ambayo tungekuwa tunatoa misaada kwa vinchi vidogo vidogo hivi ambavyo havina fedha. Lakini leo kwa sababu ya uzembe wetu, leo kwa sababu ya kutokujali, Tanzania ni miongoni mwa nchi maskini sana duniani, leo 45% ya watoto wenye umri wa chini ya miaka mitano wana uzito chini ya kiwango, wamedumaa kutokana na umaskini. Huu ni msiba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naona muda umekwisha, lakini bado kuna umuhimu kutazama upya nchi yetu. Hii ni nchi tajiri,

bado ina nafasi ya kuwafanya hawa watu waishi maisha mazuri. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. JOSHUA S. NASSARI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana. *(Makofi)*

Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu ambaye leo imempendeza kwamba Nassari na yeye nae ni Mbunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini niwashukuru sana wananchi wa Arumeru Mashariki kipekee ambao waliamua kuchagua utu dhidi ya fedha, ambao waliamua kumchagua yule ambaye hajaoa kwa sababu hakuja kusuluhisha ndoa Bungeni, ambao waliamua kumchagua asiyekuwa na kitambi kwa sababu hatujaja kucheza mieleka na ambao walimchagua kijana mdogo wakiamini anaweza kuwa dogo janja akayafikisha matatizo yao Serikalini na panapohusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeipitia taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu ya Serikali Kuu na kwa kweli wakati nikiisoma nikajiuliza maswali mengi sana; nikajiuliza hivi hii ni nchi au ni *SACCOS?* Kwa sababu unashangaa kwamba watu kila siku wanachota pesa kama unavyoweka kwenye *SACCOS* kesho unakuja unachota, keshokutwa unachota. Ukienda China, wanadai kwamba ukila rushwa, ikisadikika kwamba umekula au umetoa rushwa adhabu yako unanyongwa. Leo tunasema kwamba bidhaa za Kichina ni *fake,* lakini sheria zao sio *fake,* za kwetu ndio *fake. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona mapungufu kwenye matumizi mabaya ya fedha za umma. Manunuzi yanafanyika bila kufuata taratibu na kanuni au sheria zilizowekwa. Ukiangalia kwenye kitabu hiki, naomba kunukuu, tunaelezwa kwamba kwa mwaka wa fedha 2009/2010 manunuzi ya umma shilingi bilioni 50, milioni 685 na vilaki kadhaa na pesa zingine kwamba hizi zote zilitumika kufanya manunuzi ambayo

hayakufuata taratibu au sheria ya manunuzi ya umma na kwenye hizi fedha unaambiwa kwamba Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali, iliongoza kwa kutumia shilingi bilioni 49. Sasa hii ni Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ambayo Watanzania wanaamini kwamba ndio wanaofahamu vizuri Sheria za Manunuzi na ndio wanaopaswa kuzifuata kwa usahihi, halafu ndio wanaoongoza kutokuzifuata sheria hizi wakati wakifanya manunuzi kwa kutumia fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini vilevile ripoti inaonesha kwamba kumekuwa hakuna kumbukumbu, kumbukumbu za fedha za manunuzi hazitunzwi. Leo ni aibu unakuta shilingi bilioni 362 hizi fedha ukiongeza kidogo tu ni sawasawa na nusu trilioni ambazo zina uwezo wa kulipa walimu mishahara zaidi ya 100,000 kwa mwaka mzima kwenye nchi yetu. Lakini hizi fedha zimetumika na kumbukumbu hazitunzwi yaani hazionekani, nyaraka ni pungufu maana yake ni nini? Hatuna uhakika kama kweli haya manunuzi yalifanyika au hizi fedha ziliishia kwenye mifuko ya watu wachache. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini sio hayo peke yake, kumekuwa na matumizi ysiyokuwa ya ulazima. Ripoti inaonesha kwamba mpaka tarehe 30 Juni, 2010 magari ya Serikali yenye thamani ya shilingi trilioni tano, ina maana Serikali yetu inamiliki magari yenye thamani ya shilingi trilioni tano na kila siku baada ya siku magari yanazidi kununuliwa, magari ya gharama kubwa na magari ambayo uendeshaji wake vilevile ni wa gharama kubwa kupindukia. Sasa hii ni aibu kwamba tunaambiwa tunamiliki magari ya shilingi trilioni tano, wakati ukienda kwenye Majimbo yetu, ukienda Arumeru Mashariki, hakuna magari ya wagonjwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sio hivyo peke yake, lakini vilevile unakuta kwamba hata haya magari yanavyonunuliwa Japan, gharama ambayo Serikali inatumia ni tofauti na gharama halisi ambayo mtu binafsi akienda kununua magari haya anakuwa analipa. Hii inaonesha kwamba kuna wizi

mkubwa tena wa mchana kweupe. Sasa hii inasikitisha sana kwamba unakuta Wizara mbili kwenye Serikali yetu hazina majengo zinapanga; wanapanga na kwa Wizara ya Afya peke yake wanalipa shilingi milioni 38 kila mwezi. Maana yake kwa mwaka wanalipa shilingi milioni 456. Kwa miaka mitatu, miaka minne peke yake kwa hizi fedha ambazo wanalipa kwenye pango, Wizara ina uwezo wa kujenga ofisi na ikajitosheleza, zikatumika kwa miaka mingi ijayo tukaacha kuendelea kulipa kodi kuliko kulipa pango. Hii ni aibu sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio sababu tunafika mahali tunaingia huku Bungeni mahali ambapo tunaamini kwamba hili ndilo jengo kuu la kufanya maamuzi kwenye nchi yetu, halafu anakuja Waziri siku ya jana anakwambia hajaiona ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwenye ukaguzi maalum wa Shirika la Viwango Tanzania *(TBS).* Halafu leo asubuhi anakuja Naibu wake anatuambia kwamba hiyo ripoti anayo. Halafu cha ajabu, mimi hapa mkononi hiyo ripoti ninayo, ni Mbunge mpya, nimeingia huku juzi; halafu Waziri, anasema hana. Sasa mimi hii inanishangaza na kwa kweli napata wasiwasi sana, sijui ni mahali gani tunapolipeleka Taifa letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi nakubaliana kabisa na mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati. Mapendekezo yote yaliyotolewa na Kamati, nafikiri yanapaswa kuungwa mkono na Wabunge wote *across parties* bila kujali tofauti ya vyama vyetu kwa sababu kazi tuliyotumwa huku ni kuja kuwasimamia Watanzania na ninasikitika kwamba leo tunajadili fedha za wananchi lakini Waziri wa Fedha hayupo. Jana tulikuwa tunachagua Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki, hili Bunge lilikuwa limejaa, Mawaziri wote walikuwepo; leo tunaikanyaga Serikali kuisimamia kuhusu fedha zetu, Mawaziri hawapo. Kwa hiyo, kwa kweli, mimi inanishangaza sana kwamba kwenye uchaguzi wa Wabunge tupo, lakini kwenye kusimamia fedha zetu hatupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mimi niseme tu kwamba naungana na ninakubaliana kabisa na mapendekezo ya Kamati na ninaomba tusivunje hili Bunge, kabla hatujaondoka, tukubaliane kwa sauti moja kwamba lazima Serikali iwajibike na sitegemei kama alivyosema Mheshimiwa Kangi Lugola kwamba yeye ameomba Mungu ndege ya Rais isije ikawekwa mafuta ikaanguka; mimi wala siombi ya Rais, zile ndege zinazopandwa na walalahoi za Watanzania ambazo leo hii zinawekwa mafuta ambayo pengine yamechakachuliwa, niombe Mungu kwa leo isianguke hata moja wakati tukisubiri Waziri kesho akitoa tamko na pengine achukue maamuzi magumu. Kama Wizara imemshinda, aachie ngazi Watanzania na watu wengi ambao wana uwezo wa kufanya kazi na wako *committed.* Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii na mimi niweze kuchangia kwenye Kamati hizi muhimu ambazo zimeshikilia nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme haya kwa niaba ya vijana wa Tanzania. Vijana wa Tanzania, wananchi wa Tanzania wakiwepo wa mkoa wa Mara na Wilaya ya Bunda kwa ujumla wamenituma nianze kwa kusema hivi yote yanayoendelea, watu kushindwa kutimiza wajibu wao, fedha za umma kuendelea kupotea na kuliwa, chanzo kikubwa ni Serikali hii hapa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kabla sijaingia katika Bunge hili, nilikuwa nasikia taarifa za Kamati, nilikuwa nikisikia taarifa za Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali; Kamati ziliendelea kushauri, *CAG* aliendelea kushauri, lakini hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sisi kama Wabunge, sisi kama vijana humu ndani bila kujali itikadi zetu tunaleta kilio cha Watanzania waliowapa ridhaa Serikali kwa mujibu wa Ibara ya

nane, kwa kuwachagua ili waweze kushughulikia matatizo ya Watanzania ikiwepo na kudhibiti ubadhilifu wa fedha, lakini hakuna chochote kinachofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baba yangu aliniambia ukiona mtu mzima anakudanganya ujue anakudharau, lakini sitaki niamini kama Serikali inawadharau Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ningependa niende kwenye hoja, nianze kuchangia suala zima la *DAWASCO,* kila siku Wabunge wamekuwa wakitoa kilio chao kikubwa katika Shirika la *DAWASCO* suala zima la kushindwa kuthibiti upotevu wa maji, kushindwa kuondoa tatizo la maji katika jiji la Dar es Salaam, lakini pia kilio kikubwa kilikuwa kwenye Mamlaka ya Maji Mijini.

Mheshimiwa Naibu Waziri hapa wakati akijibu maswali Bungeni alikuwa ameelezea kwamba kufikia mwaka 2015 Serikali itafanikiwa kupunguza tatizo la upotevu wa maji kwa asilimia 20 ilifikia asilimia 20 kwa maana kwa sasa hivi kwa mujibu wa ripoti ya *performance* za mamlaka ya maji mijini inaonesha wazi kabisa nchi zilizoendelea zimeweza kudhibitii la upotevu wa maji na imebaki asilimia nne tu. Malengo ya Serikali tutoke kwenye zaidi ya asilimia 50 kufikia asilimia 20 kufikia mwaka 2015. Lakini cha kushangaza kwa mujibu wa taarifa ya *DAWASCO* wameweza kupunguza asilimia ya upotevu wa maji ni asilimia tatu tu leo, mwaka 2012 kwa hiyo, mpaka mwaka 2015 wataweza kupunguza asilimia tisa tu lakini cha kushangaza Waziri ameendelea na mtindo ule ule wa kuwapa Watanzania matumaini hewa huku wakijua wanashindwa kuwezesha mamlaka za maji, wanashindwa kuwapa fedha za kutosha kwa ajili ya kukamilisha miradi ya maji, wanashindwa kuwapa fedha za kutosha kwa ajili ya kukarabati miundombinu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ripoti hii ya *performance* ya Mamlaka ya Maji kwa mwaka, mamlaka zote

za maji zinapoteza bilioni 2.5 kwa sababu tu ya uchakavu wa miundombinu na maji kupotea, mbali na kwamba baadhi ya watumishi wasiokuwa waaminifu wanajiunganishia maji kiholela. Lakini mimi na Kamati yangu tulitembelea *DAWASCO,* tulitembelea na baadhi ya Mamlaka za Maji ukiwepo na mradi mkubwa wa maji wa Ruvu Chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri alipokuwa akijibu maswali hapa Bungeni, bado kwa kitendo kile kile cha kuendelea kutoa ahadi hewa za Watanzania huku akijua kabisa hakuna fedha wala hawana mpango wa kupeleka fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi kwa sababu tunajua fedha ambazo wanazitegemea kutoka kwa wahisani kwa kukamilisha miradi ameendelea tena kutoa ahadi hewa hapa kuhusiana na mradi wa Ruvu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ule mradi mpaka kukamilika mbali ya kwamba tayari umeshaanza na unatarajiwa ukamilike mwakani, bado zinahitajika milioni 15; lakini kwa habari nilizonazo kwa mwaka huu Wizara ya Maji kwa mwaka huu imetenga bilioni 18 tu, halafu jana Mheshimiwa Naibu Waziri anaendelea kuwaongopea Watanzania kwa kuwapa matumaini hewa eti anasema mradi wa maji utakamilika mwakani, utakamilikaje, utakamilika vipi wakati hela hakuna?

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii yote tunashindwa kuweka vipaumbele, tunashindwa kutenga fedha zetu wenyewe za ndani kwa ajili ya mahitaji ya msingi na mwaka jana wakati nachangia nilisema tutenge fedha kwa ajili ya kukamilisha miradi ya mahitaji muhimu kama maji kwa fedha zetu za ndani tumalize na Dar es Salaam, mhamie na kwetu kule Mara, kule Bunda na wenyewe waondokane na tatizo la ukosefu wa maji safi na tangu Uhuru. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niende kwenye Shirika la *MSD,* tunajua Watanzania wamekuwa wakitoa kilio chao kikubwa kwa ukosefu wa Madawa na *MSD* imekuwa

ikilalamikiwa sana kushindwa kufikisha dawa kwenye hospitali yetu hasa mikoani. Lakini hii yote inatokana kusukumiziana mizigo kwa sababu Serikali na yenyewe haitimizi wajibu wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haipeleki fedha *MSD* kwa wakati, leo kwa mujibu wa ripoti ya *CAG* Serikali inadaiwa bilioni 40, nisingekuwa na tatizo kama hizo bilioni 40 zingekuwa zinaenda kununua choroko, maharage, bilinganya, lakini hizi hela za kununua dawa za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, za kununua vifaa vya Watanzania kwa ajili ya kupeleka hospitalini, lakini haifanyiki hivyo. Kwa kweli hii hali Watanzania imewachosha na mimi niwaambie vijana tuna kauli mbiu yetu leo tuko zaidi ya asilimia 65, mwaka 2015 tutakuwa zaidi ya asilimia 80 na tunasema kabisa kama maandiko yanavyosema asiyefanya kazi na asile, asiyetimiza wajibu wake 2015 atakiona cha moto. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongelea mambo ya *MSD,* lakini pia naomba niongelee uwekezaji usiokuwa na tija na hapa naomba niguse *EPZ* sina tatizo na uwekezaji, lakini uwekezaji wa *EPZ* unaenda sambamba na kuchukua ardhi ya Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikizungumzia Bunda, tangu mwaka 2007…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kumalizika muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bulaya, kengele ya pili tayari.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba muongeze muda kwa ajili ya haki za Watanzania tunapojadili mambo muhimu kama haya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa kwa ushauri, Mheshimiwa Masoud Salim atafuatiwa na Mheshimiwa Halima Mdee ameingia sasa hivi nadhani hajajiandaa, Mheshimiwa Masoud Abdallah Salim.

**MHE. MASOUD ABDALLAH SALIM:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru. Awali ya yote napenda kumshukuru Mwenyezi Mungu *Subhana Watallah* aliyetuwezesha uzima na afya njema hadi nikichangia taarifa hizi tatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini awali ya yote kwa niaba ya Chama changu cha Wananchi *(CUF),* niwapongeze Waheshimiwa Wabunge kwa kumchangia Mheshimiwa Taha Taslima kuwa miongoni mwa Wabunge wa Wabunge la Afrika Mashariki. Kinachoonekana tangu asubuhi baada ya kuwasilishwa kwa taarifa hizi tatu, malalamiko yote yanaonekana Serikali haijajipangia vizuri matayarisho yake kwenda kusikiliza au kutekeleza hotuba ya uzinduzi ya Mheshimiwa Rais kwa Bunge hili. Naomba niikumbushe Serikali, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wakati akizindua Bunge hili alisema nanukuu; "wizi, uzembe, ubadhirifu hautavumiliwa." *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kinachoonekana wizi, uzembe na ubadhirifu unaendelea kuvumiliwa, ukiangalia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za Mitaa ambayo tumepewa, unaangalia waziwazi kwamba kuna tatizo Kishapu, Sengerema, Longido, Ludewa, Moshi na Manispaa ya Ilala. Lakini kinachoonekana kwamba fedha zinaondolewa kwenye akaunti ya Halmashauri, zinaingizwa kwenye akaunti ya mtu binafsi lakini hakuna hatua zinazochukuliwa, hilo ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ripoti inaeleza kwamba Waheshimiwa Wabunge wengi wameeleza kuna Halmashauri 36 zimelipa mishahara hewa shilingi milioni 961.3, lakini hakuna

hatua yoyote ya Serikali ambayo imewachukulia watu hawa ambao wamewalipa mishahara hewa, hili ni tatizo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kinachonishangaza mimi ni kwa nini wakati Mheshimiwa Rais akihutubia Bunge hili aliposema pia kwamba ripoti za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, atazipa uzito unaostahili, mategemeo yangu mimi Rais na Mawaziri ni Serikali lakini uzito unapotolewa, taarifa inapotolewa lakini hakuna uzito wowote, mimi hilo napata mashaka na baadhi ya watendaji. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi kwa hili sishangai sana, wenzangu Waheshimiwa Wabunge ambao mmeingia mara hii nataka niwaambie tu kwamba ukiangalia mwaka 2006/2009 jumla ya Halmashauri 30 zilibainika na wizi, uzembe, ubadhirifu na ufisadi, watendaji 921 walipelekwa mahakamani, katika kipindi hicho cha kushangaza hakuna kilichofanyika. Hukumu iliyotolewa hailingani kabisa na jinsi ya fedha walivyoziiba. Watuhumiwa (watendaji) 14 walishushwa madaraka, hiyo ni aibu kubwa kwa Serikali, hivyo hiyo ni uhukumu? Mtendaji mmoja akapewa akashushwa cheo chake lakini pia vilevile akashushwa mshahara na mtendaji mmoja akapewa onyo akome kuiba ili akaibe zaidi sehemu nyingine, hiyo ni aibu kwa Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watendaji 921 sasa sisi tunapiga kelele sana muda huu hapa lakini mimi sishangai, kwa sababu ni jambo lililozoeleka kwa Serikali kuwalinda wanaochukua fedha, wabadhirifu hawa wezi na mafisadi ni jambo la kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili ni tatizo kubwa. Naomba niwakumbushe Wabunge wenzangu na hasa mliongea mara hii, ukiingia na ukiangalia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali mwaka 2006 mafisadi wamechukua shilingi bilioni 2.3, hakuna aliyekamatwa. Ripoti hiyo mwaka 2007/2008 kuna bilioni 3.5 wamechukua, hakuna

aliyekamatwa.  Mwaka 2008/2009 kuna bilioni 3.1 ikaendelea hivyo hivyo mpaka mwaka 2009/2010 bilioni 11.1 ripoti ambayo tumepewa juzi hii ubadhirifu na ufisadi ni bilioni 12.9 hakuna anayekamatwa. Lakini ukienda magereza walioiba kuku, mbuzi, ng'ombe wapo tele, hiyo ndiyo hali halisi ya Serikali. *(Makofi)*

Sasa Waheshimiwa Wabunge ambao mmeingia mara hii mie toka asubuhi nilikuwa nawasikiliza kwa makini sana baadhi yenu. Lakini nawaambieni hiyo ndiyo hali halisi, wale wezi, wabadhirifu, mafisadi wa kweli kweli nchi hii hawakamatwi na magerezani hawapo. Waliopo magerezani walioiba mbuzi, ng'ombe, kuku pamoja na mazao utawakuta kibao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ni aibu kwa Serikali, Serikali ikubali mapungufu yake, tunachosema sisi taarifa zikitolewa zifanyiwe kazi, maoni, ushauri na mapendekezo yanayotolewa na Waheshimiwa Wabunge, Serikali iyapitie, iwe na namna ya kuyafanyia kazi. Lakini kama kila siku tunakuja hapa tunatoa maelezo yetu kwa hisia zetu kali lakini Serikali inakaa kimya ni tatizo kubwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nawaambia, nawakumbusha kwamba hali hii tunayokwenda nayo ni jambo moja baya sana. Ninachosema Mheshimiwa Rais hivi karibuni alizungumza au alisema ni vyema tuandae utaratibu wa kuweza kuondoa/ kupunguza baadhi ya watu magerezani kwani zinatumika bilioni 18 kwa mwaka kuwalisha wafungwa. Ukiangalia mwaka 2001/2006, wezi, mafisadi, wabadhirifu wa mali ya umma wamechukua jumla shilingi 4,403,000,000/= na aibu kubwa kwa Serikali ilipoona angalau wanataka kuficha ficha baadhi ya ukweli Serikali ilikwenda mahakamani ikashitaki kesi 321, kati ya kesi hizo 321 ni aibu kubwa shilingi 4,403,000,000/= hakuna fedha iliyopatikana, tulipohoji Serikali hapa tukauliza tatizo ni nini wakasema fedha hizo hazikupatikana kwa sababu wahusika wametoroka, wengine wamefariki dunia. Hiyo ni aibu kwa Serikali, sasa wametoroka mmewatorosha? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wote basi Taarifa Rasmi ya Bunge *(Hansard)* angalieni Serikali tarehe 31 Januari, 2008 wanasema wamefariki dunia basi wote, shilingi 4,403,000,000/=! Sasa nyie Waheshimiwa Wabunge mkizungumza hapa, mimi naangalia haki ya Mungu mwaka 2001/2009 hali halisi ilivyo ndiyo hii hii wanaiba kweli kweli nchi hii wanaendelea kupeta tu na ushahidi wote upo ambao nautoa, ukiniambia nitoe ushahidi nitakwambia ninao majibu mmetupa Serikali, tatizo nini kwa Serikali?

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali haitaki kukubali ukweli kupokea maoni, ushauri na mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge juu ya ubadhirifu wa hao watu ambao wamechukua fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka niseme tu kwamba jambo hili ni baya sana na si vizuri hata kidogo Serikali kupunguza maoni ya mapendekezo ya Waheshimiwa Wabunge. Nataka niseme tu kwamba hali hii ambayo Serikali inaendelea kuwaachia baadhi ya mafisadi kuendelea kupeta katika nchi hii na baadhi ya wanyonge mkawaweka magerezani, kwa sababu wao tu hawana uwezo wowote wa kifedha ni jambo baya sana. Tunaelekea kubaya, kuna haja Serikali mkae kitako mjue hali halisi ilivyo, jinsi maisha ya wananchi yalivyo magumu, lakini maskini ya Mungu wale akinama ntilie vyakula vyao vinamwagwa, ni hatari sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hivi ni lini hii Serikali itasikia, tunasikia Serikali sikivu, tumesikia kilio chenu Waheshimiwa Wabunge, mambo yapo mbioni, michakato, tatizo ni nini kwa Serikali? Au jengo latudhuru, tubadilishe lingine tuelekeeni Kigamboni basi kama tunadhurika hapa na hamsikii, nashukuru sana. *(Makofi)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia, lakini vilevile

niwasihi Wabunge wenzangu tusilalamike, jukumu letu sisi ni kuisimamia Serikali. Pale ambapo tunaona Serikali haitekelezi kile ambacho tunaagiza, tuna jukumu la kutoa azimio na kufanya chochote ambacho tunataka kufanya kama Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, utaratibu wetu wa kulalamika, utaratibu wetu wa kunung'unika ndiyo unawajaza viburi Mawaziri waliokuwepo hapo mbele. Ndiyo maana Tanzania yetu imefika sasa kwamba mtu akiwa Mbunge, akichaguliwa kuwa Waziri anachowaza yeye ni kwenda kupiga *deal.* Baadhi ya Mawaziri wako hivyo, tumeona, tumemsikiliza Mheshimiwa Kangi Lugola, nimemsikiliza kwa makini nilikuwa ofisini, anazungumza kwa namna gani Mawaziri badala ya kwenda kutekeleza wajibu ambao Rais amewaamini, kumsaidia kuongoza hii nchi wanafanya mambo ndivyo sivyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo maana Wabunge wanalalamika, mimi hiki ni kipindi cha pili, Mheshimiwa Kafulila kasema kweli ukisoma *Hansard* mambo ambayo yanalalamikiwa leo ndiyo mambo ambayo tuliyajadili Bunge lililopita, Mawaziri wamejisahau. *(Makofi)*

Kuna baadhi wanafanya kazi, lakini kuna wengi wanadhani kwa kupewa Wizara, kupewa shangingi, kwa kupewa nafasi ya kusaini mikataba ni sehemu ya kupata pesa na majuzi nilisikitishwa sana kwa kuona kwa kiasi gani Mawaziri wetu hawako *serious.* Lilipoulizwa swali kuhusiana na mashamba kule Kapunga Mbarali, aliuliza Mbunge hapa kwamba jamani maeneo ya wananchi yamemwagiwa sumu na mwekezaji?

Mheshimiwa Naibu Spika, Naibu Waziri wa Kilimo anasimama hapo anatoa majibu kama vile hilo suala lilikuwa halijawahi kumfikia, kama vile hilo suala lilikuwa halijawahi kujadiliwa kwenye Vikao vya Bunge, kama hivyo hilo suala halijawahi kutolewa maazimio kufuatia taarifa ya Kamati ya

Hesabu za Mashirika ya Umma mwaka 2009 kuhusiana na suala la Kapunga. *(Makofi)*

Maeneo ya wananchi, eneo la wanakijiji linalokaribia hekta 1800 limechukuliwa na mwekezaji kwa kushirikiana na watu wa Serikali ambao siyo waaminifu kinyume na utaratibu. Kamati yetu ikasema kupitia Mwenyekiti wetu, alikuwa Zitto, Serikali ikaji-*commit* lakini utashangaa miaka miwili na nusu au mitatu baadaye Waziri amesahau, hajui kinachoendelea, anatoa ahadi mpya, ndiyo Mawaziri wetu, nchi itakwenda?

**MBUNGE FULANI:** Haiendi!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Haiwezi kwenda! Kwa hiyo, mimi nawaomba Wabunge wenzangu ifike kipindi hawa watu kwa sababu wanalipwa, mara Waziri akienda Jimboni kuna mambomambo huko, wanalipwa ili wafaye kazi za wananchi. Kama hawafanyi kazi za wananchi, tuna uwezo wa kuwazuia katika mazingira mbalimbali, mamlaka hayo tunayo. Tuache kulalamika, tukilalamika, wananchi waliotuchagua watatushangaa! Watashangaa kwamba Wabunge tumewapeleka wakaisimamie Serikali lakini wao wanageuka walalamikaji, wananchi wafanye nini? Tutekeleze wajibu! Naomba katika hili masuala ya itikadi tuweke pembeni, tunapojadili masuala ya msingi tuache kuangalia u-CCM, u-CUF, u-CHADEMA na u-TLP. Tukiamua kumwadhibu Waziri, tunamwadhibu kwani ni jukumu letu kufanya hivyo. Kwa hiyo, mimi naomba tuache kulalamika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili, Kamati ya Mashirika ya Umma imezungumzia masuala ya viwanda nadhani pia kwa sababu ya muda hawakuweza kupata nafasi ya kuzungumzia kwa kina taarifa ya ufuatiliaji wa mashamba na viwanda hasahasa mashamba kwa sababu viwanda wamei-*capture* vizuri sana shughuli ambayo imefanywa na *CHC*. Tumekuwa tukizungumza kwamba watu wezi, mafisadi na kadhalika lakini kuna taarifa huku zinatisha. Zinatisha kwa nini?

Kuna huyu mtu anaitwa Chavda sijui amekufa au yuko hai? Watu wa aina ya akina Chavda kama kweli wapo hai wanatakiwa wakamatwe kama wezi wengine. *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Wanyongwe!

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Wakamatwe na wanyongwe, kwa nini tunasema hivi? Taarifa hapa inamwonyesha Bwana Chavda katika mashamba makubwa matatu tofauti yenye ukubwa wa kati ya hekta 5000-6000, mashamba matatu tofauti kwa ajili ya dili zilezile ambazo Mawaziri tuliowapa ridhaa kipindi kile wakamuuzia eneo hilo kwa bei chee! Alichokifanya Bwana Chavda, akaenda kuchukua mkopo kwa mashamba yote matatu, baada ya kuchukua mkopo kwa dhamana ya shamba, mali ya Watanzania ambao wengi hawana ardhi akachikichia, shamba akalitelekeza, eti Serikali inasema inaangalia itamlipaje fidia mtu mwingine aliyeuziwa na Benki ya *CRDB* ambapo waliuza shamba lile kwa sababu lilitumika kama *security* ili eti atafutwe mwekezaji mwingine, lugha nyepesi kwa masuala mazito!

Mheshimiwa Naibu Spika, tumetoka Arumeru, ardhi Tanzania itatumwagisha damu baadaye, kila unapokwenda ni mgogoro wa ardhi. Akija mgeni, Waswahili tuna msemo usemao `mgeni njoo mwenyeji apone'. Tanzania akija mgeni kwenye suala la ardhi, msemo unakuwa `mgeni njoo mwenyeji asulubike'. Leo Mtanzania wa kawaida ni vigumu kupata hekari moja ya ardhi, wanaishia kuwa wavamizi, lakini kuna wajanja wachache, wenye fedha, wanaojua kula na viongozi Serikalini, wanapewa maeneo chee, hawayaendelezi na Serikali ina-*incur* gharama mara mbili, hatuoni haya?

Waheshimiwa Wabunge, mimi naomba, hawa watu sisi ni vijana, watoto na wajukuu zetu sisi tutawaachia nini? Hawa watu wazima wanatuangusha, inawezekana wanaona *future* yao miaka 10 mbele wameshakatika, sisi tuna miaka 30 au 40 mbele mnataka mtuachie nini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa dhati, Bunge tuna meno, haiwezekani mashamba 14 makubwa yenye ukubwa kati ya hekta 4000-5000 watu wamechukua, wameyatelekeza halafu Serikali haichukui hatua, inabembelezana nao, kama ninyi siyo wadau, kwa nini hamchui hatua? Kwa hiyo, naomba sheria ichukue mkondo wake, tunavyohukumu mafisadi wengine na hawa ni mafisadi vilevile kama wanashindwa kusimamia mali za Watanzania. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, suala lingine ni la *TBS*, ninasikitika majibu ya Mawaziri na ni kwa mtindo huohuo wa masuala ya ardhi. Hapa kuna *report* ya *CAG,* anasema makampuni yamepewa kinyume na utaratibu, makampuni hayana vifaa, makampuni hayalipi tozo kwa *TBS* lakini bado wanarudiwa kupewa mikataba, eti Waziri anasimama hapa anatoa majibu mepesi, Waziri anasimama hapa anaongea lugha nyepesi, wataalamu wanashauri hii kampuni haifai kupewa kazi hii kwani haina uwezo, lakini wanalindwa. Kwa hiyo, mimi naomba Wabunge tusimame, tumechoka kulalama, msilalame kwani wananchi watawarushia mawe.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Halima Mdee na sasa ni Mheshimiwa Esther Matiko atafutiwa na Mheshimiwa Godfrey Zambi.

**MHE. ESTHER N. MATIKO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipatia nafasi hii ili niweze kuchangia kwenye hoja ya Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kweli inafedhehesha sana na huwa wakati mwingine nakaa najiuliza, kabla sijaingia Bungeni nilikuwa nikiwasikia mnaweka mijadala kuhusu mikataba mbalimbali mibovu inavyoingiwa kama ya *Dowans*,

*TRL* na mingine. Wakati mwingine nilikuwa siwaamini Wabunge, lakini nimeingia Bungeni na kwa bahati nzuri au mbaya nikaingia kwenye Kamati ya Hesabu za Mashirika ya Umma, huko nayaona makubwa yaani yananizidi umri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna siku nilikuwa nachangia nikasema, kipindi ambacho tulikuwa tunapitisha sheria kuhusu ununuzi wa vitu vilivyotumika. Nilisema tatizo kuna watendaji Serikalini na kwenye mashirika ya umma kwa ujumla siyo waadilifu, wengi waliguna. Watendaji unakuta wana maslahi binafsi na siyo maslahi ya taifa hili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitajikita katika uingiaji wa mkataba kwenye suala la Shirika la Ndege la *ATCL*. Taarifa ya *report* ya Mashirika ya Umma imebainisha kabisa kwamba *ATCL,* watendaji wake kwa kupitia pia na Wizara husika ya Miundombinu kwa wakati huo na pia nafikiri na Waziri wa Fedha alihusika, waliamua kukodi ndege ya *Air Bus 420214* lakini kabla haijakodiwa ndege hii kuna fedha za walipa kodi zilitumika kuwaweka wataalamu kuchunguza kama ndege hii inafaa au haifai.

Mheshimiwa Naibu Spika, wataalamu wakasema ndege hiyo haifai kwa sababu ikikodishwa tu itafanya kazi kwa miezi sita na itawajibika kwenda kutengenezwa matengenezo makubwa. Watendaji hawa na wengine wote ambao walikuwa wanahusika kwa sababu walitanguliza maslahi binafsi wakaendelea na kukodisha ndege ile. Ndege imekodishwa, imekuja Tanzania, imefanya kazi miezi sita ikaenda kutengenezwa Ufaransa, mpaka tunavyoongea ndege iko Ufaransa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchakato wenyewe una utata, mchakato wa kukodisha ndege hii umeingiwa mwezi Oktoba, 2007, Waziri mwenye dhamana ya kutoa mikopo ametoa dhamana mwezi Mei mwaka 2008 kinyume kabisa na sheria inavyosema ya utoaji wa mikopo Serikalini ya mwaka 1974.

Hiyo haijatosha, wamekiuka hii mikataba, ndege imekuja, imefanya kazi miezi sita imekwenda Ufaransa mpaka leo, tumeambiwa kwenye taarifa kwamba gharama sasa hivi ni shilingi bilioni 108 ambayo tunadaiwa na kampuni ya Lebanon kwa ile dhamana ambayo Serikali iliweka, ina maana Serikali yetu ndiyo itawajibika kutoa fedha hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna gharama ya matengenezo ambayo Wafaransa wanatudai ambayo ni takribani shilingi bilioni tano (5), kwa sababu ni dola za Kimarekeni milioni tano (3). Sasa mimi najiuliza maana siyo tu tunapata hasara kwa ndege kukaa Ufaransa bali Taifa linapata hasara kwa kuendelea kulipa fedha ambayo mpaka miaka sita (6) ya kukodishwa ndege hii iishe labda tungekuwa na uwezo wa kununua ndege mpya kabisa ya *Airbus* tena siyo kukodisha kwa sababu baada ya muda itakuwa tena siyo shilingi bilioni 108 bali itakuwa zaidi ya hapo na kwa uelewa wangu mdogo tu ndege aina ya *Airbus* kama tuliyokodi na *brand new* siyo zaidi ya dola bilioni 200.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi huwa najiuliza Serikalini huku tuna washauri kweli au tu ni *object* imekaa pale hata haiwazi wala haifikirii? Mimi nasikia uchungu, Mheshimiwa Magdalena amesema wapigwe risasi lakini mimi natamani sijui wapewe adhabu ipi ambayo wanakufa ndani ya nusu saa yaani wasikie maumivu kila dakika. Inaumiza sana. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kwa sababu Kamati yangu ilipendekeza katika ukurasa namba 46 kuhusiana na Shirika la Ndege la Tanzania, naomba kurekebisha mapendekezo yale kwa sababu Kamati ilipendekeza kwamba *management* ichukuliwe hatua, lakini hii siyo kazi ya *Management* tu bali na Mawaziri husika wa kipindi hicho nao waingizwe katika suala hili kwa sababu ili dhamana itolewe Waziri wa Miundombinu, sasa hivi ni Waziri wa Uchukuzi mwaka 2007/2008 ilikuwa ni Wizara ya Miundombinu, lazima amwombe dhamana Waziri wa Fedha na Waziri wa Fedha naye ili atoe

dhamana inatakiwa awe amechunguza hayo yote na inaniuma zaidi kwamba wataalamu walikataa lakini wenyewe wakaenda. Kwa hiyo, naomba mapendekezo yasomeke kama hivi:-

"Bunge liunde Kamati Teule ya kuchunguza mchakato mzima wa ukodishwaji wa ndege hii aina ya *Airbus*".

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba iandikwe hivyo, mapendekezo nayatoa, mkiona yanafaa yachukuliwe lakini kiukweli, naomba Bunge lako Tukufu liunde Kamati Teule ituambie ni nini kipo nyuma ya pazia kwenye mchakato mzima wa kukodisha ndege ya *ATCL,* vinginevyo tutakuwa tunalia kila siku, fedha za walipa kodi zinachukuliwa, wachache wanakula na Tanzania tunabaki kuwa kichwa cha mwenda wazimu. Hizo fedha ambazo zimetumika na ambazo zinaendelea kuingiza hasara, zingeweza kufanya maendeleo mazuri tu kwenye nchi yetu ambapo leo hii tunavyoongea shule nyingi hazina madawati, tangu miaka ya 1984 mimi nasoma, mtoto wa Matiko nakaa chini kwenye vumbi mpaka leo mwaka 2012 watoto wanaandikia chini, hakuna madawati, haya ma-*billions* ya fedha yangeweza kununua madawati, watoto wetu wakapata elimu iliyo bora na siyo bora elimu. Hawa watendaji wachukuliwe hatua inavyotakiwa, hii itakuwa ni funzo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba pia nizungumzie kuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Manunuzi ya Umma kwa ufupi kabisa. Tumekuwa tukiongelea suala hili siyo tu kwa Mashirika ya Umma, naona kuna ubadhirifu mkubwa hata kwenye ngazi za Halmashauri. Muda ni mfinyu sana lakini kama wenzangu walivyotangulia kulalamika, inabidi tuwe tunapewa muda mrefu ili tuweze kuzichambua ripoti zote tatu maana zinatumia fedha za Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia katika Mashirika ya Umma, aidha kwa makusudi au labda tunakuwa tunachagua watendaji ambao hawana weledi wa hiyo fani, ukiukwaji ni

mkubwa sana na ukiuliza sababu wanazokupa hazina msingi. Kwa maoni yangu, naona inakuwa ni mwanya tu wa watendaji kama ninavyoendelea kuamini mpaka ambapo watakaponiaminisha kuwa ndivyo sivyo, wanatumia mwanya ule kujinufaisha wao, sheria zinawekwa lakini hazifuatwi, msemo wa Mheshimiwa Halima Mdee tunabaki tunaendelea kulalamika, hatuchukui hatua, mapendekezo yanaandikwa hayafuatiliwi, ikija mwakani tena tunaongeza idadi ya mapendekezo lakini hayafuatiliwi. Sasa tunaomba sana sheria zifuatwe na watendaji ambao hawafanyi inavyotakiwa wachukuliwe hatua na siyo kusubiri Wabunge waje waongee Bungeni ndiyo mchukue hatua. Tunajua kabisa kila mtendaji ana bosi wake ambaye anawajibika kwake, wachukulieni hatua na wataogopa, msikumbatiane, tuache kabisa na tuwe wazalendo, inauma! Mkiona vijana hapa tunasimama tunalalamika, tunaumia, tunahisi basi labda ninyi mnatunyanyapaa kwa sababu mmeshaishi vya kutosha na mnaona labda fedha mlizopata zitawapeleka kidogo mbele hamuangalii kizazi ambacho kiko nyuma yenu, tunaomba kabisa, mmpewa dhamana, fanyeni kazi vilivyo ili tupate Tanzania yenye neema.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Esther Matiko na sasa tunahamia CCM, Mheshimiwa Godfrey Zambi, atafuatiwa na Mheshimiwa Ally Keissy Mohamed.

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nami pia nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kuchangia taarifa zilizotolewa na Wenyeviti wa Kamati zinazosimamia hesabu za Serikali Kuu, Mashirika ya Umma na Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Mwenyekiti, naomba nisitofautiane na wenzangu wote waliozungumza, hali ya Serikali yetu kwa ujumla kwa matumizi ya fedha ni mbaya na wengine wanafika mahali wanasema kwamba Serikali hii kwa sasa, hasa kwenye

matumizi ya fedha, imebaki kuwa kama Shamba la Bibi, ndiyo ni kama Shamba la Bibi maana Bibi akiwa na shamba lake hata wezi wakiingia hana nguvu za kuwafukuza, ndiyo ilivyobaki Serikali yetu sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nasema hivyo kwa sababu taarifa hizi zote Waheshimiwa Wabunge mmezisikia na wala Serikali wasiseme hapa tunawaonea, tunasema kweli. Kila Mwenyekiti aliyesimama amelalamikia matumizi mabaya ya fedha za Serikali, hivi mimi nashangaa kuna sababu gani ya kuunda ofisi kubwa ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali, anatumia pesa nyingi kwa ajili ya kufanya ukaguzi wa hesabu za Serikali za Mitaa, *POAC* na Serikali Kuu na anakwenda mpaka Balozi za nje, wanatumia fedha nyingi sana na wanatoa taarifa nzuri sana ambazo zina mapendekezo, zinaletwa hapa Bungeni zinakaliwa, hazifanyiwi kazi yoyote, ina maana gani ya kuendelea kuwa na ofisi ya *CAG*? Mimi nadhani tuifute tu maana kwa kufanya hivi tunamkatisha tamaa *CAG* katika kufanya kazi hii. Siyo tu tunamkatisha tamaa lakini pia ni matumizi mbaya ya fedha za walalahoi wananchi wa Tanzania kwa sababu ni kodi zao ambazo zinafanya ofisi ya *CAG* waende kufanya kazi hii nzuri wanayofanya ambayo kazi yenyewe hiyo Serikali haitaki kuipa umuhimu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nadhani Mheshimiwa Rais kama anatusikia, ana sababu ya kufanya mabadiliko makubwa tu ndani ya Serikali yake maana kwa mwendo huu hatuwezi kufika lakini pia Serikali ya Chama cha Mapinduzi ijue kwamba hii ni *advantage* kwa Vyama vya Upinzani, maana tunafanya makosa, wanakwenda kwa wananchi kwenye uchaguzi wanayasema hayahaya na wananchi watayasikia. Maana Serikali inaacha kuhangaika na watendaji, wamenyamaza, limebaki Shamba la Bibi kama nilivyosema na Mwenyekiti wangu Mheshimiwa Mrema asubuhi kwamba nchi hii itajengwa na wenye moyo na itaendelea kuliwa na wenye

meno, ndiyo hivyo sasa hivi tunavyoendelea katika nchi hii, ndivyo ilivyo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano Kitabu cha Hesabu Kuu ambacho kimesomwa na Mheshimiwa Cheyo asubuhi, matumizi ya fedha ambayo na wenzangu wamezungumzia katika ukurasa wa 15, matumizi mabaya ya fedha za Serikali ni shilingi 50,685,371,565.58. Sasa mimi nashangaa kama kuna Idara ambazo zimetumia fedha hizi vibaya Wakuu wa Idara hizo, Mawaziri wa Wizara hizo wanafanya nini mpaka sasa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo! Maana Mheshimiwa Rais aliwaambia Mawaziri msilalamike, ninyi ndiyo viongozi wa Wizara, mnalalamika nini? Maana kama kuna ubadhirifu wa fedha, Mawaziri hamjachukua hatua, maana yake ni kwamba mmeshindwa! Muungwana kama umeshindwa kazi unaondoka mwenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niwashauri Wabunge wa Chama cha Mapinduzi, twendeni kwenye *party caucus* tukafanye maamuzi, maana hatuwezi kufanya maamuzi ndani ya Bunge. Twendeni kule tukafanye maamuzi, maana Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi inatutia aibu sasa, inatia aibu. Serikali yetu inatuponza kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaeleze mambo machache. Mwaka jana kule kwangu Mbozi, Serikali imeshindwa kuwapa wananchi mbolea kwa wakati, mwezi wa tatu ndiyo wanaleta mbolea. Mbolea gani unapandia kule Mbozi na Mkoa wa Mbeya kwa wanaoujua mwezi wa tatu? Hata wale wachache waliopeleka vocha, Serikali mpaka sasa hivi haijawalipa fedha. Tunarudia makosa ya mwaka jana, tuna Serikali hapo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kule Mbozi, Idara ya Kilimo imechimba mabwawa hewa kwa shilingi milioni 720,

tunaiambia Serikali wanasuasua kwenda kuchukua hatua. Mkurugenzi anachofanya sasa ni kuhamisha wale ambao inawezekana labda walifanya haya makosa, tutakwenda jamani?

**MBUNGE FULANI:** Hatuwezi kwenda!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Hatuwezi kwenda!

Mheshimiwa Naibu Spika, ngoja niwaambie, Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Hesabu za Serikali, alifanya *Special Audit* Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Niwaambie yaliyokutwa pale, shilingi bilioni sita zimetafunwa na watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kishapu. Niwaambie matumizi mabaya yalivyo kwa ufupi sana. Kughushi kwa salio katika akaunti – shilingi milioni 235; hundi zilizoghushiwa na kulipwa zaidi ya vibutu katika akaunti za *CHC* Maendeleo, *EGPF*, *TACAIDS* na *DASP* - shilingi milioni 500; Fedha zilizohamishwa bila idhini ya Mkurugenzi na kutumika kinyume na malengo - shilingi bilioni 1.6; uhamisho wa fedha ambazo hazikufika kwenye akaunti husika - shilingi bilioni 1.9; uhamisho wa fedha kwenye akaunti zisizofahamika – shilingi milioni 452; malipo yaliyofanyika kwa walipwaji wasiofahamika - shilingi milioni 689; fedha ambazo hazikuhamishwa kutoka akaunti ya maendeleo kwenda akaunti ya maji – shilingi milioni 88; matumizi yaliyofanywa kinyume na malengo katika akaunti ya maji – shilingi milioni 338; fedha ambazo hazikuhamishwa kutoka akaunti ya maendeleo kwenda akaunti ya Mfuko wa Afya wa Pamoja – shilingi milioni 244; fedha ambazo hazikuhamishwa kutoka akaunti ya maendeleo kwenda akaunti ya TACAIDS - shilingi milioni 53 na matumizi ya fedha ya Mfuko wa Afya ya Jamii *(CHF)* yasiyoidhinishwa - shilingi milioni 126. Jumla yake ni shilingi bilioni 6.7, hawa Wakurugenzi hawa wamefanya makosa haya kati ya mwaka 2007 na 2008 mpaka leo wapo kazini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hizi Kamati za Bunge, mimi nadhani tunapoteza muda tu, ni kama tunafanya mchezo wa kuigiza. Watu wamezungumza mambo mazito hapa, lakini hamna kazi yoyote inayoendelea kufanyika!

Mheshimiwa Naibu Spika, Halmashauri zote ambazo tumeenda kuzikagua zina madudu, hakuna Halmashauri iliyo salama kabisa, hamna! Bajeti ya Serikali zaidi ya asilimia 60 – 65 yote inaenda kutumika kwenye Halmashauri zetu katika nchi hii. Sasa kama Halmashauri moja inaweza ikawa na matumizi mabaya ya shilingi bilioni sita, hii ni hatari!

Mheshimiwa Naibu Spika, kulifanyika *Special Audit* kule Rombo, kuna madudu kwelikweli, bado watumishi wengine Rombo wako kazini mpaka leo. Kumefanyika *Special Audit* Kilosa, mtumishi mmoja ambaye ametumia fedha vibaya amehamishiwa Halmashauri ya Lindi pale, wapo kazini. Tumemwita Mheshimiwa Waziri Mkuchika na mambo mengine haya tulimpa lakini bado mpaka leo anakwambia Serikali inayafanya uchunguzi. Sasa *CAG* mmemuweka wa nini kama Serikali inafanya uchunguzi? Eeh, *CAG* anafanya kazi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ni lazima tuangalie na utaratibu pia wa vyombo vyetu mbalimbali vinavyohusika katika nchi hii. Mimi nadhani kuna *syndicate* ya ulaji wa fedha za Serikali. Iko hujuma, lakini nataka niitahadharishe Serikali yangu ya Chama cha Mapinduzi, Vyama Vingi ambavyo vilizipatia nchi zao uhuru leo havipo madarakani, wananchi wamechoka. Wananchi wanachoka, halafu tunapokuja Bungeni tunakuja na *statements* rahisirahisi tu. Mimi sitashangaa kama tunaenda kwenye uchaguzi mwaka 2015 tukashindwa, siwezi kushangaa hata kidogo! *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaona uchungu Serikali yangu imeshindwa lakini ndiyo uzembe huu wa Serikali tunaouzungumza Wabunge kila siku, *business as usual*, watu

wanaendelea na maisha. Kama walivyosema wenzangu, mara nyingi watu ambao wameiba shilingi kumi, wameiba vitu vidogodogo, hawa ndiyo wanashughulikiwa kweli, wale mafisadi wa dhati hakuna, hawaguswi. Hawaguswi hawa maana hawa ni *untouchables*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kwa utaratibu huu, Serikali ya Chama cha Mapinduzi, tukishinda mwaka 2015 tumshukuru Mungu. Lakini tukishinda mwaka 2015, mwaka 2020 kama *business as usual* sijui kama tutakwenda. Naomba niisihi Serikali hii ifanye kazi lakini Mawaziri ambao wameshindwa kusimamia Wizara zao, naomba nirejee taarifa hii ya Kamati ya Hesabu za Serikali, matumizi mabaya ya hesabu za Serikali, Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali walisema wenzangu shilingi bilioni 49 matumizi mabaya na yasiyoeleweka ya fedha za Serikali. Shilingi bilioni 49 na hii ndiyo Idara ya Mhasibu Mkuu wa Hesabu za Serikali, hivi huyu Mhasibu wa Hesabu za Serikali mpaka leo yuko ofsini? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka leo yuko ofisini huyu? Serikali inafanya uchunguzi, inafanya utafiti, baadaye watatwambia mchakato unaendelea wa kuangalia kama ana makosa au hana makosa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi, shilingi milioni 320 watu wako kazini. Sekretarieti ya Mkoa wa Mwanza, shilingi milioni 54, Wizara yenyewe ya Fedha ya Mheshimiwa Mkulo anayetutunzia fedha zetu, shilingi milioni 373 bado na wao wako ofisini. Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Kimataifa shilingi milioni 212 na pointi, Tume ya Kudhibiti Dawa shilingi milioni 40, Idara ya Magereza shilingi milioni 358, jamani hii nchi kweli ipo hivi? Nchi ipo kweli hapa?

**WABUNGE FULANI:** Haipo!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Hatuwezi kwenda!

**WABUNGE FULANI:** Hamna!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mimi nadhani tunapoisema na kuikosoa Serikali ya Chama cha Mapinduzi, ichukue hatua. Mimi nasikitika, alisema Mheshimiwa Nassari hapa kwamba anasikitika Waziri wa Fedha ambaye tunapaswa tumseme hapa Bunge ayasikie haya, hayupo, Waziri Mkuu ambaye anatakiwa aone namna ambavyo Serikali yake inasemwa hapa mbele, hayupo! *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niseme jambo la mwisho…

**NAIBU SPIKA:** Ya pili tayari!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Ya pili!

**NAIBU SPIKA:** Eeh, tayari!

**MHE. GODFREY W. ZAMBI:** Aah, haya ahsante bwana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Godfrey Zambi. Mheshimiwa Ally Keissy atafuatiwa na Mheshimiwa Amina Amour.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru na mimi kupata nafasi ya kuchangia maneno mawili, matatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kabisa, mimi nilizungumza mapema kabisa kwamba, hizi hotuba zote zirekodiwe, akae mwenyewe Rais Kikwete na Waziri Mkuu na

wasaidizi wake, kwa muda wasikilize maoni ya Wabunge wote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pili, namwomba Rais aondoe upole, kama yuko Brazil au wapi, anasikia, upole umemzidi, aache upole. TAKUKURU haina kazi katika nchi hii, wanakula mshahara wa bure. Ije hapa ajenda kabisa, tuache taasisi ya TAKUKURU, kwa sababu tunalazimisha TAKUKURU lakini hawana faida yoyote, wanakamata wezi wa kuku, papa hata mmoja hajakamatwa, sangara hata mmoja hajakamatwa, ni vidagaadagaa tu ndivyo vinakamatwa. TAKUKURU haina faida ndugu zangu, wanakula mshahara bure. TAKUKURU wenyewe wanakula rushwa, matumbo yao yako mbele kama wengine. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hili Shirika la *TBS* linalindwa na Waziri, Naibu Waziri na Katibu Mkuu wa Wizara. Wanaingiza mbolea feki, wanaua wakulima wetu. Mbolea feki, *trip* zaidi ya nane zimeingia katika nchi hii, wamekubali kuziuza. Mafuta mengi hayana kiwango, *oil* feki, Waziri anamtetea Mkurugenzi wa *TBS*, huyu Waziri anafaa? Katibu Mkuu anafaa? Hawafai waondolewe mara moja! Walipigiwa kura Majimboni kwao, wao ni Wabunge kama sisi bwana. Hakuna Waziri aliyesomea hapa wala hakuna cheo cha Waziri, yeyote anaweza kuwa Waziri akafanya kazi. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilizungumza tangu mwanzo kwamba, Makatibu Wakuu ndiyo wakorofi. Ndugu zangu Serikali hii wanasema ni maskini wakati ni tajiri. Misafara ya viongozi ndugu zangu mtashangaa, gari 40, gari 50. Kwa macho yangu nimeona mimi Kiongozi anakwenda na msafara kama ilivyo katika nchi za Kifalme za Kiarabu zenye kuchimba mafuta, hamuwaonei wanachi huruma? Msafara gari 40, gari 50 mnakwenda wapi? Unamtisha nani nchi hii? Nani hajaona gari hapa? Nani hajaona gari? Unamtisha mtu wa kijijini unakwenda na msafara wa gari 40 au gari 60 wakati wananchi hawana fedha ya kula, dawa hakuna! *(Makofi)*

**MBUNGE FULANI:** Keissy sema Mheshimiwa!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Tunakuja kuripoti, leo watumishi wa Halmashauri wana fedha kuliko Halmashauri. Mtumishi wa Halmashauri, mfagiaji, mtu mdogo, ana fedha kuliko Serikali ya Halmashauri yake, ametoa wapi fedha hizo? TAKUKURU iko pale mbele ya mlango wake. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watumishi wamekuwa na fedha kuliko Serikali. Leo wanaiendesha Serikali kwa fedha zao, fedha za wananchi! Ndiyo maana kila siku hapa kila kitu ni rushwa, chaguzi ndogondogo rushwa, chaguzi kubwa kubwa rushwa kwa sababu wafanyakazi wanachukua kodi ya wananchi. Ndugu zangu tunakwenda kubaya. Angalieni nchi zingine wamepigana mapanga kwa ajili hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi niko Kamati ya *PAC*, siku moja nilikunywa dawa za usingizi, nilichanganyikiwa, kila Wizara ikija mamilioni ya fedha yamechezewa, kila Wizara, mamilioni ya fedha yamechezewa, nikamwambia Mwenyekiti wangu Mzee Mapesa, mimi leo nimechanganyikiwa naenda kulala mapema. Hii Serikali inakwenda kubaya tena kwenye shimo la kuteleza. *(Makofi/Vicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nchi yenye neema, ina sukari na asali lakini mnaipeleka kubaya. Leo ilikuwa tusaidie nchi inayofilisika kama Ugiriki, tungeenda kuikopesha. Nimeuliza hivi kabla ya uhuru mlikuwa mnategemea misaada kutoka Ulaya ili kuendeleza nchi? Si mnaona nchi ilikuwa inaendelea bila misaada ya Wazungu! Baada ya uhuru tu madeni, madeni, leo ni shilingi trilioni 14 tutazitoa wapi sisi hizi? Kila Mtanzania hata mtoto mdogo anadaiwa shilingi milioni 350 tukizigawa nani atalipa? Wajukuu na kila mtu, anadaiwa shilingi milioni 350, tutatoa wapi fedha sisi? Mmekula nyie tukalipe sisi! *(Makofi/Vicheko)*

**MBUNGE FULANI:** Mawaziri!

**MBUNGE FULANI:** Waondoke Mawaziri.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu misamaha ya kodi, uuzaji wa mashamba, naomba mikataba yote irudiwe upya. Mtu anauziwa shamba ekari 16,000 kwa shilingi milioni mbili au tatu, shamba lenye likiwa na majengo chungu nzima mle ndani, mna kila kitu lakini mtu anauziwa kwa shilingi milioni mbili au tatu tena bila kutangaza. Leo watumishi wa Halmashauri wanachukua fedha kutoka kwa wananchi bila risiti, hawaweki nakala chini. Kama Mbunge ninatoa ripoti kwamba, huyu mwizi, kaiba. Nimetoa ripoti mimi mpaka barua kwa Makamu wa Rais, *PCCB*, mfanyakazi badala ya kutumia mafuta ya petroli lita 450 kaandika lita 4500, nimetoa ripoti lakini hakuna hatua inayochukuliwa na leo nimepigiwa simu asubuhi kwamba anakwenda kukusanya fedha kule vijijini, kuchukua fedha za wavuvi, kuiba. Hii Serikali inakwenda wapi? Mtu anaiba mafuta, nimepeleka ripoti na barua sehemu 15, lakini hachukuliwi hatua, bado mtumishi yule yuko kazini na anatamba, mtamfanya nini? *PCCB* iko mbele ya macho yake, wanakula naye pamoja? Ndugu zangu tuangalie tunakokwenda, waoneeni huruma wananchi vijijini. Hawana barabara, hawana dawa, hawana kila kitu, wanakula mlo mmoja kwa siku lakini nyie hapa mnakula milo mitatu mpaka vyakula vinabaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, huu utaratibu wa magari kukaguliwa nje ndugu zangu mnakosesha Watanzania kazi. Watanzania wanakagua kule nje wakati magari yamejaa hapa? Ati wanasema magari yana mionzi ya nyuklia, si unafiki, si uongo huu? Mmeyachezea tangu mwaka 2002 mpaka leo shilingi bilioni 25 zimekwenda kwa Mawakala nje, zingesaidia vijana wa Tanzania wenye gereji hapa na wangeokoa magari. Kuna mafundi wazuri hapa katika nchi yetu, mnaenda kuwapa watu kazi huko *certificates* wanatoa barabarani, wala hawakagui gari lolote. Leo Katibu Mkuu anamsaidia

Mkurugenzi eti acha afanye kazi yake. Nawaambia mbaya siyo Mkurugenzi wa *TBS*, bali ni Katibu Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara. Nasema Serikali iwachunguze mali zao. Huyu Katibu Mkuu, Wizara ya Viwanda na Biashara, wamchunguze mali zake ili kwanza waone kama ni halali, kuanzia kijijini kwake, kwa mjomba wake, shangazi yake, dada yake! *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi naunga mkono lije Azimio hapa Bungeni, wezi wote, mafisadi wote tuwanyonge. Mnaleta Miswada ya ajabu ajabu tunapoteza muda hapa sisi! Leteni Miswada ya maana kuokoa nchi. Tukinyonga watu 10 hapa, wataogopa. Leteni Muswada hapa kwamba mwizi yeyote wa mali ya umma, bora uniibie fedha zangu mfukoni kuliko fedha za watu wengine, unaiba mpaka za maskini kipofu. Kwa hiyo, Muswada uletwe hapa, tulete Sheria mwizi yeyote wa mali ya umma anyongwe na mali yake irudishwe kwenye Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, watu wengine wanatuona sisi kama tumekuja kucheza Bungeni. Niliwaambia ndugu zangu Wabunge hapa mkiwapigia watu makofi mnaharibu, niliwaambia hili Bunge si la kupigiana makofi, hili ni Bunge la kazi na kazi ionekane. Tuchunguzane wenye kupata mali kinyume cha sheria, tutaokoa nchi yetu. Nchi ina deni la shilingi trilioni 14, sisi tunacheka badala ya kulia? Hizo fedha mlizokopa nyie Ulaya zimefanya kazi gani katika nchi yetu hii? Tuonesheni wapi zilikwenda, kama zingine hazikubaki kule kule Ulaya kwa faida yenu na watoto wenu. Kwa hiyo, nawaomba ndugu zangu kitu kimoja, tulete sheria hapa, tuchunguzane aliyepata mali kinyume cha sheria anyongwe na tutaifishe mali yake iwe ya Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Naibu Spika, mnasema watumishi hewa, watumishi hewa wako Kiwira, wamekaa pale hakuna kinachofanyika ni watumishi hewa. Shirika la Ndege lina watumishi kuliko idadi ya ndege, ni watumishi hewa. Wanakula fedha za wananchi, watumishi hewa hao. Shirika la Reli wako

watumishi hewa, treni haziendi Kigoma, haziendi Mwanza, watumishi hewa wanakula mishahara yetu. Lazima twende kwa wakati, tuwe na wafanyakazi watakaofanya kazi kwa kiasi kinachotakiwa na walipwe kwa jasho lao. Mmeweka wafanyakazi 800 Kiwira na Serikali inapeleka fedha kila mwezi lakini hakuna kinachozalishwa pale Kiwira na watu hawachukuliwi hatua. Hamna kuoneana haya, nimesoma naye nampa kazi huyu, hakuna hapa. Kwa sababu nilisoma na huyu bwana, nampa kazi huyu kwa sababu nimesoma na fulani, mtoto wa shangazi, mtoto wa baba, hakuna na sheria ifuate mkondo wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii hotuba tunayotoa hapa mjifungie ndani Mawaziri, Makatibu wenu, Rais na Waziri Mkuu msikilize kilio cha wananchi. Sisi tumechaguliwa na wananchi kama mlivyochaguliwa nyie. Hatukuja hapa kuushangaa Mji wa Dodoma bwana, hatukuja kukaa Dodoma hapa. Mnatuletea mpaka mbolea feki, mnapeleka mbolea feki kule Nkasi, wakulima hawapati mahindi. Kusema kweli huyu bwana achukuliwe hatua za kinidhamu, ikiwezekana tumnyonge hata kesho Jumanne, sijui Jumatano. *(Makofi/kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, haya Serikali maskini ndugu zangu lakini inakwenda kudhamini watu mpaka asilimia 150. Serikali mtu anakuja na *briefcase* unamdhamini wakati wewe mwenyewe huna fedha, fedha ni za Wazungu. Hii ni Serikali kweli, unamdhamini mtu asilimia 150? Leo waliodhaminiwa wote hawana fedha za kulipa wameshafilisika, mtadai nini, trilioni tatu mmedhamini watu? Serikali ina uchungu na watu wake! Ni Mbunge gani amedhaminiwa? Mtu anakuja na *briefcase* unamdhamini, eti mwekezaji. Mwekezaji aje na fedha zake bwana. Unakwenda kudhamini watu wanakuja na *briefcases*, shilingi trilioni tatu za nchi yetu wakati nyie wenyewe mnadaiwa shilingi trilioni 14. Ndugu zangu Wabunge tuwe wakali, sasa hakuna Bunge la mchezomchezo kuchezeanachezeana hapa, watu wanaliwa fedha wakati wananchi wa vijijini hawana huduma zozote. Tangu bajeti

hakuna fedha ambayo imekwenda kwenye Wilaya kusaidia maendeleo. Mimi Jimbo langu tangu nimepata Ubunge hamna hata kisima cha maji ambacho kimechimbwa wala kukarabatiwa.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa!

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Ally Keissy.

**MHE. AMINA ABDALLAH AMOUR:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, mimi pia nitagusia kidogo matumizi mabaya ya fedha za umma. Matumizi mabaya ya fedha za umma hudumaza maendeleo. Wengi walizungumzia hapa kuhusu mishahara hewa, mimi pia nitagusia kidogo halafu niwakumbushe jambo moja. Mishahara hewa tulipiga kelele kikao kilichopita lakini alikuja Waziri hapa akatoa kauli yake akasema ni mwisho tena kuonekana mishahara hewa. Ameshaunda Kamati ambayo itashughulikia kubaini wafanyakazi hewa wote nchi nzima kwa siku moja. Nataka kumuuliza Waziri, je, hiyo siku haijafika au lini atafanya kazi hiyo? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tulijaribu kumwuliza siku gani, akasema siku hiyo itakuwa ni siri, ni mapema mno kutuambia wakati ule lakini alisema siku hiyo moja yeye na wataalamu wake tayari watabaini kila aliyekuwa mfanyakazi hewa na atatolewa kabla ya bajeti inayokuja. Sasa namwuliza Waziri tumebakia na miezi minne jambo hilo mpaka leo hajalifanya,

atalifanya lini? Hayupo hapa, lakini yupo Naibu wake atampelekea salamu. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kiwango cha misamaha ya kodi holela. Kiwango cha misamaha ya kodi holela imefikia asilimia 18 ya mapato ya nchi. Kwa nchi za wenzetu kama Kenya mpaka sasa ni asilimia 11 na haizidi hapo. Sisi tumeshafika asilimia 18 na huwa tunasema tunataka tupate wawekezaji wengi lakini tukitazama Kenya wana wawekezaji wengi kuliko sisi. Sasa mimi naiomba Serikali kwa suala la misamaha ya kodi iongee na wale wote waliotakiwa kupewa misamaha hiyo, nashauri wasisamehewe, ifutwe kabisa bila kujali mikataba iliyowekwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia nachangia habari ya Halmashauri. Kuna udanganyifu unaofanywa na Halmashauri, hiyo *CAG* amesema wakishirikiana na Benki, wanaghushi cheki kwa kuandika *amount* zisizokuwepo wakati mwingine wanafikia hata kutoa *overdraft* kwa wenyewe tu Halmashauri na Benki bila kibali maalum. Kwa hivyo, naiomba Serikali, jambo hilo ni jambo zito, liwachukulie hatua mara moja. Sio waseme kwa maneno au kuchukua mfano uliokuwepo sasa kumhamisha Mtendaji hapa na kumweka pengine. Wachukuliwe hatua kali mara moja ili kukomesha mambo haya. Bila ya hivyo, kazi hii itaendelea ikiwa huyu hakuchukuliwa hatua na mwingine hakuchukuliwa hatua itakuwa kila siku mambo haya yanazidi kuendelea na tutakosa uchumi kwa kila siku. Nchi yetu sasa hivi tunakabiliwa na mambo mengi, umaskini, hiyo bajeti yenyewe haitazamiki. Haipo na bajeti imeshakwisha hata miezi sita haijafika. Kwa hivyo, ni vizuri tuyafanye hayo kwa kuwachukulia hatua haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine nilitaka kuzungumzia juu ya habari ya kusimamia miradi ya maendeleo. Halmashauri 41 mpaka sasa hazijapelekewa fedha za miradi ya maendeleo. Kwa hivyo na hili pia walione

Serikali na iweze kuwapelekea haraka miradi ya maendeleo. Pia miradi ya afya haijakwenda kwenye Mfuko wa Afya wa Jamii, haijapelekwa eti kwa kisingizio akaunti haijafunguliwa. Kwa hivyo, hiyo si kisingizio fedha zipelekwe na akaunti ifunguliwe haraka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hayo machache, naomba nikae kwa sababu mengi yameshasemwa na wenzangu siwezi kuyarudia tena. *(Makofi)*

**MHE. PETER J. SERUKAMBA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma hivi vitabu, kwanza niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote tatu. Kama umesikiliza maneno yaliyosemwa na Wabunge, mimi Wabunge niwaombe jambo moja, tusilalamike! Tunayo nafasi ya kuisaidia nchi yetu kwa vile Kanuni zinaturuhusu. Mawaziri hawa tunavyoongea hapa wanatuona watu wa hovyo tu, hawa wanapiga kelele wataondoka, tutaondoka lakini kwa sababu hatutaki kutumia Kanuni zetu tukija hapa tukimfukuza mmoja baada ya mwingine, watafanya kazi hawa. Yanayoendelea nchi hii hayaeleweki, haiwezekani! Mna Serikali, haya yanafanyika haiwezekani! Kila jambo linalotokea, kila Wizara kuna jambo la hovyo. Mawaziri wapo wala hawajali na sisi tunakuja hapa tunalalamika. Amesema Mheshimiwa Zambi, nawaomba Wabunge wa CCM twende kwenye *caucus,* tufanye kazi tuliyotumwa. *We cannot not allow* haya yanayoendelea.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukisoma ripoti ya Mzee Cheyo, ukurasa wa 11, hili lenyewe nalifahamu vizuri sana, tumepitisha fedha hapa ya miradi ya barabara shilingi trilioni 1.2 wakati tunapitisha tulikuwa na deni la shilingi bilioni 420 ambalo halikuwa sehemu ya bajeti. Mpaka leo tunavyoongea, zimetoka shilingi bilioni 380 peke yake. Maana yake tumelipa deni, bajeti hatujalipa, maana yake ni nini? Miradi 14 yote imesimama na miradi iliyokwishaanza ikisimama tunalipa *interest*. Hii ni *EPA* kuliko *EPA* mnayoisema. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitawapa mfano, barabara moja ile ya kutoka Isaka kwenda Lusahunga, ya *Straburg*, amesimama toka mwezi Agosti na kila mwezi tunamlipa *interest 2.7 bilion*. Tunapofika miezi 10 tutakuwa tumemlipa shilingi bilioni 27 za *interest* peke yake, Serikali iko hapa na Wabunge tunapiga kelele badala ya kufanya kazi. Lazima wanaohusika tuwachukulie hatua. Haiwezekani tunakaa hapa, tunapitisha bajeti anakuja mtu, basi kama fedha zimekosekana aje kwenye *mini-budget* atuambie jamani *projection* zetu haziwezekani, hatujapata fedha. Ni kwa sababu Serikali hii inalidharau Bunge hili. Bunge hili toka tumeanza hatujafanya kazi ya Kibunge, tunafanya kazi ya kulalamika. Kwenye Halmashauri zetu kinachoendelea Mungu ndiye anajua. Nenda *ATCL*, Mungu ndiye anajua, nenda Bandari, Mungu ndiye anajua, Mawaziri wanafanya wanayoyataka. Nenda *CHC* Mungu ndiye anayajua, nenda Wizara ya Maliasili na Utalii yanayoendelea Mungu ndiye anajua, *TANESCO* Mungu ndiye anajua. Wabunge tuko hapa tunasema, nawaombeni Wabunge wa CCM tuisaidie nchi yetu. Kama kuna mtu atatulaumu lakini itakuwa tumeisaidia nchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, twendeni tukakae kwenye Kikao cha Chama, Waziri ambaye tunaona hatusaidii tumwambie tupishe, tumwambie Rais atafute mwingine. Tukisubiri Rais afanye hatofanya, tutakuwa tunalalamika tu. Twendeni tukamsaidie afanye kazi hii. Wenzetu wa Mabunge yaliyopita walifanya, eeeh, watu walifanya. Mbilinyi aliondolewa humu ndani, Iddi Simba aliondolewa humu ndani, Ngasongwa aliondolewa humu ndani, sisi tunaogopa nini? Watakuja wanatudanganya wanadhani wao wana akili kutushinda sisi, tufanye kazi ya Kibunge. Yanayoendelea huko kwenye korosho, ni hatari, kwenye sukari ni hatari, mnauza mpaka mbolea *fake* halafu Waziri wa Kilimo yupo, kila Waziri yupo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kwenye ukurasa 55, tumeona shilingi bilioni 50 zimepotea, Mawaziri wako Ofisini, hakuna anayejali. *TBS* hakuna anayejali na tunanyamaza tu. Mimi nawaombeni sana Waheshimiwa Wabunge tutekeleze jukumu letu, haiwezekani tukae hapa kama walivyosema wenzangu na sisi tuwe sehemu ya kupiga kelele angalau liwepo kundi moja katika Taifa hili ambalo lina nia njema tutatue matatizo yetu. Tukifanya hivyo, nawaambieni hakuna Waziri atafanya vitu vya mchezo lakini kama wanafanya, hamna anayewauliza tatizo ni nini, Wabunge wale watapiga kelele, watakaa, tena wanasema si wanataka wasikike Majimboni, ndio lugha zao. Wanadhani tunapoongea juu ya matatizo ya nchi hii nia yetu tunataka tusikike na sisi eti tumesema. Sasa tuseme, tuamue tutumie Kanuni, hicho ndicho ninachowaomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukianza kuyasoma haya na kuyasema yako mengi. Leo tunavyoongea bajeti hii, tena walisema leo shilingi 1.3 trilioni, Waziri wa Fedha amefanya *reallocation* bila ya kuliambia Bunge na watu tumekaa tu hapa. Watakuja mwezi wa Juni watatupiga maneno tutapitisha bajeti. Naomba tuingie kwenye historia jamani, liwe Bunge la kwanza ambalo litasema hapana. Umefika wakati vizazi vyetu vitatukumbuka kama tutaamua kusema hapana, tuseme leo, wala sio kesho.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nakushukuru. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Mheshimiwa Felister Bura mchangiaji wetu wa mwisho kwa siku ya leo.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, sina tofauti na Mbunge aliyekaa kwa maoni yake aliyoyasema kwa sababu wananchi wanaumia na sisi Wabunge tunaumia na tunasemwa mitaani kwamba hatuisimamii Serikali yetu, ifike muda sasa tuisimamie. Hatuwezi kupiga kelele kila siku

kwamba matumizi mabaya ya Halmashauri, matumizi mabaya Serikalini lakini wenzetu wanakula nchi. Haiwezekani jamani! Haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza, kwa nini hawa Wakurugenzi wa Halmashauri wanateuliwa, kwa nini wasifanye usaili kama Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma? Kwa nini? Kwa sababu wanateuliwa na anajua kumchukulia hatua mpaka atoke Ofisini ni suala refu, kwa hiyo wamejenga kiburi kwamba acha waseme. Wanafanya makosa, wanahamishwa, hakuna hatua inayochukuliwa na kwa sababu wameteuliwa, hakuna muda wa kusema kwamba tutaangalia ufanisi wake. Wakurugenzi wa Mashirika ya Umma, juzi tumepitisha Mifuko ya Hifadhi ya Jamii, miaka mitano mitano. Wakurugenzi wa Halmashauri nao wafanyiwe hivyo, wafanye usaili, tupime kazi zao wanafanyaje kazi kwa usaili. Mkurugenzi ameibiwa shilingi bilioni sita (6) bado yuko ofisini, amefanya nini tunamhesabu kwamba amefanya kazi kwa ufanisi, haiwezekani!

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeshangazwa sana na ripoti ambayo iko mbele yangu ya Kamati ya Mheshimiwa Cheyo, Kamati inayoshughulikia Hesabu za Serikali. Hapa naona Serikali ina deni la shilingi trilioni 14.4 zaidi ya bajeti tuliyoipitisha mwaka jana. Hivi kweli hali nzuri kwa Mtanzania, maisha bora kwa Mtanzania itakujaje? Deni la shilingi trilioni 14.4 halafu tunawaambia Watanzania kwamba uchumi wa nchi hii unakua, uchumi unakua hivyo? Deni linakuwa kwa asilimia 39.5, uchumi unakua kwa asilimia 6.5 halafu unawaambia Watanzania uchumi unakua, hivi ni kweli jamani? Watanzania wanajua, wamesoma, tusiwadanganye kwamba uchumi wa nchi hii unakua, haukui, deni linakua kwa asilimia 39 maisha bora hawatayaona. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia taarifa pia wanasema kwamba dhamana, kuna mtu ameamua tu anaweka dhamana, anadhamini Mashirika ya Umma na ya

Binafsi mpaka imefikia asilimia 96.8. Lakini sheria inamtaka mwisho wa kutoa dhamana za Serikali ni asilimia 70, huyu mtu amefanywa nini, Serikali imenyamaza kimya. Amefanywa nini huyu mtu, amevunja sheria za nchi, lakini yuko ofisini anakula nchi, anaishi kwa raha kwenye kiyoyozi, anafanya kazi ofisi yenye kiyoyozi, hajafanywa jambo lolote. Hebu sasa Serikali yetu ichukue hatua kwa wale ambao wanavunja sheria kwa makusudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa ya *POAC* ukiangalia gawio la Serikali kutoka kwenye Mashirika ya Umma, limeshuka toka shilingi bilioni 40 hadi shilingi bilioni 28.7 hebu angalia huo utendaji. Deni linakua kwa asilimia 39, uchumi unakua kwa asilimia sita (6%), lakini Mashirika ambayo yanatakiwa yatoe gawio kwa Serikali, gawio limepungua tangu shilingi bilioni 40 hadi shilingi bilioni 28.7. Tunataka maisha bora kwa Mtanzania yatakuja?

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la *MSD,* ndio waagizaji wa dawa na vifaatiba kwa nchi nzima, lakini dawa zikifika bandarini ni siku 21. Wagonjwa wanakufa Dodoma, wananchi wanakufa Kigoma, wananchi wanakufa Bukoba, lakini dawa ziko bandarini kwa siku 21 kwa sababu taratibu za *TRA* haziruhusu, lakini wafanyabiashara wa kawaida wanaoleta nguo na viatu mizigo yao haikaguliwi *fast track,* inakaguliwa huko kwenye *bond* yao, *MSD* yenye kubeba dawa za wagonjwa za Watanzania dawa zao zinakaa siku 21 hazijatoka bandarini, tunakwenda wapi ndugu zangu?

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nisikilizie dawa zikimaliza muda. Bohari lao limejaa, kuna dawa zilizoisha muda, lakini kuomba kibali Wizara ya Afya miezi sita (6), yaani kuomba kibali ili dawa zile ziharibiwe miezi sita (6). *MSD* iko Dar es Salaam, Wizara ya Afya iko Dar es Salaam, Waziri yuko Dar es Salaam, Naibu yuko Dar es Salaam, Katibu Mkuu yuko Dar es Salaam, miezi sita kupata kibali? Hivi kweli hayo maisha bora kwa Mtanzania tutayafikia mwezi gani? Kama huo ndio

utaratibu na *MSD* kupata fedha za kuagiza dawa, maana wakiagiza dawa ni miezi sita hadi miezi tisa ndio dawa zinaingia nchini. Fedha za kuagiza dawa wanapelekewa Novemba, Desemba unategemea dawa zitakuwepo hospitalini, unategemea Mtanzania atapata hizo dawa mwaka gani? Mwezi Novemba au Desemba Wizara ya Fedha ndio inapeleka fedha *MSD*, dawa hizo tunazitegemea zitafika lini Kigoma, Dodoma na zitafika lini kwa watumiaji kwenye zahanati mbalimbali?

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba wahusika, Wizara ya Fedha mmekwamisha mambo mengi kwa wananchi, mmekwamisha mambo mengi, Fedha za Maendeleo mpaka leo asilimia 30 halafu tunasema tunaendelea, halafu tunasema Watanzania tunaendelea asilimia 30 watafanya nini? Baraza la Madiwani litafanya nini wakati Fedha za Maendeleo ni kidogo sana kuliko fedha za matumizi. Lakini pamoja na udogo wake asilimia 30, nimesoma kwenye ripoti ya Kamati ya Mzee Cheyo wanasema mpaka mwezi Mei, 2010, Wizara ya Nishati na Madini ndiyo ilipelekewa fedha za maendeleo kwa mara ya kwanza. Mwezi Mei 2010 wakati tunajadili bajeti ya mwaka mwingine wa fedha unategemea kitu gani? Unategemea kwamba mipango yote ya maendeleo itafanyika? Mwezi Mei na mwezi Juni tuko hapa tunajadili bajeti, kwa kweli watumishi wa Serikali mnatuangusha. Mnatuangusha jamani! Serikali hii inachukiwa kwa sababu ya watendaji, hebu watendaji waamke sasa. Waziri wa TAMISEMI tusikie wangapi wamesimamishwa kazi, wangapi mmewafukuza kazi ndani ya Wizara ya Fedha, wangapi wamesimamishwa kazi na wangapi wamefukuzwa kazi kwa kutotimiza wajibu wao lakini hayo yote yanasemwa na wala sio mara ya kwanza, Wabunge wanasema mishipa imewatoka shingoni lakini matokeo yake ni bure kabisa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna Baraza la Taifa la Uwezeshaji Kiuchumi liliundwa mwaka 2004 kwa Sheria Namba 16 lakini Baraza hili halijaweza kufanya kazi mpaka leo kwa

sababu halijawezeshwa. Zinahitajika shilingi bilioni 25.5 tu Baraza hili litumike kwa ajili ya kuwaneemesha wananchi lakini halijapewa fedha mpaka leo ninavyoongea, ufanisi utatoka wapi?

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**WABUNGE FULANI:** Taarifa!

**WABUNGE FULANI:** Mwongozo!

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Felister Bura tuanze na taarifa halafu, miongozo miwili? Kwanza ni taarifa.

## T A A R I F A

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE):** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 68, nilitaka tu kulitaarifu Bunge hili kwamba Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Mustafa Mkulo yupo kikazi Washington, *World Bank,* kwa ajili ya kufanya maandalizi ya bajeti. Huu ni mkutano wa ratiba, wa utaratibu ambao ulipangwa kwa tarehe hizo na kuna mikataba ambayo amekwenda kusaini kwa niaba ya nchi hii sio kwamba hayupo humu ndani.

Pili, Mheshimiwa Waziri Mkuu yupo hapahapa katika eneo la Bunge, anatusikiliza na wasaidizi wake tuko hapa. Kwa hiyo, kutokumwona kwenye Kiti kile sio kwamba hasikilizi, yuko katika eneo la Bunge hilihili. Nilitaka kutoa tu taarifa hiyo Mheshimiwa Naibu Spika.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu. Miongozo ile miwili hebu wasimame tena, ni Mheshimiwa Masele halafu Mheshimiwa Machali.

## MWONGOZO WA SPIKA

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, natumia Kanuni ya 68(7). Katika Bunge la mwezi Februari, niliomba mwongozo wako kuhusiana na makampuni ambayo yalikuwa yanapaswa kulipwa *stimulus package* pamoja na fidia ya hasara kwa makampuni haya yanayouza pamba na mpaka leo sijapata majibu yoyote na tukimaliza Bunge hili tunabakiza miezi miwili kuanza musimu wa pamba na mpaka sasa hakuna uhakika wa Mabenki kuweza kukopesha makampuni hayo. Kwa msingi huo, wakulima mpaka sasa hawana uhakika kama pamba yao ambayo wamelima msimu huu itanunuliwa. Kwa hiyo, nilikuwa naomba mwongozo wako nipatiwe majibu ya mwongozo ambao niliomba katika Bunge lililopita mpaka leo hii sijapewa.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana. Mheshimiwa Machali.

**MHE. MOSES J. MACHALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Mimi ninasimama pia kwa mujibu wa Kanuni ya 68(7) kuweza kuomba mwongozo wako. Muda mfupi Waheshimiwa Wabunge wengi wameonekana kuchangia kwa uchungu sana juu ya mwenendo mzima wa Serikali hasa kufuatia taarifa ambazo zimewasilishwa na Wenyeviti wa Kamati tatu. Kubwa zaidi ni taarifa ambayo imetolewa na Mheshimiwa Mbunge Peter Serukamba kwamba Kampuni ya Struburg imesimama kufanya kazi tangu mwaka jana na leo hii Serikali inalazimika kuilipa takribani shilingi bilioni 2.7 kampuni hiyo ama kwa uzembe ama kwa sababu ya kukosekana kwa fedha. Sasa naomba mwongozo wako kwa nini Serikali isitupe taarifa hapa Bungeni juu ya watu walioingia mikataba ya aina hiyo, aidha, kukosekana pesa leo hii Serikali inalazimika kutumia fedha za walipa kodi kwa kiasi kikubwa namna hii, halafu matatizo yanaendelea kujitokeza katika maeneo mbalimbali. Naomba mwongozo wako juu ya hili.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Zitto.

**MHE. KABWE Z. ZITTO**: Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa naomba nipate ufafanuzi kutoka kwa Mnadhimu Mkuu wa Serikali. Ametoa taarifa hapa kwamba Mheshimiwa Waziri wa Fedha yuko Washington kwa ajili ya maandalizi ya Bajeti. Bunge lilitoa ratiba ya hoja za Kamati hizi ambazo zimewasilisha taarifa zake leo ambapo Kamati mbili, Kamati ya *PAC* na Kamati ya *POAC* zinaihusu Wizara ya Fedha moja kwa moja, Kamati ya *LAAC* inahusu Wizara ya Fedha pamoja na Wizara ya TAMISEMI.

Mheshimiwa Naibu Spika, ukiangalia *itinerary* kwa mwaka za Mawaziri wetu hakuna Waziri anayeongoza kusafiri kama Waziri wa Fedha na ukiangalia matatizo ya Wizara katika Serikali hakuna Wizara inayoongoza kwa matatizo na inayoongoza kwa kutokuchukua maamuzi na Mawaziri wenzake wanajua, kama Wizara ya Fedha; na sababu kubwa ni kwa sababu Waziri wa Fedha hakai ofisini. Waziri wa Fedha anabadilisha ndege kutoka nchi moja kwenda nchi nyingine, mikutano ya kwenda Washington na kadhalika anaweza akawakilishwa ama na Naibu Waziri, ana Manaibu Waziri wawili au Katibu na ana Manaibu Makatibu Wakuu watatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mnadhimu Mkuu wa Serikali aeleze *is it in order* kwa Waziri wa Fedha wakati wa taarifa ya utekelezaji wa bajeti kwa Kamati mbili zinazomhusu moja kwa moja, zinajadiliwa ndani ya Bunge na anatakiwa yeye a-*respond*; aende kwa Wazungu kutafuta asilimia 30 ya misaada ambayo tunapewa; *is it in order?* Mheshimiwa Mnadhimu Mkuu wa Serikali na unaweza ukasimama kabisa kwa kujiamini na kulipa taarifa Bunge kwamba Waziri wa Fedha, Waziri anayeongoza kwa kusafiri, hakai akasikiliza hoja za matumizi ya Serikali tukiwa kwenye Kamati na unamtetea? Mheshimiwa Mnadhimu Mkuu naomba ufafanuzi wa jambo hili.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zitto ulitakiwa hoja yako uielekeza kwangu.

**MHE. KABWE Z. ZITTO**: Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niilekeze kwako.

**NAIBU SPIKA**: Ahsante sana.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA**: Mwongozo wa Spika!

**NAIBU SPIKA**: Jamani mwongozo tena? Basi kwa kifupi sana kwa sababu ya muda tafadhali.

**MHE. PETER J. SERUKAMBA**: Mheshimiwa Naibu Spika, mimi nilitaka nipate tu ufafanuzi vizuri kwenye maelezo yaliyotolewa na Serikali kwamba Waziri wa Fedha amekwenda Washington kwa ajili ya maandalizi ya Bajeti. Hivi kweli Bajeti ya nchi hii inaandaliwa Washington? Nataka kujua; tuna mpango wa mwaka unaokuja ambao utasomwa hapa Bungeni, utajadiliwa na Bunge ambapo ninaamini mpango utakuja na watu wa Tume ya Mipango na Waziri wa Fedha ni *component* muhimu sana katika mpango huo, ambao huo mpango ndiyo unazaa bajeti. Kwa hiyo, mnataka tuamini na Watanzania waamini bajeti ya nchi hii inatengenezewa Washington?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nilidhani nimeeleweka kwa sababu nimetoa taarifa, narudia tena, Mheshimiwa Waziri wa Fedha yupo Washington. Nimetumia *terminology* fupi kusema maandalizi ya bajeti kwa sababu Bunge hili ndilo lenye jukumu hilo, nilifikiri ndiyo lugha inayofahamika. Labda niseme kwa kirefu sasa kwamba, katika kalenda ya *IMF* na *World Bank* huu ndiyo wakati wao wanakutana yaani hawatamsubiri Waziri wa Fedha wa Tanzania apange ratiba yake ili aende kwa muda wake. Kwa hiyo, kuna Mkutano wa *IMF* na *World Bank*, kama nchi tuna *interest* na Mkutano huu na sio leo kila mwaka huwa anakwenda. Kwa hiyo, huu ni mkutano, sisi ni wanachama lazima tuhudhurie na hutuwezi kukataa ukweli

kwamba kuna fedha ambazo tunazipata kutoka *World Bank*, sio leo wala sio kesho na amefuatana na Naibu Waziri wa Maji ambaye naye amekwenda kufuatilia masuala ya miradi ya maji na fedha ambazo kila mara hapa Bungeni huwa tunapiga kelele kwamba miradi ya vijiji kumi haiendi, huu ndio mkutano wamewaita Mawaziri hawa waende kutatua matatizo haya ya Tanzania. Hili ni jambo muhimu kuliko kutokwenda lina maslahi mpana kwa Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilitaka kusema Mheshimiwa Waziri wa Fedha ametumwa katika jambo lenye maslahi ya nchi sio kuliko hapa, huwezi kusema kuliko hapa. Mimi nimesema hajaenda kufanya mambo yake kama Mkulo amekwenda kufanya mambo makubwa ya nchi.

Nataka kumuuliza ndugu yangu, hebu tuulizane tu, ukiniambia kwamba Waziri wa Fedha anasafiri kuliko Waziri yeyote hapa, hata akili ya kawaida nakataa. Hivi Waziri wa Mambo ya Nje anasafiri namna gani? Tuseme ukweli, tunaweza kuwa tumeumizwa sana na utendaji na watendaji wa Serikali kutokana na taarifa za *CAG* lakini isisababishe tukazua mambo mengine. Kwa hiyo, Waziri wa Fedha amekwenda kwa safari hiyo lakini katika orodha ya Mawaziri wanaosafiri sana, orodha niliyonayo hata mimi, maana anayotoa vibali vya safari ni Mheshimiwa Waziri Mkuu, Waziri wa Fedha hawezi kuwa wa kwanza kusafiri kuliko Mawaziri wote. Mimi ndiyo najua zaidi kwa sababu niko Serikalini. Naomba kutoa hiyo taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Waziri Mkuu kwa majibu hayo. Niseme tu wakati mwingine ni vema Waheshimiwa Mawaziri kama kuna jambo ambalo linakuhusu mkaaga tu Meza tukalitaarifu Bunge mapema ili watu wasitafsiri kwamba kuna nia mbaya kwa kutokuwepo kwenu. Lakini pia ni matumaini yetu kwamba wakati wa kujadili Mpango basi Mheshimiwa Waziri atakuwa amerudi kwa sababu ni jambo muhimu sana. Itakuwa ni

vigumu sana kuendelea kujadili Mpango kama Mheshimiwa Waziri wa Fedha atakuwa hayupo hapa, itakuwa ngumu kweli! Itakuwa ni vizuri kama mambo haya yatakuwa yamepungua huko akarudi akawepo kwa sababu tunapojadili Mpango na kuweka vipaumbele vya mambo haya ni vizuri sana awepo.

Mwisho limekuwepo suala la *stimulus package,* mara ya tatu sasa kwa hesabu yangu tangu alipoulizwa na Mheshimiwa Masele, likaulizwa tena hapo katikati na limeulizwa tena leo. Sasa hili Mheshimiwa Waziri wa Nchi, naomba maelezo yake kwa kifupi sana, kwa sababu muda haupo upande wetu.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (SERA, URATIBU NA BUNGE)**: Mheshimiwa Naibu Spika, nadhani Mheshimiwa Mbunge alikuwa na orodha ya watu ambao hawakutendewa haki ambao walistahili lakini hawakupewa. Ndivyo wanavyosema na kwamba angefurahi wale watu walipwe ili wajiandae waweze kufanya manunuzi ya pamba, walipe madeni yao ya Benki, ndicho walichosema. Anao watu ambao walistahili kupata lakini amekuwa anawaulizia hapa hawakupata. Kwa hiyo, anaomba taarifa kwamba wale watu ambao anawajua walistahili kupata hawakupata, lini watapewa ili waweze kulipa mabenki na waendelee na biashara yake. Ndiyo swali lake?

**NAIBU SPIKA:** Ni hivyo Mheshimiwa Masele? Kwa sababu ya muda kwa kifupi sana.

**MHE. STEPHEN J. MASELE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii. Kwenye orodha ambayo Waziri wa Fedha aliiweka, makampuni yaliyokuwemo mle mengine hayakustahili na makampuni yaliyostahili hayajapata. Tangu mwaka 2008 yanaendelea ku-*service* mikopo ambayo ilitakiwa ilipiwe na Serikali ilivyoahidi kwamba wanunue pamba na ile shilingi 80/- ingelipwa na Serikali. Sasa kinachotokea sasa hivi yale makampuni haya-*qualify* kukopeshwa tena na Benki na yasipokopeshwa hayawezi kuingia sokoni na yasipoingia sokoni

maana yake pamba yote iliyolimwa mwaka huu haitanunuliwa, ama itanunuliwa na wachache ambao watashikilia bei na kushusha bei ya pamba ambayo inaenda juu sasa hivi. Kwa hiyo, hoja yangu hapa Serikali ije na majibu kwamba ni lini itamaliza suala hilo ambalo iliahidi katika Bunge na Mheshimiwa Rais aliahidi.

**NAIBU SPIKA:** Nakushukuru sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi linahataji muda. Nilichanganya na orodha ambayo Mheshimiwa Spika aliwahi kuagiza wakati fulani kwamba iwe *laid down* Bungeni, sasa nilidhani kwamba Mheshimiwa Masele bado yupo kwenye mstari uleule wa jambo ambalo lilitakiwa liwekwe mezani kabla lakini hili litahitaji muda na kwa sababu umetaka mwongozo wetu tutawasiliana na Serikali tuone namna ya kurudi.

Vilevile suala la Mheshimiwa Machali la matumizi ya shilingi bilioni 2.7 kwa mwezi kwa kampuni ile na lenyewe tutalitolea maelezo katika muda mwafaka.

Baada ya maelezo hayo, muda wa shughuli zetu umekamilika, tutaendelea na masuala haya kesho na mchangiaji wa kwanza atakuwa Amina Mwidau, Mheshimiwa Jerome Bwanausi, Mheshimiwa Stephen Masele, Mheshimiwa Christowaja Mtinda, Mheshimiwa Susan Kiwanga na wengine wataendelea kama kawaida.

Kwa maana hiyo, naomba kuahirisha shughuli za Bunge hadi kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 1.54 usiku Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 19 Aprili, 2012 Saa Tatu Asubuhi)*